



*Seyidna Ahmad a.s. aliyetimiza bishara ya ujaji wa Yesu mara ya pili katika zama hizi. Amekuja jinsi alivyotokea Eliya mara ya pili kwa sura ya Yohana Mbatizaji. ‘Mwenye masikio na asikie’.*

# **YESU KAFIA WAPI?**

**J. D. Shams**

# **YESU KAFIA WAPI?**

**Mwandishi:Maulana J. D. Shams**

**Mfasiri: Muhammed Said Kibindu**

**© Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania**

**Chapa ya Tatu: 2006  
Nakala: 1000**

**Kimechapwa na  
Ahmadiyya Printing Press  
P.O. Box 376  
Simu: 2110473, Fax 2121744  
Dar es Salaam  
Tanzania.**

**ISBN 9987 - 438 - 03 - 2**

# YALIYOMO

|                     |    |
|---------------------|----|
| Dibaji .....        | v  |
| Neno la Mbele ..... | vi |
| Utangulizi .....    | ix |

## SURA YA KWANZA:

|                                  |   |
|----------------------------------|---|
| Karaa kutoka katika Injili ..... | 1 |
| Maombi ya Yesu .....             | 1 |
| Je, Yesu alikuwa mlaaniwa? ..... | 5 |
| Kufufuka kwa Watakatifu .....    | 6 |
| Ishara ya Nabii Yona .....       | 8 |
| Ndoto ya Mkewe Pilato .....      | 9 |

## SURA YA PILI:

|                           |    |
|---------------------------|----|
| Ushahidi wa Matukio ..... | 11 |
| Masuala .....             | 12 |

## SURA YA TATU:

|   |    |
|---|----|
| Maelezo ya Kiakili kuhusu kisa cha Kufufuka ..... | 25 |
|---|----|

## SURA YA NNE:

|                                      |    |
|--------------------------------------|----|
| Ushahidi wa maandishi ya Kale .....  | 35 |
| Giza linashuka ardhini .....         | 35 |
| Tetemeko la Ardhi .....              | 36 |
| Pilato anakabidhi mwili .....        | 39 |
| Yesu aponywa .....                   | 40 |
| Mayahudi wanapata shaka .....        | 41 |
| Ndani ya Pango .....                 | 42 |
| Yesu anatoroka Pangoni .....         | 44 |
| Yesu anajifanya mkimbizi .....       | 46 |
| Maoni ya Mfasiri wa Kijerumani ..... | 48 |

## SURA YA TANO:

|                                   |    |
|-----------------------------------|----|
| Sanda ya Yesu .....               | 50 |
| Je, Kristo kafia msalabani? ..... | 51 |

|   |     |
|---|-----|
| <b>SURA YA SITA:</b>  |     |
| Maoni ya Utabibu wa Kisasa .....                                | 56  |
| <b>SURA YA SABA</b>   |     |
| Je Yesu alipaa Mbinguni? .....                                  | 62  |
| Kujitokeza ghafla .....   | 63  |
| <b>SURA YA NANE:</b>  |     |
| Imani hii ya kwamba Yesu alifia msalabani na amepaa .....       |     |
| mbinguni imepatikanaje? .....                                   | 70  |
| <b>SURA YA TISA:</b>  |     |
| Paulo na Upagani .....  | 84  |
| Je, Yesu alitabiri juu ya kusulubiwa na kufufuliwa kwake? ..... | 91  |
| <b>SURA YA KUMI:</b>  |     |
| Ukombozi au Kafara .....  | 94  |
| <b>Sura ya Kumi na Moja:</b>                                    |     |
| Yesu anakwenda India .....                                      | 110 |
| Kaburi la Musa .....  | 112 |
| Makabila yaliyopotea ya Wana wa Israeli .....                   | 113 |
| Waisraeli katika India .....                                    | 118 |
| Ujumbe wa Yesu .....  | 129 |
| Mtakatifu Thomas katika India .....                             | 131 |
| Yesu anawatafuta kondoo wengine .....                           | 138 |
| <b>SURA YA KUMI NA MBILI:</b>                                   |     |
| Maisha ya Yesu yasiyojulikana .....                             | 142 |
| Mabudha na Yesu .....   | 142 |
| <b>SURA YA KUMI NA TATU:</b>                                    |     |
| Yus Asaph na Yesu .....   | 155 |
| <b>SURA YA KUMI NA NNE:</b>                                     |     |
| Bishara Kuu .....   | 167 |

## **DIBAJI**

Ni furaha kubwa kuweka mbele ya wasomaji wa lugha ya Kiswahili kitabu hiki kinachoeleza kwa utaalamu wa hali ya juu sana baadhi ya matukio ya muhimu yaliyotukia katika maisha ya Yesu lakini yalikuwa katika uficho kwa muda mrefu. Mwandishi wa kitabu hiki ni marehemu Maulana J. D. Shams aliyekuwa Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Uingereza kwa miaka kumi toka mwaka 1936 hadi 1946. Alikitunga kwa lugha ya Kiingereza.

Marehemu Maulana Shams alipenda sana kitabu hiki kifasiriwe kwa Kiswahili ili waijuao lugha hii nao waweze kunufaika na elimu iliyomo ndani yake. Lakini sasa tafsiri hii inapoona mwanga wa ulimwengu huu, mwandishi mwenyewe hayupo duniani. Aliaga dunia tangu miaka 16 hivi iliyopita. Twamwombea marehemu Maulana Shams malipo bora ya utumishi wake; Mwenyezi Mungu ampatie makazi mema katika Pepo za daima za radhi yake.

Pia twamshukuru Ndugu M. S. Kibindu wa Dar es Salaam, Afisa katika idara ya Ardhi Jijini humo, ambaye ni Mwanajumuiya mwenye kujitolea sana kwa ajili ya shughuli za dini, ambaye alichukua jukumu la kukturafsiri kitabu hiki kwa lugha fasaha ya Kiswahili. Yu mshairi hodari wa lugha ya Taifa, na bila shaka wasomaji wa gazeti la "Mapenzi ya Mungu" wanasoma mara kwa mara mashairi yake na tenzi zake. Yu bingwa wa lugha ya Kiswahili, kwa hivyo, wasomaji wa kitabu hiki wataweza kujiongezea elimu kuhusu tukio la msalaba na mambo chungu nzima yaliyotendeka baadaye pamoja na kupata utamu wa lugha yenyewe.

Twatoa tafsiri hii kwa kumtegemea Mola wetu mtukufu asaa atawaongoza wengi kwa njia hii kwenye ukweli usiobatilika. Na neno letu la mwisho ni kwamba sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu.

**JAMIL R. RAFIQ,  
Mbashiri Mkuu**

**Masjid Ahmadiyya  
Nairobi**

**Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya  
Nchini Kenya.**

## NENO LA MBELE

Maulawii Shams amenitunukia heshima kubwa sana kwa kuniomba niandike neno la mbele kwa ajili ya utunzi wake mzuri sana na wenye kutia nuru. Nami nimefurahi kuipokea kazi hii kwa mikono miwili.

Ili dini ishike nafasi yake ya asili na ya halali katika maisha ya kiroho ni lazima ijengwe juu ya misingi ya ukweli; na kutafuta ukweli na kuufafanua ni moja ya shabaha za Uislamu. Maulawii Shams kwa hakika ametia bidii nyingi sana katika utafiti wake na matokeo yake ni kwamba ameweka mbele yetu sanaa ambayo imetengenezwa kwa umahiri na ustadi ambao hata wanasheria wakuu wanaulilia ngoa. Matokeo ya utafiti wake ameyaratibu kwa ufasaha na kwa uwazi sana. Hata hivyo kwa kuwa mlainifu katika kuzitoa hoja zake huenda hazitakubalika kwa wale wanaofasiri imani kuwa nyongeza katika vitu ambavyo haviwezi kuthibitishwa. Maulawii Shams ameufagia uwanja uliokuwa umejaa visa na fikra nyingi za upotofu na hapana shaka yeye amefutilia mbali dhana zote hizi mbaya bila ya masikhara. Mara nyingine inadaiwa kwamba Ukristo umefikia daraja la juu sana katika dini, lakini dai la namna hiyo linawezaje kuafiki hali ya Ukristo ambao itikadi na misingi yake yote inaweza kuthibitishwa kuwa ni mibovu? Yesu alikuwa mtume aliyeletwa na Mwenyezi Mungu ili atangaze ukweli kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli. Ukweli huo hivi sasa unahesabiwa kuwa unapatikana katika mfumo wa imani na itikadi zinazohubiriwa kwa jina la Ukristo katika kila pembe ya dunia waishiyo binadamu, lakini imani na itikadi zote hizo ziko kinyume na mafundisho ya Yesu. Ni kiasi gani cha mafundisho ya Yesu kinachopatikana katika Ukristo wa leo? Jawabu ni kwamba hakuna kabisa. Sasa basi, kama Ukristo wa leo umejitenga kabisa na mafundisho ya Yesu, kuna maana gani kusema kwamba Ukristo umefikia daraja la juu kuliko dini zote? Ingawaje kitabu hiki si kikubwa kwa umbile, lakini ni kikubwa sana katika ufanisi; na sura zote zilizomo ndani yake zinafanana kwa umuhimu na kwa kupendeza ingawaje wasomaji wengi wanadai kwamba zenye

kusisimua ni sura ya kufufuka na kupaa, na hususa ile ya kupaa. Hapana shaka kwamba Maulawii Shams ametia mwangaza katika suala hili la kutatanisha, na ushahidi mpya anaoutoa unakiuka mashaka ya kila mtu. Ushahidi huu mpya unahitaji kuchunguzwa na kufikiriwa sawa na uamuzi usitolewe haraka haraka bali utolewe bila ya upendeleo na vile vile jambo la maana ni kwamba mtu asipandwe na hasira kwa kugundua ukweli ulio kinyume na mawazo yake ya awali au yale ambayo ameyasikia kabla hajasoma kitabu hiki.

Udhaifu wa imani ya Wakristo na hususa kuhusiana na kupaa unaonekana na kudhihirishwa na tabia za wafuasi wa Ukristo ambao kila mara wanaukwepa mjadala wa swali la muhimu sana. Swali lenyewe, anasema Bwana W. Carew Hazlitt ni kwamba, “Je kuna mtu yeyote wa kuaminiwa ambaye alishuhudia kwa macho yake kitendo hiki cha kupaa na hatimaye akawafahamisha wale ambao wametufikishia maelezo ya tukio hilo sawa na haya tuyasikiayo hivi leo? Utafiti wa jambo hili kwa jumla unakwepwa, siyo tu na wapenzi wa Ukristo, bali pia na wapinzani mbalimbali kama vile Viscount Amberely na W. R. Cassels. Dakta Mosley, bila ya kutoa ushahidi wo wote anadai ya kwamba kupaa ni jambo lenye uhakika kama yalivyo mambo mengine katika historia.

Ambapo Dakta R. J. Campbell naye pia bila ya kutoa ushahidi wowote anadai ya kwamba kisa chote hiki ni sahihi kimaneno na pia kimatendo. Hata hivyo wote wawili hawaambatanishi ushahidi wowote kwenye madai yao ya kufufuka wala ya kupaa. Bwana F. C. Conybeare anaandika kwamba katika zama hizi za kisasa watu hawakubali kubabaishwa bali wanataka kujua kama kitendo cha kupaa kilitokea kweli. Hilo ndilo suala bayana ambalo Askofu Gore pamoja na wengine ambao ni wapenzi na wapinzani wa Ukristo wanajaribu kulikwepa ambapo Maulawii Shams amelijibu kikamilifu na kwa uwazi sana.

Suala hili pia limejibwa na watu wengi, licha ya utafiti mbalimbali na maelezo yawezayo kupatikana ndani ya maktaba za kila namna. Kwa ufanuzi zaidi hapa ninamnukulu tena Bwana F. C. Conybear akisema, “Je baada ya mjadala wote huu isingalikuwa rahisi kuwaambia watu

kuwa kisa hiki ni ngano za watu wa kale tu? Kwa vyovyote vile wao si watoto wachanga. Sasa kwa nini basi baadhi ya viongozi wa dini wanaona ugumu kusimama juu ya mimbari na kutoa maoni yao kuhusu masuala mbalimbali ya kielimu na badala yake wanapendelea kuficha elimu yao?"

**DUDLEY WRIGHT,**  
**(Phil. D. F. S. P.)**

## **UTANGULIZI**

Suala ambalo nitalijadili katika kijitabu hiki ni la muhimu sana kwa vile linahusiana sana na imani za dini kuu tatu, yaani dini ya Kiyahudi, Ukristo na Islam.

Mayahudi wanaamini kwamba kwa kumuwamba kwa misumari msalabani na kama ilivyoaminiwa kote, kwa kumfisha kifo cha “laana” Wayahudi wakathibitisha bila ya shaka yoyote kwamba Yesu alikuwa nabii mwongo.

Wakristo wanakubaliana na Wayahudi ya kwamba ni kweli kabisa kuwa Yesu alikufa kifo cha “laana”, lakini wao wanadai kuwa alikufa kifo hiki eti kwa sababu ya kuwakomboa binadamu. Mtakatifu Paulo anasema katika Wagalatia 3: 13 kwamba, “Kristo ametuokoa na laana ya Sheria kwa vile ye ye amelaaniwa kwa ajili yetu, kwani imeandikwa: amelaaniwa kila atungikwaye mtini.”

Marejeo haya yanahusiana na kumbukumbu la Taurati 21 :23 “Yule ambaye ametungikwa amelaaniwa na Mwenyezi Mungu”. Wakristo pia wanadai kwamba kifo cha Yesu juu ya msalaba kilichofuatiwa na kufufuka kwake ni msingi muhimu wa Ukristo. Katika Waraka wake kwa Wakorintho, Mtakatifu Paulo anasema: “Na kama Kristo hatafufuka, basi mahubiri yetu ni kazi bure na imani zenu pia ni kazi bure.” (15: 14). Kinyume na imani hii iliyoenea siku hizi, Mwenyezi Mungu amedai ndani ya Kurani Tukufu kwamba Yesu ni mmoja wa Mitume wake aliyetumwa kwa ajili ya kondoo waliopotea wa Nyumba ya Israeli ambaye kwa rehema yake, Mwenyezi Mungu amemwokoa na kifo cha laana kilichokusudiwa na Maadui zake, na akamfisha kifo cha kawaida kama walivyokufa mitume wengine.

Kwa hiyo kama tutahakikisha kwamba Yesu hakufa msalabani bali aliteremshwa akiwa amezimia na kwamba baadaye aliishi na kukamilisha ujumbe wake na mwishowe kufa kifo cha kawaida, tutakuwa tumethibitisha pia kwamba Wayahudi na Wakristo

wamepotoka katika sehemu ya maana sana ya imani zao. Na sitakuwa nimetia chumvi kama nitasema kwamba Ukristo wa siku hizi ambao umesimamishwa juu ya msingi wa kifo cha “laana” utafutika mara moja.

Katika kuzichukua Injili kuwa ndiyo ushahidi wa madai yetu kwamba Yesu hakufa msalabani ni lazima tuzingatie hoja zifuatazo:-

1. Thomas Paine anaandika kwamba mikutano ya Nice na Laodicea ilifanyika yapata miaka 350 baada ya muda usemwao kuwa ndiyo wakati alipoishi Yesu mwenyewe: na hivi vitabu ambavyo kwa pamoja vinaitwa Agano Jipyä vilipigiwa kura ya ndiyo au hapana kama tunavyofanya wakati wa kupitishwa muswada wa sheria. Vitabu vingi sana ambavyo vilifikishwa mikutanoni vilipata hapana nyingi na kwa hiyo vikakataliwa. Hivi ndivyo Agano Jipyä lilivyopatikana. “Kwa hali ilivyo, wao walitoa uamuzi wao kwa kupiga kura ya kuchagua ni vitabu vipi viachwe kando mionganini mwa lundo la vitabu vilivyoletna mkutanoni. Vitabu kadhaa vilikataliwa, vingine kama vile Apocrypha vilitiliwa mashaka, na vile ambavyo vilipata ndiyo nyingi vikapitishwa kuwa Neno la Mwenyezi Mungu. Kama kura ingeviangukia hivyo vilivyokataliwa, basi watu wote ambao hivi sasa wanajitata Wakristo wangalikuwa na imani tofauti na hii waliyo nayo hivi leo, kwani imani ya Mkristo mmoja inasababishwa na kura ya Mkristo mwingine”.
2. Kwa hiyo vitabu hivyo si Neno la Mwenyezi Mungu, na wala Wainjilisti hawakudai kwamba vitabu hivyo ni Neno la Mungu.
3. Vitabu hivyo viliandikwa baada ya kupita miaka mingi sana tangu kusulubiwa kwa Yesu “Wakati ambapo ilikuwa vigumu sana kwa waandishi hawa kukusanya habari zenyé kuaminika na kuziratibu vizuri kwa akili zao hazingeweza kuvikariri vitendo vyote jinsi vilivyofuatana wakati wa pilika pilika za kwenye mlima wa Calvary.”
4. Habari zilizovurungika na zinazopinzana ambazo

zinapatikana katika Injili zote nne ni ushahidi madhubuti ya kwamba habari zilizomo humo ni za mashaka mashaka na kwa hiyo zinaweza kuwa za ukweli au za uwongo.

5. Utafiti wa siku hizi umebainisha ya kwamba mwandishi wa Injili ya nne hakuwa Yohana wanafunzi wake Yesu bali mtu mwingine. Aya ya 24 ya Sura ya mwisho ya Injili hii inabainisha jambo hili. Kadhalika maandishi ya awali ya Kiebrania ya Injili ya Matei yalipotea na mtunzi wa hii Injili inayoonekana hivi sasa ni mtu asiyejulikana. Na wengine wawili, yaani Marko na Luka hawakuwa wanafunzi wa Yesu.
6. Hapana shaka yoyote kwamba kazi ya historia aghlabu inaathiriwa na imani za kibinagsi na tabia ya mwandishi wa historia hiyo.
7. Mambo mbalimbali yaliyotajwa katika Injili zote nne kama vile ukoo wa Yesu, kusulubiwa na kupaa kwake ni lazima vifanyiwe uchunguzi kwa namna ile ile kama tunavyochunguza mambo mengine ya kihistoria. Ushahidi wa kiakili ni lazima upatikane. Katika kuchunguza mambo yaliyopita ni lazima tuuchekeche ushahidi kwa uangalifu sana ili tuweze kutofautisha baina ya yale yenye kuaminika na yale yasiyoaminika na kuyakubali yale ambayo akili ya binadamu inaweza kuyapokea kwa kuyalinganisha na mengine ya namna hiyo.
8. Mwishowe, katika kuichunguza hii habari ya kusulubiwa na kufufuka kwa Yesu ni lazima tukumbuke ya kwamba Injili ziliandikwa katika wakati ambapo kwa sababu hii au ile, kifo cha Yesu juu ya msalaba kilikuwa kinaaminiwa na watu wengi ingawaje si na firka zote zilizokuwa zikijiita za Kikristo. Kwa hiyo kama ukigundua kwamba matukio fulani yaliyotajwa katika Injili hayakuitaja imani hii ni kwa sababu matukio hayo yalikuwa

ya muhimu sana hivi kwamba isingewezekana kuyasahau wakati wa kuratibu mambo yaliyotokea.

Kwa sababu ya umuhimu wa suala hili ninamwomba kwa moyo wa thabiti kila msomaji wa kijitabu hiki ayafikirie kwa uangalifu yote yale ambayo atayasoma na wala asiwe na upendeleo. Akifanya hivyo basi bila shaka atafikia uamuzi ulio sahihi na wa haki.

Kwa hiyo basi, wakati kitabu hiki kinachapishwa kwa mara ya tatu, ninapenda kutia nyongeza ifuatayo katika sehemu hii ya utangulizi.

Mnamo mwezi Agosti 1939 muda mfupi tu kabla ya kuzuka kwa vita kuu ya pili ya dunia, mimi nilichapisha tangazo kwa kichwa cha maneno “KABURI LA YESU NCHINI INDIA”. Mamia ya maelfu ya vipeperushi vyenye tangazo hili vilichapishwa. Niliwahi kutawanya kiasi cha vipeperushi elfu nne katika jiji la London na vitongoji vyake na mara hali ya nchi ikavurugika nami nikaahirisha utawanyaji huu hadi vita imalizike. Baada ya vita kumalizika na ulimwengu mzima kupata nafasi ya kuwa huru tena, wabashiri sita wa Kiislamu kutoka Qadian India, wakafika katika jiji la London. Kama kawaida wao walinijia makao makuu ya Msikiti wa London. Nikiwa ninasaidiwa na wabashiri hawa nikafanya mpango wa kuvitawanya tena vile vipeperushi. Nakala nyingi pia zilipelekwa kwa njia ya posta katika nchi mbalimbali za Ulaya na Amerika. Licha ya utawanyaji wa vipeperushi hivi, mimi niliweza vile vile kuchapisha kitabu kiitwacho “YESU KAFIA WAPI”. Karatasi zile pamoja na hiki kitabu vililetia msisimko jijini London hususa mionganoni mwa viongozi wa dini amba walishlushwa na kwa hiyo wakalazimika kutafakari sana juu ya uvumbuzi huu mpya. Magazeti mengi ya London yalitangaza makala ndefu ndefu kuhusu jambo hili. Gazeti liitwalo “Wimbledon Borough News” lilichapisha makala yenye maneno mia tatu (300) kuhusu uvumbuzi huu wa kaburi la Yesu. Katika makala hii mhariri ameandika:-

“Imam Shams pia ameudhihirisha ukweli kwa muhtasari

ndani ya taarifa aliyoichapisha katika vipeperushi kwa njia ya tangazo. Mamia ya maelfu ya vipeperushi vyenye tangazo hili vimetawanywa pahala pengi pamoja na hapa hapa Wimbeldon” (W. B. News 22 - Februari, 1946).

Makala hii ilichokoza maoni mbalimbali kutoka kwa wasomaji Baada ya makala zake kwenye matoleo ya tarehe 1, 8 na 29 Machi 1946 chini ya vichwa vya maneno: “Kwa nini kaburi halifunuliwi?” “Masomo kuhusu Msalaba, “Yesu kafia Wapi?” “Kaburi la Yesu,” n.k., mhariri akaanza kutangaza maoni ya wasomaji.

Mwandishi mmoja Bwana M. J. amesema, “Imani ya kwamba Yesu Kristo hakufa msalabani kama ilivyoelezwa na Imam Shams ambaye ni Mwislamu, katika gazeti lako la wiki ya jana, ni imani ambayo hata baadhi ya Wakristo wanaiafiki”.

J. D. Turner ameandika: “Kwa hakika kama kusingalikuwa na kufa na kufufuka kama inavyosimuliwa katika Agano Jipy, ninaamini ya kwamba misingi yote ambamo Ukristo wa siku hizi umesimama ingefagiliwa mbali, na kwa hali hiyo basi Kanisa litategemea nini?” (Toleo la 13 March 1946). Na jawabu langu kuhusu swali lako “Kwa nini kaburi halifunuliwi” ni kwamba kwa kuwa wakazi wa Kashmir wanaamini kuwa kaburi hilo lilikuwa la nabii, hawataruhusu lifunuliwe mpaka kuwepo na haja na msukumo mkubwa kutoka katika “Ulimwengu wa Kikristo”. Walakini nimelijadili suala hili kinaganaga katika kitabu changu, “Yesu kafia Wapi? Na nimehakikisha kwa ushahidi wa kihistoria kwamba kaburi linalosemwa ndilo hasa kaburi la nabii Yesu.

Mhashamu J. Stafford Wright, M. A. Mkufunzi Mwandamizi katika Oak Hill college amedokeza kuhusu kitabu na vipeperushi vyangu vya tangazo katika makala yake chini ya kichwa cha maneno “Uvamizi wa Kiislamu nchini Uingereza” ambayo ilitolewa na gazeti la kila wiki la mjini London liitwalo “The Life of Faith” la tarehe 15 Mei 1946, akisema:-

“Wiki chache zilizopita mwanafunzi mmoja alikabidhiwa kipeperushi chenyе taarifa na jamaa mmoja wa kihindi. Kipeperushi hicho hakikuwa na taarifa ya Kikristo bali ya Kiislamu. Magazeti ya mjini London yamekwisha tangaza picha za kikundi cha Wabashiri wa Kiislamu ambaо wamekuja kuwasilimisha Waingereza. Utawanyaji wa vipeperushi hivi ni ushahidi wa shughuli yao hii. Tangu wakati huo vipeperushi vingi vya namna hii vimekwisha tawanya.”

Taarifa iliyo katika vipeperushi hivi ni kwamba Masihi Aliyeahidiwa amekwisha kuja katika dhati ya Hadhrat Ahmad (1835-1908). Katika karatasi hizi pia kuna picha ya linalosemwa kuwa ni “Kaburi la Yesu” katika mtaa wa Srinagar mjini Kashmir. Taarifa hii fupi ilizungumzia juu ya ushahidi kwamba Yesu hakufa msalabani bali alihamia katika nchi ya India na kufia huko.

Barua iliyoandikwa katika Msikiti wa London ilileta jibu ambalo liliambatanishwa pamoja na kitabu kiitwacho “Yesu kafia wapi? Kitabu hiki kina kurasa 128 na kimetungwa na kutawanywa na Imam wa Msikiti wa London Maulawi J. D. Shams. Tawi la Uislamu linaloshughulikia tablighi hii ni Jumuiya ya Ahamadiyya ambayo kuihusu hilo gazeti liitwalo The Life of Faith lilitangaza makala moja iliyoandikwa na Mhashamu A. R. Pittwy aliye kasisi nchini Kenya ambaye alikutana na waendeshaji wa tablighi hii katika nchi ile. Jumuiya hii muundo wake ni wa kiubashiri, na ingawaje baadhi ya Waislamu wanaihesabu jumuiya hii kuwa haitangazi Uislamu sahihi, kwa hakika jumuiya hii inakaribiana sana na suna ya Muhammad hivi kwamba inaweza kuhesabiwa kuwa ndiyo inayowakilisha imani ya Muhammad.

Kitabu hiki ni shambulio lililotungwa kwa uangalifu sana dhidi ya Ukristo na mwishoni mwake kinalifafanua zaidi lile wazo ya kwamba Yesu alikwenda India na akafia huko. Ni wazi ya kwamba yako mambo matatu ya Kikristo ambayo yanaweza kushambuliwa. Nayo

ni kifo cha Yesu, Kufufuka kwake na kupaa kwake. Yote hayo yanatakiwa yathibitishwe kuwa ni ya uwongo. Kwani, nadharia iliyopo ni kwamba Yesu alizimia tu juu ya msalaba, akarudiwa na fahamu alipokuwa ndani ya kaburi na baadaye akakutana na wanafunzi wake na kuagana nao kabla hajaelekea India ambako hatimaye akafariki. Ni fedheha isiyokwisha tukiwa kama Wakristo ya kwamba nchi yetu iwe inashuhudia uvamizi wa Kiislamu wa namna hii. Lakini sababu ya ajizi ya Waingereza kama ilivyo hivi sasa, inawezekana sana ya kwamba kiasi fulani cha tablighi hii kitaenea sana. Kwa hali hiyo ni jambo la maana pia kujiweka tayari kukabiliana na uvamizi huu.”

Gazeti la mjini London liitwalo “Psychic News” la tarehe 20 Aprili 1946 lilitangaza picha ya kaburi la Yesu katika mji wa Srinagar jimbo la Kashmir pamoja na maelezo kwamba “Hapa katika mtaa wa Khanyar, Srinagar Kashmir kuna kaburi hili ambalo linaaminawa na Waislamu kuwa ndilo kaburi la Yesu. Waislamu hao wanataka lifanyiwe uchunguzi.”

Gazeti hilo pia lilitangaza tamko kuhusu ushahidi wa jumuiya ya Ahmadiyya juu ya kifo cha Yesu. Mhariri alianza makala yake kwa maneno yafuatayo:-

“Tumeitangaza picha hii pamoja na maelezo yake kwa kuamini ya kwamba itawapendeza wapenzi wengi wa mambo ya kidini ambao huenda hawana habari juu ya madai kwamba Yesu hakufia katika eneo la Calvary kama inavyodaiwa na Makanisa tangu miaka elfu mbili iliyopita.”

Hili pia ni jambo la kihistoria nasi hatupendelei upande wo wote. Wasomaji wanaweza kujiamulia wenyewe juu ya suala hili baada ya kusoma tamshi lifuatalo:- Baada ya kutoa muhutasari mfupi wa haja zilizomo katika kitabu changu “Yesu kafia wapi?” gazeti hilo lilihitimisha makala yake kwa maneno: “Hii ni nafasi nzuri sana kwa wachimbuaji wa mabaki ya kale”

Katika gazeti liitwalo Psychic News la tarehe 11 May 1946 Mhariri wake ameandika: Picha tulioitangaza hivi majuzi ya kaburi linalosemekana kuwa la Yesu na ambalo liko katika Srinagar, Kashmir imesababisha tupokee barua nyingi kutoka kwa wasomaji wetu baadhi yao wakiunga mkono maoni ya Jumuia ya Waislamu Waahmadiyya na wengine wakipinga.”

Yafuatayo hapa chini ni maoni ya watu wawili kuhusu suala hili:-

Bwana George Rulf wa Heaton, New Castle on Tyne ameandika barua ndefu na kusema: “Nilipendezwa sana na makala yako kuhusu madai ya jumuiya moja ya Kiislamu ya kwamba Rabi Yesu hakufa msalabani bali alihamia Kashmir kupitia Uajemi na Afghanistan na hatimaye akafariki na kuzikwa mahali paitwapo Srinagar. Habari hii inalingana sana na masimulizi yaliyotolewa zamani sana na mtawa mmoja maarufu sana kuhusu kashfi aliyoiona. Bali mimi ninaonelea ya kwamba wakati umeshafika sasa kwa watu kujiepusha na kuvikubali kuwa ni sahihi hivi visa vya kidini ambavyo havina msingi wowote. Mtawa huyo amesema kwamba hakufikiria kuwa tungeweza kumkuliza swali kama lile, lakini kwa kuwa tulimuuliza, na kwa kuwa alituahidi kuwa kila mara atasema kweli basi ilimlazimu atuambie ingawaje alihofia ya kwamba habari hii ingewachukiza watu wengi wenye kufuata mambo ya kikasuku.

Alianza kwa kusema kwamba katika zama zile hili jina Yesu lilikuwa limeenea mahali pengi kama vile lilitivo jina Smith.

Maoni yangu kuhusu jambo hili ni kwamba Rabi Yesu hakujulikana kwa jina la Yesu katika zama zake bali alijulikana kwa jina lake halisi, yaani Yoshua. Ni baadaye tu wakati visa vya Injili vilipokuwa vinakusanywa ndipo wakusanyaji wa visa hivi wakaligeuza jina Yoshua na kuliita kwa lafidhi ya Kigiriki YAYZOUS ambalo kwa matamshi ya lugha yetu ni Yesu. Sababu ya kutumia jina YAYZOUS badala ya Yoshua ni kwamba kabla ya Yesu alikwisha pita mtume mwengine ambae jina lake ni Yoshua pia.

“Hivyo wakusanyaji wa habari za Injili wakaonelea ya kwamba kwa kuwa nabii anayeitwa Yoshua alikuwapo kabla ya Yesu, kama wangaliamua kumwita Yesu Yoshua wa pili, jambo hili lingewatatanisha watu. Kwa maoni yangu ninafikiria kwamba uamuzi wao huu ni wa busara.”

Mtawa huyu amesema kwamba kashfi aliyoiona ilihuiskana na kushtakiwa na kuhukumiwa kifo watu wanne. Watu hao ni askari jeshi, mnyang’anyi, mwalimu aliyekuwa anasafiri na mtu mwingine ambaye simkumbuki vema kwa kuwa daftari nililoandika habari hii liko mbali nami wakati huu.

Ilitokea ya kwamba watu wote hawa wanne jina lao lilikuwa Yoshua. Jambo hili liliwababaisha sana wakusanyaji historia wa siku za baadaye ambao walichanganya habari za ma-Yoshua wote wanne na kuonekana kana kwamba kilikuwa ni kisa cha Yoshua mmoja. Kwa hakika Yesu aliishi na kufikia umri wa uzee na alihamia nchi nyingine. Lakini mtawa huyo amesema kwamba ingawaje Yesu aliishi kiasi hiki, yeye (Yesu) hakupunguza chochote katika utukufu wa Bwana mmoja ambaye mtawa huyo alimpenda na kumtukuza sana.

Maoni yangu kuhusu jambo hili ni kwamba kisa hiki cha “Mkombozi wa Msalaba” ni uzushi wa hali ya juu ambao ilitungwa na kuandikwa na makasisi wa karne ya tano, sita na saba na watu wa zama zile walichukizwa sana walipotakiwa kuva misalaba shingoni mwao na walilibeza sana shauri hili.

Lakini viongozi wa dini waliwalazimisha watu hao kwa kuwatia hofu, huzuni na mashaka ili lengo lao hili litimie. Kwa hiyo kuanzia hapo umetwishwa hiki kitu cha kuhuzunisha sana kiitwacho “Ijumaa Njema” na kisa cha mtu mmoja aitwaye Mkombozi ambaye ingawaje kifo chake kinasemekana kuwa ndicho kilichomfanya yeye awe mbebaji wa madhambi ya waumini wote wa Kikristo, na waliosalia wote ambao si waumini waingie motoni.

Bibi N. E. Clark, wa Heatheroft, N. W. 11 amesema:

"Marejeo ya Kimaandishi kuhusu Kaburi la Yesu yanayopatikana katika "Murrary's Handbook of India" ambacho kilitangazwa nchini India, Burma na Sri Lanka yanaashiria kwenye maandishi I. S. A. (Jesue) yaliyochorwa katika ukuta wa msikiti mjini Fatehpur. Michoro yote hii inaweza kuonekana katika makala iitwayo "Miftaahut-Tawarikh, iliyomo ndani ya kitabu kiitwacho "Hafed Prence of Persia" kilichotungwa na Bwana John Ellis na kupigwa chapa mjini Agra ambamo imesemwa pia ya kwamba Yesu alihamia nchini India."

### **"FREE THINKERS" (WAFIKIRIAJI HURU)**

Hapa chini ninanukulu baadhi ya vifungu vyta maneno vinavyopatikana katika makala zilizochapishwa katika gazeti maarufu la mjini London liitwalo "Free Thinkers" la Jumapili tarehe 2 June 1946 chini ya kichwa cha maneno "Christian Evidence on Ice" yaani Ushahidi wa Kikristo (umesimama) juu ya barafu. Habari kuu katika makala hii ilihusikana na Hotuba ya Askofu wa London aliyekuwa rais wa mukutano wa mwaka wa Christian Evidence Society (Jumuiya ya Mashahidi wa Kikristo) uliofanyika katika Ukumbi wa Caxton.

Wasikilizaji wa hotuba hiyo walikuwa kiasi cha watu hamsini ambao wengi wao walikuwa wazee na idadi ya wanawake ilikuwa katika uwiano wa mmoja kwa kila wanaume watano. Huu ni ushahidi waziwazi ya kwamba imani ya Kikristo inapoteza mshiko wake kwa haraka sana na wanaume ndiyo wa kwanza kuiachilia kamba hii ya Ukristo.

"Tulikuwa na tabia ya kudhani kwamba sisi ndiyo tumo katika uwanja wa kazi ya kueneza dini. Hivi sasa ndiyo tunatambua kwamba kumbe hatuko peke yetu katika kazi hii ya kuzagaza imani ya kidini. Hivi sasa siyo tu tunapata mashambulio ya kupinga imani ya dini yetu bali kwa hakika tunakabiliwa na dini pinzani."

Jambo hili lilizusha fikra nyingi miongoni mwa watu mbalimbali. Baadhi yao walijuliza, “Je majeshi ya Kiislamu yanajitayarisha kuvamia sehemu zetu takatifu?” Wengine wakajiuliza “Jee kuna mpango wa kuishamiri dini ya Kibaniiani?” Jawabu la maswali yote haya ni hapana. Wasiwasi wote huu umechochewa na huyu Askofu ambaye alilaona watu wa Mashariki wakitawanya vijigazeti katika kituo kimoja. Vijigazeti hivyo vilikuwa na picha ya hekalu moja la kihindi ambalo lilisemekana kuwa chini yake ndipo ulipo mwili wa Yesu Kristo. Askofu huyu akaongeza kusema, “Kukata hukumu ya kwamba kama kaburi hilo likifumuliwa mabaki ya mwili wa Yesu yataonekana ni madai ambayo si ya kisayansi moja kwa moja”. Akasema kwamba hii ni dini nyingine ambayo immeanzisha utaratibu kabambe wa mahubiri.

Tangu nihudhurie mkutano huo ndipo niliweza kukipata kijitabu hicho kinachosemwa. Kinaitwa, “Yesu kafia Wapi?” Mtunzi wa kitabu hiki ni J. D. Shams na kinatoka katika Msikiti wa Wimbledon. Ni chenye faida nyingi kwa wale ambao hawakatai kudadisiwa kwa Yesu. Maoni yaliyomo ndani ya kitabu hiki ni kwamba Yesu hakufa Msalabani bali aliihama nchi ya Palestina baada ya jaribio la kutaka kumwua msalabani. Haya ndiyo maoni yaliyoshikwa na Bwana Thomas Henry Huxley na yakafafanuliwa zaidi kwa njia ya kubuni na Bwana George Moore katika kitabu kiitwacho “The Brook Kerith” .

## **TANGAZO LA MWISHO**

Mnamo mwezi May 1946 nilitangaza taarifa ifuatayo kwa njia ya vipeperushi maelfu kwa maelfu. Viongozi wa dini walipelekewa vipeperushi hivi kwa njia ya posta na maelfu ya watu mjini London waligawiwa vipeperushi hivi vya Taarifa hiyo iliyokuwa na kichwa cha maneno:-

**UPINZANI KWA KANISA  
YESU ALIKUFA KIFO CHA KAWAIDA KABURI LAKE  
LIMEGUNDULIWA INDIA**

Vipeperushi laki moja vilitawanywa jijini London. Jambo la muhimu lililoelezwa ndani ya vipeperushi hivyo ni kwamba “Yesu hakufa Msalabani bali aliepukana na kifo na akaelekea India ambako hatimaye akafa kifo cha kawaida. Kaburi lake nchini India limegunduliwa na Mtume Ahmad wa Qadian Punjab, India ambaye bishara ya kufika mara ya pili kwa Yesu imetimilizwa katika nafsi yake.

Baadhi ya magazeti yamechapisha sehemu kubwa ya taarifa hiyo pamoa na maoni mbalimbali ya wasomaji ambapo gazeti lingine limechapisha picha ya kaburi hilo pia. Zaidi ya hayo mimi nimepokea barua chungu nzima ambazo walioziandika walikuwa na shauku kubwa na kuhusu jambo hili. Watu hawa wote walipelekewa kitabu changu kiitwacho “Yesu kafia Wapi? Ndani ya kitabu hiki nimelijadili suala hili kinagaubaga na nimethibitisha kwa njia ambayo itamfanya msomaji asiye na upendeleo akubali ya kwamba Yesu hakufa Msalabani bali alikufa kifo cha kawaida kama mitume wengine wa Mwenyezi Mungu.

Wasomaji wengi wamefikiria kwamba inawezekana sana ya kuwa habari hii ni ya kweli na wakaomba maelezo zaidi. Mmoja wao ameandika:-

“Taarifa hii inaonekana kuwa inakubalika akilini” Mwingine ameandika: “Nikiwa Mkristo asilia na mtafutaji ukweli, maoni yako yamenivutia sana kwa vile yanakubaliana na maoni ya kila mtu binafsi yake, n.k.

Wengi mionganoni mwa wale ambao wamekisoma kitabu changu wamegundua ya kwamba ni cha kupendezza na kushawishi sana. Kwa mfano mtu mmoja ambaye aliniandikia ili nimpelekee vitabu

vya namna nyingine ameandika: "Ni chenye kushawishi sana nami naamini kwamba ni cha kweli. Lakini baadhi ya watu wengine na hususa Wakatoliki wa Roma, badala ya wao kuomba maelezo zaidi wameandika:-

1. Uvumbuzi huo ni fedheha na ni uzushi.
2. Ni mashambulio ya kikatili juu ya Biblia ambayo ni maneno ya Mwenyezi Mungu.
3. Yesu yu Hai.
4. Yu aishi ili akomboe.

Mkatoliki mmoja Mroma ameandika:-

Mmedanganywa sana na mtu mmoja ambaye ama ni majununi anayejidanganya mwenyewe au ni mzushi mfano wa wale ambao nawahakikishieni kuwa wamewahi kutokea humu humu nchini mwetu."

Baadhi ya makasisi walikuwa wenyewe matusi na kurukwa na akili sana hivi kwamba walijaribu kuwapokonya wale waliokuwa wanatawanya vitabu hivyo ili wavichane na baadhi yao walivipokea na kisha wakavichana. Wote hao ninapenda kuwaambia ya kwamba mwenendo wao si mzuri na hauwezi kuwafalia lolote. Wakumbuke ya kwamba hata Yesu Kristo mwenyewe alitukanwa vibaya sana na wapinzani wake, Waandishi na Mafarisayo. Tusiwe na uadui baina yetu katika haya mambo ya dini. Sisi Waislamu tunaamini ya kwamba Yesu alikuwa mtume wa Mungu na kwamba kama walivyokuwa mitume wengine, yeye pia aliteswa na wapinzani wake ambao walishindwa kutimiza lengo lao la kumfisha kifo cha laana. Kufufuka, kupaa na madai ya kwamba yeye anaishi mbinguni ili kuwakomboa binadamu wote ni mawazo ya upotofu.

Muhammad (Amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake) alikuwa Mtume mkweli wa Mwenyezi Mungu ambaye alipewa sheria kamilifu. Mafundisho yote mazuri yanayopatikana katika vitabu vya mitume wengine yote kwa pamoja yamekusanywa ndani ya mafundisho ya Kiislamu.

Kama kuna Askofu ye yote au kasisi ye yote au viongozi wengine wa dini ambao wana maoni tofauti basi na wajitokeze hadharani na kujibu hoja zilizomo katika kitabu changu “Yesu kafia Wapi? Mimi nipo tayari wakati wo wote kuthibitisha madai yangu iwapo mtu ye yote mpenda haki atataka nifanye hivyo. Huu ni mtihani ninaoutoa kwa kanisa. Mwishowe ninapenda kudhihirisha utashi nilio nao juu ya Waingereza wa kawaida ambao hawana upendeleo bali kuyapima mambo kwa akili na kwa hekima na wala hawafuati jambo kikasuku. Bila shaka hatimaye watu hao watapata amani na utulivu wa moyo. Mwishowe kabisa ninapenda kurejea maneno ya mwisho kuhusu uchambuzi wa kitabu hiki yaliyoandikwa na Profesa Qazi Aslam M. A. Mkuu wa idara ya Saikolojia katika Chuo Kikuu cha Karachi:

“Maulana Shams ameandika kitabu cha maana na chenye kupendeza sana ambacho kitathibitika kuwa msingi wa juhud zinazofanywa kwa niaba ya Uislamu ambazo Waahmadiyya wanazishinikiza kwa ufaulu mkubwa sana katika nchi za Magharibi. (Sunrise August 3, 1946).

Kwa msaada wa Mwenyezi Mungu, matumaini yaliyodhiihirishwa na uchambuzi yanaanza kuonekana kwa vile wabashiri wetu wanalieneza wazo hili kila mahali katika nchi za magharibi. Toleo la kitabu hiki kwa lugha ya Kidachi lilitangazwa na Bwana N. Kluwer Deventer katika nchi ya Netherland mnamo mwaka 1959 na toleo kwa lugha ya Malayalam (Kihindi) lilitangazwa mnamo mwaka 1958. Tafsiri kwa Kijerumani imo mtamboni na baada ya muda mfupi itatolewa. Na tumuombe Mwenyezi Mungu ili awakomboe ndugu zetu Wakristo kutokana na kumwabudu mtu ambaye ameletwa ili kutangaza ibada juu Mungu mmoja.

**J. D. SHAMS**  
**1959**



بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

*Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu*

## YESU KAFIA WAPI?

### SURA YA KWANZA

### KARAA KUTOKA KATIKA INJILI

#### 1. MAOMBI YA YESU

Wakati Yesu alipotangaza madai yake ya kuwa Masihi alichukua hadhari kubwa sana juu ya usalama wake. Wakati fulani aliwatahadharisha wanafunzi wake ya kwamba wasimwambie mtu ye yote kuwa yeye alikuwa yule yule Yesu Kristo (Mat. 16:20). Mara nyingine, wakati wapinzani wake walipofanya njama ya kumwua, aliacha kutembea hadharani mionganini mwa Mayahudi na badala yake akaenda kuishi mahali pa upweke (Yohana 11 :53). Si hivyo tu bali pia alijificha asiweze kuonekana nao (Yohana 12:36). Alipotambua azma ya Wapinzani wake ya kutaka kukomesha kazi yake kwa mabavu na ikiwezekana kumwua yeye, Yesu alienda kujificha mahali ambapo walipajua wanafunzi wake tu. (Yohana 18: 1,2). Kisha alijua kwa njia ya ufunuo au kutokana na utii wa kinafiki aliokuwa nao Yuda na kwa vile wakati huu Yuda hakuwapo, kwamba yeye Yesu atasalitiwa na Yuda na kwamba ni lazima atatiwa mbaroni. Kwa wakati huo hakuona njia yo yote ya kuepuka kukamatwa isipokuwa kumwomba sana Mwenyezi Mungu Mwenye Nguvu kwa kujitupa mbele yake ili atibue mipango ya adui zake na kumwepusha na adhabu ya kifo.

Kutokana na maelezo yanayopatikana katika Mathayo 26, Marko 14 na Luka 22 inaelekea kwamba Yesu alienda Gethsemane pamoja na baadhi ya wanafunzi wake akawataka wasali na kuomba msaada wa

Mwenyezi Mungu lakini wao wakapiga usingizi. Aliwaamsha mara mbili ili wakae macho na kuomba lakini hatimaye akashindwa na kuwaacha waendelee kulala.

Yeye mwenyewe akaomba kwa unyenyekevu sana akisema: "Abba, Baba, yote yanawezekana kwako, niondolee kikombe hiki. Lakini si kama nitakavyo mimi bali kama utakavyo Wewe. (Marko 14:36).

Sehemu kubwa ya usiku huu aliitumia kwa kufanya maombi ya namna hii. Baada ya kutokea malaika kutoka mbinguni, ambaye alikuwa alama ya kukubaliwa kwa maombi yake, yeye akazidi kuomba kwa unyenyekevu mwangi sana. Aliomba weee mpaka jasho lake likadondoka ardhini kama matone ya damu (Luka 22:24).

Tafsiri ya maombi haya ya Yesu ni kwamba anaomba aepushwe na kifo siyo kwa sababu anaogopa kuyatoa maisha yake katika njia ya Mwenyezi Mungu, bali anaomba hivyo ili matakwa ya Mwenyezi Mungu juu ya Mtume wake yatimizwe dhidi ya matakwa ya maadui zake. Hii ndiyo maana ninayoilewa mimi kuhusu msemo wa Yesu kwamba: "Siyo nitakavyo mimi bali utakavyo wewe". Kama Yesu angalijua kwamba Mwenyezi Mungu anataka afe msalabani basi asingeomba na kusema, "Yote yanawezekana kwako, niondolee kikombe hiki", yaani kikombe cha umauti ambacho maadui zake wamekishikilia mdomoni pake ili anywe umauti huo.

## **KIKOMBE KILIONDOLEWA**

Tunaamini kwamba maombi ya Yesu yaliyotajwa hapo juu yamepokelewa. Tunaamini hivyo kwa sababu zifuatazo:-

1. Yesu mwenyewe anadai kwamba Mwenyezi Mungu ameyasikia maombi yake: "Baba ninakushukuru wewe kwa sababu umeyasikia maombi yangu, nami ninajua kwamba wewe unanisikia mimi kila mara" (Yohana 11 :42). Pia anawahimiza watu wengine wafanye maombi na anawaambia kwamba Mwenyezi Mungu atayapokea maombi yao. (Marko

11 :24). Akazidi kusema, “Ni nani mionganoni mwenu ambaye kama mtoto wake atamwomba mkate, ye ye atampa jiwe, au kama amemwomba samaki atampa nyoka? (Mathayo 7:9, 10) Sasa basi, ikiwa hata maombi yake Yesu mwenyewe aliyoomba kwa khushui ya kweli na ambayo yalikuwa ya maana sana kwa vile yalihusikana na kifo chake msalabani yalipuuzwa, maagizo yake kwa wanafunzi wake kwamba wanatakiwa kufanya maombi juu ya yote wayatakayo na tamshi lake kuwa maombi yao yatapokelewa havitakuwa na maana yoyote. Kwa hiyo, hatuna uchaguzi mwingine isipokuwa kukubali ya kwamba Mwenyezi Mungu aliyakubali maombi yake na hivyo akamwepusha na kifo cha laana.

2. “Kuhusu kupokelewa kwa maombi yake tunaweza kurejea karina zifuatazo kutoka katika Zaburi” Kwa sababu mbwa wamenizunguka; makundi ya waovu yamenizunguka; walinitoboa mikono yangu na miguu yangu LAKINI EE MOLA WANGU USIWE MBALI NAMI: EWE NGUVU YANGU, FANYA HARAKA UJE KUNISAIDIA. Kwani ye ye hajadharau wala kupuuza mateso ya anayeteswa, wala ye ye hafichiki machoni mwa anayeteswa; bali wakati alipomlilia YEYE ALIMSIKIA” (Zaburi 22:16, 24). Vilevile katika Zaburi 34 tunasoma: “Ni mateso mengi ayapatayo mcha Mungu Humwokoa katika yote hayo. Huilinda mifupa yake yote. Hakuna hata mmoja unaovunjika”. Katika Yohana 19:23, 36 na vifungu vya Zaburi vilivyotajwa juu vinamhusu Yesu Kristo. Kulingana na kifungu cha pili itakumbukwa kwamba mifupa ya wezi wawili waliotundikwa pamoja na Yesu ilivunjwa ambapo ya Yesu iliachwa bila ya kuvunjwa. Hivyo Mwenyezi Mungu aliposikia maombi yake akamwokoa na kifo cha “laana”.
3. Yesu mwenyewe aliamini ya kwamba Mwenyezi Mungu amesikia maombi yake na kwamba hatakuwa msalabani. Ndiyo sababu alipojisikia hali mbaya sana kwa maumivu ya kupigiliwa

msalabani na alipoonekana kana kwamba hawezi kuokolewa, ndipo mwanzoni aliingiwa na wasiwasi na kuanza kulia kilio cha kukata tamaa, “Mola wangu Mola wangu, mbona Umeniacha? (Mathayo 27:46), Mwenyezi Mungu Hakumwacha. Alikuwa ametayarisha njia ya kumwokoa. Walakini kama tutaa mini ya kwamba alikuwa msalabani, basi itatubidi tukubali pia kwamba Mwenyezi Mungu alimwacha. Lakini hii itakuwa kinyume na maneno yake, “Tazama, ile saa iliyosemwa kuwa itakuja sasa imewadia, ninyi wote mtatawanyika kila mmoja na kwao na kuniacha mimi peke yangu, lakini kwa hakika mimi siko peke yangu kwa sababu baba yu pamoja nami”. (Yohana 16:32).

4. Maandishi yote matakati fu yanakubaliana kwamba Mwenyezi Mungu Hupokea maombi ya wacha Mungu na kwamba hapokei maombi ya waovu na maadui zake. Kwa mfano tazama katika Zaburi 18:6 na 66: 18-20. Vile vile Yeremia 29-13 na Ayubu 22-27. Mahali pengine tunasoma pia ya kwamba, Tunajua kwamba Mwenyezi Mungu Hawasikilizi wenye dhambi, lakini kama mtu ni mcha Mungu na mtekelezaji wa aliyoyaagiza Yeye, Mwenyezi Mungu Humsikia” (Yohana 9:31). Kwa hiyo kama tutakanusha kuwa Mwenyezi Mungu Hakuyasikia maombi ya Yesu hatuna njia nyininge isipokuwa kuamini vile vile ya kwamba Yesu alikuwa mwenye dhambi na wala si mcha Mungu ambaye alitenda sawa na matakwa ya Mwenyezi Mungu. Na kuamini hivi juu ya mtu kama Yesu ambaye alikuwa mtume wa Mungu ni ukafiri wazi wazi. Tunasoma katika kitabu cha Waebrania kuhusu maombi haya ya Yesu: “Ambaye katika siku za uhai wake alipofanya maombi na kujitupa mbele ya Mwenyezi Mungu kwa kilio kikuu chenye machozi mengi, ndipo Mungu alimwokoa na kifo na maombi yake kuhusu kile alichohofu yalipokelewa” (Waebrania 5:7). Hivyo basi Mayahudi walishindwa katika hila zao na Mwenyezi Mungu alimwokoa mcha Mungu huyu Yesu kutokana na kifo cha laana.

## **JE YESU ALIKUWA MLAANIWA?**

Yesu aliwaambia wapinzani wake: “Ole wenu Waandishi na mafarisayo, wanafiki, mmewazuilia watu ufalme wa mbingu, kwani hamuingii humo ninyi wenyewe wala hamtoi nafasi kwa wale wanaotaka kuingia” (Matthayo 23: 13).

Tena anasema: “Yule asiyeamini atalaaniwa” (Marko 16:16) Sasa basi, Mafarisayo waliamini kwamba walimfisha Yesu kifo cha laana na kama habari hii ni kweli kama anavyothibitisha Mtakatifu Paulo, hapo tena, kulingana na sheria yao wenyewe watakuwa wamehakikisha waziwazi kwamba Yesu alikuwa mtume mwongo na kwamba kwa sababu hiyo wao walikuwa na haki ya kumkataa na hivyo hawatalaaniwa kwa hatua yao hiyo.

Ukichukulia maana halisi ya neno “mal’uni”, mlaaniwa hawezi kuwa mtume na mpendwa wa Mwenyezi Mungu, kwa sababu mtu hawezi kuwa mal’uni mpaka uhusiano wake na Mwenyezi Mungu ukatike na mpaka moyo wake uondokwe na mapenzi na elimu kumhusu Mwenyezi Mungu. Si hayo tu bali vile vile mtu huyo awe amenyimwa rehemaa na baraka za Mwenyezi Mungu. Mtu huyo ni lazima awe mkosefu kama vile shetani na awe adui wa Mwenyezi Mungu. Na hii ndiyo sababu shetani huitwa “Mal’uni”.

Kuhusu mtu mcha Mungu na mtakatifu kama alivyokuwa Yesu, ambaye alidai kuwa yeye ndiye nuru ya ulimwengu, mpendwa wa Mungu na kwamba Mungu Amepokea maombi yake je, tunaweza kuamini ya kwamba alilaaniwa na Mwenyezi Mungu na kwamba hakuwa na uhusiano Naye na kwamba moyo wake ulikuwa umejawa na makosa na ukafiri? Kwa kutilia maanani ukweli huu tunalazimika kukataa uwezekano wa Yesu kufa juu ya msalaba ambako kungemfanya awe mlaaniwa.

## KUFUFUKA KWA WATAKATIFU

Hoja ya tatu yenyewe kuhakikisha kwamba Yesu hakufa juu ya msalaba inapatikana katika sura ya 27 ya Injili ya Mathayo: "Makaburi yakafunguliwa na miili mingi ya watakatifu iliyolala humo ikaamka, na wote wakatoka nje ya makaburi yao baada ya kufufuka kwake yaani (Yesu) na wote walielekea kwenye mji mtakatifu ambako walijitokeza mbele ya watu wengi (Mathayo 27:52, 53). Ni dhahiri ya kwamba tukio hili haliwezi kukubalika katika maana yake ya neno kwa neno kwa sababu kama lingekuwa na maana hiyo ya neno kwa neno tusingeshindwa kupata marejeo fulani fulani kuhusu tukio hili la ajabu ambalo limekiuka uwezo wa binadamu. Lakini hatukuti marejeo yoyote ya muhimu kuhusu jambo hili na ni Injili ya Mathayo iliyolitaja jambo hili ambapo wenzake wengine watatu hawakujali kulitaja. Lingekuwa jambo la kweli basi Mayahudi wangalipata nafasi nzuri sana ya kuwaliza hawa watu waliofufuka kuhusu ukweli wa Kristo. Na kama wangepata ushuhuda wa watu hawa bila shaka Mayahudi wangalimkubali Yesu bila ya hoja zaidi. Ngoja nimrejee Thomas Paine kuhusu kisa hiki:

"Ni jambo rahisi sana kusema uwongo, lakini ni vigumu pia kuuthibitisha uwongo baada ya kuutamka. Mwandishi huyu wa Injili ya Mathayo alitakiwa atuambie walikuwa akina nani hawa watakatifu waliofufuka na kurudi mjini tena, vile vile atuambie baadaye wakawaje na ni nani aliyeaona – maana huyu bwana hakuweza kujasiri kusema kuwa aliwaona ye ye mwenyewe. Si hivyo tu bali pia atuambie kama hao watakatifu wake kwa waume walikuja uchi na miili yao ya kawaida; au aseme kuwa walikuwa wamevaa na atuambie hizo nguo walizipata wapi; halafu atuambie iwapo kila mke alifikia kudai mumewe na kila mume kudai mkewe pamoja na mali zao na walipokewa vipi na wenyeji wao; kisha atuambie sijui walifanyaje kuzipata tena mali zao zilizokuwa zinamilikiwa na watu wengine kimabavu au kisheria? Au atuambie iwapo hawa watu walikuwa tena au pengine walirudi kwenye makaburi yao wakiwa wazima na kisha wakajifukia wenyewe. Ni la ajabu sana ya kwamba kundi la watakatifu lifufuke halafu pasiwe na watu wa

kuwatambua wala kusiwe na aliyewaona na kisha hili suala lisigusiwe tena na wala hawa watakatifu wasiwe na la kutuambia! Wangalikuwa mitume wa zamani ambao (kama tunavyoambiwa) walitabiri kuhusu mambo haya, bila shaka wangalikuwa na mengi sana ya kutuambia. Wangetuambia kila kitu na tungalipata nafasi ya kusikia bishara za watu waliotoka kuzimu ambao wangeliandika taarifa kadhaa zenyenye kufafanua na kusahihisha bishara zao za zamani tulizo nazo hivi sasa. Wangelikuwa Musa, na Harun, na Yoshua na Samuel na Daudi, kusingepatikana Myahudi hata mmoja katika mji wa Yerusalem ambaye asingebaki bila ya kubadili dini yake. Angalikuwa Yohana Mbatizaji na watakatifu wengine walioishi katika zama zake, kila mtu angaliwatambua nao wangalihubiri huko na huko na kujipatia sifa kuliko wanafunzi wengine wa Yesu. Lakini badala ya hayo, watakatifu hawa wamewevezeshwa kuchungulia kidogo tu kama kibuyu cha Yona (Yunus) katika usiku, wasiwe na lolote walifanyalo ila kutoweka tena asubuhi yake” (The Age of Reason by Thomas Paine). Hapana shaka ya kwamba kama tutafuata maelezo ya Mathayo neno kwa neno hatutakuwa na njia ila kupambana na maswali yote haya, lakini ukweli ni kwamba aya hii kama asemavyo Ahmad, Masihi Aliyahidiwa, inaashiria kwenye kashfi iliyoonwa na wacha Mungu fulani na ni jambo linalojulikana ya kwamba kashfi za namna hiyo zinaweza kutafsiriwa kama vile Yosefu (Yusufu) alivyotafasiri ndoto ya Farao (Furauni). Ni jambo la kupendeza sana ya kwamba kwenye ukurasa wa 289 wa kitabu kimoja cha Kiarabu kiitwacho TA'TIR-UL-ANAM, kihuksikanacho na tafsiri ya ndoto ambacho kiliandikwa miaka 600 iliyopita na mtaalam maarufu wa tafsiri za ndoto, Sheikh Abdul-Ghani Nablusi, tunasoma: “Kama mtu maarufu, ambaye amefungwa gerezani, atatolewa ndani ya gereza hilo na ataachiliwa huru”. Sasa basi kwa vile kashfi hii ilionwa wakati wa kufufuka kwake, maana yake hapa ni wazi ya kwamba alioneckana kana kwamba ni mfu na kwamba baada ya-kuzimia kwake ambako kuliwafanya watesi wake wadhanie kuwa amekufa, hatimaye ye ye alitolewa ndani ya lile pango alikokuwa amefungiwa. Kwa kifupi ni kwamba kashfi hii ambayo ilionwa na watu fulani wacha Mungu iliwabainishia ya kwamba Yesu hakufa bali

alikuwa kana kwamba ni mfungwa ndani ya kaburi ambamo baadaye akatoka na kuelekea mahali kwenye amani.

## ISHARA YA NABII YONA

Yesu alipotakiwa na Mayahudi awaonyeshe ishara alisema: “Kizazi kiovu na cha zinaa kinataka kionyeshwe ishara nacho hakitaonyeshwa isipokuwa ishara ya nabii Yona, kwani kama vile Yona alivyokaa michana mitatu na mausiku matatu katika tumbo la nyangumi, ndivyo hivyo Mwana wa Adamu atakavyokaa michana mitatu na mausiku matatu katika moyo wa nchi” (Mathayo 12: 39, 40).

Usemi huu wa Yesu umekata shauri moja kwa moja: Mayahudi walitaka kumwua lakini akaepukana na kifo hicho. Walifanya kila wawezalo ili kumwua lakini Mwenyezi Mungu akamtoa mikononi mwao. Hivyo kupona kwake kulitosha kuwa ishara kwa Mayahudi. Maneno ya Yesu yanaonyesha jinsi ishara itakavyoonyeshwa na njia itakayotumiwa katika kumtoa mikononi mwa maadui zake wauwaji. Yeye atatiwa katika matumbo ya ardhi kana kwamba ni mfu, lakini utaratibu wake utakuwa sawasawa na ule wa Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi. Alipokuwa tumboni mwa nyangumi Yona hakuwa mfu bali alikuwa hai. Kadhalika Yesu alitakiwa abakie hai ndani ya moyo wa ardhi. Kwa kuilinganisha habari yake na ile ya Yona, Yesu alibainisha waziwazi jinsi atakavyookoka.

Alikuwa aingie katika pango akiwa hai na atoke humo akiwa hai kama vile Yona alivyoingia katika ‘pango’ lake akiwa hai na kutoka humo akiwa hai. Bishara hii ya Yesu inafutilia mbali lile wazo ya kwamba yeye alikufa kifo cha “laana” juu ya msalaba.

## **NDOTO YA MKEWE PILATO**

Wakati Pilato alipokuwa ameketi juu ya kiti cha hukumu, mkewe akamsihi akisema, usimfanye lolote mtu yule ambaye ni mwenye haki kwa sababu leo hii nimeteswa sana katika ndoto kwa sababu ya mtu huyu (Mathayo 27: 19).

Onyo hili ambalo Mwenyezi Mungu alilitoa kwa Pilato kupitia kwa mkewe wakati ule ule wa kufunguliwa kwa mashtaka ni dalili ya matakwa ya Mwenyezi Mungu yaliyofunuliwa kwa Pilato ambaye yeye mwenyewe aliamini kuwa Yesu hana hatia na kwamba ni husuda tu iliyowafanya Wayahudi wamtie matatani (Mathayo 27: 18). Kama hakukuwa na mpango wa kumwokoa Yesu, ni nini basi maana ya hii ndoto aliyoonyeshwa mkewe. Wakati Herodi alipotaka kumwua Yesu zama za utoto wake, Joseph alipewa habari za hila hii mbaya kwa njia ya ndoto ili ayaokoe maisha ya Yesu. Joseph alizingatia onyo aliloona katika ndoto hii na akawahamishia Yesu na mama yake katika nchi ya Misri (Mathayo 2: 13). Kadhalika Mwenyezi Mungu alibainisha dhamiri yake kwa mkewe Pilato. Pilato alimtoa Yesu kwa maadui zake walipomtisha kwamba watamshitaki kwa Kaisari ikiwa atamwachia huru Yesu (Yohana 19: 12). Hata hivyo yeye alifanya mipango ya siri ili kwa vyo vyote vile Yesu aepukane na kifo. Aliuchelewesha muda wa kuanza mashtaka mpaka ilipofikia jioni sana siku ya Ijumaa, akijua ya kwamba ilikuwa mwiko kwa Mayahudi kumwacha mtu ye yote juu ya msalaba baada ya kuingia giza la siku ya Sabato. Muda uliobakia kwa kusulibiwa Yesu ulikuwa mfupi sana hivi kwamba Yesu asingeweza kufa msalabani. Ilikuwa muda wa masaa matatu tu ambayo kwa vyo vyote vile hayatoshi kumfanya mtu afe. Yule mtu aliyyeteuliwa kuendesha shughuli ya kuwasulubisha watu alimhurumia sana Yesu na kulingana na maneno ya Luka, mtu huyo aliamini kuwa Yesu ni mcha Mungu. Hali kadhalika yule Askari aliyevunja miguu ya wezi wawili waliotundikwa pamoja na Yesu hakuivunja miguu ya Yesu. Zaidi ya hayo kuna mtu mmoja asiye na uhusiano wowote na Yesu ambaye kwa haraka sana akafika huko alikotundikwa Yesu. Mtu huyo

alikuwa tajiri mkubwa aliyeitwa Yusufu wa Arimathaya ambaye aliquwa mwanafunzi wa kisirisiri wa Yesu aliyeamua kumfuata Yesu kwa siri kwa kuwaogopa Mayahudi kama tunavyoambiwa na Injili ya Yohana. Huyu Yusufu wa Arimathaya akamwomba Pilato ili auchukue mwili wa Yesu kinyume na kawaida iliyokuwapo, Pilato alimruhusu kuuchukua mwili huo bila ya kumdadisi mtu huyu ambaye aliquwa hamjui. Kisha yeche huyo pamoja na Daktari mmoja aitwae Nikodemus waliuchukuwa mwili wa Yesu na kuuhifadhi sawa na mipango yao. Hawakumzika katika kaburi la kawaida bali walimhifadhi katika pango ambalo Joseph alilichonga kwenye mwamba katika bustani yake. Ndani ya pango hilo waliweza kumtibia bila ya kuonekana na Mayahudi ambao kwa wakati huu walikuwa wakijishughulisha na sherehe zao za kidini za siku ya Sabato ambayo ni siku takatifu. Baada ya kutibiwa kikamilifu na kupona majeraha yake Yesu alitoka ndani ya lile pango. Hivyo tunaona waziwazi jinsi Pilato alivyofanikwa katika mipango yake ya kumwepushia kifo Yesu na kutimiza matakwa ya Mwenyezi Mungu ambayo yalidhihirishwa kwa mkewe kwa njia ya ndoto tulioitaja hapo awali.

## SURA YA PILI

## **HUKUMU**

### **USHAHIDI WA MATUKIO**

Ushahidi wa mambo yaliyotokea nimeuita hukumu ili huenda wasomaji wangu wakaelewa vizuri zaidi. Wakati fulani kulitokea ubishi mkubwa sana baina ya kundi la Waislamu na Wakristo kuhusiana na suala la Yesu kufa kifo cha "laana" na kufufuka kwake. Waislamu walikihesabu kifo cha "laana" kuwa ni tusi kubwa sana alilotukanwa Yesu ambaye ni mmoja wa Mitume wa Mwenyezi Mungu, ambapo Wakristo walikihesabu kuwa ni neema ya kimbingu kwa ajili ya binadamu. Ikatoka ya kwamba Wakristo waliwashitaki Waislamu kuhusiana na suala hili na shauri lao hili likasikilizwa na majaji wawili waelekevu na wenye kujitegeremea. Baada ya kulisikiliza shauri hili walitoa hukumu ifuatayo:-

**MKRISTO (K) - dhidi ya - MWISLAMU (M)**

**YAHUSU: KIFO CHA YESU MSALABANI NA KUFUFUKA  
KWAKE.**

Hili ni shitaka linalohusu tukio muhimu sana la kihistoria. Mushtaki K alilileta shitaka hili mnamo tarehe 8 April dhidi ya Mwislamu M ambaye hakubali kwamba Yesu kafa kifo cha laana. Katika pande zote mbili kuhojiana masuala yafuatayo yakazingatiwa kuwa ndiyo kiini cha mashitaka.

- 1 . Je Yesu alikufa msalabani?
2. Je alifufuka?
3. Je alifufuka na mwili wa kimalaika au mwili wenye nyama na mifupa?

Shauri hili lilisikilizwa kwa muda wa siku mbili ambapo pande zinazohusika zilitoa hoja za kuthibitisha madai yao. Baada ya kusikiliza pande zote na kuyachuja yale yanayoelemea upande huu au

ule tumeamua kutoa uamuza wetu ufuatao bila ya kupendelea upande wowote. Ushahidi wa K ambaye ndiye aliyetakiwa kuyathibitisha masuala alioleta mbele yetu umegawanyika katika taarifa nne zilizoandikwa ambazo K anadai kuwa ziliandikwa na mashahidi walioyaona matukio haya kwa macho yao wenyewe, yaani mtakatifu Mathayo, Marko, Luka na Yohana ambao waliziandika taarifa hizi kwa msaada wa ufunuo wa Mwenyezi Mungu. Lakini katika kuzichambua taarifa hizi, hazikuthibitika kuwa zinakubalika kisheria. Kwanza hazina saini za hao mashahidi wanaosemekana kuwa waliyashuhudia mambo haya wala hazina dalili yo yote inayoonyesha kwamba ziliandikwa kwa msaada wa ufunuo wa kimbingu. Walakini kwa kuwa taarifa hizi zinasemekana kuwa ndizo za zamani kupita zote kuhusu jambo hili tumeshindwa kuzipuuza moja kwa moja. Sasa na tuangalie jinsi zinavyoweza katika kutoa hukumu ya masuala yaliyotajwa hapo juu.

## **MASUALA**

Masuala haya matatu yanahusiana sana hivi kwamba haiwezekani kulijadili moja bila ya kugusia lingine. Kwa hivyo inatulazimu tuyachambue kwa pamoja. Ushahidi uliotolewa na kuhusu masuala haya unahitilafiana sana.

Mashahidi hawa wanne wanahitilafiana siyo tu katika mambo madogo madogo, la, bali wao wanahitilafiana hata katika mambo ya muhimu sana.

### **1. MSALITI PAMOJA NA WASAIDIZI WAKE**

Mathayo na Marko wanasema kwamba Yuda (ambaye alimsaliti Yesu) akiwa pamoja na idadi kubwa ya watu waliotokana na makasisi wakuu na wazee wa miji mbalimbali walikuja Gethsemane. Lakini Luka anasema kwamba makasisi wakuu pamoja na waangalizi wa hekalu na wazee wenyewe ndiyo waliokuja kumkamata Yesu. (Luka 22:52).

### **2. JINSI YESU ALIVYOKAMATWA**

Mathayo, Marko na Luka wanasema kwamba Yuda aliwapa ishara hao waliokwenda kumkamata Yesu akisema kwamba, “YEYOTE NITAKAYEMBUSU” basi ndiye huyo huyo; mkamateni. Ndipo akamwendea Yesu na kusema, Bwana wangu Mtukufu, na kisha akambusu. Na Yesu akamwambia, “Rafiki, unatoka wapi?” Ndipo wakaja kumtia mbaroni Yesu na kuondoka naye. (Mathayo 26:47-49). Lakini Yohana anatoa maelezo tofauti kabisa kuhusu kukamatwa huko. Kulingana naye, Yuda alipofika pamoja na hilo kundi la watu, Yesu AKAJITOKEZA MBELE YAO NA KUWAULIZA: MNAMTAFUTA NANI? Wakamjibu: Yesu wa Nazareti. Yesu akajibu: Ndiye mimi. Na Yuda pia alikuwa amesimama kati yao. Aliposema haya wakarudi kinyumenyume na wakaanguka chini. Yesu akawauliza tena swalilie lile na wakajibu vile vile. Yesu akasema: nimekwisha waambieni kuwa mimi ndiye Yesu. Kwa hiyo kama mnanitafuta mimi waacheni hawa waende zao. Kisha Petro akalikata sikio la kulia la mtumishi wa Kasisi Mkuu. Ndipo wakamchukua Yesu na kumtia mbaroni. (Yohana 18: 3, 8, 10,12).

3. Luka na Yohana wanasema kwamba sikio la mtumishi wa Kasisi Mkuu lilitatwa kabla ya kukamatwa kwa Yesu lakini Mathayo na Marko wanasema kwamba lilitatwa baada ya kukamatwa kwake.

4. Mathayo anasema kwamba, Yuda alijijutia mwenyewe na akavichukua vipande thelathini vya fedha na kuvirudisha kwa makasisi wakuu na wazee ambao walikataa kuvipokea, lakini ye ye akavitupa sakafuni ndani ya hekalu na AKAENDA KUJINYONGA MWENYEWE. MAKASISI WAKUU PAMOJA NA WAZEE WAKASHAURIANA NA WAKAVICHUKUA VILE VIPANDE VYA FEDHA NA KUNUNUASHAMBA LA MFINYANZI ili kuzikia wageni. Na shamba hilo likaitwa “Shamba la damu” (Mathayo 27: 3, 8). Mashahidi wenzake wale watatu hawasemi lolote kuhusu jambo hili, isipokuwa tu katika Matendo, taarifa ambayo inasemekana kuwa imeandikwa na Luka tunasoma Petro amesema kwamba: YUDA MWENYEWE NDIYE ALIYENUNUA SHAMBA HILO

KWA MALI PO YA UOVU WAKE NAYE AKITANGULIZA KICHWA AKADONDOKA CHINI NA KUPASUKA VIPANDE VIPANDE mbele ya watu na matumbo yake yote yakatoka nje (Matendo 1:18)

5. MBEBAJI MSALABA: Mathayo na Marko wanasema: "Mtu mmoja wa Kirene aitwae Simon ndiye aliyetakiwa kuubeba msalaba wake mpaka mahali paitwapo Golgotha, yaani mahali pa mafuvu. (Mathayo 27: 32, 33). Maelezo ya Yohana ni kwamba Yesu mwenyewe akiwa amebeba msalaba wake ndiye aliyekwenda sehemu iitwayo mahali pa mafuvu. (Yohana 19: 17).

6. Kisha hawa mashahidi wanne hawakubaliani katika kunukuu maandishi ambayo wanasema kuwa yaliwekwa juu ya kichwa cha Yesu alipotundikwa msalabani.

Mathayo: "Huyu ni Yesu Mfalme wa Mayahudi".

Marko: "Mfalme wa Mayahudi".

Luka: "Huyu ndiye Mfalme wa Mayahudi".

Yohana: "Yesu wa Nazareti, Mfalme wa Mayahudi" ,

7. Mathayo na Marko wanasema kwamba wale wezi ambao walisulubiwa pamoja na Yesu walimkebehi. Lakini Luka anasema kwamba mmoja wao alimkebehi lakini mwingine alimwonya na kumwambia, "Je wewe humwogopi Mungu?" Kisha akamwambia Yesu, "Bwana wangu", tafadhali nikumbuke mimi wakati utakapoingia katika ufalme, na Yesu akamwaahidi kwamba atakuwa naye peponi siku ile ile (Luka 23:39,43). Na Yohana hata hakutaja wala kudokeza juu ya mazungumzo haya ya maana baina ya wasulubiwa watatu.

8. MUDA WA KUSULUBIWA: Marko anasema, "Ilikuwa SAA YA TATU wakati walipomsulubisha" (Marko 15:25). Lakini Yohana anasema ilikuwa karibu SAA YA SITA wakati Pilato alipomtoa Yesu kwa Mayahudi. (Yohana 19:14). Mathayo na Luka wanasema tu ya kwamba kuanzia saa Sita hadi Saa Tisa nchi yote ilifunikwa na giza.

9. YESU ALIKUFAJE? Yesu ALIPOLIA TENA KWA SAUTI YA JUU, akakata roho (Mathayo 27:50). Marko anasema “ALILIA KWA SAUTI YA JUU na akakata Roho” (Marko 1 5:37). Luka anasema, “Baada ya kulia kwa sauti ya juu akasema, “BABA MAISHA YANGU NAYAKABIDHI MIKONONI MWAKO” na baada ya kusema hivyo akakata roho,” (Luka 28:46), Yohana anasema “Kwa hiyo Yesu ALIPOIPOKEA SIKI akasema IMEKWISHA na AKAINAMISHA KICHWA CHAKE na kukata roho”, (Yohana 19:30).

10. KWA NINI MLINZI WA MAKABURI ALISEMA KUWA ALIKUWA MCHAMUNGU NA MWANA WA MUNGU? Mathayo anasema, “Mlinzi wa makaburi pamoja na hao aliokuwa nao walipoliona tetemeko la ardhi pamoja na mengine wakaogopa sana wakisema, “Bila shaka Huyu alikuwa Mwana wa Mungu” (Mathayo 27:54). Marko anasema “Mlinzi wa makaburi alipoona ya kwamba Yesu ALILIA NAMNA ILE NA KUKATA ROHO, akasema, Bila shaka mtu huyu alikuwa Mwana wa Mungu” (Marko 1 5:39). Luka anasema, “Mlinzi wa makaburi alimtukuza Mungu akisema kwamba mtu huyu alikuwa mcha Mungu” (Luka 23:47).

11. YUSUFU WA ARIMATHAYA ALIKUWA NANI? Mathayo anasema kwamba alikuwa MWANAFUNZI WAKE YESU. Marko na Luka wanasema kwamba alikuwa MSHAURI MHESHIMIWA ambaye pia alikuwa akingojea kuingia katika Ufalme wa Mwenyezi Mungu. Yohana anasema kuwa Yusufu alikuwa MWANAFUNZI WA YESU KISIRISIRI KWA KUHOFU ASIADHIRIWE NA MAYAHUDI.

12. Mtu huyu Yusufu ambaye alikuwa mkubwa alimwendea Pilato na kuomba apewe mwili wa Yesu, Pilato akamkubalia bila ya kufanya UDADISI WO WOTE. Haya ndiyo madai ya Mathayo na Yohana. Lakini Marko na Luka wanasema kwamba alimruhusu BAADA YA KUPATA MAELEZO KUTOKA KWA MLINZI WA MAKABURI. Kisha yeye peke yake akaiviringishia maiti hiyo kitambaa cha bafta na kuilaza ndani ya pango alilochonga katika mwamba. Hivi ndivyo asemavyo Mathayo, Marko na Luka ambapo Yohana anasema

kwamba hakuwa peke yake bali ye Ye Yusufu pamoja na Nikodemus ndiyo walioulaza mwili wa Yesu katika pango. Kadhalika wanahitilafiana kuhusiana na matukio yanayohusikana na kufufuka kwa Yesu baada ya kusulubiwa kwake.

### **1. NI NANI ALIYEKUWA WA KWANZA KUJA PANGONI NA ILIKUWA WAKATI GANI?**

Mathayo anasema kwamba katika mwanzo wa mapambazuko ya kuamkia siku ya mwanzo wa wiki, Maria Magdalena na Maria mwingine walikwenda kulikagua pango. Marko anasema walikwenda asubuhi sana **WAKATI WA KUCHOMOZA KWA JUA**.

Ajuavyo Yohana ni kwamba walikwenda mapema kukiwa bado kungali giza. Kisha, Mathayo na Marko wanasema kwamba kulikuwa Maria wawili, lakini Luka anasema kwamba waliokwenda ni Maria Magdalena, Joanna, Maria mamaake James na wanawake wengine. Kinyume na yote hayo Yohana anasema kwamba aliyeqwenda ni Maria Magdalena tu.

### **2. TETEMEKO LA ARDHI NA MALAIKA**

Mathayo anatuambia, “Na tazama, kulikuwa na tetemeko la ardhi kubwa kwani malaika wa Bwana akashuka kutoka mbinguni na akaja kulifungua jiwe la mlango na **KUKETI JUU YAKE**”

Wenzake watatu wote hawasemi lolote kuhusu hilo tetemeko la ardhi wala kuhusu kufunguka kwa jiwe na malaika kuketi juu yake. Kulingana na maelezo yao, hakuna ye yote aliyeketi juu ya jiwe. Marko anasema kwamba wakati wale Maria wawili walipofika pangoni wakakuta lile jiwe lilikwisha funguliwa tayari. Na walipoingia ndani ya pango wakamwona **KIJANA AMEKETI** mkono wa kulia nao wakaingiwa na hofu. Luka anasema kwamba mlikuwamo na Watu **WAWILI** nao hawakuwa **WAMEKETI** bali walikuwa **WAMESIMAMA**. Naye Yohana anasema kwamba **WOTE WAWILI WALIKUWA WAMEKETI NDANI YA PANGO** mmoja ndani kabisa na mwingine mlangoni.

### **3. NANI ALIYEKUWA WA KWANZA KUTANGAZA**

## **KUPAA KWA YESU?**

Mathayo anasema kwamba, “Yule malaika ambaye alikuwa ameketi juu ya jiwe aliwapasha habari akisema kwamba, ‘Hayupo hapa’ kwa sababu amepaa” Marko anasema kwamba wale watu wawili walioketi ndani ya pango ndiyo waliowaambia akina Maria habari hizi za kupaa. Luka anasema kwamba baada ya akina Maria kuingia pangoni hawakuuona mwili wa Yesu na katika kushangaa, wale watu wawili waliokuwa wamesimama ndani ya pango waliwaambia, “Hayupo hapa, bali amepaa”.

Lakini mwenzao Yohana ana maelezo tofauti kabisa. Yeye anasema kwamba “Alipoona jiwe limeondolewa mlangoni, Maria Magdalena alikimbia na kumwendea Petro na yule mwanafunzi mwingine ambaye alipendwa sana na Yesu na kusema wamemchukua Bwana na hatujui walikomlaza. Wote wakaja wanakimbia mpaka pale mahali na wote wakaingia pangoni ambamo wakazikuta zile shuka za bafta zimeachwa mle zikiwa zimefungwa pamoja na kile kilemba alichokuwa anafungwa kichwani. Baada ya kuyaona yote haya wakarejea nyumbani. Lakini Maria akasimama pale pale kandokando ya pango huku akilia na kuchungulia chungulia mle ndani ya pango. Katika kufanya hivyo akawaona malaika wawili wakiwa wameketi nao wakamwliza “Mwanamke unalilia nini?” Alikuwa bado hajamaliza kuwajibu ambapo aligeuka nyuma na kumwona Yesu amesimama ambaye kwa mara ya kwanza alimdhania kuwa ni mtunza bustani lakini hatimaye akamtambua kuwa ndiye baada ya kuzungumza naye.

## **4. NANI ALITANGAZA MAAGIZO YA YESU?**

Mathayo anasema kwamba yule malaika aliyeketi juu ya jiwe aliwaambia wale Maria wawili kwamba “Enendeni haraka mkawaambie wanafunzi wake kwamba yeye amefufuka kutoka katika wafu na zingatieni kuwa yeye ameshatangulia kwenda Galilea, nanyi mtakutana naye huko. Nimekwisha waambieni”. Walipokuwa njiani kwenda huko Yesu akakutana nao na akawapa ujumbe huo huo. Marko anasema kwamba yule mtu aliyeketi ndani ya pango ndiye

aliywapa ujumbe huo. Luka hasemi kwamba wale watu wawili waliokuwa pangoni waliwapa ujumbe wo wote wanafunzi wake Yesu. Walakini Yohana anasema kwamba Yesu mwenyewe ndiye aliywagiza Maria kuwa waambie nduguzo kwamba mimi “Ninapaa juu kwa baba yangu aliye pia baba yenu na ambaye ni Mungu wangu kama alivyo Mungu wenu ninyi”.

### **5. JE, AKINA MARIA WALIUFIKISHA UJUMBE?**

Mathayo hasemi jambo lo lote kuhusu suala hili kulingana na aya ya 16 ya Sura ya 28 inaelekea kwamba waliufikisha ujumbe huu. Lakini Marko anasema ya kwamba wao waliondoka haraka haraka na kukimbia huku wakitetemeka na kuhofu na wala hawakusema lolote kwa mtu yejote kwani waliogopa. Luka anasema kwamba wanawake hao waliwaambia wanafunzi kwamba Yesu amepaa na Yohana anasema kwamba Maria aliwaaambia hao wanafunzi yale ambayo aliambiwa na Yesu.

### **6. JE UJUMBE HUU WALIUPOKEAJE?**

Mathayo hasemi lolote kuhusu jambo hili. Marko anasema “Waliposikia kwamba yungali mzima na kwamba Maria alimwona, hawakuamini”. Luka anasema kwamba maneno ya akina Maria yalioneckana kama hadithi za kipumbavu mbele ya wanafunzi wa Yesu na hawakuyaamini. Yohana yuko kimya kabisa kuhusu jambo hili.

### **7. YESU ALIKUTANA NAO WAPI KWA MARA YA KWANZA?**

Mathayo anasema kwamba (mara baada ya kusikia yale maagizo) wanafunzi hao kumi na mmoja wakaelekea kwenye mlima ambao Yesu aliwaashiria hapo mapema. Nao walipomwona wakamwabudu ingaweje baadhi yao walimtilia mashaka. Marko anasema, “Kwanza alimtokea Maria, kisha akajitokeza kwa sura nyingine mbele ya wanafunzi wake wawili, na kisha akajitokeza mbele yao wote kumi na mmoja walipokuwa wakila nyama na akawashutumu sana kwa utovu

wao wa imani na kuwa na mioyo migumu kwa sababu hawakuwaamini wale ambao walimwona baada ya kufufuka.

Ni dhahiri kwamba Luka anampinza kwani ye ye anasema kwamba Yesu alikutana na hao wanafunzi wake kumi na mmoja mjini Yerusalem jioni ya siku aliyofufuka. Yohana anamwunga mkono Luka akisema kwamba Yesu alijitokeza bila ya kutazamiwa pale mahali ambapo wanafunzi wake walikuwa wamekusanyika “Kwa kuwahofia Mayahudi” (Yohana 20: 19).

“Kutokana na mifano iliyotajwa hapo juu ambayo imetokana na matamshi ya mashahidi wanne wa mshtaki, sisi tunatoa uamuzi ufuatao:

1. Maelezo ya mashahidi hawa wanne hayawezi kuitwa Matakatifu na wala hayakufunuliwa na Mwenyezi Mungu.
2. Hakuna hata taarifa moja miengoni mwa hizo nne ambayo kwetu sisi inaonekana na ushadidi wa ana kwa ana au tuseme kwamba imetokana na habari zenye kuaminika. Kwa mfano mmoja wao anasema kwamba wakati wa kukamatwa kwa Yesu, makuhanu wakuu pamoja na wazee walikuwapo lakini mwингine anakanusha habari hii. Mmoja wao anasema kwamba Yesu alichagua mlima fulani wa Galilea ambako alikuwa akutane na wanafunzi wake na akakutana nao mahali hapo kama ilivyopangwa. Mwingine anasema kwamba mkutano huo ulifanyika mjini Yerusalem. Taarifa kama hizi haziwezi kuwa zimeandikwa na wanafunzi wake kwani wao walijua mahali ambapo mkutano huo ulikuwa ufanyike kwa sababu mashahidi wote wanne wanasema kwamba wanafunzi wote kumi na mmoja walihudhuria mkutano huo.

Kadhalika baadhi yao wanasema kwamba Yuda ambaye alimsaliti Yesu, aliliwezesha genge la watu kumtambua Yesu kwa kuibusu mkono wa

Yesu; lakini mmoja wao anakanusha habari hii na kusema kwamba alikuwa Yesu mwenyewe ambaye alijitambulisha kwa watu hawa.

Matokeo ni kwamba ushahidi wao ni wenyewe kupinzana. Kwa hiyo bila ya kusitasita tunatangaza ya kwamba taarifa hizi si maelezo ya mashahidi walioshuhudia ana kwa ana bali ni zile ambazo msingi wake ni uvumi na wala hazitaji chanzo cha habari hizi. Maelezo yao kwamba Yesu alifia msalabani na kwamba alifufuka kutoka wafu hayawezi kuchukuliwa kuwa ni ya kweli hata kama tukichukulia kwamba waandishi wa maelezo hayo walikuwa wanafunzi wa Yesu kwa sababu wakati wa kukamatwa kwake wao walimwacha peke yake na wakakimbia. Petro ambaye alifuatana na Yesu mpaka kwenye jumba la makuhani wakuu taarifa hizi nne zinamtia hatiani kwa kusema uwongo mara tatu. Kulingana na taarifa hizi nne hakuna hata mtu mmoja miongoni mwa wanafunzi wa Yesu ambaye alikuwapo wakati unaosemekana kuwa Yesu alikufa wala ule unaosemekana kuwa alifufuka. Kwa hiyo hatuna njia nyingine isipokuwa kusema kwamba ushahidi huu hautoshi kuthibitisha matukio muhimu ambayo kama mlalamikaji asemavyo, ulimwengu mzima unayategemea hayo ili upate kuokoka.

Baada ya maelezo hayo hapo juu yafuatayo ndiyo maelezo ya mshitakiwa akitaja matukio muhimu kwa muhtasari na kutoa hoja za kumtetea Yesu kutokana na madai kwamba alikufa kifo cha laana na kudai kwamba aliposhushwa msalabani alikuwa amezimia tu<sup>a</sup>.

## 1. Masaa matatu ya kuwambwa msalabani hayatoshi kifo<sup>b</sup>.

---

- a. Hoja ambazo zimeelezwa kwa kirefu katika sura iliyotangulia hazikurudiwa tena katika sura hii.
- b. Ilikuwa wajibu wa walini pamoja na jemedari wao. Kuhakikisha kwamba mwili wa Yesu hauondoshwi makaburini. Ilikuwa lazima kufanya hivyo kutokana na uhakika juu ya kifo kwa vile mara nyingine ilichukua

siku tatu kwa mtu kufa na hasa kifo cha namna hii kilitokana na kulazimishwa kwa mwili kubakia pamoja bila ya kujisongeza na vile vile njaa ya muda mrefu (Euseb. H. E. VIII, 8 sen, Provo 3), lakini katika aliokaa Yesu walikuwa wazima, na miguu yao ilibidi ivunjwe ili kuwaua lakini Yesu alisamehewa asivunjwe miguu yake (Yohana 19:32).

4. Damu na maji vilitoka mara moja wakati Askari alipomchoma Yesu kwa mkuki kwenye ubavu wake wa kulia. Hii ni dalili waziwazi kwamba damu yake liliwa bado inatembea. Hivyo basi alikuwa mzima.
  5. Baada ya kutolewa msalabani mwili wake hawakupewa maadui zake bali walipewa marafiki zake. (Yohana 19:38).
  6. Ille haraka na shauku waliyoonyesha rafiki zake katika kuupata mwili wake inaonyesha waziwazi kwamba walikuwa na nia ya kumwokoa kwa kuelewa dhahiri kwamba bado hajafa.
  7. Hatua ya Mayahudi ya kupeleka walinzi kwenye pango ulikolazwa mwili wake vile vile inaonyesha kwamba hawakuwa na uhakika juu ya kifo chake. Wangalikuwa na hakika kwamba amekufa wasingalijali cho chote kama wanafunzi wake wangeiiba ulinzi huu iliwezekana kwa wasulubiwa kuteremshwa na kupona (kama ilivyokuwa katika kisa kiitwacho Gandokes: Herod VII 194) na kama ilivyo katika kisa cha rafiki yake Josephus ingawaje ni mmoja tu aliyepona miongoni mwa watatu (Dictionary of Bible, W. Smith 1893).
2. Pilato alishangaa jinsi gani Yesu anaweza kufa kwa muda na uzoefu wake wa siku nyingi kwamba muda ule haukuwa mrefu wa kuweza kusababisha kifo. Pilato, Yusufu na Mlinzi wa makaburi wote hawa walikuwa wakimtakia mema Yesu. Hivyo basi kwa sababu ya huruma yao hii walitaka wamwokoe Yesu kutoka katika kifo.
  3. Wezi wawili ambao walibakia msalabani kwa muda ule ule

maiti yake. Sababu inayotolewa kwamba “isije wanafunzi wake wakaja usiku na kumwiba na kuwaambia watu kwamba amefufuka kutoka katika wafu” (Matayo 27:62) ni ya kichekesho kwa sababu kama wanafunzi wake wangalisema hivyo, wangalijibiwa kuwa kama amefufuka basi na ajitokeze mbele ya watu na baada ya kujitokeza wangalimkamata tena. Hivyo basi sababu ya kweli ya kupeleka walinzi kule pangoni ni kwamba hawakuwa na hakika juu ya kifo chake.

8. Pilato hakupenda Yesu asulubiwe na hakuna jambo ambalo lingalimfurahisha zaidi kuliko hili la kumwokoa. Na kwa hakika alifanya juhudhi nyingi sana za kisirisiri ili kumwokoa Yesu. Njozi aliyoiiona mkewe ndiyo iliyomshurutisha kufanya kila aliloliweza ili kumtoa Yesu mikononi mwa maadui zake.
9. Maaskari pamoja na jemedari wao hawakuta Yesu afe. Ndiyo sababu hawakumvunja miguu. Vile vile maaskari walijifanya kuwa wamelala wakati wa kulinda kwao. Hii yote inaonyesha kwamba wao walimhurumia Yesu.
10. Kaburi ambamo mwili wa Yesu ulilazwa lilikuwa pango lilidochongwa ndani ya jiwe kubwa. Pango hilo lilikuwa na wasaa wa kuwezesha watu kadhaa kukaa humo bila ya taabu. Pango hili ni mali ya rafiki yake mpenzi ambaye alifanya kila awezalo ili YESU apate fahamu na kisha apone kabisa. Mnamo Jumapili, siku iliyofuatia siku ya sabato, Mayahudi waliruhusiwa kwenda kuzuru Pango lile. Lakini asubuhi na mapema kukiwa bado kuna gizagiza Yesu hakuwapo ndani ya Pango lile. Kifuniko cha lile Pango kilikuwa kimeondolewa na mwili wa Yesu haukuwamo ndani ya lile Pango. Baada ya muda mfupi Yesu alionwa na Maria ambaye kwa mara ya kwanza alimdhania kuwa ni mtunza bustani. Yamkini alijifananisha na mtunza bustani ili asijulikane na Mayahudi na kukamatwa tena na kuwekwa juu ya msalaba mara ya pili.
11. Aliwapelekea habari wanafunzi wake akiwaagiza waondoke

pale na kuelekea katika majimbo ya Galilaya, akiwaambia kwamba yeche atatangulia na kwamba watakutana naye huko. (Mathayo 28:7). Aliondoka Jerusalemu haraka haraka kwani alijua kwamba baada ya muda mfupi Mayahudi watajua kwamba ametoka pangoni na hivyo wataanza kumtafuta.

12. Alijihadhari sana asije akakamatwa tena na Mayahudi. Kwa hiyo aliamua kukutana na wanafunzi wake tu; na hata hao pia hakukutana nao hadharani bali alikutana nao kisirisiri au vichakani kandokando ya njia. Na ingawaje alikutana nao lakini hakukaa nao kwa muda mrefu, akajifichaficha mpaka akasikia njaa na kiu. (Matendo 10:41). (Luka 24: 42) Aliwaambia wale wanafunzi wake waliomdhania kuwa ana mwili wa kiroho kwamba, “Tazama mikono yangu na miguu yangu; mimi ni yule yule: nishikeni na niangalieni, kwani kiumbe cha kiroho hakina nyama na mifupa kama hii mnionayo nayo” (Luka 24:38 - 39).

Thomaso ambaye hakuami kwamba waliyemwona wanafunzi wenzake ndiye Yesu aliombwa aziguse kovu za misumari kwa vidole vyake. (Yohana 20:27).

Na “Marahamu ya Yesu” au “marahamu ya Wanafunzi” ni dawa iliyotengenezwa na wanafunzi wake ili kuyatibu majeraha yake. Matukio yote haya yanaonyesha waziwazi kwamba Yesu alitoka ndani ya lile pango akiwa na mwili wake wa kibinadamu ukiwa na vidonda alivyopata msalabani. Baada ya kuulinganisha ushahidi huu na ule uliotolewa na K tunaonelea ya kwamba hoja zinazotolewa na M zina uzito zaidi na zinakubalika akilini. Kutokana na uchunguzi wetu tunaamua kwamba kwa kuwa mlalamikaji K hakutoa hoja zenye kutegemewa na za kuifanya mahakama iamini ushahidi wake, yeye ameshindwa kuthibitisha shitaka lake. Hivyo basi, hakuna ushahidi kwamba Yesu alifia msalabani.

Kutokana na hayo ni dhahiri pia hakufufuka. Mtu ye yote mwenye akili timamu anaweza kugundua taarifa zinazopinzana zilizotolewa na

mashahidi wanne wa mlalamikaji, kwamba alipoteremshwa msalabani Yesu hakuwa amekufa. Alizimia tuu. Na baadaye akapata fahamu. Alitoka nje ya pango akiwa na mwili wake wa kibinadamu ilitengenezwa kwa udongo. Mlalamikaji K ameshindwa kulijibu swali ya kwamba kama Yesu alitoka Pangoni akiwa na mwili wa kiroho, je ule mwili wake wa kibinadamu ulikwenda wapi?

Kadhalika hakuweza kulijibu swali ya kwamba ikiwa Yesu hakusaidiwa na rafiki zake je alizipata wapi zile nguo alizovaa ambazo zilimfanya Maria Magdalena amdhanie kuwa ni mtunza bustani? Alikuwa amevaa nguo zaidi ya moja mwilini mwake. Je alizipata wapi? Nguo zake mwenyewe zilichukuliwa na maaskari na zile “Sanda” zilikuwa zimeachwa mle pangoni. Zaidi ya hayo, mashahidi wawili ambao walishuhudia kwa macho yao mambo yote haya yakitokea, yaani Yusufu wa Arimathaya na Nikodemu ambao ndio waliouchukua mwili wa Yesu na kuulaza katika Pango na kuona yote baadaye, hawa wawili hawakuitwa na mlalamikaji ili waje kuhojiwa na katika taarifa za maandishi zilizotolewa na mashahidi wanne wa mlalamikaji hakuna mahali popote paliposema kwamba Yusufu na Nikodemu nao waliamini kwamba Yesu alifufuka kutoka katika wafu.

Kwa hiyo basi hatuna njia yo yote isipokuwa kulifutilia mbali shitaka hili. Hivyo basi, sisi tunalifuta shitaka hili.

**Imetiwa Saini na  
X. Y.**

**Imetiwa Saini na  
A. Z.O**

## SURA YA TATU

## **MAELEZO YA KIAKILI KUHUSU KISA CHA KUFUFUKA**

Hapa chini nayanakili maelezo ya kiakili kuhusu kisa cha kufufuka kama yalivyoandikwa na wanazuoni wawili mashuhuri ambao wamezichunguza kwa makini taarifa nne za waandishi wa Injili.

Kwanza Profesa Heinrich Eberhard Gottlōbe Paulus ( 1761-1861 ) ambaye mnamo mwaka 1789 alikuwa Profesa wa lugha za Kimashariki (Professor of Oriental Languages) katika Chuo cha Jena. Na mnamo mwaka 1793 akafanikiwa kuwa Profesa wa Elimu ya dini daraja la tatu. Alikuwa mwanachama wa Baraza la Elimu la Bavaria (Bavarian Educational Council) kuanzia mwaka 1807 hadi 1811. Mnamo mwaka 1811 alikwenda katika Chuo cha Heidelberg akiwa Profesa wa Elimu ya dini na akabakia katika Chuo hicho mpaka alipofariki. Katika kitabu chake kiiwacho THE LIFE OF JESUS (Maisha ya Yesu) Profesa huyu ameandika:

“Kufufuka kwa Yesu ni lazima kurudishwe katika hoja ile ile (yaani kazikwa kabla hajafa) kama tukitaka kuzingatia ukweli ya kwamba wanafunzi wake walimwona akiwa na mwili wake wa asili ukiwa na kovu za misumari mikononi mwake na ya kwamba walimwona akila chakula mbele yao. Kwa hakika kifo kinachosababishwa na kusulubiwa huletwa na hali ya kukauka mwili ambayo huanzia kwenye ngozi na kuingia polepole hadi ndani kabisa. Kifo cha namna hii hutokeea taratibu zaidi kuliko namna nytingine yo yote ya kifo. Katika kitabu chake kiiwacho CONTRA APOINEM, Josephus ametaja ya kwamba Titus alimtunukia nafasi ya kuteua watu watatu aliowaua mionganoni mwa waliokuwa wakisulubiwa katika mji wa Tekoa ili washushwe msalabani. Wawili mionganoni mwa hao watatu walioshushwa walikufa lakini mmoja wao akapona. Walakini Yesu “alikufa” kwa haraka ya ajabu. Ukelele wa juu aliopiga mara tu kabla kichwa chake haki jainama, unaonyesha ya kwamba nguvu zake zilikuwa bado hazijaisha na kwamba kilichotokea ni kuzimia kwa daraja

ya juu ambako kunafanana na kifo. Katika kuzimia kwa namna hii hali ya kulia kwa anayesulubiwa inaendelea mpaka anapoishiwa nguvu.

Hii peke yake huhakikisha kwamba utaratibu wa kufa umekamilika na kwamba kifo kimeshatokea. Katika kisa cha Yesu na kama ilivyo katika visa vya watu wengine ile cheche ya uhai ingalizimika pole pole isingalikuwa kudra ambayo ilifanya kazi kimiujiza kwa upande wake Yesu, na kudra hiyo mara nyingine ilijitokeza kuwasaidia watu wengine kwa uwazi zaidi kwa njia ya ujuzi na uangalizi wa binadamu. Kile kidonda cha mkuki ambacho twakifikiria kuwa kilikwaruzwa kwenye ngozi tu kwa hakika kilipenya mpaka ndani kabisa na kilisaidia kuitoa damu iliyomiminika ndani isigande kule na kuleta madhara. Lile kaburi lenye ubaridi na yale manukato vilieendelea kuukamilisha mpango wa kufufuka mpaka hatimaye ile dhoruba pamoja na tetemeko la ardhi vilimkurupusha Yesu kutoka katika usingizi wa kuzimia akapata fahamu. Kwa bahati nzuri lile tetemeko la ardhi vile vile lilisaidia kuliondoa lile jiwe lililokuwa limeufunika mlango wa kaburi. Bwana akazivua zile nguo za kaburini na akavaa nguo za bustani. Hiki ndicho kilichomfanya Maria kama tuambiwavyo katika Yohana 20: 15; akamdhania kuwa ni mtunza bustani. Alintuma mwanamke huyu awaambie wanafunzi wake akutane naye Galilaya na kwamba ye ye anatangulia kwenda huko. Kwenye mji wa Emmau, wakati giza lilipokuwa linatanda, alikutana na wafuasi wake wawili ambao kwa mara ya kwanza walishindwa kumtambua kwa sababu uso wake ulikuwa umebadilika sana kwa sababu ya mateso. Lakini ile tabia yake ya kushukuru wakati wa kuuvunja mkate na zile kovu za misumari zilizokuwa katika mikono yake iliyonyanyuliwa viliwatambulisha ye ye alikuwa nani. Wafuasi hawa wakamjulisha waliko wanafunzi wake na mara ile akarudi Jerusalemu na kujitokeza mbele yao bila ya kutazamiwa. Haya ndiyo maelezo ya kile kinachoonekana kuwa ni utatanishi kati ya maaagizo yake ya kukutana nao Galilaya na kujitokeza kwake katika mji wa Jesuralemu”.

“Kwa njia hii Yesu alikaa pamoja nao kwa siku arobalni, akitumia sehemu ya muda huo kukaa nao kule Galilaya na kutokana na mateso

aliyoyapata alikuwa na uwezo wa kuhimili taabu. Aliishi kimya kimya na akapata nguvu kwa muda mfupi aliojitokeza mbele ya wafuasi wake na kuwafundisha. Alipohisi mwisho wake unakaribia alirudi Jerusalemu. Kwenye mlima wa Mizeituni, wakati wa asubuhi aliwakusanya wafuasi wake kwa mara ya mwisho. Akainua mikono yake ili kuwabariki, na akiwa ameinua mikono yake kuomba baraka akajitenga nao. Wingu likatanda kati yao na yeye hivi kwamba hawakuweza kuona anaelekea wapi. Alipokuwa akitoweka mbele yao walibakia wamesimama watu wawili mashuhuri waliokuwa wameva nguo nyeupe. Watu hawa walikuwa mionganoni mwa watumishi wake wa siri katika mji wa Jerusalemu. Watu hawa waliliambia lile kundi la wafuasi wake kwamba hapakuwa na haja ya kungojea pale bali waondoke. “Kule hasa alikofia Yesu wao hawakuwa na habari na kwa hiyo wakaamua kuelezea kwamba kule kuondoka kwake ni kupaa.”

Pili Bwana Ernest Brougham Docker, Jaji wa Mahakama ya Wilaya, Sydney ameandika kitabu chenye maana sana kahusu suala hili. Kitabu hiki kinaitwa IF JESUS DID NOT DIE UPON THE CROSS (Kama Yesu hakufa msalabani) ambamo ameuchambua ushahidi wa Injili zote tamthili ya Jaji anavyochunguza ushahidi wa kesi. Hapa chini ninanakili maoni yake kuhusu ufufuo:

“Mawazo ya kwamba miili iliyokufa inaweza kuhuishwa tena yalikuwa yameenea katika zama alizoishi Bwana wetu (Kristo) na vile vile kwa mamia ya miaka kabla na baada ya zama hizi na hususa katika sehemu zote zile ambako utafiti wa kisayansi ulikuwa bado haujaendelezwa. Tunao mfano mmoja katika historia ya Eliya na mifano miwili katika historia ya Elisha: Kuna mifano mitatu lliyotajwa katika Injili. Licha ya ule wa Yesu mwenyewe iko mingine miwili katika Matendo ya Mitume(Sura ya 16). Irenaeus anasema kwamba kulikuwa na visa vingi ambapo “roho llierudi katika mwili uliokufa na mtu yule akawekwa chini ya uombezi wa kanisa”.

Tukio moja la kupendeza kuhusu imani hii kwa wakati huu limeelezwa katika makala hiyo inawahusu watu wasio na fikra za kisayansi na imetolewa chini ya kichwa cha maneno, “SCHWEITZER as

MISSIONARY (HIBBERT) JOURNAL, JULY 1914, ukurasa 885  
Mhashamu huyo anasema:-

"Kitu kinachowaathiri sana wazalendo ni matumizi ya dawa ya kutia ganzi. Wasichana wasomao katika Shule yetu ya misheni huwaandikia barua wasichana wenzao wasomao Ulaya. Katika moja ya barua za namna hiyo imeandikwa: "Tangu daktari afike hapa kuna mambo mengi ya ajabu yanayotokea. Kwanza anawaua wagonjwa kisha anawatibu na hatimaye anawahuisha. Ni sifa gani kubwa kuliko hii ambayo mfanyakaji mambo ya ajabu anaitamani?"

Na katika kifungu cha maneno kifuatacho ambacho kimetolewa kutoka katika (Physical Culture and Health, July 15, 1912) inaeleke ya kwamba hata matabibu wenyewe ujuzi wanaweza kukosea wakadhania kwamba kifo kimeshatokea kumbe kikawa bado. Kifungu hicho cha maneno kinasomeka kama ifuatavyo:-

'Kumhuisha Mfu' ni jina la ala moja maarufu iliyogunduliwa na Mjerumani mmoja. Imepewa jina kinamna yake "PULMOTOR" na imetumiwa kwa mafanikio makubwa sana katika kuwatibusi watu ambao matabibu wakuu wameshawatangaza kuwa wameshakufa, ikawaponyesha na si hivyo tu bali pia ikawarudishia afya nzuri na siha timamu. Kijana mmoja aitwaye Haas alikuwa ameishiwa na pumzi kwa sababu ya kuvuta hewa iliyotoka kwenye makaa ya mawe. Marafiki zake walimpa huduma ya kwanza kwa muda wa masaa matatu lakini wakashindwa kumpatisha fahamu. Akahesabiwa kwamba amekufa. (Uk.17).

Baada ya kutumia PULMOTOR kwa muda wa masaa matatu kijana yule aliweza kusimama na kuonyesha mshangao mkubwa na kutoa shukurani na kutangaza kwamba alijisikia yu mzima kama alivyokuwa kabla ya kuvuta hewa ile. Daktari mmoja ambaye aliiwta kabla ya ile PULMOTOR kutumiwa baadaye alisema kwamba sawa na elimu ya tiba Haas alikuwa katika hali ya ufu wakati daktari huyo alipofika. Akaongeza kwamba Haas ni mtu wa tano kuhuishwa.

Katika kitabu kiiwacho TAPLOR'S MEDICAL JURISPRUDENCE, chapa ya sita, ukurasa 243 imeandikwa kwamba mara nyingine dalili za kifo zinaonekana kana kwamba zimeshatokea katika mwili wa mtu mzima na ya kwamba njia ya kuthibitisha kwamba dalili hizi si za kweli imeelezwa ndani ya gazeti liitwalo THE LANCET jalada la kwanza, 1900, ambalo kwa kuyanukuu maelezo ya kitabu kilichotajwa hapo juu chini ya kichwa cha maneno "Mazishi kabla ya kifo" Gazeti hilo linasema:-

"Bila shaka kumetokea visa vingi ambapo watu waliopatwa na hali ya kuzimia kwa sababu mshituko wa moyo au upungufu wa msukumo wa damu au mshituko wa mishipa ya fahamu au uchovu mwingi wakatangazwa kuwa wamekufa na watazamaji kwa sababu tu ngozi za miili yao hazikuwa na dalili za uhai na zilikuwa baridi na pia miili yao haikuonyesha dalili za kupumua au kutembea kwa damu. Ikiwa uamuza wa uhai au kifo kila mara utaachwa mikononi mwa watu kama hao na fikra zingine zisikubaliwe masaa machache baada ya mawazo ya kimila ya watu hawa, basi hapana shaka yo yote ya kwamba miili yenye uhai itawekwa katika hatari ya kuzikwa kabla ya kufa. Lakini ni mara chache sana jambo kama hili linaweza kutokea katika nchi iliyostaarabika ya Ulaya na hivyo kama litokee basi titakuwa limesababishwa na uzembe wa hatari" (uk. 18).

Mhariri wa gazeti hilo anasema: Hali tunazoweza kuzitegemea katika kutoa ushahidi madhubuti wa jambo hili ni kama ifuatavyo:-

1. Kutokuwapo na pumzi na upitaji wa damu kwa uchache kwa muda wa SAA MOJA ambapo chombo cha kupimia pumzi kiwe kazini kwa muda wote huo (2) kupoaa pole pole kwa mwili, wakati ambapo mikono na miguu inaanza kupoaa na baadaye kufuatiwa na mwili mzima na (3) Kadiri mwili unavyopoa hali ya ugamu ianze mara moja kuvishambulia viungo vya mwili na hatimaye mwili mzima kwa kuifanya misuli inywee pamoja. Hali za namna hii zinapoonekana basi ushahidi wa kifo umekamilika.

Kwa kuzitumia kanuni hizi katika visa vya uhuishwaji viliviyotajwa hapo juu, kama visa hivi vingalitokea katika zama za hivi sasa tusingalisita hata kidogo kusema kwamba yule mvulana wa Ki-Shunamite alipotewa na fahamu kwa sababu ya kujikunja mgongo sana kutokana na ukali wa jua; vile vile tungalisema kwamba Eutychus allpotewa na fahamu kutokana na kishindo cha kuanguka kwake; wakadhaalika tungalisema kwamba binti yake Jairus alikuwa ameshikwa na uchovu uliotokana na maradhi yake. Ilikuwa ni wale watazamaji tu ambao kwa sababu ya ujinga wao, walidhani kwamba yule msichana alikuwa ameisha kufa na wakaanza kucheka na kumzomea yule mtu ambaye alikuwa na hakika kwamba yule msichana hakuwa amekufa bali alikuwa amelala. Yule mtu alitumia lugha hiyo hiyo kumhusu Lazaro, na aligeuza msemo wake pale tu alipoona ya kwamba wanafunzi wake hawaelewi anachosema. Ndipo akarahiisisha na kuwaambia kwamba “Lazaro amekufa”.

Je kuna jambo lolote ambalo litatufanya tusite kusema kisa hiki na vile visa vya mvulana wa Zarephath, na mwili uliotumbukizwa katika kaburi la Elisha na kile cha mvulana wa Nain na mvulana wa Dorcas ni matukio yanayodhihirisha hali inayoshabihiana na kifo au hali ya kuzimia? (uk 19 hadi 20).

Sasa tumo katika nafasi nzuri ya kulisogelea lile swalii ya kwamba je ni kweli kwamba Yesu alifia msalabani au la? Tukizichukua taarifa za Injilli kama zilivyo, tunakuta ya kwamba hazina kipimo au kanuni yo yote ambayo imetumika katika kutofautisha baina ya kifo cha kweli na kifo cha kudhania, au tuseme kile ambacho kinashabihiana na kifo cha kweli. Kulikuwa na haraka haraka katika kuupeleka mwili wa Yesu kwenye kaburi. Baada ya kuzimia msalabani ilichukua muda usiozidi masaa matatu shughuli zote za kumhifadhi pangoni (kaburini) zilikuwa zimekamilika. Hakufanyiwa uchunguzi wa kitabibu kwa mfano hakufanyiwa uchunguzi na chombo cha kupimia pumzi. Zaidi ya hayo hakuna utafiti uliyofanywa katika kuwadadisi wale waliokuwa naye kwa mara ya mwisho. Hatuna ushahidi wo wote uliotoka mdomoni mwa

Yusufu wa Arimathaya ambaye aliuweka mwili wa Yesu katika kaburi alilochonga shambani kwake. Hatuna ushahidi kwa Nikodemu ambaye anasemekana alishirikiana na Yusufu na kwamba yeye ndiye aliyetoa manukato, viungo na madawa ya kumponya Yesu (marahamu). Hatuna shahidi kutoka kwa mtunza bustani ambaye kwa hali ilivyo angekuwa shahidi wa maana sana. (uk. 20).

Hakuna tamshi lo lote linaloonyesha ni wakati gani alitoka nje ya lile kaburi. Kwa mara ya kwanza alionekana na mtu ambaye hakuhusika na yale ‘mazishi’ mapema alfajiri. Kama mtu ye yote atababaishwa na hili neno mazishi akadhania kwamba kwa vile Yesu alikuwa amefunikwa ndani ya kaburi hivyo hata kama alikuwa mzima hangeweza kubakia hai kwa kukosa hewa, napenda ieleweweke hapa kwamba lile kaburi lilikuwa namna ya chumba kilichochongwa ndani ya mwamba wa jiwe ambacho kilikuwa na mlango wake uliokuwa ukifunikwa kwa jiwe la ubapa liliokatwa katika sura ya mviringo. Kifuniko hiki kilikuwa kinabiringishwa na kukwamishwa katika vishikizo ambavyo vilichongwa tamthili ya komeo pembezoni mwa mlango. Kifuniko hiki kilikuwa kinasaki kwa namna ambayo haikuweza kuzuua hewa isiingie ndani ya chumba hicho. Lakini neno mazishi linaafikiana sana na maelezo ya kwamba alipata uhai baada ya kutibiwa na Yusufu na Nikodemu usiku wa siku ile aliyosulubiwa (uk.31).

Katika kitabu chake kiitwacho THE RESURRECTION AND MODERN THOUGHT (Ufufuo na fikra za kisasa), Dakta Aparrow Simpson amekwenda mbali zaidi katika utafiti anaposema kwamba:- “Katika kuamini kama tunavyoamini kwamba ushahidi wote wa pamoja umebainisha kwamba kaburi lilikuwa wazi, tafsiri ya ukweli huu ni lazima iwe moja ya mambo mawili: Imma hii ilikuwa ni kazi ya kibinadamu tu au ilikuwa kazi ya Mwenyezi Mungu. Yaani imma mikono ya binadamu iliiondoa maiti hiyo au Mwenyezi Mungu alimfufua. Hilo hasa ndilo suala letu (uk. 47).

Mimi ninathubutu kusema kwamba hili silo suala hasa. Kama hilo ndilo suala, sasa hali ingekuwaje iwapo ile iliyodhaniwa kuwa ni maiti ukawa ni mwili wenye uhai ambao hatimaye ukarudiwa na fahamu? Mimi ninasema kwa moyo mmoja ya kwamba tafsiri inayofaa na kutosheleza ni kukubali ya kwamba kaburi lilikuwa wazi, basi kwa sababu kwamba lilikuwa wazi hakuonyeshi hali ya aina yoyote wala mwujiza (uk. 25).

“Tukirudi nyuma katika uvumbuzi wa kurejea kwa uhai kama ilivyopendekezwa hapo juu ni nini inayoweza kuwa sababu ya kiakili ya matukio yaliyoelezwa hapo juu. Kabla Yesu aliyeihuishwa hajaondolewa ndani ya kaburi ni lazima pawepo na nguo. Kama mtunza bustani akisaidia katika mipango ya mazishi je haingekuwa jambo la kawaida kwake kwenda katika nyumba yake ambayo yamkini ilikuwa bustani au nje kidogo ya bustani na kuleta nguo zake rasmi ili zitumike wakati huu wa mahitaji? Hata kama asingelishughulika na mazishi hayo hata hivyo nyumba yake ndiyo ingeendewa kwanza katika kutafuta nguo wakati huu wa mahitaji ya dharura. Mara tu Yesu alipokuwa hajambo vya kutosha aliondolewa katika pango na kupelekwa katika nyumba ya mtunza bustani na kubakia hapo mpaka alipopelekwa mahali pa usalama zaidi (uk.32).

“Kwa hiyo inawezekana sana ya kwamba Yesu alikuwa bado hajatoka katika mazingira ya bustani ile wakati Maria Magdalena na yule mwanamke mwingine walipokuja pale bustanini mapema alfajiri. Ndiyo wakapokea maagizo kutoka kwa mtunza bustani au yumkini msaidizi wake (ambao baadaye visa vya uwongo vikawageuza na kuwaita malaika wawili), kwamba Yesu amefufuka na kwamba anatarajia kurejea Galilaya. Wanawake hao pia walipata nafasi ya kuonana naye baada ya kujulikana kuwa ni rafiki zake. (uk.33). Mwandishi huyo anaendelea kusema “kama mtu ye yote binafsi kutoka sehemu yoyote ile angejaribu kuinua sauti yake na kupinga (kile ambacho kinaaminiwa na wengi, yaani kwamba Yesu alifia msalabani), sauti yake hiyo ingemezwu na miguno na kelele za watu wengi. Hata kulikuwako na nyakati katika historia ya kanisa ambapo mtu wa namna hiyo alikabiliwa na hatari ya

kuuawa kwa kuchomwa moto siyo kama shahidi bali kama kafiri". (uk.34).

Mwandishi huyo kisha anajadili iwapo Yesu kwanza alienda Galilaya na kutoka pale ndipo akaenda Damascus na kujitokeza mbele ya Mtakatifu Paulo na kisha akaelekea Babylonia akiwa katika safari yake ya kwenda Mashariki. Mwishowe mwandishi huyu anaeleza imani yake mwenyewe kwa maneno yafuatayo:-

"Kwa upande wangu ninaridhika kabisa katika kuamini kwamba, kwa vile alikuwa Binadamu basi alipitia njia ile ile, 'Njia iliyo wazi na ya kutisha ambayo ndiyo kifo' ambacho binadamu wote ni lazima wakipitie". (uk.70).

Amehitimisha kitabu chake kwa maneno yafuatayo:-

"Ni lazima nirudie kusema ya kwamba hatujui alikofia. Inawezekana ya kwamba baada ya kuyahubiria makabila yaliyopotea ya nyumba ya Israel katika sehemu zile za mbali Yesu alifia Srinagar na akazikwa katika kaburi lenye jina lake hadi tarehe hii ya leo; inawezekana kabisa ya kwamba hakutoka nje ya maficho yake ya Galilaya, bali alikuwa kifo cha taabu kutohana na vidonda vyake alipokuwa kwenye kambi yake ya upweke kandokando ya ziwa Tiberia: au pengine alifia kwenye kilele cha mlima fulani au inawezekana alifia kwenye bonde fulani ambalo limefichama hivi kwamba, "Hakuna mtu anayejua liliko kaburi lake hadi hii leo". Sisi hatujui na ni jambo jema ya kwamba hatujui. Kwa sababu ya kutojua kwetu, kwa uchache Kanisa limeepushwa na ushirikina na kuyaabudu masalia ya mwili wake; na huko mahali kusikojulikana kunaweza kuelezwu vizuri kwa kutumia beti za mwisho za shairi zuri sana ambalo lilitungwa na mkewe Alexander kuhusu mahali alipozikwa Musa. Beti hizo zinasema:-

"Ewe kaburi la upweke

Zungumza na nyoyo zetu hizi  
Zinazotafuta kujua (ukweli)  
Na uzifundishe kuwa tulivu  
Mwenyezi Mungu ana miujiza ya Neema zake.  
Njia ambazo hatuwezi kuzijua  
Anazificha ndani sana, kama ule usingizi wa siri  
Wa yule ampendaye sana”,

### **SURA YA NNE**

### **USHAHIDI WA MAANDISHI YA KALE**

Mnamo mwaka 1907 Kampuni moja ya Chicago iitwayo THE CHICAGO INDO-AMERICAN BOOK COMPANY ilitangaza kitabu kimoja chini ya kichwa cha maneno “THE CRUCIFIXION BY AN EYE WITNESS” (Kusulubishwa kuliko shuhudiwa na shahidi wa macho). Ndani ya kitabu hiki mlikuwa na barua iliyogunduliwa mjini Alexandria katika nyumba iliyomilikiwa na kukaliwa na ushirika wa “Esseens”. Barua hiyo ilikuwa imeandikwa miaka; saba tu baada ya tukio la msalaba. Mwandishi wa barua hii alikuwa mwanachama maarufu wa ushirika wa udugu wa “Esseens” mjini Yerusalem. Alikuwa akiwaandikia wanachama wenzake waliokuwa wakiishi Alexandria. Barua hiyo ilikuwa jibu la barua iliyandikwa na kiongozi (Terapeut) wa Ushirika wa kidugu wa Esseens wenyewe makao yake Alexandria ambaye alikuwa anataka kujua ukweli hasa kuhusu uvumi waliousikia kuhusiana na Yesu na kifo chake cha kishahidi kwa vile wao walijua ya kwamba Yesu alikuwa mwanachama mwenzao na aliishi na kutenda sawa na kanuni za ushirika wao.

Barua hii inahakikisha ya kwamba Yesu alikuwa mwanachama wa Ushirika wa kidugu wa Esseens. Mwandishi wa barua hii aliwahakikisha wanachama wenzie mjini Alexandria akiwaambia, “Ninawaambieni yale mambo tu ambayo ninayajua na kuyaona kwa macho yangu mwenyewe na nimeyafuatia hatua kwa hatua na kushiriki katika kutekelezwa kwake. (uk. 38).

### **GIZA LINASHUKA ARDHINI**

Mwandishi huyu anatuambia yale yaliyotokea wakati Yesu alipotungikwa na kushushwa msalabani. Barua hiyo inasema kwamba wakati Yesu alipokuwa bado yungali msalabani, “Giza likatanda ardhini na watu wakarudi mjini Jerusalem. Ikiendelea inasema: “Yesu alita kwa sauti ya juu, kwa sababu ya maumivu makali aliyokuwa nayo na pale pale akataja wimbo wa ishirini na mbili na kuomba umsaidie kumtoa katika mateso (uk. 62).

## TETEMEKO LA ARDHI

Ikiendelea barua hiyo inasema: "Kidogo kidogo joto likaanza kuwa kali zaidi lisiloweza kuvumilika na ni kana kwamba moto ulikuwa unawaka hewani na ardхиni kwa jinsi ambayo ingeziyeyusha madini mbalimbali.

Kwa sababu ya elimu yao ya kanuni ya maumbile, wanachama wa ushirika wa kidugu wa Essens walijua ya kwamba tetemeko la ardhi lilikuwa linakuja kama vile ilivyotokea katika siku za mababu zetu. (uk. 62) "Usiku ulipokaribia ardhi ilianza kutikisika sana na Jemedari wa Kirumi aliogopeshwa sana hivi kwamba aliisujudia miungu yake ya kipagani. Wengi mionganoni mwa wale walioogopeshwa waliondoka pale mahali haraka haraka na kurudi Jerusalem. Na Jemedari huyo ambaye alikuwa mtu mashuhuri na mwenye tabia ya huruma alimruhusu Yohana ampeleke mama yake Yesu karibu ya msalaba." (uk.62).

"Alipokuwa akimwambia Yohana ampeleke mama yake Yesu kwenye msalaba ilikuwa bado kuna giza ingawaje mbalamwezi ingalikuwa imetoka. Kutoka katika Bahari ya damu kukaonekana ukungu mzito mwekundu- mwekundu. Milima iliyoko kandokando ya Yerusalem ikatikisika kwa nguvu sana na kichwa cha Yesu kikaangukia kifuanini mwake. Alipokoroma kwa mara, ya mwisho kwa sababu ya uchungu wa maumivu, na kufariki, sauti kali ya namna ya mluzi ikasikika hewani na Mayahudi wakashikwa na hofu kwa sababu waliamini kwamba pepo wabaya waliopo kati ya mbingu na ardhi walikuwa wanakuja kuwaadhibu watu. Sauti hiyo ngeni na ya ajabu hutokeea kabla tetemeko la ardhi halijatoke. Na kwa vile Mayahudi walichukulia habari hii kuwa iko zaidi ya uwezo wa binadamu, Jemedari wa Kirumi hakuwa na la kufanya isipokuwa kuamini kwamba Yesu ni mtakatifu na hana hatia. Ndipo akamliwaza mama yake Yesu kwa kusema:-

"Ndugu wapenzi mmetulaumu sisi kwa vile hatukutumia njia za siri ili kumwokoa rafiki yetu kutoka katika kifo cha msalaba. Lakini mimi

ninachoweza kuwakumbusha ni kwamba sheria takatifu za ushirika wetu zinatukataza kufanya mambo hadharani na vile vile zinatukataza kuingilia kati mambo ya kiserikali". (uk 66).

## **YUSUFU NA NIKODEMU**

Barua hiyo katika kufafanua zaidi jinsi Yusufu wa Arimathaya alivyomsaidia Yesu inasema: "Kulikuwa na mtu mmoja aitwaye kwa jina la Yusufu wa Arimathaya. Alikuwa tajiri, na kwa kuwa yeye alikuwa mjumbe wa baraza la madiwani aliheshimiwa sana na watu. Alikuwa mtu mwenye hekima na ingawaje hakutokea kuwa mwanachama wa chama cho chote, lakini kisirisiri alikuwa mwanachama wa ushirika wetu mtakatifu na aliishi sawa na kanuni ya sheria za ushirika huu. Rafiki yake aitwae Nikodemu alikuwa msomi wa hali ya juu naye alikuwa mionganoni mwa walioshika madaraka ya juu sana katika ushirika wetu. Alizijua siri za viongozi wetu (Terapeutas) na mara kwa mara alikuwa pamoa nasi. (uk.66)

Baada ya tetemeko la ardhi kupita na watu wengi wakiwa wameondoka Yusufu na Nikodemu walifika msalabani. Wakapewa habari za kifo cha yule aliyesulubiwa katika bustani ya ndugu yetu karibu ya Calvery. "Kwao lilionekana ni jambo la ajabu sana ya kwamba Yesu ambaye alibakia msalabani kwa muda usiofikia masaa saba awe tayari amekufa. Hawakuweza kulihamini jambo hili na haraka haraka wakaenda mahali pale. Pale wakamkuta Yohana peke yake." Yusufu na Nikodemu wakauchunguza mwili wa Yesu na baada ya kuridhika na yale waliyoyagundua, Nikodemu akamchukua Yusufu wakaenda faragha pembezoni kidogo na pale akamwambia, "Sawa na elimu yangu ya mambo ya uhai nina hakika kabisa ya kwamba inawezekana kumwokoa". (uk.67).

Nikodemu akasema kwa sauti kubwa, "Ni lazima tuupate mwili huu kabla mifupa yake haijavujwa, kwa sababu bado anaweza kuokolewa. Kisha, kwa kukumbuka kwamba yuko faraghani,

akaendelea kunong'ona. Kuokolewa asizikwe mazishi yasiyojulikana" (uk.68). Uamuzi wao huo ukabakia siri naye John hakumwambia lolote. "Akamshawishi Yusufu aziache kando kazi zake za binafsi ili ashiriki katika kumwokoa rafiki yao kwa kwenda kwa Pilato na kumbembeleza awaruhusu kuuchukua mwili wa Yesu usiku ule ule na kuuweka katika pango lililochongwa ndani ya mwamba wa jiwe janibu ya mahali aliposulubiwa. Pango hilo lilikuwa mali ya Yusufu. "Kwa kufahamu maana ya usemi wake, mimi nilibakia pamoja na Yohana ili kuulinda msalaba na kuwazuia maaskari wasivunje mifupa ya Yesu." (uk.68).

"Baraza la Mayahudi lilikuwa tayari limeshamtaka Pilato awatume maaskari kwenda kuivunja mifupa ya wale waliosulubiwa ili wapate kuzikwa". (uk. 69). Barua hiyo inaendelea kwamba mara tu baada ya Yusufu na Nikodemu kuondoka, tarishi alikuja na kumkabidhi mlinzi makaburi amri ya kumtaka awashushe waliosulubiwa" na kuwazika.

Mwandishi wa barua hii anasema kwamba, "Mara tu tarishi alipowasili nikamkimbilia kwa kutumaini kwamba Yusufu alikuwa tayari amesha onana na Pilato, jambo ambalo kwa hakika lilikuwa haliwezekani. (Ndipo nikamuuliza): "Je umetumwa na Pilato?" "Sikutumwa na Pilato bali nimetumwa na katibu ambaye hufanya kazi kwa niaba ya Gavana katika mashauri madogo madogo kama haya". "Yule mlinzi wa makaburi kwa kuona wasi wasi niliokuwa nao, akaniangalia, nami kwa njia ya kirafiki nikamwambia: "Umeona ya kwamba mtu huyu ambaye amesulubiwa si mtu wa kawaida usimtendee mabaya kwa sababu mtu mmoja ambaye ni tajiri mkubwa hivi sasa amekwenda kuonana na Pilato ili ampe pesa kwa kuugomboa mwili huu ili uende ukafanyiwe mazishi ya kiheshima"

"Ndugu zangu wapenzi, ni lazima niwajulisheni hapa kwamba Pilato mara kwa mara aliiua miili ya waliosulubiwa kwa rafiki zao ili wapate kuizika. Na mlinzi wa makaburi alinishughulikia kirafiki kwa vile kutokana na matokeo yote yeye alitambua kwamba Yesu hakuwa na hatia. Na kwa hiyo wakati wale wezi wawili waliopigwa na

maaskari kwa marungu makubwa na kuvunjwa mifupa yao, yule mlinzi wa makaburi alikwenda kwenye msalaba wa Yesu na kuwaambia maaskari, "Msiivunje mifupa yake kwa sababu amekwisha fariki". (uk.70).

Punde si punde tarishi mmoja kutoka kwa Pilato alimjia mlinzi wa makaburi na kumwambia "Pilato anataka kujua iwapo Yesu amekufa kweli". "Ni kweli" alisema mlinzi wa makaburi, "Kwa hiyo hatukuivunja mifupa yake". Ili kuhakikisha zaidi, mmoja wa maaskari alichoma mkuki wake kwenye ubavu wa mwili ule. Mwili ule haukushituka na hii ilichukuliwa na yule mlinzi wa makaburi kuwa dalili madhubuti ya kwamba alikuwa amekufa kweli. Ndipo akaondoka haraka haraka kwenda kuandika taarifa yake. Lakini damu ilitiririka kutoka katika jeraha lile la mkuki jambo ambalo lilimshangaza Yohana na wakati huo huo kuyazidisha matumaini yangu. (uk. 71).

## **PILATO ANAKABIDHI MWILI**

Ikizungumzia juu ya maombezi ya Yusufu na Nikodemu kwa Pilato barua hiyo inaarifu:-

"Yusufu na Nikodemu walirudi. Kwa sababu ya haiba yake, Yusufu alimwathiri Pilato, naye baaada ya kujulishwa kwamba waliosulubiwa wamekwisha kufa Pilato alimkabidhi Yusufu mwili wa Yesu bila ya malipo yo yote. Kwani Pilato alimheshimu sana Yusufu na kujuta kimoyomoyo juu ya hukumu iliyotolewa. Nikodemu alipoona kwamba lile jeraha la mkuki linatokwa na damu na maji, macho yake yakajawa na matumaini mapya na akazungumza kwa uchangamfu mwingi kwa sababu ya kujua kitakachotokea. Akamchukua Yusufu hatua kadhaa kutoka pale niliposimama na vile vile kitambo kidogo kutoka pale aliposimama Yohana na kuzungumza haraka haraka kwa sauti ya chini, "Rafiki mpenzi, furahia na sasa tuingie kazini. Yesu hajafa bado, anaonekana amekufa kwa sababu tu nguvu zake zimekwisha". Wakati Yusufu alipokuwa kwa Pilato mimi nikaenda

haraka haraka kwenye makao yetu na kuchukua mimea inayotumiwa katika tiba za namna hii. Lakini ninawatahadharisheni msimwambie Yohana kwamba tunatumaini kuhuisha mwili wa Yesu, asije akashindwa kuificha siri hii kwa sababu ya furaha. Na kwa hakika itakuwa hatari zaidi iwapo watu watajua mipango yetu hii kwa sababu ikijulikana basi maadui zetu watatuua sisi sote pamoja na huyu tunayetaka kumhuisha.”

## YESU APONYWA

Barua hiyo kisha inazungumzia juu ya hatua zilizochukuliwa katika kumhuisha na kumtibia Yesu. “Baada ya hayo wakaenda haraka haraka kwenye msalaba, na kulingana na maelezo ya tiba, wakamfungua taratibu zile kamba zilizofungiwa msalabani kisha wakang’oa misumari iliyopigiliwa mikononi mwake na halafu kwa uangalifu mwingi wakamlaza chini”. (uk. 73). Pale pale Nikodemu akatandaza manukato yenyeye nguvu sana pamoja na dawa za ponyo (Marahamu) kwenye vitambaa alivyoleta ambavyo matumizi yake yalijulikana na ushirika wetu tu. Akaviviringisha vitambaa hivi mwilini mwa Yesu akijifanya kwamba alikuwa anafanya hivyo ili kuzuia mwili ule usioze mpaka baada ya sikukuu (ya sabato) ndipo ataukausha na kuuzika. Viungo hivi pamoja na madawa mengine vilikuwa na uwezo mkubwa sana wa kuponyesha. Na vilitumiwa na ushirika wa kidugu wa Esennns ambao walijua kanuni za sayansi ya tiba kwa kurudisha fahamu za wale walioko katika hali ya kuzimia inayofanana na kifo. Na hata wakati Yusufu na Nikodemu walipokuwa wakiinamisha vichwa vyao juu ya uso wake na machozi yao kumdondokea, wakawa wanampulizia pumzi zao na kuzipasha joto sehemu zake za kichwa zilizo juu ya mashavu. (uk 74).

Kisha mwili huo ukalazwa kwenye pango lililo chongwa kwenye mwamba wa jiwe ambalo lilikuwa mali ya Yusufu. Kisha wakalifukiza lile pango kwa mvuke na moshi uliotoka katika majani ya miti na mimea mbalimbali ya kutia nguvu. Na wakati mwili ukiwa umelazwa kwenye kitanda cha majani katika hali ya ukakamavu na ufu,

wakaweka jiwe kubwa kwenye mlango wa pango ili ule mvuke usambae na kulijaza pango". (uk. 75).

## MAYAHUDI WANAPATA SHAKA

Barua hiyo inazidi kusema ya kwamba Kaifa, Kasisi Mkuu wa Mayahudi ambaye alikuwa na shauku ya kujua ni nani waliokuwa marafiki wa siri wa Yesu alipeleka wapelelezi wake kisirisiri. Alimtilia shaka Pilato kwa kumkabidhi Yusufu wa Arimathaya ule mwili bila ya malipo yo yote. Yusufu ambaye hapo awali hakujishughulisha kablsa na kesi hii ya Yesu lakini sasa ameitoa sehemu aliyatayarisha kwa ajili ya mazishi yake yeche mwenyewe na kumpa msulubiwa. (uk. 76).

Baada ya kujua kwamba wana nia ya kuukausha ule mwili kwa madawa, na kwa matumaini kwamba atagundua baadhi ya njia za siri za kumshitaki Yusufu na kumtia gerezani, Kaifa alituma kikundi cha maaskari usiku wa manane kwenda kujificha katika bonde lililofichana karibu ya pango ulimolazwa mwili wa Yesu. (uk.75).

Mwandishi wa barua hiyo anaendelea kusema "Wakati; huo huo mimi pamoja na Nikodemu tulienda haraka mpaka kwa washirika wenzetu na mzee mkubwa na mwenye hekima kuliko wote aliongoza kikao cha kuteua njia bora zaidi za kumhuisha Yesu. Na ndugu wote wakakubaliana mara moja kumpeleka mlinzi kule kwenye kaburi.

Baada ya saa sita usiku na kukaribia alfajiri ardhi ilianza kutetemeka tena na hali ya hewa ikawa mbaya ajabu. Miamba ikatetemeka na kupasuka. Miali myekundu ikatoka kwenye nyufa ikiumulika ukungu mwekundu wa alfajiri. Kwa hakika huu ulikuwa usiku wa kutisha. Wanyama waliogopeshwa na tetemeko hili na walikimbia kila upande huku wakilia. Wale walinzi wa Kasisi mkuu walishikwa na hofu nyingi sana kwa kusikia miluzi hewani na ngurumo na mtikisiko wa ardhi (uk. 77).

“Mmoja wa ndugu zetu alienda kaburini kwa kuamrishwa na ushirika wetu huku akiwa amevaa gwanda jeupe la daraja ya nne katika ngazi za ushirika wetu. Alienda kwa kutumia njia ya siri ambayo ilipita mlimani na kuelekea kaburini. Njia hiyo ilikuwa inajulikana na umoja wetu tu. Wakati ule walinzi waoga wa Kasisi mkuu walipomwona ndugu yetu amevaa gwanda jeupe na kuteremka pole pole toka mlimani huku akiwa haonekani vema kwa sababu ya ukungu wa asubuhi, wakashikwa na hofu nydingi kwa kudhani kwamba malaika alikuwa akishuka toka mlimani.

“Wakati ndugu yetu alipofika kwenye kaburi aliyotakiwa ailinde, akakaa juu ya jiwe ambalo aliliondoa kwenye mlango wa pango sawa na alivyoagizwa. Ndipo wale maaskari wakakimbia na kusambaza taarifa kwamba malaika amewafukuza. (uk.78).

## **NDANI YA PANGO**

Kisha mwandishi wa kitabu hiki ameeleza juu ya yale yaliyotokea ndani ya kaburi walimouweka mwili wa Yesu.

“Masaa thelathini yalikuwa yameshapita baada ya kile kilichodhaniwa kuwa ni kifo cha Yesu. Na baaada ya kusikia sauti ndogo ndani ya pango yule ndugu yetu akaingia na kuangalia nini kimetokea. Kwa furaha isiyokadirika akaona ya kwamba midomo ya ule mwili ilikuwa inatikisika na kwamba ule mwili ulikuwa unapumua. Ndipo akaenda mara moja na kuanza kumsaidia Yesu ambapo akasikia sauti ndogo ndogo kutoka katika kifua chake. Uso wake ukarejewa na hali ya uzima na macho yake yakafunguka na kwa mshangao mkubwa yakamwajabia mwanachama mpya wa ushirika wetu.

Mambo haya yalitokea mara tu mimi pamoja na ndugu yetu wa daraja la kwanza na Yusufu tulipokuwa tunatoka kwenye kikao chetu. Yusufu alikuja kutafuta ushauri wa kusaidia”. (uk.79).

Nikodemus ambaye alikuwa tabibu mwenye uzoefu wa kazi alisema tulipokuwa njiani kwamba hali ya hewa ya aina ya pekee ambayo imeletwa na mabadiliko ya hali ya chembe mbalimbali za hewa, ni ya manufaa sana kwa Yesu na kwamba hakuwa anaamini kwamba Yesu alikuwa amekufa kweli. Na zaidi ya hayo akasema kwamba ile damu na maji ambavyo vilitoka ndani ya jeraha la mkuki ni dalili madhubuti ya kwamba uhai ulikuwa bado haujakatika. Tukiwa bado tunazungumza tukafika kwenye pango. Yusufu na Nikodemus ndiyo waliotangulia. Kwa jumla tulikuwa ndugu ishirini na wanne wa daraja la kwanza la ushirika wetu.

Tulipoingia tukamwona yule mwanachama wetu mpya akiwa amevaa gwanda jeupe akiwa amepiga magoti juu ya majani yaliyotandazwa kwenye sakafu ya pango huku akiwa amekikumbatia kichwa cha Yesu aliyeuhuishwa kifuani mwake.

Na alipowatambua marafiki zake wa ushirika wa Essenns macho ya Yesu yakaangaza kwa furaha kubwa. Mashavu yake yalikuwa na athari ya wekundu naye akasimama na kuuliza, "Niko wapi hapa?" Kisha Yusufu akamkumbatia na kumuegesha mikononi mwake na kumueleza jinsi mambo yote yalivyotokea na jinsi alivyookolewa kutoka katika kifo dhahiri kutokana na kuzimia kwa hali ya juu ambako maaskari wa Calvary walidhania ni kifo". (uk. 80).

"Na Yesu akashangaa na kujipapasa papasa mwilini mwake na huku akimsifu Mwenyezi Mungu akalia akiwa kifuani mwa Yusufu. Kisha Nikodemus akamtaka rafiki yake anywe baadhi ya viburudisho na akala tende kidogo na mkate uliochovywa asali. Na Nikodemus akampa divai anywe na baada ya hayo Yesu akawa amechangamka vya kutosha hivi kwamba aliweza kusimama mwenyewe.

Ndipo akatambua kwamba kumbe ana vidonda mikononi na ubavuni. Lakini ile dawa ambayo Nikodemus ameipaka kwenye vidonda hivyo

ilikuwa na athari ya kulainisha ngozi na vikawa tayari vimeshaanza kunywea.

## **YESU ANATOROKA PANGONI**

Barua hiyo inaendelea kusimulia jinsi Yesu alivyotoroshwa kutoka katika kaburi lile. Inasema, “Baada ya vile vitambaa vilivyoviringishwa mwilini mwake kuondolewa na ‘bandeji’ lake la kichwani kuondolewa, Yusufu akazungumza na kusema, “Hapa siyo mahali pa kubakia kwa muda mrefu, kwani maadui wanaweza kutungundua kwa urahisi na kutusaliti.” Lakini Yesu alikuwa bado hajakakamaa vema kiasi cha kumwezesha kutembea mwenyewe na kufika mbali. Hivyo akaongozwa mpaka kwenye nyumba ya Ushirika wetu ambayo ilikuwa janibu ya Calvary kwenye shamba ambalo pia ni mali ya ndugu yetu mmoja. (uk. 81).

Kijana mwingine wa Ushirika wetu wa kidugu alitumwa mara moja kwenda kumsaidia yule mwanachama mpya ambaye alikuwa akilipekua kaburi la Yesu ili kuokota na kuficha kila alama ya vitambaa alivyoviringishwa au dawa alizotumia.

Alipowasili kwenye nyumba ya huyo ndugu yetu, Yesu alikuwa dhaifu na mnyonge. Kidonda chake kilianza kuuma. Alishangazwa sana na akahesabu kwamba huu ni mwujiza mkubwa. “Mungu Amenihuisha” akasema ili kwa njia yangu, ahakikishe yale ambayo nimeyafundisha, nami nitawaonyesha wanafunzi wangu kwamba ningali mzima”. (uk. 82).

## **YESU ANAKUTANA NA WANAFUNZI**

Barua hiyo inazidi kutuambia ya kwamba marafiki wa ushirika wa Essenns walichukua kila namna ya tahadhari na uangalifu kwa ajili ya usalama wake na wakamsaidia kwa kila njia ili aweze kukutana na wanafunzi wake mjini Jerusalem, katika bonde la Messeda, katika nyumba ya Lazaro mjini Bethania, Galilaya, kwenye Mlima

Karmel na katika sehemu zingine ambako alitoa hotuba za kuwatia moyo katika imani na kazi zao. Hotuba zake pamoja na mazungumzo yake na zile habari kwamba ye ye bado yungali mzima zimetia wasiwasi mwangi mi ngom mwa watu.

## MAYAHUDI WATAHADHARISHWA

Kutokana na barua hii ni dhahiri ya kwamba ile shaka ya Mayahudi kwamba Yesu ameepukana na kifo cha msalabani ilithibitishwa na hivyo wakaanzisha juhudhi mpya za kutaka kumwua. Kuhusiana na habari hii barua hiyo inasema: “Siku moja Nikodemu alikuja kwenye makao ya umoja wetu na akatupasha habari kwamba Yusufu wa Arimathaya amekamatwa na kwamba Mayahudi wanamsingizia kuwa anahuksika na makosa ya jinai kwa vile alishirikiana na Yesu kisirisiri.” (uk. 110).

Baadaye Yusufu alitolewa gerezani kwa juhudhi za Umoja wetu mtakatifu tawi la mjini Yerusalem. Wakati Yesu alipokuwa katika bonde la mlima Karmel, “umoja wetu ulimuonya Yesu juu ya hatari ili yokuwa inamkabili ili aepukane na maadui zake na kukamilisha ujumbe wake. Kwa sababu watu wa umoja wetu walikuwa wamepata taarifa kwa njia siri kwamba mtu mmoja aitwae Kayafa alidhamiria kwenda kisirisiri na kumkamata na kumwua Yesu kwa sababu aliamini kwamba Yesu ni mdanganyifu”. (uk. 118).

“Na Yusufu alizungumza na Yesu akimwambia, ‘Je unajua kwamba watu ambao hawana elimu hata kidogo juu ya itikadi yako, wanashauriana juu ya kukutangaza wewe kuwa mfalme wa dunia na kuwafukuzilia mbali Warumi? Lakini ninakuomba usiuchafue ufalme wa Mungu kwa vita na ghasia. Kwa hiyo afadhali uchague njia ya upweke. Kaa pamoja na marafiki zako wa umoja wa Essenns ili upate kusalimika na ili itikadi yako itangazwe na wanafunzi wako. (uk. 150) “Na Yesu akaafikiana na shauri hili ya kwamba ye ye atakaa upweke” (uk. 121).

## **YESU ANAJIFANYA MKIMBIZI**

Barua hiyo inazidi kutueleza kwamba mara ya mwisho Yesu alipokutana na wanafunzi wake, alifuatana nao kwenye sehemu aipendayo sana, karibu na kilele cha Mlima wa Mizeituni ambapo mtu akiwa pale anaweza kuiona takriban nchi nzima ya Palestina kwani Yesu alitamani kwa mara ya mwisho kuiona ile nchi ambapo aliishi na kufanya kazi". (uk. 153).

Na wale wanafunzi wateule waliamini kwamba Yesu atafuatana nao kwenda Bethania. Lakini wazee wa Umoja wa Essenns walikuwa wamejikusanya kimyakimya upande mwingine wa mlima ule, wakiwa wamejiweka tayari na kumsubiri Yesu wasafiri pamoja naye kama walivyokubaliana".

"Na akawahimiza wanafunzi wake wawe na furaha na wasimame imara juu ya imani yao. Aliwaombea marafiki zake ambao alikuwa aachane nao muda mfupi ujao. Ndipo akainua mikono yake na kuwabariki. Na ukungu ukawa umetanda kuuzunguka mlima. Ukungu huo ulikuwa umechanganyika na mionzi ya jua lililokuwa likichomoza.

Kisha wazee wa udugu wa Essenn wakamletea taarifa Yesu wakimwambia kwamba wao walikuwa wakimngojea na kwamba sawa na mipango yao, walikuwa wamesha chelewa sana. Wanafunzi wake walipokuwa wamepiga magoti nyuso zao zilikuwa zimeinamishwa ardhini. Ndipo Yesu akasimama na kuondoka haraka haraka na kupotea ndani ya ukungu uliokuwa umetanda. Wakati ule wanafunzi walipoinua nyuso zao wakajikuta mbele yao wamesimama watu wawili wa ushirika wetu ambao walikuwa wamevaa magwanda meupe ya udugu wetu. Wale ndugu wawili wakawaambia wanafunzi kwamba hakuna haja ya kumngojea Yesu kwa sababu ameshaondoka. Ndipo wale wanafunzi wakateremka haraka haraka chini ya mlima". (uk. 124).

“Lakini kutoweka kwa Yesu kuliwajaza wanafunzi wake matumaini na ujasiri mpya kwa sababu sasa walijua kwamba kazi ya kutangaza neno la Yesu ni yao wao wenye kwa vile mpenzi wao Yesu hatarudi tena. Lakini mjini Yerusalem kukazuka uvumi kwamba Yesu amechukuliwa na wingu na amekwenda mbinguni. Uvumi huu ulizushwa na watu ambao hawakuwapo wakati Yesu alipoondoka. Wale wanafunzi wake hawakuukanusha uvumi huu kwa sababu ulisaidia katika kuitilia nguvu itikadi yao na kuwarubuni watu ambao walitaka aonyeshe mwujiza kabla hawajamwamini”. (uk. 125).

## **NI MFU MACHONI PA ULIMWENGU**

Sehemu ya mwisho ya barua hii kimsingi inaashiria kwenye habari za mpango uliofanywa ili kutuliza wasiwasi na mashaka waliyokuwa nayo Wayahudi ili kuhakikisha kwamba Yesu anaondoka kwa usalama katika nchi ile na kuhamia katika nchi nyingine.

Maneno ya mwisho ya barua hiyo kumhusu Yesu yanaonyesha kwamba ni Yusufu na Nikodemu tu ndiyo waliowahi kukutana naye mara tatu mahali alikokuwa akijificha. Mara yao ya mwisho ilikuwa siku ya sita baada ya mwezi kuwa duara na ilikuwa wakati ambapo mwezi huo ulikuwa ukififia kwa ajili ya mwangaza wa asubuhi. “Walikuja kwenye makao makuu ya Ushirika wetu wakiwa na nyuso zenye huzuni kwani mteule aliwa amechukuliwa kwenda mbinguni kwa Baba. Naye aliquwa amezikwa na yule daktari janibu ya Bahari ya Maiti. (uk. 128).

Kulingana na barua hii, wakati Yesu alipokuwa Anang’ang’ania kupita mitaani na kuwaambia watu kwamba Mwenyezi Mungu amemwokoa, Udugu wa Essenn ulimwambia: “Wewe huko salama katika nchi hii, kwa sababu wao wanakusaka. Kwa hiyo kamwe usiende ukifundisha mionganoni mwa watu, kwani yale ambayo umekwisha yafundisha yatadumu milele mionganoni mwa marafiki zako na wanafunzi wako watayatangaza ulimwenguni. Tunakuomba ubakie hivyo ukijulikana

machoni pa ulimwengu kwamba umekufa ilihali ungali hai ukifunikwa na pazia la upweke, hekima na wema ambao haujulikani ulimwenguni kote”. (Uk. 92).

Hali ya mambo ilivyokuwa wakati ule inaafikiana kabisa na mpango huo. Kwa hiyo ikaamuliwa kwamba Yesu abakie hivyo hivyo “amekufa machoni pa ulimwengu”. Kulingana na barua hiyo inaelekea kwamba mwandishi wa barua hiyo hakukishuhudia kifo wala mazishi ya Yesu.

Ilikuwa ni uvumi tu ambao hapana shaka ulienezwu na Yusufu na Nikodemus kama ilivyopangwa ya kwamba Yesu abakie “amekufa machoni pa ulimwengu” ili maadui zake wasianze kumtafuta. Na kama tamshi hili kuhusu kufariki na kuzikwa kwa Yesu lingalikuwa la kweli, basi bila shaka alama za kaburi lake zingalionekana janibu ya Bahari ya Maiti katika karne zilizopita. Kwa vyo vyote ni dhahiri kulingana na barua hii, ya kwamba Yesu hakufa msalabani.

## **MAONI YA MFASIRI WA KIJERUMANI**

Katika maneno yake ya mwisho mfasihi huyo wa Kijerumani anasema: “Barua hii ina mambo mengi sana ya kupendeza ambayo yanafanana na maelezo yaliyotolewa na Injili, na mwandishi wake hakushawishiwa na jambo lo lote katika kuyaratibu vizuri sana kwa njia nyepesi isiyokuwa ya kutaharuki hata kidogo” (uk. 133).

“Lakini jambo la muhimu zaidi ni yale maelezo machache ambayo yanaelezea jinsi Yesu alivyoteswa katika msalaba na jinsi alivyojaribu kijiokoa. Injili zinatuambia kwamba kwa hakika Yesu alifia msalabani, na kwa hiyo zinadai kwamba kupona kwake ni mwujiza, ambapo mtu mwenye akili timamu hauhesabu huo kuwa ni mwujiza bali hekaya tu na kutokana na hekaya hiyo anatofautisha maana ya kweli ya kisa chenyewe na ile iliyobuniwa na watu. Lakini katika

barua hii tunaambiwa vile hasa mambo yalivyotokea kwa njia nyepesi sana ambayo imefanya matukio yaliyoelezwa yaonekane kuwa ni kweli yalitokea, na sawa na hali ya mambo hayo yalitokea". (uk.140).

Katika barua hiyo ya zamani imearifiwa ya kwamba hakufa msalabani inabainisha uwezekano mkubwa wa yeze kuwa hai. Kwanza, yeze alipotewa na fahamu mapema sana hivi kwamba hata Pilato alikitilia mashaka kifo chake. Pili, sawa na utaratibu uliotumiwa wakati ule katika kuwasulubisha watu, halikuwa jambo la ajabu kwa mtu aliyesulubiwa kurejewa na fahamu. (uk. 141). Pia tunajulishwa na wanahistoria wa zama zile ya kwamba halikuwa jambo la ajabu kwa mtu aliyesulubiwa kupata fahamu tena baada ya kushushwa msalabani. Pia imehakikisha kwamba mionganoni mwa hawa wasulubiwa kulikuwako na wale ambao hawakuwa na ile mila ya Kiyahudi iliyokataza wasulubiwa kuning'inizwa misalabani usiku kucha. Mara nyingi wasulubiwa wa namna hii walining'inia juu ya misalaba kwa muda wa siku nane hadi tisa usiku na mchana ndipo hatimaye kifo kiliyaondoa mateso yao makali sana. Tunapozichunguza taratibu zilizotumiwa katika kumsulubisha Yesu, tunalazimika kukubali ya kwamba haikuwa jambo lisilowezekana kwa uhai kubakia mwilini mwake kwa muda mrefu". (uk.142).

## **SURA YA TANO**

### **UVUMBUZI WA HIVI KARIBUNI**

### **SANDA YA YESU**

## **WANASAYANSI WA KIJERUMANI WANAFANYA UVUMBUZI WA KUSHANGAZA**

Ile nguo ambayo iliviringishwa juu ya mwili wa Yesu ilionekana katika pango alimohifandhiwa baada ya mateso ya msalabani (Yohana 20:5). Nguo hii bado imehifadhiwa. Inazo alama za mwili wa Yesu zilizotokana na marahamu yaliyopakwa katika mwili wake.

Hivi karibuni kikundi cha wanasayansi wa Kijerumani kimebainisha mambo ya muhimu sana kuhusu shuka hii ya Yesu. Wameonyesha ya kwamba Yesu Kristo hakufia msalabani. Alishushwa yungali hai akiwa amezimia sana au akiwa amepigwa ganzi nzito sana. Wakati Maria Magdalena alipokwenda kule pangoni Yesu alikuwa amesharudiwa na fahamu na akajifananisha na mtunza bustani ili asikamatwe. Hivyo basi, kujitokeza kwake tena ardhini hakukuwa ufufuo bali ni kurejewa na fahamu baada ya kuzimia.

Gazeti moja la Scandinavia liitwalo STOCKHOLM TIDININGERN lilitanganza makala ya maana sana ambayo iliandikwa na mhariri wake Bwana Christer Inderlumd kuhusu suala hili katika toleo la tarehe 2 April 1957. Tafsiri ya Kiurdu ya makala hiyo imekwisha tangazwa na Sadr Anjuman Ahmadiyya, Rabwah, Pakistan chini ya kichwa cha maneno HAZRAT MASIH NASERI SALEEB PAR HARGIZ FAUT NAHEEN HU'AY<sup>a</sup>. Nachukua nafasi hii na kuifasiri makala hiyo kama ifuatavyo:-

- 
- a. Makala hii iliandikwa na Bi Ulfat Qazi na kutangazwa katika gazeti la "Review of Religions" la June 1958.

### **JE KRISTO KAFIA MSALABANI?**

Kikundi cha wanasayansi wa Kijerumani kilikuwa kinafanya utafiti kuhusu sanda ya Yesu kwa muda wa miaka minane iliyopita. Matokeo ya utafiti wao yametolewa hivi karibuni katika vyombo vya habari. Ile shuka aliyofunikwa Yesu ambayo umri wake ni miaka elfu mbili imegunduliwa katika mji mmoja wa Italia uitwao Turin. Shuka hiyo ina athari za picha ya mwili wa Yesu. "Wanasayansi

hao wamemwarifu Baba Mtakatifu kuhusu uvumbuzi huu. Lakini Baba Mtakatifu hajasema lolote.

Uvumbuzi huu umeifichua siri kubwa ya historia ya kidini ya Kanisa Katoliki. Kwa msaada wa sanaa ya upigaji picha wanasayansi hawa wamejaribu kuhakikisha kwamba ule ufufuo ambao watu walihu hesabu kuwa ni mwujiza kwa muda wa miaka elfu mbili iliyopita, kwa hakika yalikuwa ni matokeo ya kawaida ya utendaji kazi wa mwili wa binadamu au tuseme wa viumbe vyote vyenye uhai. Wamekubaliana kwa pamoja kwamba Kristo hakufia msalabani. Suala la sanda ya Yesu limekuwa likijadiliwa tangu miaka elfu moja iliyopita. Shuka hii ilipelekwa mjini Constantinople mnamo mwaka 438 kwa kalenda ya Kikristo. Aliyeipeleka huko ni Malkia Endoxi. Mara ya kwanza kabisa shuka hii ilionekana karibu ya makaburi. Ilibakia mjini Constantinople kwa muda wa miaka mia saba. Hatimaye mtu mmoja aitwae De La Roche aliondoka nayo baada ya mji wa Constantinople kushambuliwa. Wakati moto ulioziunguza nyumba za mji huo, shuka hiyo ilikuwa ndani ya sanduku la fedha. Kwa sababu ya kuyeyuka kwa sanduku hilo la fedha shuka hiyo ikafifia kidogo. Hata hivyo zile alama za mwili wa Yesu zilikuwa bado zinaonekana”.

“Watu wa Ufaransa walipata pesa nyingi sana kwa kuifanyia maonyesho nguo hii. Kutoka Ufaransa shuka hiyo ikapelekwa Turin na ilipofika hapo ikawa inaonyeshwa hadharani baada ya kila miaka thelathini na tatu. Mnamo mwaka 1898 kwa tarehe za Kikristo mwanasheria mmoja wa Kiitalia aliuelekeza ukanda uliotumiwa kuijiga picha shuka hii kwenye mwangaza wa juu na akauangalia. Alishituka kuona kwamba ukanda ule ulikuwa na picha inayoshabihiana kwa kila hali na Yesu Kristo. Wakati picha ilipochapishwa kutokana na ukanda huo, ilionyesha uso wa mtu huyu (Yesu) ambaye hakuna aliyewahi kumwona tangu miaka 1900 iliyopita. Mnamo mwaka 1931 kwa tarehe za Kikristo nguo hiyo ilionyesha tena hadharani, na mpiga picha mmoja aitwae Guisepe Enric aliipiga picha tena nguo hiyo kwa kutumia vishubaka vyatya umeme wenye nguvu ya volti 6,000 na 20,000 na wakati shughuli hii ikifanyika

alikuwepo mtu mmoja ambaye ana cheo cha juu katika kanisa. Picha hii imefichua ukweli wenyewe kutia hamasa katika akili ya mtu na kwa mara ya pili imedhihirisha kile ambacho mpiga picha wa kwanza aitwae Pia alikionyesha. Picha hiyo inashabihiana sana na michoro ya kuigiza ya uso na mwili wa Yesu ambayo wanasanaa wa Kikristo walikuwa wakituonyesha kwa muda wa miaka elfu mbili iliyopita.

“Mtu anapoangalia ile picha ambayo imechapishwa ndani ya kitabu kiitwacho DAS LINNEN KURT BERNAAT TUL TGART kilichotungwa na Hanas Naber Verlag, anaweza kuelewa Kanisa litajisikiaje kwa kuiona picha hii. Baba Mtakatifu Pius wa 9 alikuwa na maoni haya:-


“PICHA HII HAIKUTENGENEZWA KWA MKONO WA BINADAMU YE YOTE” Wanasayansi hao wametangaza ya kwamba shuka hiyo pamoja na historia vyote vinathibitisha ya kwamba picha hiyo ni ya Kristo. Utengenezaji pamoja na mfumo wa nyuzi unaonyesha ya kwamba ni namna ya shuka zilizokuwa zinapatikana mahali paitwapo Pompii. Kuonekana kwa picha mbili za mwili wa Yesu katika shuka hiyo kunaonyesha ya kwamba nusu ya shuka hiyo ilitumiwa kwa kufunika kichwa chake. Marahamu yaliyopakwa mwilini mwake pamoja na lile joto la mwili ndivyo vimewezesha athari ya picha ya mwili wa Kristo ichapishwe katika shuka ile. Damu yenye uhai ya Yesu Kristo ambayo ilinyonywa na nguo hiyo vile vile iliachaa alama katika shuka hiyo. Picha hiyo inaonyesha waziwazi alama za taji la miiba chini ya kichwa na kwenye paji la uso wa Kristo na shavu lililovimba. Na alama ya jeraha la mkuki kwenye ubavu wa kulia. Alama ya matone ya damu yaliyochuruzika kutoka katika jeraha hilo pamoja na majeraha ya misumari na vile vile alama za majeraha ya mgongoni yaliyosababishwa na msuguano kati ya mgongo wake na lile bao la msalaba. Lakini jambo la kushangaza zaidi ni kwamba katika ule ukanda wa kupigia picha, macho mawili ya Yesu ambayo yalikuwa yamefumba yanaonekana kana kwamba yako wazi.

“Picha hii inabainisha pia kwamba ile misumari haikupigiliwa katika viganja bali kwenye maungio ya viganja. Jambo lingine


linalobainishwa ni kwamba ule mkuki haukuugusa moyo wa Yesu. Bibilia inasema kwamba KRISTO ALIKATA ROHO, lakini wanasayansi hao wanasisitiza kwamba moyo wa Yesu haukuacha kufanya kazi hata mara moja.

“Pia inahojiwa ya kwamba kama Kristo angalibakia bila ya uhai kwa muda wa saa moja juu ya msalaba, damu yake ingeganda na kukauka. Kwa hiyo matone ya damu yasingalipatikana katika shuka ile. Lakini kwa vile damu ilisambaa katika shuka ile hii inaonyesha ya kwamba Kristo alikuwa hai aliposhushwa msalabani.” Ninaweza kuongeza hapa kwa uvumbuzi huu wenyewe kutia hamasa ambaou umefanywa na wanasayansi hawa wa Kijerumani, unathibitisha tu yale ambayo yalisemwa na Kurani Tukufu karne kumi na nne zilizopita. Kurani Tukufu inatangaza ya kwamba Yesu hakufia msalabani.

“Na kusema kwao (Mayahudi) Hakika sisi tumemwua Masihi Isa mwana wa Mariamu Mtume wa Mungu; ambapo kwa hakika hawakumwua wala hawakumfisha msalabani isipokuwa tu alifanywa aonekane machoni pao kana kwamba AMEKUFA MSALABANI (ni jambo la uwongo); na wale wanaohitalafiana (na wasemao kweli) kuhusu jambo hili, kwa hakika wamo katika hali ya mashaka mashaka: hawana elimu kamili kuhusu jambo lenyewe ila wanafuata dhana tu, na kwa vyo vyote iwavyo hawawezi kuifanya dhana yao iwe kweli. (Kurani Tukufu 4: 158).



*Sura ya Yesu jinsi ionekanavyo ndani ya ‘Sanda’.*



Nadharia  
akarejew

baadaye  
aka 1928

Maulana A. R. Dard ambaye ndiye aliyekuwa mhariri wa "The Review of Regions alizandikia misken za Kikristo, Wataalalatu ha wakufunzi wa elimu ya eklezia Katika kutafuta maoni yao kuhusu nadharia hii. Wamisionari wa Kikristo walimjibu kwamba wao wanaipuuza nadharia hii ya kuzimia. Wengine wakaungama wazi kwamba wao

hawajui lo lote kuhusu nadharia hii. Baada ya kuyanakili majibu yao mhariri huyo anasema:

“Kutokana na majibu haya ni dhahiri shahiri ya kwamba nadharia hii haikupuuzwa moja kwa moja. Kwa upande mwingine wao wanakubali ya kwamba nadharia imepokelewa kwa shinikizo zaidi siku hizi. Askofu wa Birmingham ameshindwa kusema iwapo nadharia hii ya kuzimia imepuuzwa moja kwa moja na wataalam wote wasio na upendeleo. Canon Street anasema kwamba wazo hili limefulufiwa ndani ya kitabu kiitwacho “THE BROOK KERITH”. Na Askofu wa Durham ambaye ni mmoja wapo mionganini mwa wataalamu wanaotumainiwa sana na Kanisa la Uingereza hakusita kusema kwamba, “ni sawa kidogo kusema kwamba nadharia ya kuzimia inayoeleza juu ya masimulizi ya Injili kuhusu kufufuka kwa Kristo imepuuzwa.” Maoni kama haya yamerudiwa katika kitabu Kilichotangazwa wiki mbili au tatu zilizopita kiitwacho “PAGANISM IN OUR CHRISTIANITY” (upagani ndani ya ukristo wetu) ambacho kimetungwa na A. Weigall.

Achilia mbali waungaji mkono shupavu wa nadharia hii ya kuzimia kama vile Paulus, Venturini, Bahrdut, na Schleiemacher,<sup>a</sup> tunaweza kutaja vitabu viwili zaidi ambavyo vimetangazwa hivi karibuni katika bara hili:-

1. “DIG HESYS OA JIREST?” Kilichotungwa na Dakta Hugo Toll (Stockholm).
2. “DE PROCESS DE JESUS” Kilichotungwa na M. Paul Roue (Paris).

Kisha kipo kile kitabu cha maana kuliko vyote hivi kiitwacho “THE CRUCIFIXION OF JESUS, BY AN EYE WITNESS” Kilichotangazwa mjini Los Angeles mnamo mwaka 1919 ambacho kimetoa maelezo yenye kudhihirisha picha halisi ya mambo yote yalivyotokea.<sup>b</sup>

---

- a. Tazama kitabu kiitwacho "The Quest of the Historical Jesus cha Albert Schweitzer, kilichofasiriwa na W. Montgomery, London, 1910.
- b. Tazama gazeti "Review of Religions," No.9 1958.

Hapa chini nayanakili maoni ya Dakta Hugo Toll aliye tabibu mashuhuri sana nchini Sweden kama valiyotolewa katika gazeti la "The Review of Religions" ameayaandika katika kitabu chake **"DOG YESESPÅKÖRSET?** Ni kama ifuatavyo:-

Kusulubu ni kitendo ambacho kilienea sana zamani za kale kabla ya zama za Yesu na Warumi walikitumia kitendo hiki mara kwa mara. Wao hawakupenda kuwaua walaaniwa wao mara moja bali kwa njia ya kusulubisha ambayo ni ya mateso yenye kuchukua muda mrefu. Lilikuwa ni jambo la kawaida na la kufurahisha kuwaangalia watu wakisulubiwa. Hapakuwa na utaratibu wo wote uliowekwa katika kuwasulubu walaaniwa wao kwa njia yo yote waipendayo. Mara nyiningine waliwafunga wasulubiwa wao kwa kamba tu na mara nyiningine waliwafunga mikono yao tu. Wasulubiwa walipata maumivu ya kimwili na pia ya kiakili na jambo bayo zaidi ni kwamba wasulubiwa walikuwa wakifedheheshwa. Warumi walikuwa na tabia ya kuwasulubu watumwa na watu wa hali ya chini na pia watendaji wa makosa ya jinai, wasaliti na wahaini. "Yumkini Yesu alining'inizwa msalabani akiwa uchi. Na wakati ule yalikuwa ni majira ya baridi ya mwaka (Yohana 18:18). Kabla ya kumsulubisha walimpa Yesu kitu fulani anywe. Hatujui vema kilikuwa kitu gani ni mchanganyiko wa divai na nyongo au ni mchanganyiko wa divai na utomvu.

of Religions" lilitotajwa hapo juu. Kama asemavyo Mhariri wa "Review of Religions" huyu Dakta Hugo ni mtu mwenye umri wa miaka 70 (mnamo 1929) na amekuwa mfawidhi wa Hospital ya Stockholm tangu 1897 hadi 1923. Daktari huyo mwenye elimu ya juu sana anahakikisha kitabibu kwamba Yesu hakufia msalabani. Tafsiri ya yale ambayo Dakta

Alipoonja akakataa kunywa. (Matayo 27:34). Wakati koo linaponywea kwa sababu ya maumivu, mtu hawezi kumeza kitu. Wakati watu wanapopata maumivu ya kiakili au ya kimwili mara nyingi wanaomba maji ili wanywe, lakini wanapopewa wanajikuta ya kwamba hawawezi kuyanywa. Jambo hili pia linaweza kuwa ushahidi ya kwamba mishipa yake ya fahamu ilidhoofika kwa muda mchache. (Matayo 27:50) anasema kwamba Yesu alilia “kwa sauti kubwa” na akakata roho (Mkazo upo kwenye neno ‘Kubwa’). Yule mlinzi wa makaburi alizingatia ukweli huu. Alijua, pengine kwa sababu ya uzoefu wake wa kazi kwamba kwa kawaida watu hawafi kwa kutoa sauti kubwa basi ni dhahiri ya kwamba alikuwa bado anayo nguvu kidogo mwilini mwake. Katika masimulizi ya Yohana ametaja matukio yenyenye kupendeza sana kwa ajili ya daktari, kwa sababu ni mambo ya kweli kabisa na yanabainisha dalili ya kupatwa na mshituko wa moyo na kuzimia. Sababu ya kawaida ya kuzimia ni kwamba damu inaondoka kichwani na ngozi ya mgonjwa inakuwa nyeupe. Kama ukimlaza chini atajisikia koo na mdomo vimekauka vibaya sana na atagugumia na kutamka neno moja tu ‘maji’. Pigo la kuzimia linaweza likabadilika na kusababisha kifo na hivyo inawezekana kwa mtu anayeelekea kwenye kifo kuwa anaomba maji. Lakini kwa kawaida mtu aliye kwenye hatua ya kufa haombi maji. Unaweza kuona jinsi midomo yake inavyokauka. Mara nyingine anaweza akanywa kijiko cha maji kama utampa, yumkini kwa sababu mtu anayekufa hana uwezo wa kukataa kitu. Walakini mtu anayezimia, baada ya kupata mateso makali ya kiu, anaanza kupotewa na fahamu. Ardhii anaiona kana kwamba inadidimia chini yake na anajiona kana kwamba anaruka. Kwa hiyo atalia yumkini kwa kutoa taarifa ya kuaga ya kwamba “N’nakufa”. Lakini mtu anayekufa ambaye anakuwa hoi kabisa kwa sababu ya kupoteza damu nyingi na mateso makali yeze huyo hawezi kutoa sauti kubwa ila tu atafunga mdomo wake na kukata pumzi. Hawezi kamwe kutamka maneno maalum “N’nakufa”. Lakini Yesu alitamka maneno waziwazi “Yametimia”. “N’nakufa”.

Aliwaombea watesi wake. Aliwaona wale Wanyang’anyi wawili wakinining’inia misalabani kabla yeze hajatundikwa. Kisha anafikiria juu ya ukombozi wake yeze mwenyewe na watu wote kwa jumla.

Kisha, kwa sababu yeye alikuwa mtoto mwema, akawa anafikiria hali ya baadaye ya mama yake. Alikuwa amefikiria kwamba ana wajibu wa kuijenga nchi ya Mwenyezi Mungu. Alifikiria kuwa huenda ataijenga kwa njia ya kuteswa. Ndipo akakumbuka ubeti wa wimbo ulioimbwa zamani na nabii Daudi, “Mola wangu Mola wangu, mbona umeniacha?” Mwishowe uchungu na hali ya kuzimia vikamlazimisha ajifikirie yeye mwenyewe. Ndipo akasema “Baba mikononi mwako na salimisha roho yangu”. Na mwisho wa yote akapiga kelele “Maji! N’nakufal!” Je huku ndiyo kufa kwa Yesu?

Injili zinatuambia tu ya kwamba “alikata roho” kwa maana ya kwamba alikufa. Yule mlinzi wa makaburi naye aliamini vivyo hivyo. Vinginevyo angaliivunja mifupa yake. Watu wanaweza kuonekana kuwa wamekufa kwa sababu yo yote ile. Wanaweza kufa kwa sababu ya hofu au mshituko wa moyo. Lakini ni watu wachache sana ambao wamekufa kwa, sababu ya kusulubiwa. Eusebio amesimulia visa mbalimbali vyatatu waliosulubiwa walikufa baada ya siku kadhaa kutokana na uchovu, njaa au kwa sababu ya kuraruliwa na ndege na wanyama mbungani. Wanyang’anyi waliosulubiwa pamoja na Yesu walikuwa hai hadi kufikia jioni na askari walilazimika kuwapiga marungu ili kuwaua. Wakati Yusufu alipomwambia Pilato kuwa Yesu amesha kufa, Pilato hakusadiki. Alianza kumhoji mlinzi wa makaburi kwa sababu Pilato alikuwa na uzoefu wa mambo haya. Yesu angaliweza kufa kwa sababu ya upotevu wa damu na uchovu, lakini haiyumkini kwamba ilitokea hivyo.

Kama Yesu angalikuwa amekufa asingaliweza kutokwa na damu. Yohana ambaye analisimulia tukio hili huenda anajua umuhimu wa kituko hiki. Wale ambao walikielewa kituko hiki hatimaye, hawakuthubutu kamwe kukiongelea. Yesu alipigwa mijeledi asubuhi. Tunajua ya kwamba kuwashaa kwingi kwa ngozi kunaweza kusababisha uvimbe ndani ya misuli na vile vile katika ngozi. Maana yake ni kwamba kadiri michapo inavyoenea mwilini majimaji ya namna fulani yanajikusanya chini ya ngozi na kufanya vivimbe. Kwa lugha ya kitabibu hii inaitwa *Epanchments Traumatiques de serosite*

*au De cofoment de fa peau*". Mmoja wa maaskari aliviona vivimbe hivi na akakikwaruza kimoja, pengine kwa sababu ya utundu au pengine kwa sababu ya ukatili na kwa hiyo akamjeruhi Yesu na damu na maji vikatoka. "Sasa Yesu akawa amezimia kana kwamba amekufa". Maskini watu wasio na elimu hawakuelewa kwamba Yesu alikuwa bado hajafa. Inaelekea kwamba walimzika katika pango la muda tu. "Walimlaza katika pango hili kwa sababu kaburi lilikuwa janibu yake". Pengine aliiона shuka ya mtunza bustani ambayo ilikuwa chafu na iliyochanika chanika". Wakati Maria anaposhindwa kumtambua yeye anasema kwa sauti ya unyonge "Maria" neno moja tu. Lakini hii inadhihirisha hali yake ya kutojiweza na ya upweke. Kisha Maria anatambua na anataka kuibusu mikono yake. Lakini Yesu anasema "Usiniguse". Mwili wote ulikuwa unauma sana kwa sababu ya vidonda. Hivyo basi hataki kuguswa.

Anaposema, "Bado sijaenda kwa baba yangu"! Anatumia lugha ile ile ya kuremba waitumiayo watu wa Mashariki.

Alikuwa na maana kwamba "Bado sijafa", lakini anajisikia amesawajika, hana furaha na anaumwa sana hivi kwamba anahisi kwamba anaweza kufa dakika yo yote ile. Kwa hivyo akawatakia kila la kheri ndugu zake. Je hiyo siyo hali kamilifu na ya kiasili ya binadamu? Yeye alipewa adhabu ndogo sana ukilinganisha na adhabu za siku zile. Alikuwa mlaaniwa na mtengwa kando. Akajizuia asilete uchafuzi nchini wakati bado yungalipo na hakuthubutu kujitokeza hadharani isije maadui zake wakamkamata tena. Amekuwa na aibu sana hivi kwamba anajificha bustanini. Na siku moja wakati akitembea peke yake kuelekea Emmau anakutana na wanafunzi wake lakini kwa muda mfupi tu. Hawakuthubutu kumsaidia na wala hawakuthubutu kufuatana naye kwa kuhofia kwamba wataonekana. Kama wanafunzi wake wangalimsaidia katika kurudisha afya yake ya zamani wasingalimwacha aende peke yake akiumwa njaa bila ya rafiki yake ye yote. Akawa anawatuma matarishi ili wawaambie wanafunzi wake akutane nao mahali pa siri. Akawa anatoweka mara kwa mara na mara ya mwisho akawaacha moja kwa moja.

Ni mara moja tu katika Mathayo 28:18, anaonekana akisema kwa kujigamba kwamba “Mimi nimepewa uwezo wote wa mbingu na wa ardhi”. Sisi madaktari tunajua maana ya kujigamba huko. Tunawaita wenye kujigamba hivyo “Dementia Paranoids” Yaani, watu waliorukwa na akili kwa sababu ya kukata tamaa.

Katika nchi za Mashariki kuna jumuiya moja ya kidini ambayo imeanzilishwa juu ya msingi wa imani kwamba Yesu aliishi baada ya kusulubiwa baadaye akasafiri kuelekea India na hatimaye akijulikana kama Izza (Isa) akastakimu Srinagar (mji wa Furaha) katika bonde zuri la Kashmir (kama Sier). Anasemekana kuwa aliishi mahali hapo mpaka alipofikia umri wa miaka 120, naye amezikwa mahali hapo hapo. Wanasema kwamba jina lake ni Yuz Asaf. Kulingana na “Enzuklopadie des Islam” 1913, B. Ukurasa 218 jina la jumuiya hiyo ni “Ahmadiya”. Mawazo haya huru ambayo yametolewa na tabibu mashuhuri sana wa Sweden, na ambayo yametolewa baada ya uchunguzi wa kiangalifu kuhusu maelezo ya Injili zote nne haukuacha nafasi yoyote ya kudhania kwamba Yesu hakufia msalabani. Na kama Yesu angalipimwa na tabibu mwaminifu aliposhushwa msalabani bila shaka yo yote yeye angalithibitisha kwamba hakufia msalabani.

## SURA YA SABA

### JEE YESU ALIPAA MBINGUNI?

Kutokana na taarifa nne za waandishi wa Injili ni dhahiri ya kwamba Yesu alitoka ndani ya kaburi akiwa na mwili wake wa asili. Wakati wanafunzi wake walipodhania kwamba ana mwili wa kiroho yeye

akasema, "Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kwamba ni mimi mwenyewe: nipapaseni muone, kwani kiumbe wa kiroho hana nyama na mifupa kama hii mnionayo nayo. Kisha akawaauliza "Je mnayo nyama?" Ndipo wakampa kipande cha samaki wa kuokwa na kipande cha sega la asali. Akavichukua hivyo na kula mbele yao." (Luka 24:39; 43). Alikutana na wanafunzi wake kwa siri au msituni kwa kuogopa asikamatwe. Tena hakujionyesha kwa watu, kama asemavyo Petro kwamba Mwenyezi Mungu aliokwisha wachagua wawe mashahidi wake, yaani sisi tulio kula na kunywa naye baada ya kufufuka kwake (Matendo 10:41).

Angalifufuka kutoka katika wafu au kama mwili wake ungalibadilishwa na kuwa wa viumbe vinavyopatikana kwenye sayari zingine, asingaliogopa kukamatwa na kufa na angejitokeza mbele ya wapinzani wake na angeliitisha mikutano ya hadhara na kutangaza jinsi alivyokikwepa na kukishinda kifo. Zaidi ya hayo yeye angalionyesha upendo kwa maadui zake kwa ku wahabiria ili wapate kumwamini. Lakini yeye alichukua tahadhari kwa ajili ya usalama wake kwa sababu alijua kuwa alikuwa na mwili wa kawa idha na hivyo aliogopa kukamatwa tena na kuuawa.

Mufasirina wengi wamefasiri aya ya 39 ya kifungu cha 24 cha Injili ya Luka kwa kuandika kwamba: "Moja ya fikra kubwa ambazo zilipinzana na imani ya kanisa la mwanzo ilikuwa ile iliyofundisha kinyume na utunzi huu na tungo nyingine kadha wa kadha, kwamba Kristo alikuwa kitu cha kukisiwa tu ambacho hakina mwili maalum na kwa hiyo hakiwezi kupata mateso kikweli kweli. Mwili huu aliopaa nao Bwana ndiyo ule ule ambao hivi sasa ameketi nao kwenye mkono wa kulia wa Mwenyezi Mungu".

Yeye aliwaauliza wanafunzi wake wana chakula cho chote na alikula mbele yao. Alitembea umbali wote ule kutoka Yerusalernu hadi Galilaya. Safari hii alienda kwa miguu siyo kwa kuitia katika barabara kuu bali kwa kuitia vicho choroni akiogopa kuandamwa. Mambo yote haya

hakuwa na haja ya kuyafanya angalikuwa kiumbe kingine licha ya binadamu.

## KUJITOKEZA GHAFLA

“Yesu alikuja wakati milango ilipokuwa imefungwa na wanafunzi wake walikuwa wamejikusanya kwa kuwaogopa Mayahudi, na akasimama kati yao” (Yohana 20: 19). Tamshi hili pia halionyeshi ya kwamba alikuwa na mwili wa ajabu. Mufasirina wengi waliofasiri aya ya 39 ya kifungu cha 24 cha Injili ya Luka wanasesma kwamba “Hatuju ni kwa namna gani mwili wenye nyama na mifupa unaweza kuingia ndani ya chumba ambacho milango yake imefungwa”.

Mimi ninafikiri kwamba kifungu hiki cha maneno hakionyeshi kwamba kujitokeza kwa Yesu kulikuwa kwa namna ya ajabu au kimwujiza bila ya kuwa na mwili wake wa kawaida. Kwa kuwaonyesha wanafunzi wake mikono na ubavu wake, yeze mwenyewe amethibitisha kwamba alikuwa na mwili wa udongo na wanafunzi wake walifurahi kumwona. Kifungu hiki kinabainisha tu ya kwamba Yesu alikuja mahali walipokuwa wamejikusanya wanafunzi wake “Kwa kuwaogopa Mayahudi” yumkini kwenye jumba lenye giza nene ambalo limejengwa kwa miti na matope. Huenda Yesu aliingia humo wakati ule ule walipoingia wanafunzi wake. Inawezekana pia kwamba kwa vile wao walikuwa wageni mjini Yerusalem, mwenyeyeji wao au rafiki zake wa umoja wa Esseen walimwingiza humo kwa kupitia mlango wa siri kwa sababu jumba hilo lilikuwa na milango mingi. Luka ambaye ndiye msimuliaji wa tukio hili ameacha kuitaja milango hii mingi jambo ambalo linaonyesha kwamba siyo sehemu ya maana, ya tukio lenyewe. Waila kudhania kwao kwamba wameona kiumbe chenye mwili wa kiroho kingekuwa sawa. Lakini Yesu mwenyewe anakanusha wazo hili na kubainisha ubovu wake kwa kuonyesha mikono yake na ubavu wake na kutoa tamshi lake waziwazi ya kwamba yeze alikuwa Yesu yule yule akiwa na mwili wenye nyama na mifupa.

Nilikuwa nimekwisha yaandika maelezo hayo hapo juu kuhusu kujitokeza kwa ghafla kwa Yesu ndani ya chumba kilichofungwa na mara tu nikakiona kitabu kilichoandikwa na mtu mmoja aitwae Docker kiitwacho IF JESUS DID NOT DIE ON THE CROSS (kama Yesu hakufia mslabani) ambamo ametoa maelezo kama yangu kuhusu kutokea huku kwa ghafla. Kwenye ukurasa wa 14 hadi 16 ameandika:-

“Baadhi ya watu wamedhania kwamba baada ya kusulubiwa Yesu akapewa mwili ulio na uwezo mkubwa zaidi kuliko mwili wa kibinadamu na kwamba mwili huo wa ajabu ulimwezesha kupita kwenye milango iliyofungwa. ‘Lakini kwa hakika hakuna sababu ya kudhania hivi. Wainjililisti watatu wa mwanzo wameyaratibu vizuri sana maelezo yanayohusu kujitokeza huku hivi kwamba hayaachi nafasi yo yote kwa mtu kudhania kwamba walichokiona wanafunzi wa Yesu ulikuwa mwili wa kiroho na wala siyo mwili wa kawaida.

“Na hata Mtakatifu Yohana hasemi waziwazi kwamba Yesu alipitia kwenye mlango uliofungwa. Tukichukulia tafsiri ya neno kwa neno ya maneno anayoyatumia Yohana kuwa sawa ni jambo linalokubalika akilini kusema kwamba Yesu ni lazima awe amebakia mafichoni mjini Yerusalem mpaka aliporejea Galilaya. Imesemwa waziwazi ya kwamba hakujitokeza hadharani. Ni wazi ya kwamba kama wakuu wa serikali wangalijua kuwa alikuwa bado mzima angekamatwa tena na kuuawa, na Mtakatifu Yohana anasema kwamba milango ilikuwa imefungwa “kwa kuwaogopa Wayahudi.” Milango inayofungwa kwa sababu hiyo ni ile ya nje tu. Mahali panapoweza kufaa kwa maficho ya namna hiyo ni kwenye nyumba ya marafiki zake ambako yeye na wanafunzi wake walikaribishwa mahali ambapo vidonda vyake vingeweza kuhudumiwa. Kufungwa kwa milango ya nje hakungeweza kumzuia kutoka katika sehemu moja ya nyumba na kwenda kwenye chumba ambako wanafunzi wake walikuwa wamejikusanya. Inawezekana pia ya kwamba yeye alitangulia kuingia katika chumba hicho nao hawakumwona mpaka aliposimama kati yao.

Ni kutokana na masimulizi ya Mtakatifu Luka kuhusu safari ya kwenda Emmau ya kwamba ikadhaniwa kwamba Yesu aliyefufuka alikuwa na uwezo wa kutokuonekana. Yohana anasema alitoweka machoni mara alipotoka nje ya nyumba.

“Dakta Arthur Wright amefikia hadi ya kudai kwamba Yesu wakati fulani alikuwa Emmau na kufumba na kufumbua akawa Yerusalem. Wakati fulani anakuwa katika ulimwengu wa kimwili na kufumba na kufumbua anakuwa kwenye ulimwengu wa Kiroho. (Christ’s claim, etc. “The Interpreter” July, 1916 p. 385). Inaelekea kwamba Dakta Wright amesahau kwamba kulingana na maelezo ya Mtakatifu Luka wale wanafunzi wawili waliondoka Emmau wakati alipofariki na walifika kwenye chumba mjini Yerusalem kabla yake. Ni vigumu kuamini kwamba Mtakatifu Luka alikuwa na maana nytingine kuliko hii ya kwamba alikwenda haraka kwa vile alitakiwa arudi Yerusalem. Jambo hili linaingia akilini zaidi hasa ikikumbukwa kwamba maelezo haya yanafuatiwa mara moja na ushahidi alioutoa Yesu mwenyewe kwamba alikuwa bado anao mwili wenye nyama na mifupa na wala si mwili wa Kiroho.

“Kama ni kweli kwamba Yesu alimuomba Tomaso aweke kidole chake kwenye kovu za misumari (Yohana 20:27); kama ni kweli kwamba aliwaambia wanafunzi wake waliomtilia shaka, “Angalieni mikono yangu na miguu yangu ya kwamba ni mimi mwenyewe nipapaseni muone, kwani kiumbe mwenye mwili wa Kiroho hana nyama na mifupa kama hii mnionayo nayo (Luka 24:39); kama ni kweli kwamba alikula mbele yao, kama ni kweli kwamba alijifananisha na mtunza bustani alipotoka kaburini, kama ni kweli kwamba alitembea kwa miguu umbali wa kutoka Yerusalem mpaka Galilaya na kama alichukua kila namna ya tahadhari ili asikamatwe tena, ni dhahiri shairi ya kwamba tamko lisemalo kuwa alijitokeza ghafla kwenye vyumba ambavyo milango yake ilikuwa imefungwa si sahihi kwa tafsiri ya neno kwa neno na kwamba mwili wake haukuwa wa ajabu bali ule uliotengenezwa kwa nyama na mifupa. Hii inaonyesha pia ya kwamba maelezo ya Wainjilisti wa mwanzo ya kwamba alipaa mbinguni baada ya kiasi cha siku arobaini tangu afufuke

ni hekaya tupu; (kama yafasiriwe neno kwa neno). Ni hekaya kwa sababu baada ya kuthibitishwa kwamba ye ye ali kuwa bado ana mwili wake wa udongo ni jambo la kipumbavu kusema kwamba wingu ambalo ni mkusanyiko wa mvuke lilimnyanya mbinguni. Hakuna wingu lenye uwezo wa kunyanya mwili wa udongo. Na hakuna kiumbe chenye uhai kiwezacho kupaa na kuingia mbinguni.

Na kama itasemwa kwamba alipata mwili mw ingine wa ajabu, sasa ule mwili wake wa udongo ulikwenda wapi? Kwa vyo vyote vile hakuuacha kaburini kwa sababu tumeona ya kwamba kwa muda wa siku chache alizoishi baada ya kile kinachoitwa kufufuka ali kuwa akitembea na mwili ule wa udongo. Kusema kwamba alipaa mbinguni akiwa na mwili wake wa udongo ni kinyume na mawazo ya mufasirina tulio wataja hapo juu na vile vile ni kinyume kabisa na mafundisho ya Yesu, kwani ye ye alisema, “Hakuna ali yepaa mbinguni ila yule ali yeshuka kutoka mbinguni” (Yohana 3:13).

Ni dhahiri ya kwamba ye ye hakushuka kutoka mbinguni akiwa na mwili wenye nyama na mifupa, hivyo basi hawezi kupanda na mwili kama huo. Kusema ya kwamba ye ye akiwa na mwili wake wa nyama na mifupa ameketi kuumeni kwa Mwenyezi Mungu ni wazo la kipagani na ni kichekesho ambacho hakina haja ya kukanushwa.

Vile vifungu vya maneno ambamo hii nadharia ya kupaa imetajwa haviamini kabisaa. Mathayo hasemi lo lote kuhusu kupaa huku. Ameeleza tu ya kwamba baada ya kutoka kaburini Yesu alikwenda Galilaya na alikutana na wanafunzi wake kwenye mlima ambao aliwaagiza wakutane naye (Mathayo 28:16).

Marko anadai kwamba Yesu alipeleka taarifa kwa wanafunzi wake akiwaambia wakutane naye Galilaya na kisha bila ya uhusiano wo wote na yale ali yoyataja mwanzo na bila ya kutoa maelezo ya mahali walipokutania anakurupuka na kusema. “Kwa hiyo baada ya Bwana kuzungumza nao akapokewa mbinguni na akaketi mkono wa kulia wa Mwenyezi Mungu” (Marko 16: 19).

Hiki kifungu cha mwisho cha maneno kisemacho, “na akaketi mkono wa kulia wa Mwenyezi Mungu” kimedhoofisha kabisa taarifa nzima kwa sababu haiyumkini ya kwamba na huyu mwandishi alikwenda huko mbinguni na akamwona Yesu akikaa mkono wa kulia wa Mwenyezi Mungu. Ukweli kuhusu vifungu kumi na viwili vya mwisho vya Injili ya Marko ni kwamba ‘viliongezwa baadaye katika ile taarifa ya asili huenda kwenye karne ya pili hivi ili pengine vichukue nafasi ya vifungu vya mwisho vya asili ambavyo vilipotea au vilifikiriwa kuwa havifai”. (Encyclopaedia Britannica, Toleo la pili, Jalada la 17, uk. 370).

Kwa hiyo maelezo ya Marko hayawezi kuchukuliwa kuwa ndiyo msingi wa itikadi hii. Maelezo ya Mtakatifu Luka ni kwamba: “Yeye alienda nao mpaka Bethania na akanyanya mikono yake na kuwabariki. Na ikatokea ya kwamba alipokuwa akiwabariki akatengana nao na akachukuliwa mbinguni”. (Luka24:5051).

Kwa hiyo kulingana na mtakatifu Luka ni kwamba alitengana na Masahaba zake, jambo ambalo ni tofauti na kusema ya kwamba walimwona akipaa mbinguni. Vile vile tunasoma katika matendo: “Baada ya kusema hayo, wote wakiwa wanamsikiliza alichukuliwa mbinguni, wingu likamficha machoni pao. Na kufichika machoni hakuna maana kwamba alipaa mbinguni. Inawezekana sana ya kwamba alikwenda juu ya mlima na kwa vile kilele cha mlima kimefunkwa na mawingu na ukungu akafichika machoni pao. Kisha, kutoka kwenye kilele cha mlima akashuka ng’ambo ya pili akiacha nchi yake na kuelekea kwenye nchi nyingine ambako atakuwa salama kutokana na uadui na njama za Mayahudi.

Yohana anaunga mkono wazo hili kwa kusema kwamba Yesu alikutana na wanafunzi wake kwa mara ya mwisho kwenye bahari ya Tiberia na akamwambia Petro: “Lisha kondoo zangu” na pia akasema, “Nifuate” na Petro akamwona yule wanafunzi aliyependwa sana na Yesu akifuata. (Yohana 21: 16, 20). Hapana shaka ya kwamba mistari hii ya

mwisho ya Injili ya Yohana inaonyesha wazi wazi kwamba Yesu hakupaa mbinguni bali alihamia nchi nyingine. Kwa hiyo ni dhahiri ya kwamba Injili za Mathayo na Yohana zote mbili zinaunga mkono wazo hili la uhamaji lakini hazisemi lolote juu ya kupaa.

Maelezo ya Marko kuhusu kile kinachoitwa kupaa yameongezwa kwenye ile taarifa ya asili na mtu asiyejulikana. Luka ambaye anataja huku kupaa kwa njia ya kubabaisha hakuwapo wakati Yesu alipowaaga wanafunzi wake na kutoweka. Ukiwa ni ushahidi zaidi wenye kuonyesha ya kwamba taarifa za watu hawa si za kutegemea tunakuta ya kwamba wao wanahitilafiana katika mambo muhimu. Mmoja wao anasema kwamba Yesu alipaa mbinguni akiwa Bethania. Mwingine anasema alipaa akiwa kwenye mlima wa Mizeituni. Watatu anasema alipaa akiwa Yerusalem. Yaani hakuna mahali maalum. Na Mathayo naye anasema alikwenda Galilaya na kukutana na wanafunzi wake lakini Yohana anasema aliwaaga wanafunzi wake akiwa Tiberia. Vurugu gani hii? Weigall ameandika:

“Kupaa hakutajwi kabisaa katika maandiko ya awali ya Kikristo kama vile Nyaraka, na wala hakukutajwa katika Injili ya awali ya Mtakatifu Marko, kwa sababu yale maneno, “Akapokelewa mbinguni” yana kauleni na yamo kwenye aya kumi na mbili za mwisho za kitabu hiki ambazo hivi sasa zinatambuliwa takriban na watalamu wote wa Biblia kwamba ziliongezwa baadaye”. Anaendelea kusema:

“Kupaa kwa namna hii kulikuwa ni mwisho wa kawaida wa hekaya za miungu ya kipagani, kama ilivyokuwa kwa hekaya za maisha ya Eliya. Mungu wa kipagani aitwae Adeonis, ambaye ibada yake ilistawi katika nchi ulimokulia Ukristo alidhaniwa kupaa mbinguni mbele ya wafuasi wake. baada ya kufufuka kwake; na kadhalika Dionysos, Herakles, Hyacinth, Krishna, Mithra na miungu wengine walipaa Mbinguni”.

Uamuzi tunaofikia ni kwamba taarifa za Wainjilisti hazifai kuwa msingi wa nadharia hii ya kupaa.

## **SURA YA NANE**

**IMANI HII YA KWAMBA YESU ALIFIA  
MSALABANI NA AMEPAA MBINGUNI  
IMEPATIKANAJE?**

Kama ni kweli jinsi tulivyohakikisha katika sura zilizotangulia ya kwamba Yesu alikuwa hai aliposhushwa msalabani, sasa kwa nini Wakristo wa mwanzo kama vile Mtakatifu Paulo na Mtakatifu Petro waliamini juu ya kufa kwake msalabani? Kwani inaonekana kutokana na nyaraka zao

ya kwamba jambo kubwa walilolihubiri ni kufa kwake msalabani na kufufuka kwake kama ifundishwavyo kwenye takriban fikra zote za Kikristo siku hizi. Hapana shaka ni lazima kuieleza hali hii kwa kirefu. Wanafunzi wa Yesu walimwacha yeye na kukimbia kwa kiwewe wakati alipokamatwa na hawakuwapo wakati wa kushushwa kwake msalabani wala wakati alipotoka kaburini. Ingawaje hakujitokeza hadharani kwa hofu ya kukamatwa tena alikutana na wanafunzi wake kwa siri au msituni tu. Kama asingalionana nao tena na kuwahakikishia kwamba amekikwepa kifo, imani yao kuhusu Umasihi wake ingepata pigo na huenda wangeritadi kwa kuona ya kwamba yule ambaye walimhesabu kuwa ndiye Masihi Aliyahidiwa kwa ajili ya Wayahudi amekufa kifocha ‘laana’. Hivyo alijionyesha tena kwao ili kuijenga upya imani yao iliyoingiwa na wasiwasi. Naam, kuepuka kwake kwenye mdomo wa kifo kulikuwa ushahidi madhubuti wa madai yake. Kuliwapa moyo sana. Baada ya kuiacha nchi yake na kuagana nao kwenye bahari ya Tiberia, kama asemavyo Yohana, wao walibakia imara. Hata walijaribu kuyahubiri madai yake kwa Mayahudi. Lakini Mayahudi waliwatesa. Baadhi yao waliuawa mara moja na wengine walipigwa mawe mpaka wakafa. Mayahudi waliyapinga madai yao, wakawakejeli na kuwazomea wakikazania kwamba wao (wanafunzi wake Yesu) walimwacha Masihi wao afe kifo cha laana. Wanafunzi wake Yesu hawakuweza kusema lolote kuhusu kuponyoka kwake wakihofia mateso makali. Kwa hiyo inawezekana sana ya kwamba waliificha habari hii na wakawa wanajibu ya kwamba Yesu amefufuka kutoka katika wafu, kwa vile Mayahudi walikwisha tangaza kila mahali kwamba amekufa. Na wakaongeza kujibu kwamba amepaa mbinguni wakiwa na maana kwamba amekwenda mahali pa usalama.<sup>a</sup>

- 
- a. Neno “Mbinguni” lilitumiwa kwa ajili ya mahali popote palipoinuka. Kwa mfano tunasoma katika kutoka (19:20) kwamba Bwana alishuka kwenye kilele cha Mlima wa Sinai na akazungumza na Musa. Iakini katika (20:22) neno “Mbinguni” linatumiwa badala ya kilele cha mlima. Zaidi ya hayo tunasoma kwamba, “Kabla Musa hajapaa mbinguni

alisema kwamba atashuka siku ya arobaini na moja wakati wa asubuhi" (Jewish Encyclopaedia chini ya neno Moses). Na katika kutoka (24:28) imesemwa waziwazi ya kwamba Musa alikwenda katikati ya wingu na likamnyanya hadi kwenye kilele cha mlima na Musa alikaa hapo mlimani kwa mchana arobaini na mausiku arobaini. Kadhalika Yesu mataifa mengine kwa sababu kwanza kabisa walijua kwamba hayo mataifa mengine hayataikubali Sheria ya Musa na sababu ya pili ni kwamba Yesu aliwakataza wasiyahubirie mataifa mengine. Katika hali ya mkoroganyo kama huu kukatokea mtu mmoja aliyeitwa Saulo ambaye baadaye akajulikana sana kwa jina la Paulo. Alikuwa huyu Paulo ambaye kwa vile hakuwa mionganoni mwa wanafunzi wake Yesu akajitangazia haki ya kuwa na cheo cha utume kwa sababu ya ndoto aliyoiona akijua kwamba bila ya kutaja ndoto hiyo madai yake yatakuwa na nafasi ndogo sana ya kukubaliwa.

## **NDOTO YA PAULO**

Ndoto aliyoiona imetajwa katika Matendo sura ya 9 na 22 na ya 26. Kama tukiyasoma maelezo yaliyomo kwenye kila sura kwa uangalifu tutaona ya kwamba yanapinzana vibaya sana.

1. ~~Kwamba na tutaona ya katika sura ya 9 na 22 na ya 26~~ hadi ya likampokea na kutoweke machoni pao. Kwa vile wanafunzi wake walimwona akienda juu ya mlima sawa na msamiati ulioelezwa hapo juu, wakasema kwamba amekwenda mbinguni.

Walakini majibu haya ya wanafunzi wa Yesu hayakuwardhisha Mayahudi kwa vile hawakumwona akipaa mbinguni. Kwa hiyo wakaendelea kuamini kwamba ye ye amekufa kifo cha 'laana'.

Zaidi ya hayo, sawa na mafundisho ya Bwana wao, mahubiri yao yalikuwa yanaelezwa kwa Mayahudi tu. Ni jambo liliilo wazi sana ya kwamba haikuwa rahisi kwa Mayahudi kumwamini Yesu kwa sababu ya kuhubiriwa na wanafuzi duni ili hali hata Yesu mwenywewe hakuweza kuyashinda mawazo yao. Kwa upande mwingine ni kwamba wao walikuwa wamekatazwa wasiineneze imani yao kwa

sita ya kwamba, "Mwanga kutoka mbinguni ulimwangazia pande zote na akaanguka chini na kusikia sauti ikimwambia, "Saulo Saulo kwa nini unanitesa? Naye Saulo akauliza ni nani wewe Bwana? Na ile sauti ikajibu, "Mimi ni Yesu ambaye wewe unamtesa. Lakini simama sasa na uingie mjini na huko utaambiwa cha kufanya. "Na wakati wote huo wale watu aliosafiri nao walismama kimya, wakiisikia sauti bila ya kumwona mtu ye yote. Lakini katika sura ya 22 mstari wa 9 anasema, "Na wale waliokuwa pamoja nami kwa hakika waliuona mwanga na wakaogopa lakini hawakuisikia sauti ya yule aliyezungumza nami."

2. Katika sura ya 9 na 22 anasema kwamba mwangaza mkali sana ulimulika pembezoni mwake yeye tu lakini katika sura ya 26 anasema kwamba mwangaza huo ulimmulika yeye na vile vile uliwamulika wale waliokuwa wakisafiri naye.
3. Katika sura ya tisa tunasoma ya kwamba YEYE peke yake alianguka chini na wengine walismama bila ya kusema chochote, lakini katika Sura ya 26 mstari wa 14 anasema ya kwamba yeye na wenzake wote walianguka chini
4. Katika sura 22 anasema ya kwamba alipouliza afanye nini Yesu alijibu, "Inuka na nenda Damascus na huko utaambiwa ni mambo gani unapaswa uyafanye. Walakini katika sura ya 26 hasemi lo lote kuhusu habari hii isipokuwa tu anasema ya kwamba Yesu mwenyewe alimwambia mambo yote aliyopaswa ayafanye.

Kwa kuwapo mkoroganyo kama huu katika maelezo ya ndoto ambayo ndiyo msingi wa madai yake ya utume, sisi tunalazimika kuutilia shaka uthabiti wake. Hata kama tukikubali ya kwamba ni kweli aliona ndoto hiyo, ndoto tupu haiwezi kuwa msingi wa kufanya madai ya utume. Walakini yeye aliukubali Ukristo akiwa mjini Damascus na pale pale akaanza kuhubiri kwenye masinagogi kwamba Kristo alikuwa mwana wa Mungu na akawazidi maarifa Mayahudi walioishi Damascus akihakikisha kwamba Yesu

anayemsema ni yule yule Kristo. Ndipo Mayahudi wakafanya njama ya kutaka kumwua, (Matendo 9:23).

Kabla ya tukio hili, wakati Stefano alipokuwa akipigwa mawe na Mayahudi mpaka akafa ye ye Paulo alikuwa amesimama pale pale na aliafiki juu ya mauaji haya. (Matendo 22:20). Na kulikuwa na mateso makali sana yaliyokuwa yameanzishwa dhidi ya Kanisa mjini Yerusalem. Waumini wote walitawanyika na kwenda sehemu zingine isipokuwa wale mitume tu. (Matendo 8:1).

### **MTAKATIFU PAULO ANAYAENDEA MATAIFA**

Hivyo basi, baada ya kushuhudia mateso yaliyoletwa na Mayahudi na kung'ang'ania kwao katika kuyakataa madai ya Yesu, na baada ya kutoridhika na maendeleo ya pole pole na yenye kukatisha tamaa ya Ukristo, Paulo alionelea afadhali ahamie katika sehemu nyingine ili aende akajifunze msimamo wake mpya. Ndipo akaenda mahali palipokuwa mbali kidogo katika eneo la kusini mwa mji wa Damascus paitwapo Arabia (Wagalatia 1:17).

Kufikiria kwake sana kukampatia wazo ambalo hata Yesu hakuwahi kuliwaza. Wazo hilo lilikuwa kwamba Ukristo uhubiriwe kwa mataifa mengine. Miaka mitatu tangu ajiunge katika Ukristo, Paulo aliamua kufanya ziara yake ya kwanza kwenda Yerusalem kwa madhumuni ya kwenda kufahamiana na Petro. (Wagalatia 1:18). Akajaribu kuijunga na kikundi cha wanafunzi wake Yesu lakini kwa mara ya kwanza wao walimkataa. Alikutana na wanafunzi hao kwa kutambulishwa na Barnaba na akawaambia juu ya ndoto yake kuwashakikishia juu ya uaminifu wake kwa jinsi alivyohubiri kwa ujasiri mwingu mjini Yerusalem kwa jina la Yesu. Kulingana na waraka wake kwa Wagalatia. ye ye alikaa na Petro kwa muda wa siku kumi na tano na kwa muda huo wote hakuona mtume mwingine isipokuwa Yakobo tu. (Wagalati 1:19).

Hadi kufikia wakati huu, wale wote ambao walikuwa wametawanyika kwa sababu ya mateso yaliyotokana na kifo cha Stefano, walikwisha

kata mbuga kabisa na walikuwa wameshafika Foenike, Kipro na Antiokia wakilihubiri neno siyo kwa watu wote ila kwa Mayahudi tu. (Matendo 11:19).

Kufikia wakati huu Paulo alikuwa amekwisha kata tamaa juu ya kuwaingiza Mayahudi kwenye Ukristo. Kwa hiyo akaamua kuyahubiria wazi wazi Mataifa mengine. Hata hivyo hii ilikuwa kinyume cha mafundisho ya Yesu. Yeye aliwakataza katakata wanafunzi wake akisema:-

“Katika njia ya Mataifa msiende na kwenye miji ya Wasamaria msiingie. Isipokuwa tu waendeeni kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli” (Mathayo 10:5,6). Na vile vile alisema, “Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli”. (Mathayo 15:24). Na tena alisema, “Si vema kuchukua chakula cha watoto na kuwapatia mbwa” (Mathayo 15:26)<sup>a</sup> Wakati wanafunzi wake

- 
- a. Zipo karaa chungu nzima ndani ya Injili zinazoonyesha wazi wazi kwamba Yesu hakutumwa ila kwa Waisraeli tu. Kwa mfano Mariamu aliambiwa na yule malaika kwamba, “Yesu ni lazima apewe ufalme wa baba yake Daudi” (Luka 1:32). “Na atatawala katika nyumba ya Yakobo
- 

milele na milele” (Luka 1:33) Vile vile “Ewe Bethelehemu kutoka kwako atapatikana Mtawala atakayewatawala watu wangu Israeli”. (Mathayo 2:6). Ile karamu ya Mlimani ilikuwa kwa ajili ya Waisrael tu. Ingawaje ni jambo la hakika kwamba watu wa mataifa mengine walikuwa wakiishi pamoja na Wayahudi nichini Palestina, Yesu kamwe hakuwahubiria. Akatabiri juu ya wanafunzi wake ya kwamba, “wakati mwana wa Adamu atakapokuwa amekalia kiti cha enzi, ninyi pia mtakuwa mmekalia viti kumi na mbili vya enzi mkiyahukumu mataifa kumi na mbili ya Israeli”. (Mathayo 19:28). Kushitakiwa kwa Yesu katika mahakama ya Pilato pia ni ushahidi madhubuti kwamba ujumbe wake ulikuwa kwa ajili ya Mayahudi tu. Pilato alimhesabu yeye kuwa “Mfalme wa Mayahudi”. (Mathayo 27: 11), na wala siye mfalme wa mataifa yote. Wakati Petro alioanza kuyahubiria mataifa mengine na kula pamoja nao wale waliotahiriwa wakamlaumu, naye hakuweza kutaja hadithi au agizo la

Akazidi kufahamikiwa ya kwamba ili kuhakikisha kwamba atapata ushindi na mafanikio mionganii mwa Mataifa mengine, yale mafundisho yaliyofundishwa na Yesu na kutekelezwa kwa uaminifu na yeye mwenyewe pamoja na wanafunzi wake ni lazima yarekebishwe. Akaonelea ya kwamba sherehe zifanywazo sawa na sheria ya Musa kamwe haziwezi kukubaliwa na wale ambao hawakuwa Mayahudi. Kwa hiyo kwa ujasiri wa kifedhuli yeye akatangaza kukomeshwa kwa sheria hiyo katika sherehe ya tafrija zote na akatoa mwongozo mpya kwa Ukristo ambao hatimaye ukawa mfumo wa mawazo na juhudhi yake ambao msingi wake ni mawazo au fikra za Kirumi na falsafa za Kiyunani. Anasema:-

Yesu ili kuhalalisha kitendo chake bali alitaja ndoto yake mwenyewe tu (Matendo 11: 1,6). Hii inaonyesha ya kwamba zile karaa kama vile “Enendeni mkayafundishe mataifa yote mkiyabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu (Mathayo 28:19) zimeongezwa baadaye. Wanafunzi wake Yesu kamwe hawakumbatiza mtu ye yote kwa jina la watu hawa watatu. Katika karaa fulani fulani neno “Mataifa” linaweza kufasiriwa kwa maana ya “makabila” ambapo katika baadhi ya karaa limetumiwa kuhusiana na ujaji wa mara ya pili wa Yesu ambao ndiyo ujaji wa Ahmad wa Qadian, Nabii aliyeletwa na Mwenyezi Mungu ili kuyaongoza mataifa yote kwenye dini ya Kiislamu.

walipojaribu kumkataza asiyahubirie Mataifa mengine, akadai ya kwamba Yesu mwenyewe alimwamuru kufanya hivyo kwenye ndoto aliyoiona mjini Yerusalem kwa maneno yafuatayo:-

“Fanya haraka uondoke Yerusalem kwa sababu hao (Mayahudi) hawataupokea ushuhuda wako kunihusu mimi. Kwa hiyo nenda nami nitakutuma mbali, kwa Mataifa Mengine”. (Matendo 22: 18,21). Ingawaje alipingwa na wanafunzi wa Yesu lakini yeye aliendelea kuyahubiria mataifa mengine na hatimaye akafanikiwa katika kazi hii. Wale wanafunzi wa Yesu ambao walikuwa wameteswa sana hatimaye wakakubaliana naye ya kwamba aendelee kufanya kazi yake mionganii mwa Mataifa mengine na wao watawahubiria Waisraeli tu. (Wagalatia 2:7; 12).

## KUKOMESHWA KWA SHERIA YA MUSA

1. “Kwa vitendo nya Sheria hakuna mtu ye yote atakayefanywa kuwa na uhusiano mwema na Mwenyezi Mungu kwa sababu Sheria ni kujua dhambi. Kwa hiyo ninasema ya kwamba mtu huwa mwema mbele ya Mungu kwa sababu ya imani na wala siyo kwa kufuata Sheria.” (Warumi 3:20,28).
2. “Kwani dhambi haitatawala juu yako kwa sababu wewe huko chini ya Sheria”. (Warumi 6: 14).
3. “Siiikatai neema ya Mwenyezi Mungu kwa sababu kama uchamungu unaletwa na Sheria, basi Kristo amekufa bure”. (Wagalatia 2:21).
4. “Tunajua ya kwamba mtu hawi mwema kwa sababu ya kuitii Sheria bali kwa kumwamini Yesu Kristo”. (Wagalatia 2:16).
5. “Sikilizeni, mimi Paulo nawaambieni ya kwamba kama mkitahiriwa basi Kristo hatawafaidia cho chote”. (Wagalatia 5:2).

Mafundisho haya ni kinyume sana na mafundisho ya Yesu ambaye wakati wa uhai wake wote alikuwa akifuata Sheria. Muda mfupi tu kabla hajakamatwa alishereheke na kula karamu ya Pasaka pamoja na wanafunzi wake (Marko 14:12,14).

Alimwambia mkoma mmoja ambaye alimponyesha ukoma, “Nenda ukajionyeshe kwa kuhani kisha utoe Sadaka kwa ajili ya kupona kwako kama alivyoamuru Musa iwe uthibitisho kwao kwamba umepona”. (Marko 1: 14).

Zaidi ya hayo yeye aliwahimiza wazitoe sadaka zao kwenye altare. Wanafunzi wake pia walikuwa wakifuata Sheria. Yule mwanamke aliyefuatana na Yesu kuja Yerusalem alitayarisha manukato na marhamu na akapumzika katika siku ya sabato sawa na amri. (Luka 23:56).

Kwa hiyo mtakatifu Paulo hakuwa na mamlaka wala haki ya kukomesha au kurekebisha maamrisho ya Sheria. Yeye hakuwa Mtume wa Masihi la bali hata hakuwa wanafunzi wa Yesu.

Sasa alikuwa na haki gani ya kusema, “Kama mkitahiriwa Kristo hatawafaidia chochote” ilihali Kristo mwenyewe (Luka 2:21 ) na wanafunzi wake wote walitahiriwa? Tena Yesu anasema: “Msidhani nimekuja kutengua sheria bali Kutimiliza”. (Mathayo 5:17). Kisha akasema, “Ni rahisi kwa mbingu na ardhi kupita kuliko yodi moja ya Sheria kufutika (Luka 16: 17).

Tamko la Paulo kwamba mtu hawi mwema kwa kufuata Sheria ni la makosa moja kwa moja. “Zakaria na mkewe walikuwa waaminifu kwa Mungu wakiishi kwa ukamilifu kulingana na amri na maagizo yote ya Bwana”. (Luka 1:6). Wanafunzi wake Yesu hawakuwa na imani kama hii ya Paulo. Kwa mfano Yakobo ndugu yake Yesu amesema “Ndugu zangu, kuna faida gani mtu kusema ana imani lakini haonyeshi vitendo? Je hiyo imani yake yavezaje kumwokoa? Kama kaka au dada akiwa uchi na hana chakula cha kila siku je mmoja wenu atawaambia, “Nendeni salama mkaote moto na kushiba, bila ya kuwapatia mahitaji yao ya maisha? Vivyo hivyo imani peke yake bila ya matendo imekufa..... Mnaona basi, kwamba, mtu hufanywa kuwa mwenye uhusiano mwema na Mungu kwa matendo yake na si kwa imani peke yake “Basi, kama vile mwili bila roho umekufa, vivyo imani bila matendo imekufa”. (Yakobo 2:14,26).

Mafundisho ya Paulo yaliyokuwa kinyume na Sheria hayakuachwa yapite kimya kimya na wanafunzi wake Yesu na watu wengine. Walishitushwa sana na upotofu huo na baadhi yao walitoka Judea na kwenda mpaka kwenye makao makuu ya mahubiri ya Paulo na kuwaambia wale waliojiunga naye kwamba, “Kama hamtatahiriwa kufuatana na maamrisho ya Sheria ya Musa hamtaweza kuokoka”. (Matendo 15:1 ).

Matokeo ni kwamba kukazuka mgogoro na mabishano kati yao na Paulo. Hii ilimfanya Paulo pamoja na baadhi ya wafuasi wake waende Yerusalem ambako mkutano uliitishwa ili kutatua tatizo hili na mkutano huo ulihudhuriwa na wazee, mitume na wanafunzi wengine wa Yesu. Mkutano huo ukawa na zogo na ubishi mkali sana. Kwa wakati huu, mahubiri ya Paulo yalikuwa yamekwisha pata nguvu na ilikuwa vigumu sana kwa mitume wengine kuyazuia. Kwa upande mwingine wale waliokwenda kuwashubiria Mayahudi tu hawakuweza kufanya maendeleo yo yote na wakaanza kukata tamaa siku hata siku, ya kupata ushindi wo wote dhidi ya Kiyahudi. Kwa kushawishiwa na matatizo haya mawili Petro alisimama na kuunga mkono mawazo ya Paulo. Mwishowe Yakobo akatoa hotuba ndefu na aliifunga hotuba yake kwa kusema:-

“Ushauri wangu ni kwamba wale mionganini mwa mataifa mengine ambao wanaelekezwa kwa Mwenyezi Mungu tuisiwafanyie matata.”

Mwishoni mwa kikao hicho watu wa mataifa mengine waliandikiwa barua ifuatayo: “Sisi mitume, wazee na ndugu zenu tunawasalimuni ninyi ndugu wa Mataifa mengine mlioko huko Antiochia, Sina na Kilikia. Kwani tumesikia kwamba watu wengine kutoka huko kwetu waliwavurugenii kwa maneno yao na kuitia mioyo yenu katika wasiwasi kwa kuwaambieni kwamba ni lazima mtahiriwe na kutii Sheria. Sisi hatukuwaamrisha kufanya hivyo..... kwani Roho Mtakatifu na sisi tumekubaliana kwamba tuisiwaitwishe mzigo zaidi ya mambo muhimu yafuatayo: Msile vyakula vilivyotolewa sadaka kwa masanamu; msinywe damu; msile nyama ya mnyama aliyenyonwa na mjiepushe na uasherati”. (Matendo 15:23, 30).

## BADALA YA SHERIA YA MUSA NI KRISTO

Alipoona kwamba juhudii zake zimepata ushindi baada ya kukubaliana kuwa awahubirie watu wa Mataifa mengine bila ya kuwalazimisha kufuata Sheria ambapo Mayahudi watakuwa wanafuata sehemu ndogo tu ya Sheria, Paulo akaruka tena mipaka

ya uwezo wake na kuhubiri kukomeshwa kwa Sheria yote siyo tu kwa Mataifa mengine bali pia kwa Mayahudi akisisitiza kwamba badala ya kufata sheria watu wawe na imani katika damu ya Yesu.

Ndipo akasema: "Sheria ilikuwa kama mlezi wetu mpaka alipokuja Kristo, ili kwa njia ya imani tufanywe kuwa wenyewe uhusiano mwema na Mwenyezi Mungu. Tangu kufika kwa hiyo imani, Sheria si mlezi wetu tena". (Waglatia 3:24, 35). Agano hili jipya limelifanya lile la kwanza kuwa kuukuu. Na cho chote kinachooza na kuchakaa ni lazima kipotee hivi punde". (Waebirania 8: 13).

Baada ya kuagwa na Paulo, wanafunzi wake Yesu waliwajibu Mayahudi waliokuwa wakiwacheka na kudai kwamba walisababisha Masihi wao afe kifo cha 'laana' kwamba Yesu amefufuka kutoka katika wafu. Lakini ilikuwa vigumu kuthibitisha kufufuka kwake. Kwa sababu yeye hakujitokeza hadharani na alibakia mafichoni kwa muda wote aliokaa pale. Alipohamia nchi nyininge wanafunzi wake walisema kimethali kwamba amepaa mbinguni. Jibu hili lilikuwa halilingii akilini zaidi kuliko lile la kwanza na pia halikuwatoshelleza Mayahudi ambao walimdhania kwamba amekufa kifo cha "laana". Wakati Paulo alipotangaza kukomeshwa kwa Sheria na kuwaondolea watu ulazima wa kutii Sheria akawaambia Mayahudi kwa majivuno makubwa kwamba ni kweli kama walivyosema wao kwamba amekufa kifo cha "laana" "Lakini amekufa hivyo ili atuokeo na laana ya Sheria ambayo imefanywa laana kwetu sisi, kwani imeandikwa kwamba amelaaniwa kila atungikwaye mtini". (Wagalatia 3:13). Wakati huu, imani ya kwamba dhambi zinasamehewa kwa kutoa sadaka na kuchinja dhabihu za wanyama ilikuwa imeenea sana mionganoni mwa Mayahudi. Ndiyo sababu mtume Mika anasema:-

"Nitakwendaje mbele ya Bwana na kumsujidia Mwenyezi Mungu? Je nitakwenda mbele yake nikiwa na sadaka zilizoungua pamoja na ndama mwenye umri wa mwaka mmoja? Je bwana atafurahishwa na maelfu ya kondoo au na mito elfu kumi ya mafuta? Je nimtoe mwanangu wa kwanza kwa sababu ya makosa yangu yaani tunda la mwili wangu

kwa ajili ya dhambi ya roho yangu?” (Mika 6:6;7). Paulo akaichukulia imani hii kuwa ndiyo msingi wa kukomeshea Sheria na ndipo akasema:

“Yesu alilingia mahali patakatifu kwa damu yake yeye mwenyewe na akatupatia ukombozi wa milele. Kwani, ikiwa damu za ngo’mbe na za mbuzi na majivu ya ndama wanayopakwa watu wenye najisi huweza kutakasa miili itakuwaje kwa damu ya Kristo ambaye kwa nguvu za Roho wa milele alijitolea mwenyewe bila ya kinyongo kwa Mwenyezi Mungu, ili damu yake itakase dhamira zetu kutokana na matendo yaletayo kifo, ili tupate kumtumikia Mungu aliye hai” (Waebrania 9:12, 14). Tena anasema: “Tunao ukombozi katika damu ya Yesu Kristo na pia maondoleo ya dhambi”. (Wakolosai 1:14).

“Kristo amekufa kwa ajili ya dhambi zetu (1 Wakorintho 1:35) (Warumi 5:1 0). Kuhusu watu wa Mataifa mengine ni kwamba wao walikuwa na imani kama hii ya Paulo kuhusu miungu kama nitakavyobainisha katika sura ijayo. Hivyo basi kusulubiwa na kufufuka kwa Yesu ndiyo kukawa msingi wa mahubiri ya Paulo kwa watu wa Mataifa mengine akiwaambia kwamba Yesu Kristo “alifufuliwa kutoka wafu kulingana na Injili yangu” (2 Timeteo 2:8). “Kama Kristo hakufufuka basi mahubiri yetu ni kazi bure na imani yenu pia ni kazi bure” (1 Wakorintho 15: 14). Kwa kuwa Paulo alikuwa Mrumi (Matendo 22:25) na kutokana na misafara yake nchini Siria n.k., alizijua silika za watu wa Mataifa; mengine akauweka msingi wa mahubiri yake juu ya mawazo ya kale ya watu wa Mataifa mengine ili waweze kuyakubali kwa urahisi.

Ni dhahiri kutokana na Agano Jipyya ya kwamba Paulo hakumwona Yesu na wala hakuwapo alipotungikwa msalabani, aliposhushwa na wakati alipotoka nje ya kaburi na kuagana na wanafunzi wake. Miaka mitatu baada ya kuijunga na Ukristo alikuja mjini Yerusalem na kukaa na Petro kwa muda wa siku kumi na tano. Baada ya miaka kumi na nne akaja tena Yerusalem ili kuwafanya mitume wakubaliane naye kuhusu ukweli wa mahubiri alioyajua yeye. Sababu iliyomfanya Paulo atangulize itikadi ya kusulubiwa na

kufufuka haikuwa nyagine isipokuwa kuwateka watu wa Mataifa mengine kwa kuikomesha Sheria ili awakomboe katika dhambi na kuwaondolea taabu ya kufuata Sheria. Miongoni mwa mitume ambao walimwunga mkono na kufuata mtindo wake wa kuhubiri ni Petro ambaye alikaa naye kwa siku kumi na tano. Tunaona katika Injili ya kwamba Petro hakuwa na msimamo na alikuwa na tabia ya kigeugeu na mtu ambaye hakuwa imara katika imani yake. Tunasoma katika Injili ya Mathayo kwamba ye ye alimwambia Yesu kwamba, “Ingawaje watu wote watakuacha lakini mimi kamwe sitakuacha”. (Mathayo 26:33). Lakini kwa muda mfupi baadaye alimkana Yesu mara tatu na akasema kwa kiapo kwamba ye ye hamjui. (Mathayo 26:72).

Paulo mwenyewe anashuhudia ya kwamba Petro alikuwa mdhaifu wa imani. Anasema: “Wakati Petro alipokuja Antiochia nilimpinga wazi wazi mbele yake maana alikuwa amekosea. Mapema kabla watu waliotumwa na Yakobo hawajawasili hapo, Petro alikuwa akila na watu wa Mataifa mengine. Lakini baada ya kufika hao, aliacha kabisa kula na watu wa Mataifa mengine, kwa sababu ya kuwaogopa hao waliotaka watu wa Mataifa mengine watahiriwe. Hata ndugu wengine Wayahudi walimwunga mkono Petro katika kitendo hiki cha unafiki, naye Barnaba akakumbwa na huo unafiki wao. Basi nilipoona kuwa msimamo wao kuhusu ukweli wa Injili haukuwa umenyooka, nikamwambia Petro mbele ya watu wote: “Ingawa wewe ni Myahudi, unaishi kama watu wa Mataifa mengine na si kama Myahudi: unawezaje basi, kujaribu kuwalazimisha watu wa Mataifa mengine kuishi kama Wayahudi?” (Wagalatia 2:11,14).

Kwa hiyo si jambo lisilowezekana kwa mtu kama Petro, chini ya tashwishi za Paulo kuonyesha imani yake juu ya damu ya Yesu na kuhubiri kinyume cha mafundisho ya bwana wake, kwa kujisingizia kwamba aliona ndoto kama alivyoona Paulo.” Petro aliona njaa sana akatamani kupata chakula. Chakula kilipokuwa kinaandaliwa akapatwa na usingizi mzito na akaona ndoto kwamba mbingu zimefunguliwa na chombo fulani kikawa kinamshukia, kilipokaribia aliona kama ni namna ya shuka ikiwa imeshikwa pembe zake nne.

Ndani ya shuka hiyo kulikuwa na wanyama wa kila aina; wanyama wenyewe miguu minne, wanyama watambaa na ndege wa mwituni. Akasikia sauti ikimwambia “Petro amka uchinje hawa wanyama ule!” Petro akajibu “Hapana Bwana, mimi sijala kitu cho chote ambacho ni najisi au kichafu”. Ile sauti ikasikika tena ikimwambia, “Usiviite najisi vitu ambavyo Mwenyezi Muungu amevihalalisha”. Jambo hili lilikaririwa mara tatu, kisha ile shuka ikarushwa juu mbinguni”. (Matendo 10:10,16).

Kama watu hawa wangalilitafakari vema jambo hili la ndoto wangalifahamu kwamba ndoto inaweza kuwa imetokana na mawazo ya mtu mwenye kuiona. Ndoto ambayo iko kinyume na neno la Mwenyezi Mungu haiwezi kuwa imetoka kwake. Kwa vile Mwenyezi Mungu alimwambia Musa kwamba, “Nguruwe ni najisi kwako, usiile nyama yake”. (Kumbukumbu la Torati 14:8), sauti aliyoisikia Petro kwamba wanyama wote ni safi bila shaka imetoka kwa Shetani na wala siyo kwa Mwenyezi Mungu.

Kuhusu Paulo ni kwamba sisi hatuwezi kutoa maelezo mazuri zaidi kumhusu yeeye kuliko vile alivyojieleza mwenyewe. Anasema: “Kwa Mayahudi nilikuwa Myahudi ili nipate kuwateka Mayahudi; kwa wale walio chini ya Sheria nami nikawa chini ya Sheria ili niwapate hao walio chini ya Sheria; kwa wale wasiofuata Sheria nami sikufuata Sheria ili niwapate hao wasiofuata Sheria”. (1 Wakorintho 9:20, 22). Na akamtoa paka tunduni kwa kusema: “Ikiwa UWONGO wangu unamfanya Mwenyezi Mungu adhihirike na kutukuka zaidi, kwa nini basi nahukumiwa kuwa mwenye dhambi (Warumi 3:7).

Siasa hii ya Paulo ndiyo iliyomfanya ayarekebishe mafundisho ya Yesu na kudai mambo ambayo vinginevyo asingaliweza kufanya. Ingawaje yeeye hakuwa mtume akajitangaza rasmi kwamba yeeye ni mmojawapo wa mitume walioishi pamoja na Yesu. Petro, kama nilivyokwisha sema hapo juu, ametangaza wazi wazi kwamba baada ya kufufuka kwake, Yesu hakujionyesha hadharani isipokuwa kwa wanafunzi wake tu, na taarifa za waandishi wote wanne wa Injili zinathibitisha vivyo. Lakini Paulo, kwa kutaka utume wake

uonekane kuwa ndiyo wa maana zaidi, akawapinga wote hao akisema kwamba Yesu “alimtokea Kefa na baadaye aliwatokea wale kumi na wawili (ilhali walikuwa kumi na mmoja tu), kisha aliwatokea ndugu zaidi ya mia tano baadaye alimtokea Yokobo, kisha akawatokea mitume wote na baada ya hao wote akanitokea mimi”. (1 Wakorintho 15:5;9).

Kwa sababu ya kuwaridhisha watu wa Mataifa mengine, Paulo na Petro na wale waliowafuata waliibadilisha dini iliyofundishwa na Yesu. Waliamini kwamba Yesu alisulubiwa akafa msalabani na baadaye akafufuka na kwamba “alilaaniwa” ili kuwakomboa katika madhambi yao. Wakawafundisha watu kwamba ilikuwa inatosha kwa mtu kuiamini damu ya Yesu ili kupata wokovu. Pole pole dini hii iliyorahisishwa ambayo tunaweza tukaiita Upaulo, ikaanza, kupata nguvu siku hadi siku mpaka ikazifagilia mbali alama zote za kanuni zilizofundishwa na mwanzilishi wa kile ambacho hivi leo kinajulikana kama Ukristo.

## **SURA YA TISA**

### **PAULO NA UPAGANI**

Yesu, kama nilivyokwisha sema katika sura iliyotangulia, aliwakataza wanafunzi wake wasiwahubirie watu wo wote isipokuwa Waisraeli tu. Kuhusu kutumwa kwake, Yesu anasema: “Sikutumwa ila kwa Kondoo waliopotea wa Nyumba ya Israeli”. Akiyafananisha mataifa mengine na mbwa anasema: “Si vema kuchukua chakula cha watoto na kuwatupia mbwa”. (Mathayo 15:24, 26).

Katika muda wake wote wa utume Yesu aliwahubiria Waisrael tu na wanafunzi wake walifanya kadhaalika. Kama Yesu angalitumwa kwa watu wa Mataifa mengine pia basi nao angaliwahubiria vile vile. Aliishi Palestina bega kwa bega na Wayahudi. Lakini kamwe hakuwahubiri watu wa mataifa. Zile karaa chache katika Injili kama vile “yafundishe mataifa yote” katika Mathayo 28:19 ambazo zinaenda kinyume na misemo ya Yesu iliyotajwa hapo juu na suna zake, imma zimeongezwa na watu wasiojulikana au neno taifa lina maana ya kabilia na wala si taifa (Tazama Encyclopaedia Biblica). Kama karaa yenyewe inahusiana na ujaji wa mara ya pili wa Yesu, bishara hiyo imetimia katika nafsi ya Ahmad (amani na baraka za Mwenyezi Mungu juu yake) ambaye ndiye mwanzilishi wa Jumuiya ya Ahmadiyya. Jambo hili nimelieleza kirefu katika kitabu changu kiiwtacho ISLAM.

Alikuwa Mtakatifu Paulo ambaye kinyume na maagizo ya Yesu na suna ya wanafunzi wake akazua wazo la kuwahubiria watu wa mataifa mengine. Haieleweki ni kwa vipi Yesu mwenyewe pamoja na masahaba zake walioishi pamoja naye hawakuweza kuelewa kazi ya kweli aliyotumwa Yesu, lakini Paulo ambaye hakupata nafasi hata mara moja ya kukutana naye au kumsikia, akaweza kujua sababu za kweli za kutumwa kwa Yesu. Sidhani kama kuna jambo la kichekesho zaidi kuliko hili.

Yesu aliwaamrisha wazi wazi wanafunzi wake kwamba, “katika njia ya Mataifa msiende” (Mathayo 10:5) lakini Mtakatifu Paulo, kwa kukasirishwa na Mayahudi kwa sababu ya upinzani wao akasema: “Mimi sina lawama, na kuanzia sasa nitawaendea watu wa Mataifa mengine”. (Matendo 18:6).

Matokeo ya kuruka kwake ile mipaka iliyowekwa na Yesu katika kuhubiri ndiyo yale ambayo Yesu alitabiri akisema: “Msiwape mbwa vitu vitakatifu wasije wakageuka kuwararua ninyi, wala msiwatupie nguruwe lulu zenu wasije wakazikanyaga” (Mathayo 7:6).

Wakati Mtakatifu Paulo alioanza kuwahubiria watu wa Mataifa mengine tabia yao ikamlazimisha kurekebisha kanuni zilizofundishwa na Yesu. Akamfanya Yesu aliyesulubiwa afanane fanane na vile walivyoiamini miungu yao. Hapa chini nitataja mifano michache ya miungu ambayo Wapagani waliiamini.

1. Katika sikuu ya Adonis ambayo ilikuwa ikifanyika Asia Magharibi au katika nchi za Kiyunani, kulikuwa kunaombolezwa kifo cha mungu huyo kila mwaka kwa vilio vya majonzi makuu hususa na wanawake. Sanamu za mungu huyo zilizovalishwa nguo kama maiti zikapelekwa kwenye mazishi kwa kutupwa baharini au katika mito. Katika baadhi ya sehemu kufufuka kwa mungu huyu kulisherehekewa siku inayofuata. Katika mji wa Alexandria watu waliomboleza kwa matumaini makubwa kwani waliimba kwamba aliyepotea atarudi tena. Kwenye mahali patakatifu paitwapo Astarte katika kitongoji cha Byblus mjini Foenike kifo cha Adonis kiliombolezwa kila mwaka lakini asubuhi yake akaaminiwa kuwa alifufuka kupaa mbinguni mbele ya wanaomwabudu. (Sir James Frazer Adonis, Attis, Osiris, Ed. 2 uk. 183 - 84, Macmillan & Co. Ltd. London 1907).

## **2. MUNGU ALIYETUNGIKWA MTINI**

Katika zama za kale kulikuwa kuhani mmoja aliyeitwa kwa jina la Attis na akawa anafanya kazi zile zile za Mungu Attis katika sikuu ya Cybele iliyokuwa ikisherehekewa wakati wa msimu wa maua, kuhani huyu aghalabu alitundikwa au kuchinjwa juu ya mti mtakatifu. Hatimaye mila hii ya kishenzi ikalegezwa na kuwekea sura hii tuionayo hivi leo ya kwamba kuhani anajitoa damu chini ya mti na badala ya yeye mwenyewe kutungikwa juu ya mti, inachukuliwa sanamu yake na kutungikwa mtini. Katika msitu mtakatifu wa Upsale watu na wanyama walitolewa dhabihu kwa mungu aitwae Odin. Mara nyingi waliuawa kwa kutungikwa mtini au kwa njia zote mbili, yaani kutungikwa mtini na kuchomwa mkuki. Yaani watu walikuwa wakifungwa juu ya mti au kwenye viguzo vya kunyongea na kisha kuchomwa kwa mkuki. Kwa hivyo Odin aliiwta Mola wa viguzo vya kunyongea au mungu wa walionyongwa na katika

picha huonekana ameketi chini ya viguzo vyatanya kunyongea. Kwa hakika mtu husema kuwa amejitoa dhabihu kwa faida ya nafsi yake mwenyewe kwa njia ya kawaida iwapo atauawa kwa kumridhisha Odin. Tunalijua jambo hili kutokana na aya zilozomo kwenye 'HAVAMAL', ambazo ni kipimo cha hatima ya maisha ya mtu. Aya hizo! ambazo hueleza jinsi mungu mmoja alivyojipatia uwezo wa kiungu kwa kujitoa dhabihu ni hizi zifuatazo:-

Ninajua ya kwamba nilining'inia juu ya mti uyumbao kwa upemo kwa mausiku mazima tisa; Nikiwa nimechomwa mkuki, ili nitolewe dhabihu kwa Odin, Mimi mwenyewe kwa hiyari yangu na kwa faida ya nafsi yangu. (Sir James Frazer, Adonis, Attis ...uk. 243 - 244).

3. Arthur Weigall anaandika ya kwamba: Mojawapo ya makao makuu ya awali ya Ukristo ni mji wa Antiochia, lakini katika mji huo huo kila mwaka kulikuwa na sikukuu ya kuadhimisha kufa na kufufuka kwa mungu Tammuz au Adonis. Neno Adonis maana yake ni Mola au Bwana. Ile sehemu iliyoko Bethelehemu ambayo Wakristo wa mwanzo waliichagua na kudai kuwa ndipo mahali alipozaliwa Yesu ni (a) mahali ambapo pana mzimu wa kale wa huyu Mungu wa kipagani Tammuz. Mtakatifu Jerome alifadhaika sana alipogundua ukweli huu, jambo linaloonyesha kwamba baada ya muda mrefu kupita watu walianza kuvurugikiwa na wakazichanganya habari za mungu Tammuz au Adonis na zile za Yesu Kristo. Mungu huyu aliaminiwa kuwa alikufa kifo cha mateso akashuka kuzimu, akafufuka na hatimaye akapaa mbinguni. Kwenye sikukuu zilizofanyika katika nchi mbalimbali, watu waliomboleza kifo cha mungu huyu, sanamu ya mwili wake ilitengenezwa na kisha ikaoshwa na kukafiniwa tayari kwa mazishi. Siku iliyofuata, kufufuka kwake kulisherehekewa kwa shangwe na vifijo. Yumkini wakiimba na kusema, "Bwana amefufuka". Sikukuu hiyo ilihitimishwa kwa sherehe za kupaa kwake ambako kulishuhudiwa na wafuasi wake. (Weigall, Paganism in our Christianity, uk. 110-111). Kuna kipengele kimoja katika visa vyatanya Injili ambacho inaelekea zaidi kwamba kimeazimwa kutoka katika dini ya

Adonis la, bali pia katika dini zingine za kipagani. Kipengele hicho ni “kushukia kuzimu” (Weigall, Paganism in our Christianity, uk. 113).

4. Dini nyingine ambayo imeyaathiri mafundisho ya Kikristo ni ile ya mungu aliyejekwa akiabuduwa katika nchi ya Sparta. Mungu huyo aitwae Hyacinth mara nyingine alijulikana kama shujaa wa mambo ya kimbingu. Iliaminiwa kwamba mungu huyo alikufa kwa dharuba aliyopigwa kwa bahati mbaya. Sikukuu yake ilikuwa ikiadhimishwa kwa muda wa siku tatu kila mwaka wakati wa msimu wa maua au mwanzoni mwa msimu wa kiangazi. Mnamo siku ya kwanza kulikuwa na maombolezo ya kifo chake. Siku iliyofuata kufufuka kwake kukasherehekewa kwa shangwe na vifijo; na mnamo siku ya tatu kupaa kwake kulisherehekewa. Michoro iliyoko kwenye kaburi lake inamuonyesha mungu huyu akiwa anapaa mbinguni pamoja na dada yake aliyejekwa bikira wakiwa wanasindikizwa na kundi la malaika au miungu jike (Weigall, Paganism in our Christianity, uk. 155).

5. Kisha tena kukawa na shughuli ya kumuabudu Attis. Huyu Attis alikuwa mchungaji mwema wa Cybele ambaye ni mama mtukufu au mara nyingine pia aliiwtwa bikira Nana ambaye aliipata mimba ya Attis bila ya kuguswa na mwanamume ye yote kama ilivyo katika historia ya bikira Maria. Lakini mara tu alipoingia katika umri wa utu uzima Attis alijikatakata mwenyewe na akafa kwa kutokwa na damu nyingi chini ya msonobari mtakatifu. Mjini Roma sikukuu hii ya kufufuka ilikuwa ikiadhimishwa kila mwaka tarehe 22 hadi 25 March. Wakati wa sikukuu hii msonobari uliangushwa mnamo tarehe 22 March kisha sanamu ya mungu ikafungwa kwenye gogo la mti huu. Kwa njia hii Attis akawa “ameuawa na kutungikwa mtini” sawa na msemo wa Biblia. Kisha sanamu hii ilizikwa ndani ya kaburi. Tarehe 24 March ilikuwa siku ya damu ambapo kuhani Mkuu ambaye alijifananisha na Attis alichota damu ya binadamu aliyetolewa dhabihu, na hivyo basi kwa maana nyingine anakuwa kana kwamba aliyejitoa dhabihu yeye mwenyewe. Habari hii inakumbusha juu ya maneno kwenye Waebrania yasemayo:-

"Kristo ametupatia mkombozi wa milele si kwa damu ya mbuzi wala ya ndama, bali kwa damu yake mwenyewe." Usiku ule wa tarehe 24 March yule kuhani alienda kulikagua lile kaburi na akakuta kwamba kuna mwangaza ndani yake na kwamba hatimaye ikagunduliwa kwamba hakuwamo mtu ye yote ndani yake, yaani kwamba katika siku ya tatu yule mungu alikuwa ameshafufuka kutoka katika wafu. Mnamo tarehe 25 kufufuka kwake kukasherehekewa kwa shangwe na vifijo. Chakula cha namna fulani kilitayarishwa na kuliwa kama Sakamenti. Kisha waumini wa kwanza wa dini ile walibatizwa kwa damu ambayo iliziosha dhambi zao nao wakasemekana kuwa wamezaliwa mara ya pili. (Weigall, Paganism in our Christianity, uk. 116-11 7).

6. Wazo la msingi katika kuabudiwa kwa Adonis ni kule kufa na kufufuka kwa mungu huyu. Yeye aliuawa na nguruwe dume, lakini nguruwe huyu ni mzimu wake yeye mwenyewe. Hivyo basi mungu huyu akawa amejiua mwenyewe. Na hili ndilo wazo lililomo katika Waraka kwa Waebrania ambamo Kristo anaelezwa kuwa kuhani Mkuu ambaye kwa kutaka kuondoa dhambi za watu akajitoa dhabihu yeye mwenyewe. Kadhaalika Mithra alichinja ng'ombe dume, lakini kumbe ng'ombe huyu alikuwa yeye mwenyewe. Ng'ombe dume na mbuzi walitolewa dhabihu kwa Dionysos, lakini kumbe hao walikuwa ni yeye mwenyewe. Naye dubu alitolewa dhabihu kwa mungu Artemis lakini vile vile dubu huyu alikuwa Artemis mwenyewe na kadhaalika. Hivyo basi, wazo la mungu kujitoa kafara yeye mwenyewe kwa ajili ya dhambi ya binadamu ni jambo ambalo lilienea sana katika nchi ulimokulia Ukristo. Na kuchinjwa kwa binadamu kwa kumithilisha vifo vya miungu wasaidivu ilikuwa ni jambo la kawaida sana. Tertulion anasema ya kwamba watoto walikuwa wakitolewa dhabihu kwa mungu aitwae Satim hadi wakati wa utawala wa Tiberius. Dion Cassius anazungumza juu ya maaskari wawili walitolewa dhabihu kwa mungu aitwae Mars wakati wa enzi ya Julius Kaiza mtawala wa Rumi. Licha ya mifano michache iliyotajwa hapo juu, tunaweza kutaja visa vingi sana vyenye kuonyesha jinsi imani ya binadamu kutolewa dhabihu ilivyokuwa imeenea sana

katika zama za Ukristo. (Wegall, Paganism in our Christianity, uk. 154-155)

Fikra za kale na kale za Kiyahudi kuhusu utoaji wa: kafara ziliwu bado zimeshikiliwa sana katika zama za Kristo. Na utoaji dhabihu ya mwana kondoo, mbuzi au mnyama mwingine kwa madhumuni ya kuondoa dhambi ilikuwa ni mila ya kawaida. Na yule mbuzi<sup>a</sup> ambaye baada ya kubebeshwa dhambi za taifa zima alifukuziliwa porini ili akaliwe na wanyama mbugani; alifanywa hivyo ili kuibadilisha kidogo mila hii. Ilimuradi tu miungu wote wa kipagani walitazamiwa kupata mateso na kumwaga damu zao kwa ajili ya binadamu ambao mimbari zao ziliwu zikichuruzika damu za watu au wanyama ambao waliteswa na kuchijwa kwa ajili ya maondoleo ya dhambi. (Weigall, Paganism in our Christianity, pp. 156 - 157).

- 
- a. Wakristo wenye fikra zisizokubali mabadiliko wanadhania kwamba yule mbuzi aliyebebeshwa dhambi alitolewa dhabihu na Yesu wakisau ukweli ya kwamba mbuzi huyo hakutolewa dhabihu bali alifukuziliwa porini akiwa hai.

Sir James Frazer anasema:-

“Kutumiwa kwa mtu au mnyama wa kiungu kama kafara ni lazima kufikiriwe sana. Maovu yanasadikiwa kuwa yanahamishiwa katika nafsi ya mungu fulani ambaye baadaye huuawa. Kwa upande mmoja tumeona ya kwamba kulikuwa na desturi ya kumwua mungu mnyama au mungu mtu ili kuyaokoa maisha yake ya kiroho yasishambuliwe na kudhoofishwa na uzee. Kwa upande mwingine tumeona ya kwamba kulikuwa na uondoaji wa maovu na dhambi kila mahali mara moja kila mwaka. Hivyo basi, kama watu walilazimika kuziunganisha mila hizi mbili, wasingalikuwa na njia yo yote isipokuwa kumfanya mungu fulani afae na kisha atolewe

kafara. Kwa hiyo huyo mungu aliuawa si kwa sababu ya kuondoa dhambi bali sababu yake ni kuyaepusha maisha yake ya kiungu yasidhoofishwe na uzee. Lakini sasa, kwa vile huyu mungu amekwisha uawa kwa vyo vyote vile watu waliona afadhali wamsukumie mateso na madhambi yao ili ayabebe na kuyapeleka kwenye dunia isiyojulikana ng'ambo ya pili ya kaburi (Sir James Frazer, "Golden Bough", part 6, The Scapegoat, uk.226- 7).

Kama imani hizi za kipagani zikilinganishwa na kisa cha Yesu aliyesulubiwa kilivyoelezwa na Mtakatifu Paulo kwa Mataifa mengine tutagundua ya kwamba kisa cha Yesu ni picha halisi ya zile mila za kipagani. Kwa hakika wanafunzi wa Yesu hawakutilia mkazo juu ya kusulubiwa na kufufuka kwake, na hatuisikii sana itikadi hii mpya mpaka Paulo aliporudi kutoka Arabia na kuanza kuyahubiri Mataifa mengine. Mtu wa kwanza kufa kwake kishahidi kumeyaathiri sana mawazo ya Paulo. Taarifa za shahidi huyu mkuu tunazisoma kwenye sura ya 6 na aya 7 ya kitabu cha Matendo. Imeandikwa kwamba Stefano "ametenda maajabu na miujiza mingi mionganoni mwa Watu" Kisha akajadiliana vikali sana na Mayahudi. Aliipinga desturi ya kienyeji ya kufanya ibada mahali patakatifu ndani ya Hekalu, na akatiwa mbaroni kwa sababu ya kumkashifu Musa na Mwenyezi Mungu. Kisha akatoa hotuba nzuri sana kuhusu maandiko matakatifu lakini hakusema hata neno moja kuhusu "kufufuka" kwa Yesu katika mzozo wote huu. Kama ye ye angalihukumiwa kwa sababu ya kumfuata 'Bwana' wake aliyefufuka mbona hasemi hivyo? Katika hotuba yake nzima ye ye angalisisitiza juu ya 'ufufuo' kuliko jambo jingine lolote. Lakini hakufanya hivyo. (Review of Religions, Vol. 27, No. 9, uk. 24).

Ni Paulo tu aliyesisitiza juu ya kusulubiwa kwa Yesu naye amejawa na kiherehere kingi sana kuhusu kufufuka kwa Yesu. Ndiyo sababu anasema. "Kama Kristo hakufufuka kutoka katika wafu, basi mahubiri yetu yote ni kazi bure" (Wakorintho 15:14).

Na ni ye ye huyo huyo ambaye amesema kwamba, “Kristo ametukomboa na laana ya Sheria kwa vile amelaaniwa kwa ajili yetu. (Wagalatia 3:13). Na ni ye ye huyo huyo ambaye akijivunia msalaba wa Yesu Kristo (Wagalatia 6:14). Kundi la awali la wanafunzi wake Yesu halikuzikubali bidaa hizi zilizoanzishwa na Paulo. Walimpinga kadri ya uwezo wao. Lakini pole pole, dini hii nyepesi ingawaje ilikataliwa na Mayahudi ikawa ndiyo dini yenyekuushinda upagani wa Dola ya Kirumi. Imani na sherehe zote za kipagani zilifanyiwa mabadiliko hivi kwamba kuabudiwa kwa mungu Attis kukafanywa kuwe kuabudiwa kwa mungu Yesu. Na mara ya kwanza kabisa Yesu kutambuliwa rasmi na Kanisa kuwa ni Mungu ilikuwa kwenye Mkutano wa Nicaea, uliofanyika mnamo mwaka 325, karne tatu baada ya kusulubiwa kwake. (Paganism in our Christianity, uk. 168). Hivyo itikadi iliyoanzishwa na Paulo ikasababisha Yesu ambaye ni kiumbe mwenye kufa ahesabiwe kuwa ni Mungu, ingawaje ye ye ametumwa ili kuja kudumisha Umoja wa Mwenyezi Mungu na kufundisha kwamba hapana apasaye kuabudiwa isipoku Yeye.

### **JE YESU ALITABIRI JUU YA KUSULUBIWA NA KUFUFULIWA KWAKE?**

Mnamo mwaka 1927, nilipokuwa mjini Damascus, mjadala wa kimaandishi ulipatikana baina yangu na Mhashamu Alfred Nelson aliyekuwa mfawidhi wa Misheni ya Kikristo mjini Damascus kuhusu suala kwamba, “Je Yesu alifia msalabani?” Katika mfululizo wa mjadala huu ye ye aliniuliza swali lifuatalo:- “Kama tukiamini kwamba Yesu hakufia msalabani, je ule utabiri wake kwamba atauawa na kufufuka siku ya tatu ni wa uwongo?” Swali lake hili nimelijibu ifuatavyo:

“Huwezi ukasema kwa yakini kwamba haya ndiyo maneno halisi yaliyotamkwa na Yesu mwenyewe. Vitabu hivi vimeandikwa katika zama ambapo nadharia ya kusulibisha ambayo ilibuniwa na Paulo ilikuwa imekubaliwa na idadi kubwa ya Wakristo.

Luka kama tujuavyo alikuwa mara kwa mara akiandamana na Paulo. Alikuwa akifuatana naye katika misafara mingi. (Matendo 16:12 na 28:13).

Walikuwa wote mjini Roma (2 Timotheo 4:11). Na kulingana na kipande kimoja cha maandishi ya zamani sana, Marko alikuwa mfuasi na mkalimani wa Petro. (Encyc. Brit. Chapa 11, J. 17, uk. 729).

Zaidi ya hayo kuna kutokuelewana kuhusu NANI hasa walioziandika injili mbili zingine. Kwa hiyo si ajabu kama tukute baadhi ya sentensi zilizomo ndani ya vitabu hivi zinaunga mkono nadharia ya Paulo. Ni lazima ikumbukwe pia kwamba maneno ya utabiri huu yanahitalafiana katika Injili zote. Kwa mfano Mathayo anasema kwamba wakati Yesu alipowaambia wanafunzi wake kwamba ye ye atasalitiwa na kuingizwa mikononi mwa watu ambao watamwua “na siku ya tatu atafufuka, wanafunzi wake walihuzuni sana”. (Mathayo 17:23). Kifungu hiki cha maneno kinaonyesha kwamba wanafunzi walielewa alichosema Yesu ndijo sababu wakahuzuni. Luka anasema kwamba Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba ye ye atakamatwa na watu fulani “Lakini wanafunzi wake hawakuuelewa msemo huu, na ingawaje wao hawakuelewa lo lote lakini waliogopa kumwuliza maana ya msemo ule.” (Luka 9:45 na Marko 9:32). Na kulingana na injili ya nne inaelekea kwamba wanafunzi hawakuwa na habari kuhusu utabiri wo wote ule usemao kwamba ni lazima ye ye afufuke. (Yohana 20:9). Na Marko anasema kwamba wakati Maria Magdalena alipowaambia wanafunzi waliokuwa wakiomboleza na kulia, kwamba Yesu yu hai na kwamba ye ye amemwona wao hawakuamini.

Kisha Yesu alijitokeza mbele ya wanafunzi wake wawili. Na hao wawili walipowaambia wenzao kwamba wamemwona wenzao hawakuamini. “Kisha akawatokea wote kumi na mmoja na kuwakemea kwa sababu ya utovu wao wa Imani na miyo migumu kwa vile hawakuwaamini wale waliomwona ye ye baada ya kufufuka kwake” (Marko 16: 10-14). Kufadhaishwa na kutokuamini kwao

kuhusu habari za kufufuka kwake kunaonyesha ya kwamba wao hawakuwa na habari yo yote kuhusu utabiri wo wote wa namna hii.

Tatu, inaweza ikasemwa kwamba sehemu ya pili ya utabiri huu “Kwamba atafufuka siku ya tatu haukutimia sawasawa. Kulingana na Yohana 20:1, na Luka 24:1, Yesu alikaa ndani ya kaburi kwa mchana mmoja na mausiku mawili na wala si michana mitatu na mausiku matatu kama alivyokaa nabii Yona katika tumbo la nyangumi. Na wala hata sehemu ya kwanza ya utabiri huu haikutimia sawasawa isipokuwa tu tunaweza kusema kwamba hali inayofanana na kifo ambayo Mtakatifu Yohana aliiiona msalabani na kumshurutisha aseme kwamba “amekufa” (ufunuo 5:6) ni methali tu. Yaani yale mateso makali ambayo atayapata akiwa msalabani na ile hali ya kuzimia ambayo itatokea baada ya mateso hayo imeitwa kwa njia ya methali kuwa ni kifo.

Kwa upande mwagine zipo bishara nyingi ambazo baadhi yake nimezitaja katika sura ya kwanza. Bishara hizi zinaonyesha kwamba Mwenyezi Mungu atamwokoa Yesu kutokana na kifo cha msalaba. Kwa hivyo ni jambo lisilokanika ya kwamba wakati kila mtu alipokuwa amekata tamaa juu ya kupona kwake, Mwenyezi Mungu alimwokoa na kifo na hivyo utabiri wa Yesu ukawa umetimia. Alikaa kaburini akiwa hai kama vile Yona alivyobakia hai katika tumbo la nyangumi.

### **SURA YA KUMI UKOMBOZI AU KAFARA**

Ni wazi kabisa kutokana na sura iliyopita ya kwamba wapagani waliamini kwamba miungu yao Adonis, Attis, Osiris, Mithra nk, ilipata mateso ya kusakaramenti, ikafa na kufufuka na kwamba ilikufa “kwa sababu ya dhambi za binadamu”. Waabudu masanamu wa zama za kale na wale waliostarabika kidogo, katika nchi mbalimbali na hususa katika nchi za Afrika ya Magharibi, walikuwa na desturi ya utoaji dhabihu za kila namna. Kwa mfano katika mila za watu wa Dahomey zilizofanyika mwaka hadi mwaka, ambazo kwa hivi sasa zimeshapigwa marufuku, mamia ya

binadamu walipatikana na balaa hili la kutolewa dhabihu. Kulikuwa na aina tatu za binadamu kutolewa dhabibu katika nchi hii. (1) Kubebeshwa dhambi za watu wote na kisha kutupwa porini, (2) kupewa risala maalum na kisha kuuawa ili aifikishe risala hiyo kwa mungu fulani. (3) kuuawa ili kufidia dhambi za binadamu wote. Hata hivyo mara nyingi aina hizi tatu za uuaji zilikuwa zikiunganishwa pamoja. Mara nyingi yule mtu aliyekusudiwa kutolewa dhabihu alikamatwa na kufungiwa mahali pa upweke. Akiwa humo kizuizini mtu huyo alilishwa vizuri sana. Ili kuyahamishia madhambi yao kwa mtu huyu watu wote walimgusa mlaaniwa huyu kwa mikono yao wakati akiongozwa kwenye maandamano ya kuelekea mahali pa kutolewa dhabihu. Wakati huu kichwa cha mlaaniwa huyu hufunikwa kwa majivu. Uwanja wa kutolea dhabihu umegawanywa katika maeneo matatu ambayo yametenganishwa kwa kuta fupi hivi kwamba mtu aliye kwenye eneo moja anaweza kumwona mwingine aliye katika eneo la pili. Eneo la kwanza lilikuwa kwa ajili ya watu wa kawaida. Pili kwa ajili ya machifu na wakuu wa dini tu, na la tatu kwa ajili ya afisa mtendaji wa utoaji dhabihu pamoja na msaidizi wake tu. Damu ya mtu huyu ilitolewa kafara kwa miungu yote.” (Encyclopaedia Britannica, Ed. 11 Sacrifice).

Wazo la kuwatoa dhabihu wanyama ili kufidia madhambi ya binadamu lilipatikana katika dini ya Kiyahudi (huenda Wayahudi waliliiga kutoka kwa Wapagani wa Babilonia), lakini kamwe hawakuamini ilikuwa halali kwa binadamu kutolewa dhabihu na wala hawakuamini kwamba Masihi atatolewa msalabani ili kufidia madhambi ya walimwengu.

Yesu mwenyewe kamwe hakusema neno lolote ambalo linaweza kutafsiriwa kwa yakini kuwa na maana kwamba msamaha wa dhambi ya asili au dhambi ya kawaida na mfungamano baina ya Mwenyezi Mungu na binadamu utatokana na kifo chake. Na kamwe yeye hakusema kwamba kifo chake kihesabiwe kuwa ni kafara. Maneno yasemayo kwamba, “Mwana wa Adamu amekuja kuyatoo maisha yake ili kufidia maisha ya watu wengi” (Marko 10.:45) yanaonekana wazi wazi kwamba ni maoni ya mtunzi wa Injilli hii na wala si maneno ya Yesu. Na hata kama yametamkwa na Yesu

yanaweza kuwa na maana tu ya kwamba kwa kuwa yeye alikuwa amejitoa muhanga ili kuwapatia furaha watu wengine, basi yeye alikuwa tayari kufa peke yake kwa ajili hii bila ya kuwashirikisha wafuasi wake.

Maneno yaliyotumiwa na Yesu kwenye Karamu ya Mwisho kwa kawaida yanafikiriwa kuwa yanaonyesha kwamba kifo chake kilikuwa cha kutolewa dhabihu na ni kafara lakini hiyo ni tafsiri mbovu ya maneno yake. Ni mbovu kwa sababu katika Injili ya Mtakatifu Marko yeye anasema, “hii ni damu yangu ya Ahadi Mpya ambayo inamwagwa kwa faida ya walio wengi”, na katika Injili ya Mtakatifu Luka anasema kwamba, “kikombe hiki ndicho Ahadi mpya katika damu yangu ambayo inamwagwa kwa ajili yenu”, na ni katika Injili ya Mtakatifu Mathayo tu ambayo ilitungwa baada ya hizo zilizotajwa hapo juu, ndimo tunakuta maneno yasemayo “kwa ajili ya maondoleo ya dhambi”. Mshauri wa wanafunzi wa chuo cha Carlisle, Bwana Hasting Rashdall ameandika kwamba “Mpinzani mkali kuliko wote wa fikra hii hatasita kuyahesabu maneno haya ya nyongeza kuwa ni maelezo ya mtunzi wa Injili hii yenye kufafanua imani yake”. (H. Rashdall, The Ideal of Atonement). Na maana ya maneno mengine kwenye kifungu hicho inaweza kuwa hii ya kwamba yeye alikuwa karibuni ayatoe maisha yake kwa ajili ya rafiki zake na kufa kwa njia hii”. (Weigall, Paganism in our Christianity, p. 160).

Kwa kuyaunga mkono madai ya Mayahudi kwamba Yesu alifia msalabani, Mtakatifu Paulo pamoja na mashabiki zake wali wahubiria watu wa mataifa, mengine habari za Yesu aliyesulubiwa na kutolewa kafara ili kufidia madhambi ya walimwengu. Paulo alifanya hivi kwa sababu imani hii ilifanana na ile waliyokuwa nayo wapagani hawa kuhusu miungu yao. Mtakatifu Paulo anasema: “Katika Yesu tunao ukombozi kwa ajili ya damu yake, na pia msamaha wa dhambi”. (Wakolosai 1:14). Pia aliita damu ya Yesu kuwa “Damu ya msalaba wake”. (Wakolosai 1:20). Na katika waraka kwa Waebrania ameiita “Damu iliyomwagwa na kutawanywa”. (Waebrania 12:24). Yohana

anasema, "Yeye ndiye fidia ya dhambi zetu na siyo dhambi zetu tu, bali dhambi za ulimwengu mzima". (1 Yohana 2:2).

Wakitoa maoni yao kuhusu habari hii ya kafara, watunzi mbalimbali wa vitabu wamesema "Kulikuwa na hasira nyingi sana katika kifua cha Mwenyezi Mungu kwa sababu ya dhambi; lakini kwa ajili ya Kristo kutolewa kafara yenyewe kudumu milele, Mwenyezi Mungu ameondoa hasira yake yote, na huo ni uadilifu".

Imani ambayo imeenea sana miongoni mwa Wakristo ni kwamba Adamu alitenda dhambi kwa kula tunda lililokatazwa na baada ya yeche kupotea, binadamu wote amba ni wazao wake wamerithi dhambi zake. Hapakuwa na njia nyingine yo yote ya kujikomboa katika dhambi hii isipokuwa kwamba Mwenyezi Mungu kwa huruma yake amlete mwanawe wa pekee ambaye hana lawama, hana dhambi wala hatia, "ni Mungu kamili na ni binadamu kamili", ambaye alipata mateso kikwelikweli, akafa na kuzikwa ili kutupatanisha sisi na Baba yake na kuwa kafara siyo tu ya kuondoa dhambi ya asili bali pia dhambi zote za kawaida za binadamu". (The Book of Common Prayer).

Kabla sijatoa maoni yangu kuhusu itikadi hii ningependa wasomaji wa Kikristo waelewe kwamba mimi sina nia wala sipendelei asilani kuwaudhi jamaa zangu. Sababu ya pekee iliyonifanya nitunge kitabu hiki ni kutaka kuweka mbele yao maoni ya Kiislamu kuhusu kusulubisha, kufufuka na ukombozi ili baada ya kuyafikiria kwa makini, lile pengo la hitilafu ya imani zetu liweze kuzibwa nasi tuwe kitu kimoja katika mambo ya kiroho na vile vile mambo ya kimwili. Zifuatazo hapa chini ndizo hoja zangu zionyeshazo jinsi itikadi hii ya ukombozi isivyokubalika akilini.

1. Nadharia hii ya ukombozi imejengwa katika misingi ya dhana kwamba wakazi wote wa dunia hii ni wazao wa Adamu na Eva amba waliishi miaka elfu sita iliyopita au mapema zaidi. Uvumbuzi wa sayansi wa hivi sasa umehakikisha kwamba binadamu alikuwapo

kabla ya hawa akina Adamu na Eva wanaotajwa kwenye Biblia (Sir Arthur Keith, New Discoveries to the Antiquity of Man). Aya za 14 hadl 17 za sura ya nne ya kitabu cha Mwanzo pia zinaonyesha ya kwamba kulikuwapo na Adamu na Eva kwa sababu Kain alisema. "Nitakuwa jambazi na mhuni humu duniani na kila mmoja atakayeniona ataniu". Na Bwana akamtia alama Kain ili ye yote amwonaye asimwue. Kisha akahama pale mahali walipoishi wazazi wake na kwenda "kuishi katika nchi ya Nod mashariki ya Edom. Akajuana na mkewe naye akapata mimba na kumzalia mwana aitwaye Enoki; na kajenga mji ambao aliuita kwa jina la Enoki"

Sasa kama hapakuwapo na watu wengine walioishi wakati ule licha ya watoto wa Adamu na Eva, kwa nini huyu Bwana alimweka alama Kain ili asiuawe na yeyote? Na yule mkewe alimpata wapi? Na huo mji aliujengwaje iwapo hapakuwa na raia wengine walioishi humo isipokuwa yeye mwenyewe?

Sura ya tano ya kitabu cha Mwanzo pia inaonyesha ya kwamba wakati wa kuumbwa kwa binadamu Mungu aliumba. wanawake na wanaume na akawabariki. Na jina alilowapa wote hao ni Adamu na waliitwa hivyo katika siku ile ile waliyoumbwa (Mwanzo 5:1-2).

Hii inaonyesha ya kwamba watu wengine pia waliitwa Adamu na lilikuwa ni jina walilopewa watu wote walioumbwa. Baada ya kuthibitisha kwamba watu wote si wazao wa Adam anayesemekana kuwa alitenda dhambi, ile itikadi ya ukombozi ambayo msingi wake ni dhambi ya Adam inakuwa pukupuku.

2. Kwa hakika hakuna mtu ambaye anaweza kuwa mudhinibu mwenye kustahili adhabu mpaka awe amevunja amri ya Mungu kwa makusudi na wala si kwa bahati mbaya. Kutokana na tafsiri hii ya dhambi, Adam hakuwa mudhinibu hata kidogo. Inadhihirika kutokana na Mwanzo 2:18 ya kwamba Mungu akimpasha habari Adam kwamba atamwambia mwenzi msaidizi. Na alipomwuliza kwa nini yeye Adam, alikula tunda la mti lilitokatazwa, Adamu alijibu sawa sawa akisema,

“Yule mwanamke ambaye ulinipa ndiye aliyenipa tunda la mti ule nami nikala”. Na yule mwanamke alipoulizwa na Mwenyezi Mungu ni mambo gani haya uliyofanya, yule mwanamke akajibu, “Nyoka alinidanganya nami nikala”. Aliungama wazi wazi kwamba yeze alidanganya tu. Jambo hili linaonyesha kwamba yeze hakumwambia Adam kwamba lile tunda alilompa ale linatokana na mti uliokatazwa. Kwa hiyo kwa hakika Adam hakutenda dhambi yo yote. Hata Mtakatifu Paulo anakubaliana na maoni kama haya anaposema kwamba “Na Adam hakudanganya, bali aliyekosa ni mwanamke ambaye Alidanganya”. (1 Timotheo 2: 14). Sababu ya kufukuzwa katika Bustani ya Eden ambayo imeelezwa katika kitabu cha Mwanzo ni ya kichekesho. Imeandikwa hivi: “Bwana Mungu akasema, “Tazama binadamu sasa amekuwa kama sisi kwa kujua mema na mabaya na sasa isije akanyoosha mkono wake kwenye tunda la mti wa uhai akalila na kuishi milele. Akamfukuza katika Bustani ya Eden”. (Mwanzo 3: 22-23).

Je unaweza kuamini kwamba Mwenyezi Mungu alimwumba binadamu ili asijue mema na mabaya? Je yeze hakumwumba katika sura yake na katika mfano wake? (Mwanzo 1:26). Kifungu hiki cha maneno kinaonyesha wazi wazi kwamba kufukuzwa kwa Adam katika bustani kumesababishwa na hofu ya Mwenyezi Mungu kwamba akikaa humo huenda akala tunda la mti wa uhai na wala si kwa sababu eti alitenda dhambi. Kwa hiyo ni wazi kabisa ya kwamba hii itikadi ya Ukombozi ambayo msingi wake ni dhambi ya Adam pia ni uwongo mtupu.

Katika Kurani Tukufu Mwenyezi Mungu anasema, “Tulimwahidi Adam hapo zamani lakini akasahau: na hatukumwona na azma yo yote ya kutenda dhambi (Kurani Tukufu 20:116).

3. Yale madai ya kwamba watu wote hutenda dhambi na kwamba hapana atakayepokelewa na Mwenyezi Mungu kwa sababu ya kufuata Sheria pasipo kuamini fidia iliyolipwa na Yesu kwa ajili ya kuondoa dhambi ya asili, ni uwongo mtupu. Tunasoma katika aya

ya sita ya sura ya kwanza ya Injili ya Luka kwamba Zakaria na mkewe wote wawili walikuwa “watakatifu mbele ya Mungu; wakitembea kila mahali wakiwa wanazingatia na kutekeleza amri za Bwana bila ya lawama yo yote.” Kulingana na imani ya Waromani Katoliki, Maria mama yake Yesu hakuwa na dhambi yo yote.

4. Dhambi ya asili ni mpango tu ambao umezushwa na Wapagani wa Kikristo na haitajwi mahali po pote katika Agano la Kale. Na maoni ya viongozi wa Kikristo kuhusu suala hili yanahitilafiana.

“Katika karne ya tano, Pelegius alitangaza ya kwamba kila mtu anao uwezo wa kuwa mtakatifu kwa juhud zake mwenyewe na akawataka wanakanisa wa Roma kuutafuta utakatifu kwa kila mmoja kufuata njia yake. Mnamo mwaka 412 rafiki yake aitwae Caelestius alishtakiwa na kuhukumiwa afukuzwe na akafukuzwa katika Ukristo kwa sababu ya uzushi uliodaiwa kwamba aliufanya kwa sababu ya kuamini kwamba Adam na wazao wake wote ni viumbe wenye kufa na kukanusha watu wote kurithi matokeo ya dhambi ya Adam na akadai kwamba watoto wale wachanga hawana dhambi na kukubali kwamba kabla ya Kristo palikuwa na watu wasiokuwa na dhambi. Pelagius alisisitiza kwamba dhambi ni kitendo na wala si hali. Dhambi ni matumizi mabaya ya uhuru wa utashi na kwamba kila mtu anahuksika na atapewa adhabu kwa ajili ya matendo yake mwenyewe tu. (Encyclopaedia Britannica, Ed. 11.).

Na dini yetu Islamu, ambayo ni dini yenye hoja za kiakili na hekima nyingi, haitambui hata kidogo mpango huu wa dhambi ya asili. Mtoto mchanga huzaliwa na khulka njema kabisa na wala si kama asemavyo Mtakatifu Paulo kwamba, “Kwa asili sisi ni watoto wa laana, yaani hasira ya Mungu ambayo imetufanya tustahili adhabu”. (Waefeso 2:3).

5. Matokeo ya kawaida na ambayo ndiyo hutazamiwa kwa mtu mwenye kula au kugusa mti uliokatazwa ni kifo: “Isije (wewe) ukafa”. (Mwanzo 3:3). Kama ni kweli kwamba kwa sababu ya kusulubiwa kwake Yesu amelipa fidia ya dhambi ya asili, basi kusingalikuwa na

mwenye kufa baada ya kusulubiwa huku. Lakini bado tunashuhudia ya kwamba adhabu ya kifo bado ipo na watu wote hufa. Si hivyo tu bali mataifa ya Kikristo yamevumbua njia za haraka na za kikatili sana za kuua watu.

6. Hii imani kwamba kwa kumwua Mwanawe asiye na hatia Mwenyezi Mungu ameleta mapatano baina ya Haki yake na Huruma yake ni jambo lisiloingia akilini. “Haki ya kiasili inawezaje kuruhusu mtu asiye na hatia atiwe hatiani hata kama amependa mwenyewe? Kudhania kwamba haki inaweza kuruhusu kitu cha namna hii ni kuvunja misingi ya kuwapo kwa haki; na maana yake ni kuivunja haki yenyewe. Katika sura kama hiyo haiwezi kamwe ikaitwa haki. Ni kisasi kisichokuwa na sababu”, (The Age of Reason, by T. Paine).

Wakati Yuda alipomwomba Yusufu amchukue yeche badala ya mdogo wake, Yusufu alijibu, “Mungu anizue sana ili nisifanye jambo kama hilo; mtu ambaye kikombe kilionekana mkononi mwake, ndiye atakayekuwa mtumwa wangu. Kwa hiyo ninyi enendeni zenu kwa amani kwa baba yenu”. (Mwanzo 44: 17).

Ushahidi madhubuti uonyeshao kwamba itikadi ya kafara ni ya uwongo na ni kinyume na Haki ya Kimbingu ni kwamba wakati wana wa Israeli walipotengeneza ndama wa dhahabu na kumwabudu kama mungu, Musa aliwaambia, “Mmetenda dhambi kuu: na sasa nitakwenda juu kwa BWANA, labda nitafanya upatanisho kwa ajili ya dhambi zenu. Musa akarejea kwa BWANA na akasema, “Aaa! watu hawa wametenda dhambi kuu, wamejifanya miungu ya dhababu. Walakini sasa ikiwa utawasamehe dhambi zao ni vema, la kama sivyo, basi ninakusihii unifute mimi katika kitabu chako ulichokiandika. Bwana akamwambia Musa, “Mtu ye yote aliyetenda dhambi ndiye nitakayemfuta katika kitabu changu” (Kutoka 32:30-33). Kwa hiyo kitendo cha kumwua mtu asiye na hatia badala ya yule mwenye hatia ni kinyume moja kwa moja na haki na pia ni kinyume na huruma. Hivyo basi badala ya Mwenyezi Mungu kuzipatanisha sifa zake za Huruma na Haki ameziteketeza zote mbili.

7. Na yale madai kwamba Yesu mwenye haki amefanywa kuwa kipatanisho cha dhambi kwa ajili ya ulimwengu mzima (1 Yohana 2:2) siyo tu hayaingii akilini bali pia ni kinyume na kaanuni za kimsingi za Agano la Kale zisemazo kwamba. “Waovu watakuwa fidia kwa ajili ya watu wema na wakosefu watakuwa fidia kwa ajili ya wasio na hatia. (Methali 21:18).

8. Ile imani ya kwamba baada ya kufa kwake msalabani Yesu alikaa motoni kwa muda wa siku tatu akiadhibiwa kwa sababu ya dhambi za ulimwengu mzima ni kinyume kabisaa na yale ambayo Yesu mwenyewe alimwambia mmoja wa wezi wawili waliosulubiwa pamoja naye. Alisema, “Amini ninakwambia, hii leo wewe utakuwa peponi pamoja nami”. (Luka 23:43).

9. Inaonekana kuwa ni jambo la kipumbavu sana kuamini ya kwamba Shetani “ambaye anasemekana kuwa ndiye aliyemdanganya Eva katika sura ya nyoka, hatimaye akamlazimisha Mwenyezi Mungu Ajionyeshe kwa sura ya Yesu aliyetungikwa msalabani badala ya yeye Shetani kuonyeshwa kwa sura ya nyoka aliyetungikwa msalabani. Kwa njia hii Wakristo wanamfanya Mwenyezi Mungu aonekane kuwa ameshindwa na yule Shetani mdanganyifu aonekane kuwa ameshinda”.

10. Na hili wazo ya kwamba kwa kuiamini damu ya Yesu mtu ataokolewa na kukombolewa kutokana na adhabu ya dhambi linapingana moja kwa moja na usemi wa Yesu ufuatao:-

- (a) “Nawaambieni, kwamba kila neno chafu ambalo watu watalitamka, watatakiwa walitolee maelezo siku ya kiyama, kwani kwa ajili ya maneno yenu ninyi mtahalisika na kwa ajili ya maneno yenu mtalaaniwa”. (Mathayo 12:36-37).
- (b) Katika Mathayo 12:32 anasema, “Ye yote atakayesema

neno kumhusu Mwana wa Adamu atasamehewa kwalo, lakini yule ambaye atasema kumhusu Roho Mtakatifu hawezi kusamehewa hapa duniani wala akhera”.

- (c) “Basi mkono au mguu wako ukikukosesa, ukate ukautupe mbali nawe; ni afadhali kuingia katika uzima hali umepungukiwa na mguu au mkono, kuliko kuwa na mikono miwili na miguu miwili na kutupwa katika moto wa milele. Na jicho lako likikukosesa, ling’oe ukalitupe mbali nawe; ni afadhali kuingia katika uzima ukiwa na chongo, kuliko kuwa na macho mawili na kutupwa jahanamu””. (Mathayo 18:9).
- (d) Ndivyo itakavyokuwa katika mwisho wa dunia; Malaika watatokea na watawatenga waovu mbali na wenye haki na kuwatupa katika tanuru ya moto; ndipo kutakuwako na kilio na kusaga meno, (Mathayo 13:45- 50).
- (e) Yesu alisema, “Kwani kama mtawasamehe watu makosa yao, baba yenu aliye mbinguni naye pia atawasamehe makosa yenu. Lakini kama hamwasamehe watu makosa yao, baba yenu naye hatawasameheni makosa yenu. (Mathayo 6: 14-15).
- (f) Kama utasoma aya 31 hadi ya 46 katika sura ya 25 ya Injili ya Mathayo utajua ya kwamba watu wema wataishi milele kwa sababu ya vitendo vyao vizuri walivyofanya humu duniani na wale ambao watakuwa mkono wa kushoto (watu waovu) “watadumu katika adhabu ya milele” kwa kutofanya matendo mema. Watu wote hawa wema na waovu watakuwa Wakristo wanaomwamini Kristo. Misemo hii ya Yesu hailingani kamwe na itikadi ya ukombozi.

11. Thomas Paine ameandika: "Ninakumbuka vizuri sana ya kwamba nilipokuwa na umri wa miaka saba hivi nilisikiliza hotuba iliyosomwa na ndugu yangu kuhusu suala la hiki kinachoitwa UKOMBOZI ULIOWETWA NA KIFO CHA MWANA WA MUNGU. Hotuba hivyo ilipomalizika nami nikiwa nashuka katika ngazi zielekeazo bustanini nikaanza kuwaza juu ya yale niliyoyasikia nikajisemea moyoni kwamba ilikuwa na maana ya kumfananisha Mwenyezi Mungu na mtu mwenye hasira ambaye kwa kukosa njia nyingine ya kujilipizia kisasi akamwua mwanawe. Na kwa kuwa nilikuwa na hakika kwamba mtu mwenye kufanya hivyo hunyongwa, sikuweza kuona madhumuni iliyosababisha kutolewa kwa hotuba kama ile. Wazo hili halikuwa mojawapo la yale mawazo ambayo husababishwa na utoto. Kwangu mimi ulikuwa ni mshawasha wa akili unaotokana na hii fikra niliyokuwa nayo kwamba Mwenyezi Mungu ni mwema sana hivi kwamba hawezi kufanya jambo kama hilo, na pia Yeye ni mwenye nguvu sana kufikia dakika hii ya leo bado ninaamini vivyo hivyo na zaidi ya hayo ninaamini kwamba mfumo wowote wa dini ambao ndani yake mna kitu kiwezacho kuishitua akili ya mtoto mdogo, mfumo huo si wa kweli". (Thomas Paine: the Age of Reason, P. 41).

12. Mkristo hapa anaweza kusema, na kwa kawaida ndivyo wasemavyo Wakristo wote kwamba, "Kama mtu fulani ananidai pesa nami siwezi kumlipa, naye anatishia kunipeleka gerezani, mtu mwingine anaweza kunipokea deni lile kwa niaba yangu". Kwa hiyo basi Yesu aliye Mwana wa Mungu ameilipa fidia ya dhambi zetu kwa kukaa jahanamu kwa michana mitatu na mausiku matatu. Hii ingekuwa sawa kama dhambi ingalifanana na deni na kwamba kinyume na alivyo Mwenyezi Mungu, mdai wa deni hili hana uwezo kabisaa na ni fukara au bahili na ni mlipaji kisasi sana hivi kwamba hata kama anajua vizuri sana kwamba yule anayemda hana uwezo wa kulipa, yeye halisamehe deni hili au kulifuta mpaka yule mtu aweze kumlipa. Lakini kama dhambi ikichukuliwa kuwa jinai, yaani uvunjaji wa amri za Mwenyezi Mungu kwa makusudi hakuna sheria yo yote ya haki ambayo itamwadhibu mtu mwingine ghairi ya yule aliyeunja amri au kama dhambi itatafsiriwa kuwa ni maradhi ya roho, basi maradhi hayo hayatapona kama dawa atapewa mtu mwingine ghairi ya yule aliye fanya dhambi. Zaidi ya hayo

Yesu hakujitolea mwenyewe, bali alianguka na kusujudu akimwomba Mwenyezi Mungu Amuepushie kifo. Na kisha kwa maneno ya kujitupa kwa Mola wake na kuangukia akasema, “Baba yangu, ikiwa kikombe hiki hakiwezi kuniepuka isipokuwa nikinywe tu, basi mapenzi yako yatimizwe”. (Mathayo 26:42).

Kisha alipokuwa msalabani alilia kilio cha kutia huruma. “Mola wangu, Mola wangu, mbona Umeniacha?”. (Mathayo 27:46). Na kumhusu Yuda ambaye ndiye aliywajulisha Mayahudi mahali alikokuwa anajificha, Yesu alisema, “Ole wake! ni afadhalii asingalizaliwa”. (Mathayo 26:24).

Je baada ya yote haya kuna ye yote mwenye akili timamu ambaye atasema kuwa Yesu alijitolea mwenyewe afe kwa ajili ya wakosefu?

Matokeo ya itikadi hii iliyozushwa ni kwamba Ulaya ambayo imekaliwa na mataifa ya Kikristo ndiyo imekuwa chemchem ya Uduharia na hata zile hisia za kuepusha utendaji dhambi zimekufa kabisa miyoni mwa watu hawa.

Mhashamu H. R. Gough ameandika: “Idadi kubwa ya watu wetu hawajali kabisa kufanya dhambi. Inawezekana ya kwamba wao wenyewe si wafisadi lakini hata hivyo hawana maadili. Akili imepumbazwa sana kwa sababu ya kulazimishwa daima kupingana na mambo ya kweli hivi kwamba hakuna mlengo wa kujua wema au ubaya. Tunaonekana kana kwamba hatuoni aibu kabisaa juu ya madhambi yetu”. (The Watchman, March, 1941, p. 93, London).

Kwa nini waone haya juu ya dhambi zao? Si Mwenyezi Mungu kwa huruma Yake amemwaga damu ya Mwanawe asiye na hatia (la bali damu yake mwenyewe) kwa kuwakomboa? Walakini itikadi hii inatoa mwanya wa kufanya dhambi na imesababisha Wakristo wa Ulaya na Amerika wafanye madhambi ya ufasiki wazi wazi zaidi kuliko mahali pengine po pote ulimwenguni. Hii si kwa Wakristo wa kawaida tu bali pia kwa wahubiri na mapadre. Angalia kwenye THE CRIMES OF PREACHERS kilichotangazwa mjini New York. THE

CRIMES OF CHRISTIANITY kilichotungwa na J. M. Wheeler (London, 1887). LIFE, kilichotungwa na mtawa wa Kenmere. INSIDE THE CHURCH OF ROME; LIFE INSIDE THE CHURCH OF ENGLAND na WHY IS CHRISTIANITY A FAILURE? kilichotungwa na kiongozi mmoja wa Kanisa na kutangazwa na Ideal Publishing Union, Ltd., London.

Kwa vyo vyote vile dhambi bado zipo na hasahasa katika ulimwengu wa Kikristo. Na sifikirii ya kwamba Ukristo wa Kipaulo unaweza kuwapatia Wakristo ufumbuzi wa kupata msamaha kwa ajili ya madhambi yao. Mtakatifu Paulo anasema; "Kwani kama tutatenda dhambi kwa makusudi baada ya kuujua ukweli, hapabakii na kafara yo yote ya kuondoa dhambi." (Waebrania 10:26). Ulimwengu wa Kikristo uliojawa na madhambi ambao unayafanya madhambi hayo baada ya kuamini kwamba Kristo amesulubiwa na kufa msalabani, utakufa katika hali hiyo hiyo ya dhambi na kulingana na usemi wa Paulo uliotajwa hapo juu ulimwengu huu wa Kikristo kamwe hautaokoka.

### **KAFARA YA KWELI**

Mnamo mwaka 1943 Katibu wa Chama cha Marafiki wa Kiislamu aliniandikia barua na ndani ya barua hiyo mwanamke huyo alieleza imani aliyokuwa nayo kwa maneno yafuatayo: "Mwenyezi Mungu amekuja kwa sura ya Kristo na kuzibeba (siyo dhambi bali na adhabu pia)". Bila ya kifo cha Yesu dhambi haiwezi kusamehewa na kuletwa utakaso. Nilimjibu mwanamke huyu kwamba imani hii ni sawa sawa na kuamini kwamba Mwenyezi Mungu amejiua mwenyewe msalabani kisha akakaa jahanamu kwa siku tatu na kwamba Yeye hana haki ya kusamehe madhambi ya viumbe Vyake ila kuviadhibu tu. Na kwamba Mungu huyu hana hiari wala huruma bali amekuwa kama hakimu ambaye analazimika kumwadhibu mkosefu sawa na sheria alizopewa na wakubwa zake. Je ni huruma gani kumwua mtu asiyе na hatia kwa makosa ya watu wengine? Umuulize mtu ye yote mwenye mtoto mmoja tu akuambie iwapo ni haki au ni huruma kufanya hivyo. Kufikiri kwamba dhambi zinaweza kuoshwa

kwa damu ya Yesu ni jambo ambalo siyo tu haliingii akilini bali pia ni kinyume na aina zote za huruma na haki. Imani juu ya Mwenyezi Mungu ambayo Uislamu umeiweka mbele ya ulimwengu ni kwamba Yeye ni Mrehemevu, Mwingi wa Ukarimu na mwenye kuwasamehe sana watumishi wake. Mwenyezi Mungu asema ndani ya Kurani Tukufu kwamba: “Ewe Mtume, waambie, “Enyi watumishi wangu ambao mmejidhulumu nafsi zenu, msikate tamaa juu ya rehema ya Mwenyezi Mungu; kwa hakika Yeye ni Msamehev u sana mwingi wa huruma.” (Kurani Tukufu 39:53).

Yeye Ndiye Bwana wa mabwana na Muumbaji wa watu wote. Anaweza kumsamehe ye yote Amtakaye na anaweza kuadhibu iwapo adhabu hiyo itamfaidisha mkosefu. (Soma fumbo la mwenye nyumba ambaye aliwakodisha watu fulani na mwishowe akasema: “Je si halali kwangu kufanya lo lote nilitakalo na watu wangu?” Kwa hiyo bwana anayo haki ya kuwasamehe watumishi wake pia).

Wakati mtu mwenye dhambi anapoanguka na kuuweka uso wake kwenye kizingiti cha Mwenyezi Mungu aliye Mwingi wa Huruma na kutubu na kuomba kwa moyo mnyenyekevu na macho yaliyojawa na machozi akidhamiria kwamba kamwe hatafanya dhambi tena, hapo ndipo Mwenyezi Mungu ambaye ana huruma nyingi zaidi kuliko ile ya baba au mama, atamhurumia na kumwokoa na kumsamehe madhambi yake. Hii ndiyo njia ambayo kwayo dhambi inaweza kuondokewa kihalali. Je hamjasoma kisa cha mfalme fulani ambaye alitaka kumwadhibu mtumishi wake ambaye alikuwa akidaiwa naye talanta elfu kumi? Lakini mtumishi huyo akaanguka na kumsujudia akisema, Bwana wangu, niwie radhi ninakuomba uwe na subira nami nitakulipa talanta zote hizo. Kisha Bwana wa mtumishi huyo aliingiwa na huruma sana na akamwachia na kumsamehe lile deni<sup>a</sup> (Mathayo 18:26, 27).

---

a. Mwanamke huyo alinijibu kwamba amekisoma kisa hicho, “Lakini bila shaka mfalme huyo alijitolea sana. Kiasi chote hiki cha raslimali?” Nikamjibu, “Fikiria iwapo binadamu anaweza kulifuta deni ingawa ni la

gharama kubwa sana je hawezi kufanya hivyo Mwenyezi Mungu aliye Mmiliki wa vitu vyote ambaye kufanya kwake hivyo hakumgharimu kitu cho chote? Kisa hiki kinaonyesha ya kwamba toba na maombi ndiyo njia ya kweli ya kupatia msamaha. Lakini wewe unaamini kwamba bila ya kuimwaga damu ya mtu asiyekuwa na hatia au tuseme bila ya kujiu mwenyewe Mwenyezi Mungu hawezi kuzisamehe dhambi za watu kihalali”.

Wakati Petro ambaye alikuwa mwanafunzi wake Yesu alipomwuliza Yesu ni mara ngapi nimsamehe ndugu yangu kama ataendelea kufanya dhambi? Je nimsamehe mpaka mara saba? Je Yesu hakujibu kwamba, “umsamehe mara sabini mara saba?” Iwapo binadamu kwa sababu ya huruma zao wanaweza kuwasamehe wale wanaowakosea bila ya kuwaadhibu hata kidogo kwa nini isiwe jambo la haki na huruma kwa Mwenyezi Mungu ambaye ndiye mwinci wa Rehema kuwasamehe wale wanaofanya dhambi pasipo adhabu yo yote? Njia ya kweli ya kupata

mwanawе; ucha Mungu wa mcha-Mungu ni kwa faida ya mcha-Mungu na uovu wa mwovu ni kwa ajili ya mwovu. Lakini kama mwovu ataachana na madhambi yake yote aliyotenda na kuzifuata amri zangu na kufanya mambo ya haki na ya kisheria, mtu huyo hatakuifa. Maovu yote ambayo ameyafanya hayatatajwa kwake. Ataishi katika wema ambao ameufanya”. (Ezekieli 18:20-22). pia soma katika 2 Mambo ya Nyakati sura ya saba aya ya 12 hadi 14; na aya ya saba sura ya 55 ya kitabu cha Isaya ambamo unyenyekevu, maombi

msamaha wa dhambi ni toba. Hivi ndivyo ilivyosemwa ndani ya Kurani Tukufu na ndivyo walivyofundisha mitume wote. Kuhusu watu wafanyao dhambi Mwenyezi Mungu anasema ndani ya Kurani Tukufu kwamba: “Wataokolewa na adhabu wale ambao watatubu na kuamini na kufanya vitendo vizuri: hawa ndiyo watu ambao Mwenyezi Mungu atawabadilishia vitendo vyao vibaya kuwa vizuri: na Mwenyezi Mungu ni msamehevu Mwingi wa rehema.” (Kurani Tukufu 25:70).

Nabii Ezekieli anasema kwamba Mwenyezi Mungu alimwambia kwamba “Roho itendayo dhambi ndiyo itakayokufa. Mwana hatabeba uovu wa baba yake wala baba hatabeba uovu wa

kuutafuta uso wa Mwenyezi Mungu na kuachana na uovu zimetajwa kuwa ndio njia ambazo kwazo madhambi yanaweza kusamehewa.

Kwa hiyo kufa kwa Yesu msalabani, kama waaminivyo Wakristo, si njia ambayo kwayo dhambi inaweza kusamehewa. Bali yenye we ni dhambi kubwa sana kuamini kwamba Mwenyezi Mungu Aliye Mwingi wa rehemu alimwaga damu ya mtu asiyekuwa na hatia kwa ajili ya dhambi za watu wengine na kumlaani mtu huyo. Ninakuambieni kwa moyo na dhati ya ukweli kwamba, achilia mbali huko kusulubiwa mara moja, bali hata kama Yesu angalisulubiwa mara elfu moja asingaliweza kuwakomboa watu kutokana na madhambi yao.

Ni dhuluma ilijoje hii ya kwamba kwa kutaka kuepukana na adhabu ya madhambi yetu tunamsingizia Yesu ambaye ni nabii mpendwa wa Mwenyezi Mungu ya kwamba amelaaniwa kwa kufia msalabani, jambo lioniyeshalo kwamba moyo wake ultengana na Mwenyezi Mungu naye akawa si mtiifu kwa Mwenyezi Mungu. Moja ya sababu zilizomfanya Mwenyezi Mungu amlete Masihi Aliyahidiwa katika zama hizi, ni kumfutia Yesu masingizio ya laana ya kifo cha msalabani. Hii ni ahadi ya Mwenyezi Mungu, na ahadi yake ni lazima itimie. Wakati hauko mbali ambapo Wakristo wote waliojaaliwa fikra nzuri na hekima wataziachilia mbali imani zao mbovu walizoziiga kutoka kwa Wapagani. Yesu alikuwa nabii wa Mwenyezi Mungu tu ambaye Mwenyezi Mungu alimwokoa na kifo cha laana cha msalabani na akamfisha kifo cha kawaida kama walivyokufa manabii wengine.

**SURA YA KUMI NA MOJA**

**YESU ANAKWENDA INDIA**

**MAKABILA YALIYOPOTEYA YA WANA WAISRAELI**

Hapa kuna swalii ya kwamba, “Iwapo Yesu hakufa msalabani na wala hakupaa mbinguni, sasa amekwenda wapi?”

Wale ambao hawajui mahali alikokwenda baada ya kuagana na wanafunzi wake kwa mara ya mwisho husema tu ya kwamba ni lazima awe amekwenda mahali fulani na amefia huko. Kwa hali ilivyo, habari zake zinafanana na mtu anayelazimika kuwaaga ndugu zake na kisha anakwenda mahali kusikojulikana na harudi tena kuja

kuwaangalia. Matokeo yake ni kwamba baada ya kupata muda fulani mtu huyo atahesabiwa kuwa amekufa. Kwa mfano Profesa Heinrich Eberhard Gottlob Paulus (1761-1851) ambaye aliamini kwamba Yesu hakufia msalabani ameandika:-

Mahali hasa alikofia Yesu wanafunzi wake hawakuju na kwa hiyo wakaamua kueleza kuondoka kwa ‘Y esu ni kupaa’ (Dr. Schweitzer, The Quest of the Historical Jesus, uk. 55) Kadhalika Bwana Ernest Brougham ambaye alikuwa Hakimu wa Mahakama ya Wilaya mjini Sydney anasema:-

“Iwapo Yesu hakufia msalabani basi ni kwa namna gani, ni wapi na ni wakati gani ambapo ye ye aliitenga na maisha haya ya kidunia? Ni lazima tukubali ya kwamba hatuna ushahidi wa kutuwezesha kulijibu swalii hili. Kwa upande wangu ninatosheka kuamini ya kwamba kwa vile ye ye alikuwa binadamu ni lazima awe amefuata njia ile ile wanayopitia watu wote, “Njia iliyonyooka na ya kutisha sana, yaani kifo ambacho binadamu wote ni lazima wakipite”. Inawezekana ya kwamba pengine Yesu hakutoka katika maficho yake ya Galilaya bali alifia huko mafichoni kutokana na majeraha makubwa aliyoleta nayo. Inawezekana amefia kwenye kambi yake ya upweke kandokando ya ziwa Tiberia au pengine amefia juu ya kilele cha mlima au huenda amefia kwenye bonde fulani hivi kwamba, “Hakuna anayejua kaburi lake liko wapi hadi hii leo”, (Docker: If Jesus did not die on the Cross? uk. 70-78).

Wale ambao kwa kuzingatia misingi ya ukweli na hoja za kiakili wanakanusha kifo cha Yesu msalabani na kupaa kwake mbinguni. Wao wanaamini kwamba amekufa kifo cha kawaida, lakini hawawezi kusema amekufa lini na wapi. Katika zama zetu hili, wakati ambapo wataalamu wa Ulaya walianza kuchukulia kisa chote cha maisha ya Yesu kuwa ni uzushi kwa sababu ya kushindwa kwao kujuwa mahali alipozikwa, sauti iliyoinuliwa kutoka katikati ya nchi ya India ilitangaza mwishoni mwa karne iliyopita kwenye kijiji cha Qadian ambacho wakati huo kilikuwa hakijulikani lakini hivi sasa ni kituo mashuhuri sana cha kuhuisha Uislamu, kwamba Yesu ambaye kwa muda wa karne nyingi aliaabudiwa

kimakosa kuwa ni Mungu, na ambaye makao yake yako katika mbingu ya tatu, kwa hakika yeche amezikwa katika Mtaa wa Khan Yar mjini Srinagar katika mkoa wa Kashmir. Sauti hii ambayo iliambatana pamoja na hoja madhubuti iliwafanya maelfu ya watu wenye hekima watambue na kuamini kwamba aliyezikwa katika kaburi lile ni Yesu mwana wa Mariamu nabii wa kondoo waliopotea wa Nyumba ya Israeli.

Uvumbuzi huu inshaa allahu mwishowe utaleta mapinduzi katika ulimwengu wa Kikristo na kusababisha mamilioni ya Wakristo kutupilia mbali imani ya kumwabudu binadamu na imani zingine walizoziiga kutoka katika upagani. Mvumbuzi wa kaburi hili la Yesu ni nabii wa zama hizi ambaye kutokea kwake kulitabiriwa na manabii wa mataifa mbalimbali na ambaye ufikaji mara ya pili wa Yesu umetimizwa katika dhati yake.

Kulingana na Kurani Tukufu na bishara ya Musa katika kumbukumbu la Taurati 18:18, Muhammad, amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake, amefananishwa na Musa, na Ahmad, amani juu yake, ambaye ndiye nabii wa zama hizi amefanana na Yesu vile yeche ameitimiza bishara ya kuja mara ya pili kwa Yesu.

## **KABURI LA MUSA**

Tunasoma katika kumbukumbu la Taurati 34:6 kwamba “Hakuna mtu ajuaye liliko kaburi la Musa hadi hii leo”. Zaidi ya hayo, hatima yake Musa, imebakia imezungukwa na visa vya uwongo tu. Kumuhusu Musa imesemwa kwamba, “Baada ya kuagana na watu wake, alikuwa anakwenda kuungana na Yohana na Elieza kwenye mlima wa Nebo ambapo kwa ghafla wingu likasimama juu yake naye akatoweka, ingawaje imeandikwa kwenye maandiko matakatifu kwamba amekufa, jambo limefanywa kwa kuhofia watu waseme ya kwamba kwa sababu ya ucha-Mungu wake usiokuwa wa kawaida amefanywa kuwa Mungu. (Ant. iv:8 na 48). Baadaye imani hii ikaenea sana ya kwamba Musa hakufa bali amepaa mbinguni kama Eliya. (Jewish Eccyclopaedia chini ya ‘Musa’). Mahali alipozikwa palibakia bila ya kujulikana kwa miaka

takribani elfu mbili mpaka alipokuja nabii ‘anayefanana’ na Musa yaani Mtukufu Mtume Muhammad (amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake) ndipo aliweza kuligundua.

Yeye (amani ya rehema za Mwenyezi Mungu juu yake) alisema kwamba “Wakati kifo cha Musa kilipokaribia yeye alimwomba Mwenyezi Mungu amwezeshe kwenda kufia hatua chache tu kutoka katika Nchi Takatifu iliyoahidiwa, naye aliwezeshwa na akafia huko. Abu Hurairah ambaye amearifu habari hii anasema kwamba Mtukufu Mtume aliongeza kusema, “Kama ningalifika mahali pale ningaliweza kuwaonyesheni kaburi lake ambalo liko kandokando ya barabara chini ya kilima chekundu kilichochongwa. (Sahihul-Bukari, Jalada la 2 uk. 191 chapa ya Misri, 1932). Kaburi hili maalum ambalo liko nchini Palestina linajulikana kwa Waislamu kama QABRU NABII MUSA yaani kaburi la nabii Musa.<sup>a</sup>

- 
- a. Dakta Philip anaandika kwamba “Kaburi la Musa” lipo baina ya Bahari ya Mauti na Mar Saba. Alama yake ni kwamba limeandikwa “Msikiti wa Nabii Musa” na ni mahali pazuri na mashuhuri sana pa kupumzikia
- 

mahuaji wa Kiislamu wakati wa msimu wa Pasaka. Niliona maandamano makubwa na ya kuvutia sana yakipita katika Lango la Mtakatifu Stefano mjini Yerusalem yakielekea kwenye bonde la mto Kedron na kwenye kaburi la nabii Musa (THROUGH BIBLE LANDS, uk. 305, katika maelezo. Kimeandikwa na Dakta Philip Schabb, London, James Nisbet & Co. Toleo jipya Septemba 1888).

Kadhalika kaburi la Yesu lilibakia limefichika ulimwenguni takribani kwa kipindi kile kile cha miaka elfu mbili na likaja gunduliwa na Ahmad, Masihi Aliyahidiwa ambaye ndiye anayefanana na Yesu na sasa linatambuliwa na mamia ya maelfu ya watu kama QABRU NABII ISA, yaani kaburi la nabii Yesu. Hii ndiyo kazi ya Mwenyezi Mungu ambayo machoni petu inakuwa shani kubwa sana. Hadhrat Ahmad, nabii wa zama hizi amelijadili suala hili kwa uwazi sana katika kitabu chake kiiwachoh MASIH HINDUSTAN MEIN (Yesu katika India), lakini kwa vile kijitabu hiki

Yale mataifa kumi na mawili yaliendelea kuungana na kuwa chini, ya kiongozi mmoja na kufanya taifa moja la watu wa moja mpaka alipokufa Solomon. Kisha mataifa kumi ya wana wa Israeli yaliiasi Nyumba ya Israeli na yakamfanya Jeroboam awe Mfalme wao, ambapo ni mataifa mawili tu ya Yuda na Benjamin ndiyo yaliyoendelea kuwa chini ya utawala wa Rehoboam. (1 Wafalme 12: 16-20). Mtengano huu unaweza kuchukuliwa kuwa ndicho chanzo kikubwa cha yale mabalaa ambayo yalizikumba zile falme mbili na kwa ujumla taifa zima la Kiebrania. Tilgath Pileseri alianza kuyateka mataifa ya Reben, Gadi, Naftal na nusu nzima ya taifa la Manase ambayo yalikuwa ng'ambo ya mto Yufrata. (2 Wafalme 15:29). Miaka michache baadaye Shalmaneser Mfalme wa Asyria akiuteka mji wa Samaria, akauteketeza, akawaondoa wakazi waliobaki wa Israeli, akawapeleka ng'ambo ya mto wa Yufrata na akawaleta wakazi wengine kuja kulima na kuishi katika nchi ile. (2 Wafalme 17:6 na 24 na 18, 10, 11). Huu ndiyo ulikuwa mwisho wa Ufalme wa Mataifa Kumi ya wana wa Israeli. Idadi kubwa ya Mapadre na mufasirina wanaamini kwamba mataifa haya kumi yaliyopelekwa uhamishoni hayakurudi tena katika nchi yao ya uzalendo. Wengine wanafikiri ya kwamba watu hawa walirudi katika nchi yao lakini wakati huo huo wanakubali kwamba kurudi huko hakuthibitishwi na historia<sup>a</sup> na siyo watu wote waliorudi bali idadi kubwa ya wana wa Israeli walibakia ng'ambo ya mto Yufrata. (A Complete Concordance to Holy Scripture kilichotungwa na Alexander Cruden, M. A. chini 'Mataifa') . Alfred Edersheim ameandika:-

- 
- a. Wazo hili siyo tu halina uthibitisho wa kihistoria bali inaelekea zaidi ya ni kidogo sana nitataja sehemu chache za muhimu kuhusu uvumbuzi huu.

## MATAIFA YALIYOPOTEA YA WANA WA ISRAELI

kwamba limebuniwa tu. Wangalirudi kwenye nchi yao ya uzalendo wangeonekana kwa wingi katika nyakati zote nchini Palestina, ambapo kulingana na historia haikuwa hivyo. Profesa fulani ameliunga mkono wazo hili la kubuniwa kwa kutaja kifungu cha maneno kisemacho “mataifa kumi na mawili” kilichomo kwenye Agano Jipyia lakini kifungu cha maneno hakiwezi kuubadilisha ukweli wa kihistoria. Katika maoni yao kuhusu Yoshua 4:2 waandishi mbalimbali wametoa maoni yao kuihusu Biblia na kusema kwamba: “Hivyo basi, hata baada ya idadi kubwa ya mataifa haya kupotelea utumwani, Mayahudi, kwa kujidaia hadhi na ahadi walizopewa Waisraeli wa zamani, waliona fahari kuyataja mataifa kumi na mawili kama yalikuwa bado yangalipo, ilihali wao ndiyo walikuwa wanayawakilisha”.


“Mtawanyiko” ule wa Babylonia ulikuwa umeshasambaa kila upande. Kwa upande wa Mashariki ulikuwa umesonga mbele hadi nchini India”.

Maoni ya H. S. Kehimkar (1830-1899) kuhusu suala hili ambayo yamo kwenye ukurasa wa sita wa kitabu chake kiitwacho THE HISTORY OF THE BENI ISRAEL OF INDIA yanaelekea kuwa ni sahihi zaidi. Yeye anasema kwamba baada ya kuanguka kwa dola ya Kiisraeli yale mataifa kumi hayakuwa yameondolewa yote, kwa sababu kulingana na mambo ya Nyakati sura ya 30, mabaki ya mataifa haya yalionekana hapa na pale nchini Palestina. Kwa sababu ya mabaki haya haikuwa kosa kutumia kile kifungu cha maneno kisemacho “mataifa kumi na mawili”.

Kwa jumla ni jambo la muhimu sana kukumbuka kuhusiana na mtawanyiko wa Mashariki ya kwamba ni Wayahudi wachache tu ambao wote kwa pamoja ni kiasi cha 50,000 ndiyo walioweza kurudi kutoka Babylonia. Kundi la kwanza liliongozwa na Zurubabel mnamo mwaka 537 kabla ya Yesu na la pili liliongozwa na Ezra katika mwaka 458-9 kabla ya Yesu. Wala hapakuwa na dharau yo yote iliyoelkezwa kwa Mataifa fulani. Wale Mayahudi ambao walikuwa na uwezo wa kifedha na kisiaza walibakia kule kule Babylonia. Kulingana na Josephus (Ant. 11:5) ambaye kimsingi anaungwa mkono na Philo, idadi kubwa inayokadiriwa kufikia mamilioni iliishi katika majimbo kandokando ya mto Yufrata. Simulizi zingine za baadaye zinasema ya kwamba katika Dola ya Kiajemi idadi ya Wayahudi ilikuwa kubwa sana hivi kwamba Cyrus alikataza wakimbizi wasirudi kwenye nchi yao isije nchi yake ikabakia bila ya watu. Mkusanyiko huu wa Wayahudi nchini Uajemi ukashadidi sana mpaka ukawa chombo chenye nguvu za kisiaza.

Hata hivyo idadi kubwa ya mataifa yale kumi ilipotelea katika taifa la Waebrania katika zama za Kristo na wamebakia huko hadi leo. (Alfred Edersheim, THE LIFE AND TIMES OF JESUS THE MESSIAH, UK. 8, 13, 16, LONDON, 1906.

Katika kitabu cha nne cha Ezra (13:39-45) imetangazwa ya kwamba yale mataifa kumi yalipelekwa kwenye mto Yufrata na Hosea aliyekuwa Mfalme katika zama za Shalmaneser. Walipitia kwenye sehemu finyu ya mto ule na kutoka pale wakaenda safari ya mwaka mmoja na nusu kuelekea mahali paitwapo Arzareth (Jewish Ency. 'Tribes'). Mnamo mwaka 586 kabla ya Yesu Nebuchadnezzar aliuvamia mji wa Yerusalem, akaliteketeza na kulichoma moto Hekalu na kuwachukua mateka wakazi wa mji huu waliokuwa na hali nzuri na mali nyingi na kuwapeleka Babylonia. Wale Waisraeli ambao walikuwa uhamishoni miaka 134 kabla ya wakazi wa Yuda kamwe hawakurejea nyumbani kwao. Kilichowapata kule uhamishoni kimekuwa na tunaamini kitaendelea kuwa jambo la uvumi usio na msingi. (Chambers Ency. 'Jews').




Sawa na ushahidi wa midomo na maandishi kutoka kwa watu mashuhuri wa Srinagar, Kashmir, aliyezikwa katika kaburi hili ni Nabii aitwaye Yus Asaf ambaye pia aliitwa Mwanamfalme, aliyefika Kashmir miaka 1900 iliyopita.

Mwandishi wa kitabu cha Historia, Tarik-i-Azami, iliyoandikwa miaka 200 hivi tangu leo, ameandika kuhusu kaburi hili kwamba:-

"Kaburi lililo baada ya kaburi la Sayyid Nasrud-Din hujulikana kuwa ni la Nabii aliyetumwa kwa wananchi wa Kashmir nalo laitwa KABURI LA NABII. Yeye alikuwa mwanamfalme aliyefika Kashmir kutoka nchi nyingine. Alikuwa mkamilifu katika wema, ukweli na kujitolea. Mungu alimchagua kuwa Nabii kwa kuwahubiri Wakashmiri. Aliitwa jina Yus Asaf". (Uk.82).

Itambulikane kwamba katika lugha ya Kiyahudi (Hebrew) Yus Asaf maana yake ni Yesu Mkusanyaji.



Ni dh  
kwam  
mbalir  
na tua  
kumi l

Utafit

juu ya  
ka nchi  
a India,  
nataifa

nistan,

Wakashmiri na Banii Israeli wa Bombay ni wazao wa Waisraeli.

- Kaburi lenyewe lilivyo ndani ya jengo. Kaburi hili linaelekea
1. Tunasoma katika Jewish Encyclopaedia chini ya kichwa cha maneno "Mataifa" kiyamba "Abraham Farissol anaifananaisha mto makabila ya Wayanuu Makabila ya Waisraeli katika nchi Ganga, yaani Garissa na anachukulia Banii Isralia wa India kuwa ni wazao wa Makabila Kumi Yaliyopotea". Msafiri wa kikristo, Vincent Milan, ambaye alikuwa mateka mikononi mwa Waturuki kwa miaka ishirini na mitano, na ambaye alikwenda hadi Fez ambapo kutoka

pale akafika India anasimulia kwamba alifika kwenye Mto Sambation, na pembezoni mwake alikuta wakiishi humo idadi kadhaa ya Wayahudi waliokuwa wamevaa nguo za hariri zenyne rangi ya zambarau. Walikuwa wanatawaliwa na wafalme saba na walipoambiwa wampongeze Sultani Salim, wakasema walikuwa hadi wakati huo, hawajampongeza Sultani ye yote wala mfalme.

**WAAFGHANISTAN.** - Kulingana na mila zao asilia Waafghanistan pia wanahuksiana na yale Mataifa Kumi yaliyopotea. Wanadai ya kwamba Nebuchadnazzar aliwaswaga hadi kwenye milima ya Ghor ambako wakati wakiwa kule waliendelea kupashana habari na Mayahudi wa Arabia. Matokeo ni kwamba wao waliziacha dini zao wakawa Waislamu (Malcom, HISTORY OF PERSIA, 11, 596, London, 1815). Waafghanistan hadi hii leo bado wanajiita “Banii Israila” na imekubaliwa kuwa sura zao zinafanana sana na Mayahudi. Madai ya kwamba wao ni wazao wa Waisraeli yanakubaliwa na waandishi wengi wa Kiislamu. Katika kitabu kiitwacho LOST TRIBES, uk. 143- 160, London, 1886, G. Moor pia amewafananisha Waafghanistan na yale Mataifa kumi.

## 2. Sir Henry Yule anasema kwamba:-

“Wataalamu wa Kiafghanistan ambao wanaijua vema historia yao wanawaita watu wao kuwa ni Banii Israaiila (neno la Kiarabu ambalo maana yake ni Wana wa Israel), na wanadai ya kwamba wao ni wazao wa Mfalme Saul (ambaye kwa lafudhi ya Kiislamu wanamwita Talut). Wanasema kwamba huyu Talut alikuwa na mwana aitwaye Yeremia ambaye naye alikuwa na mwana aitwaye Afghanna. Huyu Afghanna ndiye aliywazaa Waafghanistan. Idadi kubwa ya hawa Waafghanistan iliondolewa na Nebuchadnezzar na wakashika njia iendayo kwenye Milima ya Ghor na Feroza mashariki na kaskazini ya Hirat”.

## 3. Katika kitabu chake kiitwacho HISTORICAL AND DESCRIPTIVE ACCOUNT OF PERSIA AND AFGHANISTAN (New

York, 1843), James B. Frazer ameandika kwenye ukurasa 298 kwamba:-

“Kulingana na mila yao wenyewe wao Waafghanistan wanajiamini kuwa ni wazao wa Wayahudi. Na katika kitabu cha historia ya Waafghanistan kilichotungwa na Bwana Neematullahi na baadaye kutafsiriwa na Chama cha Wafasiri, mtunzi wa kitabu hiki cha karne ya kumi na sita ambacho baadaye kikatafsiriwa katika lugha ya Kiajemi anasema kwamba Waafghanistan ni wazao wa Afghan mwana wa Eremia mwana wa Saul, Mfalme wa Waisraeli ambaye wazao wake walichukuliwa mateka na kupelekwa kwenye milima ya Ghor, Kabul, Kandhar na Ghazni. Waliendelea kulinda hadhi na usafi wa dini yao mpaka walipojiunga na Uislamu.

4. Katika CIVIL AND MILITARY GAZETTE la tarehe 23 November 1988 mlitangazwa makala kuhusu suala hili ambamo mwandishi wake anasema: “Hao Waafghanistan wanadai kwamba uzao wao unatokana na mataifa ya Kiisraeli”. Baada ya kutaja majina yao ambayo yanalingana na ya Kiisraeli na kwamba wao pia wanasherehekeea Sikukuu ya Pasaka mwandishi huyu anasema: “Hivyo basi inawezekana kabisa ya kwamba Waafghanistan ni Waisraeli waliojichanganya katika mataifa ya Rajput na kwamba jambo hili linakubalika zaidi akilini mwangu kuwa ndio ufumbuzi pekee wa chanzo cha Waafghanistan”. Kisha anasema kwamba, A. K. Johnston ameirejea simulizi iitwayo: “Wakati Nadir Shah alipowasili Peshawar, machifu wa mataifa ya Yusufu Zais walimpa zawadi ya Biblia iliyoandikwa katika lugha ya Kiebrania na vifaa vingine ambavyo vilikuwa vikitumiwa katika ibada yao ya zamani. Vifaa hivyo ambavyo vilihifadhiwa na wale waliotangulia vilitambuliwa mara moja na wale Wayahudi ambao walipelekwa huko baadaye”.

5. H. W. Bellews ameandika kwamba:-

“Simulizi za watu hawa (Waafghanistan) zinawataja hao kuwa ni watu waliokuwa wakikaa katika nchi ya Syria wakati walipochukuliwa mateka

na Buhtanasar (Nebuchadnezzar) na kugawanya katika makoloni katika sehemu mbalimbali za Uajemi na Media. Kutoka katika sehemu hizi wao walihamia upande wa Mashariki kwenye chini ya milima ya Ghor baada ya kupita muda kadhaa, ambako majirani zao waliwaita “Banii Afghan” na “Banii Israaiila” yaani wana wa Afghan na wana wa Israeli. Katika kuunga mkono simulizi hii tunao ushahidi wa Nabii Esdras usemao kwamba yale mataifa kumi ya Waisraeli ambayo walichukuliwa mateka hatimaye walitoroka na kukimbilia katika nchi ya Arzareth ambayo inaaminika kuwa ndiyo nchini ya Hazarah ya siku hizi ambayo sehemu yake moja inaitwa Ghor. Katika TABAQUATI NASIRI mmetajwa habari kwamba katika enzi ya uchifu wa Shansabi kulikuwa na watu waitwao Banii Israaiila waliokuwa wakiishi katika nchi ile na kwamba baadhi ya watu hao walikuwa wakifanya biashara kwa wingi sana katika nchi zilizowazunguka. (Bellews: The Races of Afghanistan, uk. 15; Calcutta, 1880).<sup>a</sup>

---

- a. Sajini Meja H. W. Bellews ambaye alikuwa kwenye ziara ya kisasa katika mji wa Kabul alitoa darisa mbili (lectures) kuhusu suala hili katika
- 

United Service Institute kwenye mtaa wa Simla mnamo September 1880, ambazo zilitangazwa chini ya kichwa cha maneno “A New Afghan Question” (Swali jipya kuhusu Waafghanistan). “Are the Afghans Israelites”? . (Je Waafghanistan ni Waisrael?) na “Who are the Afghans?” (Waafghanistan ni nani?) Vijitabu hivi vilitangazwa na Cradock & Co. kwenye Station Press, Simla, 1880. Katika darisa hizi Meja Bellews amehakikisha kwamba Waafghastan ni Waisraeli siyo tu kwa kulingana na simulizi bali pia kwa kulinga na ukweli wa kihistoria uliomo ndani ya Biblia na vitabu vingine. Kama msomaji anapenda kujua habari zaidi kuhusiana na uzao wa Waafghanistan kutokana na Waisraeli, ninamshauri azisome vizuri sana darisa hizi.

6. Dr. Alfred Edersheim ameandika kwamba:- “Utafiti wa kisasa umeonyesha kwamba Wanestori na hatimaye (kwa ushahidi wa hali ya juu sana) Waafghanistan pia ni wazao wa yale mataifa

“M. Manouchi alikuwa mwenyeji wa Vinice na mganga mkuu wa Mfalmeh Orangzeb kwa zaidi ya miaka arobaini. Kwa kuwa alikuwa na nafasi ya kuziona taarifa za Dola ya Kimoghul na kwa vile aliruhusiwa kuifasiri kwa Kireno taarifa yo yote aliyoipenda ukweli uliomo kwenye habari alizoziantika kutokana na tafsiri hizi si jambo la kutiliwa mashaka”.

Akirejea maelezo kuhusu wakazi wa Kashmir ambayo ameyaona katika taarifa za Manouch, Mhashamu Marnes Hough ameandika kwenye kitabu chake kitwacho THE HISTORY OF CHRISTIANITY IN INDIA (London, 1839) kwamba:-

Katika maandishi ambayo kutokana na hayo sura hii ya nne imetungwa, mwandishi wake ametaja mambo fulani kuhusu kuonekana kwao na majaliwa ya baadhi ya wakazi wa Kashmir ambayo yatawafaa sana watu ambao katika nyakati mbalimbali wameonyesha shauku ya kutaka kuyagundua yale mataifa kumi ya Waisraeli yaliyopotea zamani. Tumeona ya kwamba yeeye amemtaja Myahudi mmoja akiwa katika mahakama ya Akbar na anaendelea kusema:-

“Kuna simulizi ya zamani isemayo kwamba wale Mayahudi ambao walichukuliwa mateka na Shalmanesar walistakimu katika nchi ya Kashmir na kwamba watu wa nchi ile ni wazao wa Mayahudi wale. yaliyopotea. (Alfred E. Edersheim: The Life and Times of Jesus The Messiah, uk. 15).

7. Colonel Sir Thomas Holdich, akiandika kuhusu Afghanistan katika toleo la kumi na moja la Encyclopaedia Britannica anasema kwamba: “Wanawake wana sura nzuri za maumbile ya Kiyahudi. (Na mara nyingi viungo vya miili ya wanaume vinafana na vya Kiyahudi”).

## 8. WAKASHMIRI

Ingawaje hatukuti mabaki ya dini ya Kiyahudi Kashmir na ya kwamba watu wote wa kule ama ni watu wasiofuata dini ya Kiyahudi au ni Waislamu, ni jambo la yakini ya kwamba kuna alama za taifa ambalo limetokana na Waisraeli. Nyuso zao na ile jinsi ya kuumbwa kwao wakazi wa hivi sasa ina kitu ambacho kinapatikana kwa Wayahudi tu ndicho kinachowatofautisha na watu wengine MUSA ni jina ambalo limeenea sana kule na minara ya zamani sana ambayo inaonekana hadi leo imewafanya wagunduliwe kuwa ni watu waliotokana na Waisraeli". (Hough: History of Christianity in India, jalada la 2 uk. 287-288; 2. Cartou: General History of the Mogul of the Mogul Empire, kilichotokana na Memoirs of M. Manouchi uk. 195-1 96).<sup>a</sup>

---

- a. Kabla ya kutaja ile simulizi ya zamani. M. Mamouchi anawaelezea Wakashmir kwa maneno yafuatayo:- "Watu hao ambao wanaikalia nchi ile ilijojaan anasa, wao ni vipande vya watu na ni wafanyakazi hodari sana ambao ni mastadi wa kulima na mashujaa katika vita" Katika maelezo ya ukurasa wa 291 Mhashamu Hough anasema kwamba, "Bwana Foster alishitushwa sana na sura zao kwa ujumla, mavazi yao na tabia zao hawa Wakashmir, bila ya kujua mapema ya kwamba kwa hakika alikuwa amefikishwa kwenye taifa la Wayahudi bila ya kutazamia". (Haya yamo kwenye Foster's Travels).
9. Katika kamusi lake la Jiografia Dakta A. Keith Johnson ameandika kwamba: "Wazalendo wa Kashmir wote ni watu warefu wenye mitambo ya miili yenye nguvu na alama za kiwanaume. Wanawake wao ni vipande vya wanamama ambao wana pua zilizokunjika kama ndoano na wana miguu na mikono ya mbinu kama ile ya Wayahudi". (Johnston: Dictionary of Geography, "Kashmir", London, 1867).
10. Katika kitabu chake kiitwacho TRAVELS IN THE MOGUL EMPIRE, 1656-1668 A.D. ambacho kimetafsiriwa na Archibald

Constable, Dakta Francois Berner ameandika kwamba: "Nilipoingia katika ufalme ule (wa Kashmir) baada ya kuivuka milima ya PIRE-PENJALE, wakazi wa vijiji vya mpakani walinishitusha sana kwa kufanana kwao na Wayahudi. Nyuso zao na tabia zao na ile hali ya pekee isiyoelezeka ambayo inamwezesha msafiri kutofautisha wakazi wa nchi mbalimbali, vyote hivyo vilionekana kwamba vinahusiana na watu wale wa zamani. Usiyachukulie haya ninayoyasema kwamba ni mambo ya kustarehesha baraza tu, kwa sababu shabihi ya Kiyahudi waliyo nayo wanavijiji hawa ilipata kudokezwa na Padre wetu mmoja wa Utawa wa Kiyesu pamoja na Wazungu wengine kadhaa zamani sana kabla mimi sijatembelea Kashmir".

Baada ya kutaja hoja chache zenye kuunga mkono maoni yake, yeye anaendelea kusema: "Hivyo basi mtaona kwamba mimi siko tayari kukanusha uwezekano wa Wayahudi kupata kuishi katika nchi ya Kashmir. Ukamilifu wa sheria yao unaweza kuwa umetetereka baada ya kupita muda mrefu ambapo pia kwa vile walikuwa katika ibada ya masanamu kwa karne nyingi, wao wakashawishika kama ambavyo hushawishika watu wengi kuifuata itikadi ya Muhammad. Ni dhahiri ya kwamba Mayahudi waliishi katika nchi ya Uajemi na vile vile katika nchi ya India kwenyaji majimbo ya Goa na Cochin"

(Bemnier: TRAVELS IN THE MOGUL EMPIRE kilichotasfsiriwa na A. Constable (1891), uk. 430-431. OUP (1914).

Katika maelezo mfasiri huyu anasema kwamba: "Alama za maumbile ya Kiyahudi walizo nazo wakazi wengi wa Kashmir zinaonekana na wasafiri wengi wa kisasa. Akizungumzia kuhusu wakazi hawa wa Kashmiri, mwanahistoria mmoja wa Kiislamu aitwae Alberuni ambaye alizaliwa mnamo mwaka 973 baada ya Kristo anasema kwamba: "Hao ni watu ambao wanajali sana nguvu za kiasili za nchi yao na kwa hiyo wanahakikisha kila mara ya kwamba wanalinda na kujenga ngome katika kila kipenyo na barabara iingiayo nchini mwao. Matokeo yake ni kwamba inakuwa vigumu sana kufanya nao biashara. Katika zama zilizopita

walikuwa wakiruhusu mgeni mmoja au wawili kuingia katika nchi yao na hususa walioruhusiwa ni Mayahudi; lakini siku hizi achilia mbali hao watu wengine, hata Baniani ambaye hawamjui vizuri hawamruhusu kuingia katika nchi yao” (uk. 206, jalada la 1, Toleo la Kiingereza, mtunzi Dakta Edward C. Sachau: London, Trubner, 1888).

11. Sir Francis Younghusband alikuwa Mwakilishi wa siasa katika Chitral mnamo mwaka 1893 hadi 1894; Kamishna wa Kingereza katika nchi ya Tibet tangu mwaka 1902 hadi 1904 na Kamishna Mkazi wa Kashmir tangu mwaka 1906 hadi 1909 ameandika kwamba: “Msafiri ambaye ni mteuzi wa kawaida tu wa mambo ya uzuri ataona wanawake wengi sana ambao ni wazuri kupindukia kila anapopita kandokando ya mto, barabarani au mitaani. Mara kwa mara ataona wanawake wenyewe uzuri wa ajabu ambao wana nyusi zenyet mpangiliano mzuri na mandhari ya Kiyahudi”. (uk. 125).

Namna nyingine za Wakashmir wa kupendeza ni Wakashmir Waislamu ambao wanapatikana mionganoni mwa wanangwa wa vijiji vilivyojengwa kwa mpango mzuri sana chini ya milima. Hapa panaonekana ile jinsi ya vizazi vyatamani kama vile vyatamani mashujaa wa Kiisraeli tuwezao kuwakumbuka. Kwa hakika baadhi ya watu wanasesha, na mimi ninakubali ingawaje sina ushahidi mwengi ya kwamba hawa Wakashmir wanatokana na yale mataifa yaliyopotea ya wana wa Israeli”.

Baada ya kuitaja ile nadharia ya Mwanzilishi wa Jumuiya ya Ahmadiyya kwamba Yesu hakufia msalabani bali aliteremshwa chini na akatoweka na kuja Kashmir ambapo hatimaye akafa na kuzikwa katika mji wa Srinagar, Sir Francis anasesha:-

“Wakati watu hawa wana maumbile ambayo yamekubaliwa kuwa ni ya Kiyahudi, ni jambo la kutia hamasa akilini mwa mtu ya kwamba nadharia hii nayo ipo; na kwa hakika kama nilivyokwisha sema kwamba zipo alama za Kibiblia ambazo huonekana katika kila sehemu ya Kashmir na hususan katika vijiji vyatamani. Kule hutakosa kila siku kumwona mchungaji wa Kiisraeli akiongoza

makundi yake ya kondoo na ng'ombe. (KASHMIR, ilivyoelezwa na Sir Franris Younghusband K. C.I. E, uk. 125, 139, 130. London, Adam & Charles Black, 1911).

Maoni haya ambayo baadhi yake yameelelezwa karne nyingi lilizopita yanaonyesha waziwazi ya kwamba Wayahudi waliotokana na yale mataifa kumi walistikimu nchini Kashmir. Maoni mawili ya mwisho ni ya Wakristo wawili ambao kwa bahati nzuri wote wawili majina yao yanafanana. Mmoja ni 'Francois' ambaye ni msafiri wa Kifaransa na mwingine ni 'Francis' ambaye ni afisa mkuu wa Kiingereza aliyefanya kazi za kijeshi na kiraia katika mikoa hii ya India.

Maoni ya huyu wa kwanza yalitolewa kabla ya kugunduliwa kwa kaburi la Yesu katika mji wa Srinagar na maoni ya wa pili baada ya kugunduliwa kwake lakini wote wawili wanaafikiana ya kwamba Wakashmiri wanaonekana kwa kila hali kuwa wametokana na jamii ya Kiisraeli. Bila shaka wao, kama aliviyotaja Sir Francis na mwezake M. Manouchi wanatokana na makabila kumi yaliyopotea ya wana wa Israeli.

Zaidi ya kufanana shabihi waliyo nayo Waafghanistan na Wakashmir kwa Wayahudi katika mandhari yao, viungo vyao vya mwili, nguo zao na baadhi ya mila zao kuna ushahidi mwingine madhubuti na wa kushawishi ya kwamba wao wametokana na Waisraeli. Ni jambo la hakika na Makazi mapya ya kizungu kama vile Canada, Australia na kadhalika yanathibitisha uhakika huu ya kwamba wahamiaji au walowezi wanayaita makao yao mapya, miji na mikoa yao kwa majina ya miji na mababu wa nchi zao za uzalendo. Ni jambo la kawaida kwa mataifa yote. Mapenzi ya namna hiyo hiyo tunayakuta yamedhihirishwa na haya mataifa kumi yaliyopotea ambayo yalikaa Afghanistan na Kashmir. Licha ya majina yao wenyewe wao waliyaita makabila, milima na mito yao kwa majina ya Mababu zao kama vile Musa Khel (mataifa ya Musa) Sulaima Zai (taifa la Sulaiman), Daud Zal (taifa la Daudi), Yusaf Zai (taifa la Yusuf). Koh-isulaiman (mlima wa Suleiman), na mto Cabul. Ikiwa kama kielelezo hapa chini

ninataja majina machache ya miji yao yanayofanana na yale ya miji ya zamani ya Syria.

|  |                      |                         |
|--|----------------------|-------------------------|
| Kuwapo kwa majina haya ya Kibiblia kunabainisha ule ukweli ya kwamba Waisraeli walipata kukaa katika sehemu hizi za India. Kuna kisa kimoja katika USUUL KAFI (kitabu cha Hadithi cha madhehebu ya Shia kilichotungwa zaidi ya miaka elfu moja iliyopita, kwenye ukurasa 18:23) kinachosema: kwamba katika nchi ya Kashmir kuliishi <i>Kashmir</i> mmoja ambaye washauri wake arobaini walikuwa <i>Marejio</i> |                      |                         |
| Wakabila zamani sana   | <i>Syria</i>         |                         |
| wati kujihisiwa wakisoma Injili, Zaburi na Maandiko matakatifu ya Ibrahimu. Waliposikia kunka kwa Mtume Muhammad (amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake) walimtuma mjumbe wao ati <i>Hima</i> (rugezunguza habari hizi. Matokayo ya 18:21 chunguzi huu karibu na Ladakh)  | <i>Cabul</i>         | <i>Waafame 9:13</i>     |
| yanwilafanya hao wote waingie katika Islamu.   | <i>Zaidon</i>        | <i>Waamuzi 18:28</i>    |
| <i>Hazarah</i>   | <i>Hazara</i>        | <i>Hesabu 33:18</i>     |
| <i>Gilgit</i>  | <i>Golgatha</i>      | Mathayo 27-33           |
| T2 <b>BANII ISRAEL</b>   | <b>WA BOMBAY</b>     | 1 Mamoo ya Nyakati 18:8 |
| Tibel  | <i>Tibbath</i>       |                         |
| Banii Israeli wa Irak semekana kuwa  | <i>Laadah</i>        | 1 Mambo ya Nyakati 4:21 |
|  | <i>Lahij Wilayah</i> | <i>Waamuzi 15:9</i>     |
|  |                      | na za kale kabla        |

ya kuja kwa Yesu. Taarifa kamili kuhusu jamii hii ya Waisraeli inapatikana katika kitabu mashuhuri sana kiitwacho THE HISTORY OF THE BENI ISRAEL kilichoandikwa na Hakim Samuel Kehimkar (1830-1899) na kutangazwa mjini Tel Avivi mnamo mwaka 1937. Mwanzoni kabisa mtunzi wa kitabu hiki anatoa taarifa za waandishi mbalimbali kuhusu jamii hii. Yeye ameandika kwamba:-

1. “Marehemu Dakta Wilson ametoa taarifa fupi kwenye Tawi la Bombay la THE ROYAL ASIATIC SOCIETY katika mukutano wake wa mwaka uliofanyika mwaka 1838 na kuitangaza taarifa hiyo katika kitabu kiitwacho LANDS OF THE BIBLE. Humo anaonyesha ya kwamba hawa Beni Israel walistakimu kwa miaka mingi sana katika nchi hii na anaonelea ya kwamba wanatokana na yale mataifa kumi yaliyopotea ya Wana wa Israeli”. Lakini katika kitabu chake kiitwacho APPEAL FOR THE CHRISTIAN EDUCATION OF THE BENI ISRAEL kilichotangazwa mnamo mwaka 1866 bwana huyu ameachana na maoni yake ya awali. Kwani katika vitabu vyake vipyta amedai kwamba mababu za Wana wa Israeli walitoka Yemen au Arabia Felix mnamo karne ya sita kulingana na kalenda ya Kikristo.
2. “Israel Joseph Benjamin (wa pili), ambaye pia ameandika taarifa kuhusu Banii Israeli katika kitabu chake kiitwacho EIGHT YEARS IN ASIA AND AFRICA (1846-1855) ambacho kimetangazwa mjini Hanover mnamo mwaka 1859, bwana huyu amemwunga mkono Dakta Wilson takriban katika sehemu zote. Yeye siyo tu anadai ya kwamba Banii Israeli ni Wayahudi halisi bali vile vile anasema kwamba hao ni wazao wa nasaba ile ile ya mataifa kumi ambayo wakati wa utawala wa Hosea ambaye alikuwa Mfalme wa mwisho wa Israeli, yalishikwa mateka na jeshi la Waasiria na kuondolewa nchini mwao”.

Kisha mwandishi huyu anaanza kuelezea historia ya awali ya hawa Beni Israel na anasema ya kwamba baada ya kuanguka kwa dola

ya Israeli na baada ya kuanguka kwa ufalme wa Yuda, mabaki ya watu hao yaliachwa nchini Palestina. "Wachache mionganoni mwa Waebrania Waliosambaa", anasema Dakta Isaac M. Wise, "walikimbilia Ethiopia, Arabia, India na Uchina. Hata hivyo idadi kubwa ya Waebrania wa Falme hizi mbili za Israel na Yuda waliishi katika Ufalme ulioziunganisha nchi za Mediteraneo na Uajemi". Mionganoni mwa Waebrania waliotawanyika ambao walikimbilia nchini India katika zama zile tunaamini ni pamoja na mababu wa ile jamii ya Kiyahudi ambayo kwa hivi sasa imestakimu kandokando ya Pwani ya Malabar na ambayo baada ya kuwasili kwa "Wayahudi weupe" ikawa inaitwa jamii ya "Wayahudi weusi". Baada ya kujadili mila na sikukuu za Kiyahudi ambazo hufanywa na hawa Beni Israel wa Bombay, mwandishi huyu anasema kwamba:-

"Tumeshataja hapo juu ya kwamba imani yetu halisi kuhusu mababu wa hawa Beni Israeli kwamba hao walikuja hapa moja kwa moja kutoka Palestina yapata miaka 175 kabla ya kuzaliwa kwa Kristo".

"Sasa ikiwa hawa mababu za Beni Israel walikuja India kutoka Yemen au sehemu nyingine miaka 1200 iliyopita au zaidi au pungufu kidogo ya hivyo, kama inavyofikiriwa, wao wangalikuwa wamesha iacha ile desturi yao ya kutoa dhabihu za nyama kama walivyofanya Mayahudi wa nchi zingine ambao wameiacha desturi hiyo tangu kuteketezwa kwa Hekalu la pili. Zaidi ya hayo, Mayahudi ambao walishikwa mateka wakati wa kuteketezwa kwa Hekalu la kwanza na hawakurudi nyumbani kwao mpaka baada ya miaka ipatayo 70, walikuwa tayari wamekwisha iacha desturi hii. Lakini kwa vile imethibitika ya kwamba desturi hii ilikuwa inaendelea kutumika mionganoni mwa Beni Israel wa India tangu muda usiojulikana, hii inahakikisha kwamba mababu wa hawa Beni Israeli kwa hakika walikuwa wao wenyewe nchini Palestina katika zama za kuwako kwa Hekalu la Pili na kwamba wao waliihama nchi hii muda fulani kabla ya kuteketezwa kwa Hekalu hili". (HISTORY OF THE BENI ISRAEL OF INDIA, uk. 5, 6, 23. Tel Aviv, 1937).

Kwa hiyo tumeona ya kwamba zamani sana kabla ya kuzaliwa kwa Yesu, idadi kubwa ya yale mataifa kumi yaliyopotea ya wana wa

Israeli ilikuwa inaishi Kaskazini, Kaskazini Magharibi, Kusini na Kusini Magharibi ya India.

## **UJUMBE WA YESU**

Yesu alikuwa Masihi kwa Wana wa Israeli na alitangaza wazi wazi kwamba, "Sikutumwa ila kwa Kondoo waliopotea wa Nyumba ya Israeli". (Mathayo 15:24). Neno 'waliopotea' linaweza kuchukuliwa kwa maana mbili. Kwa tafsiri ya neno kwa neno, au kimethali. Kwa hiyo linaweza kuwa na maana ya mataifa yaliyopotea kikwelikweli au vile vile kimethali. Kwa karne nyingi sana wao hawakuwapo katika Nchi Takatifu. Si ajabu, ndiyo maana Yesu aliwaagiza wanafunzi wake akisema, "Afadhalii waendeeni kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli". (Mathayo 10:6).

Yesu pia alitabiri ya kwamba ye ye atakwenda kuwatafuta wale wana wa Israeli ambao wamepotea na kwamba atawaona. Anasema kwamba, "Na ninao kondoo wengine ambao si wa zizi hili, hao ni lazima niwafikishie, na wataishika sauti yangu". (Yohana 10:16). Kama ilivyo, kwenye matamshi yake ya hapo juu, ye ye ametumwa kwa Wana wa Israeli tu. Kwa hiyo hawa kondoo wengine ambao hawamo mionganoni mwa Mayahudi wa Palestina wanatokana na yale mataifa kumi yaliyopotea ambayo yalisambaa katika nchi zingine. Jawabu kama hilo hapo juu pia linaweza kupatikana kutokana na usemi mwengine wa Yesu. Ye ye anasema kwamba, "Nabii huheshimiwa kila mahali isipokuwa katika nchi yake mwenyewe". (Mathayo 13:57).

Kwa hiyo kuamini kwamba Yesu hakwenda kwenye nchi nyingine yo yote ambako aliuheshimiwa ni sawa na kuamini kwamba alikuwa bila ya heshima. Kusema kwake kwamba mfano wake kutokana na njama za maadui zake walioataka kumwua unafanana na mfano wa nabii Yona pia kunaonyesha ya kwamba kama vile Yona alivyo heshimiwa na watu

wake baada ya kuwamo ndani ya turbo la nyangumi, kadhalika Yesu ataheshimiwa na wale kondoo waliopotea wa Nyumba ya Israeli baada ya kuwamo ndani ya moyo, wa nchi, yaani pango lililochongwa kwenye mwamba ambalo lilikuwa kama kaburi. Na hivyo ndivyo ilivyotokea. Yeye alikwenda katika nchi zingine walikoishi wale Kondoo waliopotea nao walimtukuzza sana. Ile simulizi ya watu wenye hekima kutoka Mashariki ambao waliizuru Palestina wakati wa kuzaliwa kwa Yesu (ambao inaelekea zaidi kuwa walikuwa Waisraeli, kwa sababu hakuna taifa lolote zaidi ya hao ambalo lilikuwa kwao, "Yu wapi yule ambaye amezaliwa ili awe Mfalme wa Mayahudi?") ilikuwa na kidokezo ya kwamba Yesu ataheshimiwa na wale Kondoo ambao walikuwa wakiishi katika nchi za Mashariki.

Yesu pia ametaja fumbo moja linalodokeza habari hiyo hiyo. Anasema, "Mnafikiraje? Ikiwa mtu anao kondoo mia na mmoja wa kondoo hao amepotea, si anawaacha wale tisini na tisa na kwenda milimani kumtafuta yule aliopotea? Na anapomwona anamfurahia zaidi yule mmoja kuliko wale tisini na tisa ambao hawakupotea?" (Mathayo 18: 12-13).

Kama haya yaliyomo kwenye fumbo hili ni ya kweli, na kama ni kweli kwamba Yesu alikuwa mchungaji mwema, na kama ni kweli kwamba yale mataifa kumi yalipotea na kusambaa katika nchi zingine kwa kutekwa na mataifa mengine ikiwa kama adhabu yao kwa ajili ya kuiacha njia ya haki na kama ni kweli ya kwamba yeye ametumwa kwa Kondoo waliopotea wa Nyumba ya Israeli, basi bila shaka ulikuwa wajibu wake mkubwa kwenda kuwatafuta Kondoo hawa waliopotea na kufurahi baada ya kuwaona.

Yesu ambaye tunamwamini kuwa ni nabii mkweli na mpendwa wa Mwenyezi Mungu hawesi kuza wajibu aliopewa na Mwenyezi Mungu. Alipoona kwamba Mayahudi wa Palestina hawako tayari kumkubali na walitafuta kila njia ya kumwangamiza, yeye aliihama nchi ile na akaenda kuwatafuta Kondoo waliopotea ambao hawakuwa wa zizi hii la Mayahudi wa Palestina.

## **MTAKATIFU THOMAS NCHINI INDIA**

Kabla sijaendelea na kuzifuatia nyayo za Yesu baada ya kuondoka Palestina ningependa kusema maneno machache kuhusu ziara ya kijasiri ya Mtakatifu Thomas aliyekuwa mmoja wa wale wanafunzi kumi wa Yesu ambaye ima aliongozana na Bwana wake katika safari yake ndefu au alifuatia baadaye ili kwenda kutimiza wajibu wake wa kuwahubiria Kondoo waliopotea wa Nyumba ya Israeli waliokuwa wakiishi Mashariki ya mbali na India. Ni lazima ikumbukwe kwamba alikuwa Mtakatifu Thomas ambaye baada ya kuziona kovu za misumari katika mikono ya Yesu alipata uthibitisho madhubuti ya kwamba mtu aliyemwona hakuwa zezeta bali ni Yesu mwenyewe akiwa na mwili wake wa kibinadamu. Na kwa njia hii yeye akawa shahidi wa kudumu ya kwamba Yesu hakufa “kifo cha laana”. Ni ukweli ambao umeeneea sana ya kwamba Mtakatifu Thomaso alikwenda India na akafia huko.

1. Dakta Francis C. Burkitt ambaye ni Professa wa mambo ya Dini katika chuo kikuu cha Cambridge anasema kwaba:-

“Eusebius (H. E.III. 1, 1,) anasema kwamba Thomas alikuwa Mwinjilisti wa “Parthia” yumkini kwa sababu Edessa ambako baadhi ya mifupa yake ilihifadhiwa mara nyingine kunaitwa Edessa ya Waparthia. Mifupa hii ilijulikana sana kwamba imeletwa Edessa kutoka India na utunzi mmoja ujulikanao kwa jina la MATENDO YA THOMAS ni ushahidi na mwongozo mkubwa kwa ajili ya Ukristo wa awali katika nchi zilizoko Mashariki ya mto Yufrata. La ajabu ni kwamba jina la Mwanafunzi huyu wa Yesu limetajwa kuwa ni Yuda bin Thomas na pale pale inaelezwa moja kwa moja ya kwamba ye ye alizaliwa pacha na Yesu Kristo”<sup>a</sup>

---

a. Kuitwa kwake pacha aliyezaliwa pamoja na Yesu Kristo

pengine maana yake ni kwamba mionganini mwa wanafunzi wake ni yeye tu ambaye alifuatana naye hadi India na akahubiri ujumbe wa Yesu kwa vile kazi ya Yesu ndiyo lilikuwa kazi yake yeye vile vile. Wala hakuna sababu yoyote madhubuti ya kumfanya yeye aitwe “pacha aliyezaliwa pamoja na Yesu”.

Inadaiwa ya kwamba haya MATENDO ni mambo ya kihistoria sana na kwamba mahali ambapo MATENDO haya yalifanyika panasemekana kuwa ni kusini mwa India. Kwa bahati mbaya Eusebio anaonelea ya kwamba ufanuzi wa MATENDO haya ya Thomas ambao unaonyesha shughuli zake nchini India unamhusisha na sehemu ya Kaskazini Magharbi<sup>a</sup> ya India na nchi iliyoko baina ya India na Mesopotamia. “Wakristo wa Mtakatifu Thomas ndilo jina ambalo mara kwa mara linatumika kwa kuwataja Wakristo wa makanisa ya Kusini mwa nchi ya India. Wazo linalonasibishwa na historia yao linahusiana sana na ile historia ya MATENDO YA THOMAS hivi kwamba ni afadhali historia ya matendo hayo ishughulikiwe hapa hapa.

---

- a. Ufanuzi huu unaafikiana na nadharia yetu Kaskazini Magharibi ndiyo Kulingana na simulizi hiyo Mtakatifu Thomas alianzilisha makanisa ya Kikristo katika sehemu za Malabar (Pwani ya kusini Magharibi) na kisha akafika Mylapur sehemu ambayo hivi sasa ni kitongoji cha Madras ambako mzimu wa kumbukumbu ya kifo chake cha kishahidi ulijengwa upya na Wareno mnamo mwaka 1547, na mzimu huo bado umesimama juu ya mlima wa Mtakatifu Thomas ambapo msalaba sehemu ambako idadi kubwa ya yale mataifa kumi yaliyopotea ilistakimishwa. Yesu na mwanafunzi wake (Mtakatifu Thomas) mwanzoni walifikia katika, sehemu za Kaskazini Magharibi na kisha Thomas alitumwa na Yesu kama walifuatana au kama Yesu alitangulia basi Thomas kwa hiyari yake mwenyewe aliamua kwenda kusini Magharibi ambako pia kulikuwa na Waisraeli waliostakimu katika sehemu zile.

unaonekana ukiwa na michoro ya kipahlavi ambayo ni ya zamani za karne ya saba. Tunajua kutokana na Cosmos Indocoplenstes ya kwamba kulikuwako na Wakristo waliotoka Uajemi (Mashariki ya Syria) na bila shaka waliotokana na madhehebu ya Nestori katika nchi ya Ceylon, katika jimbo la Malabar na sehemu za Galiana, Kaskazini ya Bombay kabla ya mwaka wa 55 kwa kalenda ya Kikristo. (Encyclopaedia Britannica toleo la 14 chini ya ‘Mtakatifu Thomas’).

kwa kalenda ya Kikristo. Aliwaita Wanazareti kwa sababu neno Wakristo lilikuwa bado halijaanza Kutumiwa” (Matendo ya Mitume 11:26). (The Spectator No. 5634, June 19, 1936, p. 1124, London).

3. Askofu mkuu Lord Lang (aliyekuwa Askofu Mkuu wa Canterbury), alisema kwenye hotuba yake iliyotangazwa kwa njia ya Radio kwamba: “Simulizi ya kwamba Mtakatifu Thomas alikwenda India bado hazijakanushwa na hapana shaka yoyote kwamba Ukristo nchini India una mizizi mirefu. (Great Britain and the East, December 3, 1936, London).

Katika kitabu chake kiiwacho INDIA, A. SHORT CULTURAL HISTORY ukurasa 92-93, H. G. Rawlinson ameandika kwamba:-

“Mmoja wa wana mfalme wa kabila la ki-saka (Indo- Parthian) aliyekuwa akiishi katika mji wa Taxila ambaye kwa Wagiriki anajulikana kwa jila la Grondophames ni mtu wa maana sana kwetu, kwa sababu kulingana

2. Baada ya kuzuru jimbo la Travancoire Mhashamu Yeats Brown ameandika kwamba:-

“Madhehebu ya zamani sana ya Kikristo siyo tu katika jimbo la Travancore bali pengine katika ulimwengu mzima ni ile iitwayo Syro-Malankaran ambayo wafuasi wake wanadai ya kwamba Mtakatifu Thomas mwenyewe ndiye aliyembatiza mtu wa kwanza wa madhehebu hiyo alipowasili katika pwani mnamo mwaka wa 59

na “Matendo ya Thomas” ambayo hayakubaliwi rasmi (apocripha), Mtume huyu Thomas alifika katika baraza la mwana mfalme huyu kuhubiri Ukristo. Hapo awali kulikuwako na utatanishi mwingi iwapo ni kweli kwamba Mtakatifu Thomas alipata kufika India au la, lakini utafiti wa hivi karibuni unaelekea zaidi kuthibitisha ya kwamba kisa hiki cha zamani kina misingi ya ukweli wa kihistoria. Batholomeo na Thomas walitumwa kwenda kuihubiri Injili katika nchi za Mashariki. Yamkini Thomas alifika Taxila kwa kupitia njia ya baharini kutoka Alexandria hadi katika baraza la Grondophames, kwani Taxila kilikuwa ni kituo cha kimataifa cha utamaduni Kilichozoea kuwasikiliza kwa moyo mkunjufu waalimu kutoka katika nchi za kigeni. Hata hivyo kazi yake ya ubashiri ilivurungwa na uvamizi wa Lusha ambapo Thomas alilazimika kukimbia. Akarudi kinyumenyume akifuatia nyayo zake hadi kwenye mdomo wa mto Indus na kutoka pale akaabiri kwenye mashua hadi Muziris ambako ni Koloni la Warumi lililokuwa katika pwani ya Malabar. Katika safari yake hii ya kuelekea Muziris alipata nafasi ya kuteremka katika bandari ya Socotra. Aliwasili mnamo mwaka wa 52 baada ya kuzaliwa Kristo na akaanzisha kanisa nchini Malabar. Miaka ishirini baadaye alizihamishia shughuli zake za mahubiri katika Pwani ya Mashariki ambako aliuawa kishahidi na kabilia la Wabrahmini. Mabaki ya mwili wake yamehifadhiwa ndani ya Kanisa kubwa lililojengwa kwa kumbukumbu yake katika mji wa Myalpore janibu ya Madras<sup>a</sup> Gondophoma ambalo ni neno la Kiajemi lenye maana ya “Mletaji Ushindi”. Katika maelezo ya Kiamenia kuhusu kisa hiki neno Gondophomes limetamkwa Gathaspar. Kutohana na neno hili likapatikana jina Gaspar ambalo ndilo jina la “Majus” wa pili mionganoni mwa wale waliokuja kumwona Yesu alipokuwa mtoto mchanga (uk. 92-93).

---

a. J. N. Farquhar. “The Apostle Thomas in Southern India”. John Rylands Library Bulletin, 1927, p.20

Askofu wa Uganda I. W. Brown ameandika kwamba:-

Kuna ushahidi ya kwamba neno “India” lililomo katika Matendo lina maana ya hii hii India ya siku hizi au tuseme lile jimbo la mipakani lililopo Kaskazini Magharibi nichini Pakistani. Mfalme Gundaphouls na nduguye Gad hivi sasa wanajulikana kuwa ni watu mashuhuri sana katika historia, ambao walikuwa wakiitawala dola ya Kihindi (Scytho-India empire), Mashariki na Magharibi ya mto Indus yapata mwaka wa 19 hadi 45 A. D. Kulikuwa na Koloni kubwa kidogo Kaskazini -Magharibi ya India mnamo karne ya kwanza ambalo huenda ndilo lililowashawishi wamisionari wa kwanza wa Kikristo kuelekea kule. Ziko taarifa zingine za kweli ambazo zinaonyesha ya kwamba mahubiri ya Mtakatifu Thomas yalifika Kaskazini. Katika kitabu kiiwacho “Book of Fate” cha mwaka 196 baada ya kuzaliwa Kristo, mtu mmoja aitwaye Bardisan anaongelea juu ya wakristo wa Parthia wakiishi pamoja na wapagani – jambo ambalo linaweza kuwa ~~janahikinambayo angajiti kwa jina hili kama Kepartihialotu kwa India~~ <sup>janahikinambayo angajiti kwa jina hili kama Kepartihialotu kwa India</sup> ~~Buto~~ <sup>Bato</sup> kaaä na wanadai ya kwamba wao ni wazao wa waumini wa Mtakatifu Thomas na wanavyo vitabu na mabaki ya vitu vya kale kuthibitisha jambo hili. Kwa bahati mbaya hakuna mtu ye yote nje ya Jumuiya hii ambaye alipata kuruhusiwa kuuona ushahidi huu.<sup>a</sup>

- 
- a. Maneno haya yanatokana na ukurasa wa 47 wa kitabu kiiwacho “Indian Christians of St. Thomas” ambayo ni maelezo yanayohusu kanisa la zamani la Kisyria la Malabar kama yalivyoelezwa na L. W. Brown, Askofu wa Uganda ambaye hapo awali alikuwa Mkuu wa Chuo cha Kerala United Theological Seminary Trivandrum, Travencore na wakati fulani alikuwa Kasisi Mkuu wa Fesus and Downing College, Cambridge, Cambridge at the University Press 1956.

na uvamizi wa majeshi ya Kusha yapata mwaka wa 50 baada ya kuzaliwa Kristo. Pia inasemekana kuwa bado kuna mataifa ya Kikristo yanayoishi Kaskazini mwa India, lakini yanaificha imani yao isijulikane na wenza. Kwa mfano katika sehemu za Indus kuna Jumuiya moja

3. Maandishi matakatifu ya Kisanskrit ya zamani ambayo yanaonekana kwenye sarafu za kale na maandishi ya Kiarami ambayo ni moja ya maagizo yaliyotolewa na mfalme Asoka ambayo yamepatikana mijini Taxila yanathibitisha ukweli huu. (Journal of the Asiatic Studies (1915) pp. 340-347 Henfed, Egriphraphia India, XIX, pp. 251-252. Tazama pia: N. A. Faris, The Arab Heritage.

4. Camb. Hist. India, uk.580-5.

5. R. A. Trotter, The History of Christianity in Sind, Conference, February, 1947. CHRISTIANS AND CHRISTIANITY IN INDIA AND PAKISTAN by P. Thomas, George Allen Unwin Ltd., London, 1954.

nchi hizi kwanza. Hadi leo hii makabila mengi yanayoishi kwenye mipaka ya India na Afghanistan yanadai ya kwamba yametokana na Waisraeli.

Baada ya kuihubiri Injili katika himaya ya Gundaphoros nchi zingine zikaomba zipatiwe huduma za Mwanafunzi huyu. Kwa vile alikuwa ni mtu mwenye bidii iliyozidi kiasi, Thomas hakuweza kujisikia kuwa yuko katika amani hata kama kulikuwa na nchi moja tu ambayo ilikuwa bado haijafikishiwa habari za maisha na mafundisho ya Bwana. Hali ya kutokuwapo na sheria ambayo ilikuwa imeenea sana katika Bara Hindi wakati ule, na habari za kuwako kwa jamii nyingi za Kiyahudi katika bandari za Pwani ya Magharibi ndizo sababu ambazo zilimlazimisha Mwanafunzi huyu aondoke katika dola ya Gundaphoros na kuelekea Pwani ya Malabar.

Inawezekana sana ya kwamba Mwanafunzi huyu wa Yesu alisafiri kwa njia ya Gundaphoros na akaihubiri Injili katika himaya yake kabla hajaitwa na watu wa kusini mwa India. Inawezekana ikasemekana hapa kwamba jimbo la Parthi pia lilihusika na shughuli za Mwanafunzi huyu. Katika nchi ya Uajemi na Afghanistan ambazo kwa wakati ule zilikuwa chini ya utawala wa Parthia. Kulikuwa na idadi kadhaa ya Mayahudi mionganii mwa wale waliotawanyika na shauku ya Mwanafunzi huyu kuwafikishia ndugu zake Habari Njema za kufika kwa Masihi ndio iliymfanya azifiki

Hivyo basi, kwa kuzitembelea sehemu yalimokuwa yanaishi yale makabila kumi yaliyopotea Mtakatifu Thomas alitekeleza wajibu ambao Yesu aliwapa wanafunzi wake wote akiwaambia “Afadhalii waendeeni Kondoo waliopotea wa Nyumba ya Israeli”.

Mtakatifu James naye aliitekeleza amri hii kwa kuandika Waraka ambao aliutuma kwa makabila yote kumi na mbili po pote yalipokuwa. Aliuanza Waraka wake kwa maneno yafuatayo: “Kutoka kwa James mtumishi wa Mungu na Bwana Yesu Kristo, kwa mataifa yale kumi na mbili ambayo yamesambaa nje ya nchi hii; Salaam”.

### **YESU ANAWATAFUTA KONDOO WENGINE**

Injili ya nne inabainisha ukweli ya kwamba Yesu alikutana na wanafunzi wake kwa mara ya mwisho kwenye bahari ya Tiberia. Akala pamoja nao kisha akaagana nao kwa mara ya mwisho na kuondoka kimoja hadi leo. Swali ni kwamba alikwenda wapi? Injili hii haina jawabu lolote. Walakini katika Matendo na Nyaraka za Mtakatifu Paulo tunasoma ya kwamba Yesu alionekana na Mtakatifu Paulo karibu ya Damascus kwa njia ya ruya. Lakini kifungu cha 1 Wakorintho 15:8 kimewafanya baadhi ya mufasiriina kuamini kwamba katika wakati ambapo Mtakatifu Paulo aliingia katika Ukristo, ambao ni baina ya miezi sita na kumi na mbili baada ya tukio la msalaba Yesu alikuwa bado yungali katika nchi ya Syria. Hakimu Docker, ambaye alikuwa Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Sydney anatoa maelezo yafuatayo kuhusu kisa cha Saulo kuingia katika Ukristo:-

“Kwa kuona kwamba hawezi kusalimika tena nchini Galilaya Yesu alianza safari yake ya kuyazuru yale mataifa ya Israeli yaliyopotelea katika nchi za Mashariki. Alipitia Damascus ambapo alikaa kwa muda mrefu kidogo kiasi cha kumwezesha kumpata mwanafunzi Anania pamoja na wengine. Hii inaweza kuwa ndiyo sababu

iliyowafanya viongozi wa Kiyahudi watumé kikosi cha kufanya vurugu katika sehemu zile. Kiongozi wa kikosi hicho alikuwa Saulo. Alipojua kwamba Saulo anakaribia kuwasili, Yesu alijitokeza kama alivyojitokeza yule Eliya wa zamani, na kwenda kukutana na adui yake huyo Saulo. Nuru ya utukufu iliyonekana katika wajihì wa Yesu ndiyo iliyomfanya huyu mtesi wake ageuke na kuwa mwanafunzi wake. Kukaa kwao pamoja yumkini kuliendelea kwa siku kadhaa ndani ya nyumba ya Anania au popote pale ambapo Yesu alikuwa aikaa. Hata hivyo, kufika kwa ujumbe huu wa Kiyahudi kulimpa ishara Yesu kwamba haikuwa salama tena kwa upande wake kubakia mjini Damascus. Ndipo akaelekea Bablonia akiwa njiani kuelekea nchi za Mashariki.

Maelezo haya yanaungwa mkono na Bwana Johannes Weiss katika kitabu chake (PAUL AND JESUS, uk. 31). "Ruya ya Paulo na kuingia kwake katika Ukristo ni mambo ambayo kisaikolojia hayakubaliki isipokuwa tu kama tukichukulia ya kwamba alikutana naye ana kwa ana na akaathiriwa sana na shani na utukufu wa Yesu". (Docker, IF JESUS DID NOT DIE UPON THE CROSS, uk. 75-76).

## **YESU KATIKA NISIBUS<sup>a</sup>**

Katika kitabu chake kiitwacho MASIH HINDUSTAN MEIN, Masihi Aliyeahidiwa akiachilia mbali zile simulizi zilizotiwa chumvi, anatoa taarifa ifuatayo kutoka katika kitabu kiitwacho RAUZA TUSSAFA (uk. J 30-135), ambacho ni kitabu mashuhuri sana cha kistoria:-

- 
- a "Nasbus (ambao watu wa Assyria waliuita Nasibina), na siku hizi unaitwa Nezib au Nasibin, ni mji wa zamani sana ambao pia ni ngome iliyoko Kaskazini. mwa Mesopotamia janibu ya mahali ambapo mto Mygdonia (ambao siku hizi unaitwa Jaghjagha) unatiririka kutoka mlimani kwa mfereji mwembamba. Mji huu una wakazi wapatao 4000 na wengi wao ni Mayahudi (Encyclopaedia Briannica, Toleo la pili).

“Yesu (amani juu yake) aliiwtwa “Masihi” kwa sababu alikuwa msafiri mashuhuri sana. Alikuwa akivaa skaafu ya sufu kichwani mwake na kanzu ya Sufu mwilini mwake. Alikuwa na fimbo mkononi mwake. Alitangatanga kutoka nchi hadi nchi na kutoka mji hadi mji. Jua lilipozama alilala po pote pale alipokuwa. Alikula majani ya nyika, alikunywa maji ya porini na alifanya safari zake zote kwa miguu. Akisafiri kutoka nchini kwake aliwasili Nasibini, mji ambao uko mamia ya maili kutoka nyumbani kwake. Pamoja naye walikuwako wanafunzi wake wachache ambao aliwatumwa kwenda kuhubiri mjini. Walakini wakati ule mji mzima ulikuwa umeenea habari za uwongo na uvumi mwingi kuwalhusu Yesu (amani juu yake) na mama yake. Kwa hiyo Gavana wa mji ule aliwatia mbaroni wanafunzi wale na akaamuru Yesu aletwe mbele yake. Yesu aliwaponya baadhi ya

Taarifa hii fupi, anasema Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) inaelekeza kwenye kukubali ya kwamba katika misafara yake,- Yesu (amani juu yake) alifika Nasibin, mji ambao upo baina ya Mosul na Syria. Kama mtu anasafiri kutoka Syria kuelekea Uajemi atapita katika mji huu. Nasibin uko maili 450 kutoka Yerusalem na maili 150 kutoka katika mpaka wa Uajemi. Mpaka wa Mashariki wa nchi ya Uajemi unagusana na mji wa Herat ulioko Afghanistan. Ndiyo kusema ya kwamba mji wa Herat umo katika mpaka wa Magharibi wa Afghanistan. Kutoka Herat hadi kwenye Upenyo wa Khaiber ni kiasi cha umbali wa maili 500.

watu kimiujiza na akafanya miujiza mingine. Kwa hiyo mfalme wa jimbo la Nasibin pamoja na majeshi yake na watu wake wote wakamwamini”<sup>a</sup>

---

a. Mwandishi amezitaja habari hizi za ukweli chini ya kichwa cha maneno, “Kukimbia kwa Yesu toka Yerusalem na kudhihirika kwa baadhi ya miujiza katika safari yake.”

Taarifa iliyotajwa hapo juu ya RAUZA TUS-SAFA kwa vyovyote vile ni sahihi hasa ukichukulia ya kwamba baada ya kukataliwa kwake na kuteswa na Waisraeli nchini Palestina, Yesu aliihama nchi ya Palestina,

“Balaa la kutisha sasa liliwakumba Mayahudi waliokuwa Mesopotamia na hususa wale ambao walikaa katika Bablonia. Pia kulikuwako na mji wa Nisibis uliokuwa katika mkondo huu huu wa mto Jaghjagha. (uk. 314).

Katika kitabu hicho hicho tunasoma taarifa ya Bwana Jaabir Mwenyezi Mungu awe radhi naye) ya kwamba Yesu alikuwa akitangatanga mara kwa mara. Alienda kutoka nchi moja hadi nyingine na jua lilipokuchwa alilala mahali po pote lilipomchwea. Hapo alikula majani ya nyika na kunywa maji safi.

Kisha tena katika hicho hicho tunakuta taarifa ya Bwana Abdullaahi bin Omar ambayo inasema hivi:-

“Mtukufu Mtume (amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake) alitangaza ya kwamba wapendwa zaidi wa Mwenyezi Mungu ni watu ambao ni “GHARIB”. Alipoulizwa ni nini maana ya GHARIB alijibu kwamba, “Ni watu kama vile Yesu Masihi ambao huzihama nchi zao wakiwa na imani zao”. (Jalada la 2 uk. wa 34 na 71 na Jalada la 6 uk. 51).

Taarifa hizi kumhusu Yesu siyo tu ni za zamani sana bali pia zinapatikana katika vitabu vyenye kutegemewa vya Hadithi za Kiislamu. Kama Yesu alibakia nchini Palestina katika maisha yake yote, basi hawezি kustahili kuitwa “Chifu wa Wasafiri”. Kwa hiyo na akafika Nasibin. Kuhama huko kuliafikiana na ujumbe wake. Josephus ambaye ni mwana historia maarufu sana wa wakati ule anatuambia ya kwamba wakati ule mji wa Nasibin ulikuwa umekaliwa na Mayahudi waliotokana na yale mataifa kumi yaliyopotea. Anasema hivi:-

kulingana na taarifa hizi ambazo zimetufikia kutoka sehemu mbalimbali zenye kujitegemea, hatuna uchaguzi mwingine isipokuwa kuamini ya kwamba Yesu alikimbia kutoka Palestina na kusafiri kutoka nchi hadi nchi na hatimaye akafika India. Hivyo basi akastahili aitwe “Chifu wa Wasafiri.”

## **SURA YA KUMI NA MBILI**

### **MAISHA YA YESU YASIYOJULIKANA**

#### **“MABUDHA NA YESU”**

Ushahidi mwingine uonyeshao ya kwamba Yesu alipata kwenda India ni maandishi ya kale ya Mabudha ambayo imetajwa waziwazi ya kwamba Yesu alikwenda India na akalihubiri neno la Mungu hapa na pale. Katika kitabu chake kiitwacho BOOK TRAVEL ambacho kilitangazwa mnamo mwaka 1911, John Pinkerton anasema, “Wamishonari kadhaa wamefikiria ya kwamba katika vitabu vya zamani vya ma-Lama (viongozi wa Kibudha) mmebakia baadhi ya alama za dini ya Kikristo ambayo sawa na fikra zao, yamehubiriwa katika sehemu zile wakati wa zama za wanafunzi” (yaani baada ya kufariki kwa Yesu) (Pinkerton, “A General Collection of the Best and Most Interesting Voyages and Travels in All Parts of the World”, Vol. 7, p. 554, London, 1811).

Baada ya kumalizika kwa vita baina ya Waturuki na Warusi (1877-1878), msafiri mmoja wa Kirusi aitwaye Nicholas Notovitch alizitembelea nchi nyingi na hatimaye mnamo mwaka 1887 alifika India. Akiwa katika moja ya ziara zake kwenye hekalu la Mabudha akajulishwa na mkuu wa ma-Lama ya kwamba kulikuwako na kumbukumbu za zamani sana zenye kuyasimulia maisha ya Yesu na lile taifa la Magharibi katika jumba la makumbusho la Lassa. Aliporejea Ulaya aliziratibu zile taarifa zinazoyahusu maisha ya Yesu. Akiwa na dhamiri ya kuzitangaza, akamkabidhi taarifa hizi Mhashamu Pilato aliyejewa Askofu Mkuu mtendaji wa Kiev. Ingawaje Askofu huyo aliamini ya kwamba uvumbuzi huu ulikuwa wa maana, hata hivyo alimzuia mtu huyu asizitangaze akidai kwamba kama zikitangazwa itakuwa ni kinyume cha matakwa yake. Alipoulizwa kwa nini itakuwa kinyume cha matakwa yake alikataa kutoa maelezo. Mwaka mmoja baadaye mtu huyu alipata nafasi ya kufika mjini Roma na akamkabidhi muswada huu Kardinali mmoja alikuwa na cheo kikubwa chini ya Baba Mtakatifu.

“Kwa nini unataka kuuchapisha muswada huu? Alisema Kardinali huyo. Hakuna atakayeutia maanani na utajitafutia maadui chungu nzima ukifanya hivyo na kama haja yako ni kupata pesa basi mimi ninaweza kukulipa fidia katika hasara uliyopata kuutayarisha muswada huu”. Hali yake ya asili ilimzuia bwana huyu asiikubali takrima ya Kardinali yule. Hatimaye akaufikisha muswada wake huu mbele ya Kardinali Roteli ambaye alikutana naye mjini Constantinople. Yeye pia alipinga muswada huu usitangazwe kwa kusingizia ya kwamba wakati wa kutangazwa kwake ulikuwa bado haujawadia. Akaongeza kusema kwamba, “Kanisa linaumia sana kutokana na huu welekeo mpya wa mawazo yasiyokuwa ya kiungu: na kwa kuutangaza hutakuwa umefanya isipokuwa kuwapatia silaha mpya wapotoshaji wa itikadi ya mafundisho ya Kikristo”. Mwishowe bwana huyu alikitangaza kitabu chake chini ya kichwa cha maneno, “MAISHA YA YESU YASIVOJULIKANA”<sup>a</sup> akiongeza ya kwamba, “Kabla ya kukikosoa kitabu changu jumuiya za Kisayansi zinaweza, bila ya kutumia gharama nyingi kutayarisha ujumbe wa kwenda

kuzuru sehemu hii ambao kazi yake itakuwa kuichunguza miswada hii katika sehemu ile ile inakopatikana na kwa njia hiyo, kuthibitisha thamani zake kihistoria” (Loranger Translatori: “The Unknown Life of Jesus,” uk. 8, 9, 12, New York 1895).

---

- a. Ndani ya jumba la makumbusho la Uingereza nimeona tafsiri mbili za kitabu hiki ambacho hapo awali kilitangazwa kwa lugha ya Kifaransa. Tafsiri moja ilifanya na Alexina Loranger na kutangazwa na Rand McNally & Co., Chicago na New York, 1894. Nyingine ilitayarishwa na Violet Crisp, London, Hutchinson & Co. Marejesho yangu yametokana na tafsiri ya kwanza.

“Sasa taifa zima la Wayahudi lilikuwa na hofu ya Wababylonia na Waseleukia kwa sababu Wasyria wote walioishi katika sehemu zile walikubalina na Waseleukia kuwapiga vita Mayahudi. Kwa hiyo wengi wao walijikusanya na kwenda Naarda na Nisibis ambako walipata usalama kutokana na nguvu za miji ile na pia kutokana na wakazi wa miji ile ambao walikuwa wengi sana na wote walikuwa wakakamavu kana kwamba ni wanajeshi”. (The Works of Flavius Josephus. Whitson’s Translation, with notes b Sir C. W. Wilson, Vol. 3, p. 324, London, 1889).

Kutoka Nasibin Yesu alipita nchi ya Uajemi na kuwasili katika nchi ya Afghanistan. Kutoka Afghanistan alipitia katika jimbo la Punjab na hatimaye akaingia Kashmir. Kulingana na visa vya kale

Walii mmoja wa Kiislamu aitwae Abu Bakr. Muhammad Attartushi anamtaja Yesu kuwa ni chifu wa Wasafiri.

inaonekana kwamba Yesu alifika Tibet na majimbo mengine ya India, lakini kwa yakini inaelekea ya kwamba aliishi na hatimaye akafia nchini Kashmir.

Moja mionganoni mwa sababu nyingi zilizofanya Yesu aitwe Masihi, ameandika Masihi Aliyahidiwa a.s. ni kwamba ye ye alikuwa msafiri mashuhuri sana. Katika ukurasa wa sita wa kitabu chake kiiwtacho SIRAAJUL-MULUUJKI kilichochapishwa nchini Misri mwaka 1306,

Kadhaalika katika LISAANUL-ARABI ambalo ni kamusi maarufu sana la Kiarabu tunasoma ya kwamba “Yesu aliitwa MASIHI kwa sababu alisafiri-safiri kuko na huko na wala hakukaa mahali pamoja.

Katika KANZUL-UMMAL ambacho ni kitabu kikubwa sana cha Hadidhi za Mtukufu Mtume wa Uislamu pamoja na masahaba zake, tunasoma ya kwamba Abu Hurairah (Mwenyezi Mungu alimfunulia Yesu maneno yafuatayo: “Ewe Yesu, tembea huko na huko, isije ukajulikana na kuteswa”. Mwandishi huyu ameandika kwenye kitabu hiki kwamba:-

“Katika ziara yangu moja kwenye moja ya sehemu zenu, za ibada, Lama mmoja alinizingumza habari za mtume fulani, au kama mnavyoita ninyi, Buddha fulani aitwaye Isa. “Je unaweza kuniambia chochote kuhusu mtume huyo?” Nilimwuliza. Akajibu kwamba “Jina la Isa linaheshimwa sana mionganini mwa wengi isipokuwa Makuhani Wakuu ambao wamezisoma taarifa za kale kuhusu maisha yake”. (uk.90).

“Kwa kuwa Hekalu letu ni moja mionganini mwa yale yenye bahati nzuri, hivi sasa tayari lina idadi kubwa ya miswada ambayo mimi mwenyewe nimewahi kuisoma katika muda wangu wa mapumziko. Mionganini mwa nakala hizi nimegundua maelezo ya maisha na matendo ya Isa, ambaye alihubiri nchini India na mionganini mwa wana wa Israeli”. (uk.91) “Zile taarifa za msingi zinazohusu maisha ya Isa zimeandikwa kwa lugha gani?” Niliuliza. Akajibu, “Taarifa zinazoyaelezea maisha ya Isa na ambazo zimeletwa Nepal kutoka India na kisha zikafikishwa Tibet kutoka Nepal zimeandikwa katika lugha ya Kipali na kwa wakati huu ziko Lassa. Lakini tunayo nakala moja ambayo imeandikwa kwa lugha yetu wenyewe yaani lugha ya Kitibet”. (uk. 93).

“Hatimaye, akiwa amelemewa na maswali yangu ya kuvutia akayachomoa majalada mawili makubwa sana ambayo magamba yake yametengenezwa kwa mbao nyembamba, na karatasi za

kurasa zake zilikuwa zimegeuka rangi ya manjano kwa sababu ya ukuukuu. Ndipo akanisomea taarifa ya maisha ya Isa ambayo niliinakili kwa uangalifu sana kwa msaada wa mkalimani wangu. Maandiko haya ya ajabu yameandikwa katika muundo wa aya zilizotengana ambazo aghalabu hazina uhusiano”. (uk. 96).

Kulingana na maandiko haya ya kale, wakati Isa (Yesu) alipokuwa wa miaka kumi na tatu, wakati ambapo Mwisraeli hutazamiwa kuo, Isa aliondoka nyumbani kwa baba yake na kwenda nje ya Yerusalem. Aliongozana na baadhi ya wafanya biashara na akasafiri kuelekea Sind ili ajiimarishe katika maneno ya kiungu na kujifunza sheria za Mtukufu Buddha. (uk. 107). Alipokuwa mwenye umri wa miaka kumi na nne kijana Issa (Mungu ambariki) alisafiri zaidi hadi akaivuka nchi ya Sind na kwenda kukaa na Ma-Arya. Umashuhuri wa jina lake ulienea katika sehemu zote za Kaskazini ya Sind. Alipokuwa akipita kwenye nchi ya mito mitano na Radjipoutada, watu waliokuwa wanamwabudu mungu Djaine walimwomba abakie pamoja nao”. (uk. 107).

Kisha akazuru Juggernaut katika jimbo la Orsis. Makuhani wa Brahma walimfundisha kuyasoma ma-Veda, kuponya wagonjwa kwa njia ya maombi, kufundisha na kuyaeleza Maandiko Matakatifu, kutoa pepo katika miili ya watu na kuwarejeshea hali ya kibinadamu. Alidumu kwa miaka sita katika Juggernaut, Rajegriha, Benares na miji mingine mitakatifu. Wote walimpenda kwa sababu Isa aliishi kwa amani na Wavaisya na Wasoundra ambao aliwfundisha Maandiko Matakatifu. Lakini Wabrahma na Wakashatriya walimpinga. (uk. 108).

Hapa chini nitataja baadhi ya mafundisho yaliyomo kwenye maandishi haya ya kale ambayo Yesu aliyahubiri kwa watu wa India.

1. “Mungu Baba hatofautishi baina ya wanawe ambao wote anawapenda sawasawa”. (uk.109).

2. "Mche Mungu wako, mpigie magoti yeye tu, na umtolee sadaka yeye tu".
3. Isa alikanusha kuwako kwa Trimourtia na kujitokeza kwa mungu Brahma katika sura ya mungu Vishnou, Siva na wengine, akisema kwamba, "Mwamuzi wa milele ambaye Ndiye Roho wa milele, dhati yake ndiyo ile Roho Moja isiyogawanyika - ambayo imeenea ulimwenguni kote. Roho hiyo peke yake ndiyo inayoumba, inayomiliki na kuvitia uhai vyote". Yeye peke yake ndiye aliyeazimia kuumba na akaumba. Yeye ndiye aliyekuapo tangu azali na ataendelea kuwako daima kudumu. Hakuna anayefanana naye imma huko mbinguni au hapa duniani. Mwumbaji huyu hana anayeshirikiana naye katika uwezo wake. Tazameni ya kwamba vitu vyenye uhai havishiriki katika uwezo wa Mwumbaji Mtukufu. Basi imekuwaje mnafundishwa ya kwamba vitu visivyo na uhai vinashirikiana Naye? Jueni ya kwamba hii si sawa kwa sababu ni yeye tu ndiye Mwenye uwezo wa juu kabisa". (uk. 110).

"Akataka ulimwengu uwe na ukawa. Na amemwandalia binadamu ardhi, maji, wanyama na vyote alivyoviumba na ambavyo ameviwekea utaratibu madhubuti kwa kupanga ajali ya kila mmoja". "Hivi karibuni laana ya Mwenyezi Mungu itashushwa juu ya binadamu kwa sababu amemsahau Mwumba wake na kuyajaza mahekalu yake kwa uvundo na kuabudu viumbe mbalimbali ambavyo Mwenyezi Mungu ameviumba kwa ajili yake. (uk. 111).

"Makuhani na wapiganaji walipofahamikiwa na mazungumzo ya Isa kwa Wasoudra waliamua kumwua. Ndipo wakawatuma watumishi wao kwenda kufanya kazi hii ya kumwua nabii huyu Kijana". (uk. 112). "Lakini Isa, alipotahadharishwa na Wasoudra juu ya hatari hii, akakimbia wakati wa usiku kutoka Juggernaut mpaka mahali alipozaliwa Mtukufu Buddha. Miaka sita baadaye, akaondoka Nepal na akapitia kwenye milima ya Himalaya na akateremka katika bonde la mto Rajputana na kuelekea upande wa magharibi akiwahubiria

watu mbalimbali kuhusu ukamilifu wa hali ya juu wa binadamu". (uk. 119).

"Wakati Isa alipowasili Palestina, alienda huku na kule akiuimarisha kwa neno la Mwenyezi Mungu ujasiri wa Waisraeli, ambao walikuwa tayari kufa chini ya uzito wa kukata tamaa kwao, na maelfu walimfuata ili kusikiliza mahubiri yake", (uk. 126).

"Lakini watawala wa miji walimwogopa na wakapeleka taarifa mbaya kumhusu yeze kwa Pilato aliye kuwa Gavana wa Yerusalem, ambaye aliamuru ya kwamba mhubiri Isa akamatwe na kufikishwa mbele ya Makuhani. Akawaamuru Makuhani wataalamu na wazee waelekevu wenye asili ya Kiebrania wamhukumu ndani ya hekalu" (uk. 127).

"Wale wazee wa kiebrania, baada ya kumsikiliza Isa wakamwarifu Gavana kwamba tumemwona yule mtu ambaye unamshitaki kwamba anawachochea watu wetu kufanya maasi, tunesikiliza mahubiri yake na tunajua ya kwamba yeze anatokana na watu wetu". (uk. 131).

"Yule Gavana aliwatuma majasusi wake na hatimaye Isa akatiwa mbaroni na Pilato akawakusanya watawala wakuu, makuhani, wazee na wanasheria kwa madhumuni ya kuwafanya wapitishe hukumu juu ya Isa. Kisha Isa akaletwa kutoka gerezani na akakalishwa mbele ya Gavana katikati ya wezi wawili ambao walikuwa wahukumiwe pamoja naye". (uk. 140).

"Lakini wao walimwambia Pilato kwamba, Hatuwezi kuibeba dhambi kubwa ya kumlaani mtu asiye na hatia na kuwaacha huru wezi wawili, jambo ambalo ni kinyume na sheria zetu. Kwa hiyo fanya 'upendavyo'. Baada ya kusema hayo wale makuhani na wazee waelekevu walitoka nje na kuosha mikono yao katika chombo kitakatifu wakisema "Sisi hatuhusiki na kifo cha mtu mwenye haki". (uk. 143).

Kisha kwa amri ya Gavana, Yesu alipigiliwa msalabani kwa misumari na wale wezi wawili nao wakapigiliwa pia. Alibakia msalabani mchana kutwa na jioni akafa. Siku ya tatu baadaye, yule Gavana aliwatumwa maaskari zake kwenda kuuchukua mwili wa Isa na kuuzika mahali pengine kwa kuhofia ya kwamba isije watu wote wakaasi. Siku iliyofuata umati ulikwenda kwenye pango ulikuta ya kwamba lile pango liko wazi na ndanimwe hamna kitu. Ndipo uvumi ukatapaka saa ile ile ya kwamba Mkuu wa Mahakimu amewatumwa malaika zake kuyachukua mabaki ya mwili wa mtakatifu huyu". (uk. 145).

Katika kitabu chake kii twacho CHRIST IN INDIA, F. A. Plattner ameandika ya kwamba:-

"Katika sehemu za Leh tumekumbana tena na kisa cha ziara za Kristo kwenye sehemu hizi. Postamasta wa Kihindu wa Leh na wafuasi kadhaa wa Budha kutoka Ladak walituambia ya kwamba mjini Leh, kwenye sehemu ambayo haiko mbali sana na Bazar, mpaka hii leo kuna bwawa ambalo janibu yake kuna mti wa zamani sana. Kristo aliwahubiria watu chini ya mti huu kabla hajaondoka kwenda Palestina. Pia tumesikia kisa kingine kihucho jinsi Kristo wakati yungali kijana alivyofika nchini India akiwa katika msafara wa wafanya biashara, na jinsi alivyoendelea kujifunza hekima ya hali ya juu katika sehemu za Himalaya. Tulisikia taarifa zinazohitilafiana kuhusu kisa hiki ambacho kimeenea sana katika sehemu zote za Ladak, Sinkian na Mongolia, lakini taarifa zote hizi zinakubaliana kuhusu jambo moja ya kwamba wakati alipotoweka nchini Palestina Kristo alikuwa katika nchi ya India au Bara la Asia. Haidhuru kitu kujua ni kwa namna gani na ni wapi kilikoanzia kisa hiki. Inawezekana ya kwamba kimetokana na Wanestori. Jambo la maana ni kuona ya kwamba kisa chenyewe kinasimuliwa kwa ukweli mtupu". (uk. 29).

Kuhusiana na jambo hili, mwandishi wa kitabu hicho anasema: "Ni lazima kudokeza hapa ya kwamba katika zama hizo za kale sana, na kwa hakika ndivyo ilivyo hata katika zama zetu hizi ya kwamba

katika nchi za mashariki, maisha ya hadhara yameshitadi zaidi katika masoko ambamo matukio ya siku nzima na habari za kutoka mataifa ya nje hutawanywa na misafara ya wafanya biashara ambao kwa kawaida walifuatana na idadi kadhaa ya madaruweshi ambao kila mara walikuwa tayari kusema yote waliyoyaona na kuyasikia njiani ili wapewe chakula. Kwa hakika hii ndiyo ilikuwa njia yao ya pekee ya kjitafutia riziki. (uk. 150).

“Miswada yote miwili niliyosomewa na, Lama wa jumba la Watawa wa Himis ilikusanywa kutokana na nakala mbalimbali zilizoandikwa kwa lugha ya Kitibet iliyotafsiriwa kutoka katika nyaraka za kale zilizo mali ya Maktaba ya Lassa na ambazo zimeletwa kutoka India Nepal na Maghada miaka mia mbili baada ya Kristo. Habari zilizo humo ambazo zinamhusu Yesu zimechanganywa ovyo na kupachikizwa bila kuwa na uhusiano wala mshabaha na matukio mengine ya zama zile” (uk. 151).

“Kwa sababu ya ile desturi ya makuhani wa Kihindu ya kukusanya habari zao, hatuwezi kuyatilia maanani sana maandiko yao. Kuhusiana na habari za kusulubu ni kwamba hatujui lo lote kuhusu msimuliasi wa kisa hiki au kwa uchache yeye alipataje kuwa pale. Je yeye alikuwa mwaminifu au si mwaminifu? Kwa upande mwingine, katika Injili tunasoma utabiri wa Yesu kuhusu hali ya baadaye ya Mayahudi ambamo alisema ya kwamba kwa sababu ya kumpinga yeye, wao watanyang’anywa Ufalme wa Mbinguni. Ndiyo kusema hakuna nabii watakayetokea mionganini mwao kwa siku zijazo, na jambo hili limetimizwa kimatendo. Kwa hiyo sina shaka yoyote katika kusema ya kwamba simulizi zilizomo katika nyaraka za Kibudha haziwezi kuchukuliwa moja kwa moja kuwa hazina dosari yo yote kwa kulinganishwa na simulizi za Injili. Uamuzi wa msingi ambao tunaweza kuufikia kutokana na maandiko haya ya kale ni kwamba ni kweli ya kwamba Yesu alikwenda India akaishi huko kwa muda mrefu na katika muda huo alilihubiri neno la mungu kwa watu wa India. Mafundisho yanayonasibishwa kwake ambayo baadhi yao nimeyataja hapo juu, kweli ni ya kiungu na yanastahili kuwa yametokana na nabii”

Kama Yesu asingalikwenda India kusingalikuwa na haja kwa wanahistoria na Kibuddha kutaja habari za mahubiri yake nchini India. Kwa upande mmoja wao wasingaliweza kukanusha kwamba ye ye hakuwahi kuhubiri kule, na kwa upande mwingine wao waliona ya kwamba mafundisho yake ni ya hali ya juu zaidi kuliko yale ya wafuasi wa Buddha na Brahma. Kwa hiyo, ili kuonyesha utukufu wa Gautama Buddha waliyavuruga yale matukio kwa makusudi na badala ya Kubainisha ukweli ya kwamba Yesu alikuja India alipokuwa Nabii na kuyanasibisha mafundisho haya kwake ye ye tangu awali, wao wakayanasibisha kwa Buddha wakisema ya kwamba Yesu alikuja India katika ujana wake ili kuепukana na ndoa na kujifunza sheria za mtukufu Buddha. Kwa hivi sasa ni jambo lisilo na shaka ya kwamba dini ya kibudha haikupata kusikika nchini Palestina katika zama za Yesu. Na “Mapenzi ya nyumbani yameshnikizwa sana katika kifua cha binadamu hivi kwamba hakuna awezaye kuvunja uhusiano wote na ndugu zake wa damu isipokuwa tu kama hana budi ya kufanya hivyo. Lazima ya namna hii haikupatikana katika maisha yote ya Yesu isipokuwa baada ya kuепukana na kifo cha msalaba kwa njia ya ajabu, wakati ambapo maisha yake mwenyewe nchini Palestina yalikuwa katika hatari ya kutolewa mara kwa mara.

Liko jambo lingine ambalo ninafikiri ni vema lijadiliwe hapa. Maisha na mafundisho ya Budha yana uwiano na yanafanana sana na maisha na mafundisho ya Yesu hivi kwamba mufakirina wengi wametangaza ya kwamba Ukristo tu ni mafundisho ya dini ya Buddha.

Dakta K. S. MacDonald ameandika kwamba:- “Bwana R. C. Dutt ameianza sura inayozungumzia habari za dini ya Buddha na Ukristo katika kitabu chake kiitwacho ANCIENT INDIA kwa maneno yafuatayo: “Maadili ya msingi na mafundisho ya dini ya Buddha yanafana sana na yale ya Ukristo hivi kwamba muungano wa namna fulani baina ya mifumo hii miwili ya dini ulikuwa ukihisiwa tangu

zamani sana". (MacDonald: The Story of Barlaam and Joseph; introduction, p. XIVII, Calcutta, 1895).

Dakta Ernest J.I Eitel ameandika kwamba:- "Wasomaji wateuzi ni lazima wawe wameshagundua katika taarifa hii fupi kuhusu maisha ya Buddha kwamba kuna vipengele vingi ambavyo vinalingana moja kwa moja na vile vinavyohusiana na maisha ya Mkombozi wetu kama zilivyoripoti Injili zote. "Tunaambiwa ya kwamba Sakyamuni Buddha alishuka kutoka mbinguni, alizaliwa na bikira alikaribishwa na malaika, alipokewa na mzee mtakatifu ambaye alipewa uwezo wa kupata ruya za kinabii, alitolewa wakfu hekaluni, alibatizwa kwa maji na baadaye akabatizwa kwa moto. Aliwashangaza wataalamu wengi kwa werevu na majibu yake, aliongozwa na roho kwenda nyikani, alijaribiwa na shetani, alikuwa rafiki ya watu wa kawaida na wenye dhambi, alibadilishwa sura alipokuwa mlimani, alishukia kuzimu, akapaa mbinguni. Kwa kifupi, kwa kutoa kipengele kimoja tu cha kusulubiwa kwa Kristo takriban kila alama ilioonekana katika maisha ya Yesu alama hiyo hiyo inakutwa imesimuliwa katika hadithi za kibuddha kuhusiana na maisha ya Sakyamuni Gautama Buddha. Lakini basi, huyu Buddha aliishi na kufariki miaka 275 au pengine miaka 543 kabla ya kuzaliwa kwa Kristo. Sasa tutayakubalije maoni ya mtu anayetaka kutufanya tuamini kwamba Yesu alikuwa India kwa muda wa miaka kumi na nane iliyopita baina ya ujana na utu uzima wake na kurejea akiwa na umri wa miaka thelathini na kuigiza na kuyaonyesha maisha na matendo ya Sakyamini Buddha? Au je sisi ambao tunaamini ya kwamba mafundisho ya Yesu hayakutokana na mtu mwagine tumekokotwa kwenye kisingizio kibaya cha kulikwepa suala la msingi kwa kudhania kama wadhanivyo baadhi ya mapadre wa utawa wa Kiyesu kwamba shetani, kwa kuyajua mapema mambo machache kuhusu maisha ya Masihi Aliyahidiwa, alimpotosha na kumfanya maisha yake yote yafanane na yale ya Sakyamini Buddha? (Eitel: lecture on Buddhism, Third Edition, London, 1884, p. 16).

Kwa hiyo ni jambo la muhimu kutafakuri juu ya swali hili ya kwamba, "Kwa nini kulikuwako na kufanana kwangi sana baina ya Buddha na

Yesu?" Ma-Arya wanasema ya kwamba Yesu aliifahamu dini ya Kibuddha kutokana na safari zake nchini India na baada ya kuipata elimu ya ukweli unaoyahu maisha ya Buddha, aliitumia kuzitengeneza Injili zake aliporudi nchini kwake. Walakini haya ni makosa yasiyokuwa ya uaminifu kwa upande wa ma-Arya. Si kweii hata kidogo ya kwamba Yesu alijua India kabla ya tukio la msalaba. Yeye hakuwa na haja yoyote ya kufanya safari ya namna hii wakati ule. Walakini haja ya kufanya safari ya namna hiyo aliipata wakati Mayahudi wa Sham (Syria) walipomkataa na kama waaminivyo, walipomfisha msalabani. Hivyo basi baada ya kuitoa huruma yake yote na shauku yake ya kuhubiri kwa faida ya Mayahudi na baada ya Mayahudi kuwa wagumu wa miyo kwa sababu ya tabia yao mbaya kwa kiasi ambacho hawangeweza kuukubali ukweli, Yesu kwa kufahamishwa na Mwenyezi Mungu kwamba yale mataifa kumi ya Mayahudi yалиhama kuelekea India, alifunga safari kuelekea sehemu zile. Na kwa vile baadhi ya Mayahudi walikuwa wameshaingia katika dini ya Buddha, hapakuwa na njia nydingine kwa nabii huyu mkweli isipokuwa kuyaelekeza mawazo yake kwa wafuasi wa dini ya Buddha. Wafuasi wa dini ya Buddha walikuwa wakitazamia kufika kwa Masihi 'Buddha'. Kwa hiyo vyeo vyake Yesu pamoja na baadhi ya mafundisho yake ya kiroho kama vile, "Mpende adui" "Msiyazuie maovu" na kama ilivyotabiriwa na Gautama Buddha kuhusu ujaji wa Matiyya (Masiha) mwenye ngozi nyeupe, yote haya yaliwafanya makuhani wamtambue Yesu kuwa ndiye Buddha waliyekuwa wakitazamia. Pia inawezekana ya kwamba baadhi ya majina, mafundisho ya wema na ukweli kuhusu maisha ya Yesu warneyanasibisha kwa Buddha kwa makusudi au pengine bila ya kufahamu, kwa sababu Wahindi bado hawajatoa ushahidi wa kuridhisha wa uzoefu wao katika kuyaratibu mambo ya kihistoria. Matukio yanayohusiana na Buddha hayakupata kuandikwa katika mpango maalum mpaka wakati wa zama za Yesu.<sup>a</sup>

---

a. Dakta Eitel ameandika kwamba: "Inaweza kuthibitishwa ya kwamba takriban kila tone la rangi hii ya Kikristo ambalo hadithi za Kibuddha.

Kwa hiyo makuhani wa Kibuddha walikuwa na nafasi nzuri sana ya kukinasibisha kwa Buddha kila walichopenda. Baada ya kuhadithia baadhi ya hii mifano ya mafundisho ya wema Masihi Aliyeahidiwa ameandika:-

“Ifahamike ya kwamba mafundisho haya ya wema na hii jinsi ya kuyahubiri, yaani kuongea kwa njia ya mafumbo (ambayo ndiyo ilikuwa njia yake Yesu) pamoja na mambo mengine, vyote hivyo vinaonyesha mara moja ya kwamba haya yalikuwa maigizo ya mafundisho ya Yesu. Wakati Yesu alipokuwamo nchini India na kwenda anahubiri hapa na pale ndipo wafuasi wa Buddha walipokutana naye, na baada ya kumwona yeche kuwa ni mtu mtakatifu na mtu mwenye baraka waliyaratibu matukio haya katika vitabu vyao. La bali wao walimtangaza kuwa yeche naye Buddha kwa sababu ndiyo hali ya asili ya binadamu ya kwamba anajaribu kukishikilia kitu kizuri kila anapokikuta. Hali hii inapatikana kwa kiasi ambacho watu wanajitahidi kukumbuka dokezo lolote la kiakili bila ya kujali dokezo hilo limefanywa na nani.

Dakta Hermann Oldenberg ameandika kwamba:

zilizokuwako katika karne zilizoandikwa kwa lugha ya Kipali. Na kwa hiyo tuko huru kabisa kusema ya kwamba hapakuwa na taarifa yo yote ya maisha yake katika zama zile”. (Oldenberg: Buddha, His Life, His Doctrine, His Order, p. 78, William and Norgate, 1882).

“Kwa hiyo inawezekana sana ya kwamba wafuasi wa imani ya Kibuddha wameandika taswira nzima ya mafundisho ya Injili katika vitabu vyao - Vipengele vyote vinavyofanana vinatokana na ukweli ya kwamba Yesu alizuru India na ziara yake hii ilikuwa bahati nzuri sana kwa wafuasi wa

“Kabla ya kuandika chochote kumhusu Buddha ni lazima litangulizwe tamshi hili la msingi ya kwamba: taarifa ya maisha ya Buddha haikutufikia kutokana na taarifa za kale, yaani zile taarifa

dini ya Kibuddha kutohana na kuishi kwake miongoni mwao kwa muda mrefu”.

Kwa fikra zangu haya ndiyo maelezo yanayokubalika akilini na ndiyo yanayoweza kutoa jawabu la kuridhisha kwa lile swali ya kwamba: “Ilikuwaje mpaka matukio yanayohusiana na maisha ya Yesu na mafundisho yake yakatambaa na kuingia katika vitabu vyta Kibuddha na kunasibishwa kwa Gautama Buddha?”

## **SURA YA KUMI NA TATU**

### **YUS ASAPH NA YESU**

Hii ndiyo hoja ya mwisho lakini siyo ndogo kuliko zote kuhusiana na ziara ya Yesu nchini India. Katika kurasa zilozotangulia nilikwisha lijadili lile tamko ya kwamba Yesu hakufia msalabani bali alitoka nje ya pango akiwa na mwili wake wa udongo, alikutana na wanafunzi wake kisirisiri alipokuwa nchini Palestina, kisha ili kuyahubiri mataifa kumi yaliyopotea ya wana wa Israeli, alikwenda Nasibin, kisha Uajemi, kisha Afghanistan na hatimaye kwa kupitia sehemu za Punjab akafika Kashmir.

Masihi Aliyeahidiwa ambaye Mwenyezi Mungu alimfunulia kwamba, “Masihi bin Maliamu amekufa” alisikia kutoka kwa wenyeji wa Kashmir kwamba katika mtaa wa Khan Yar mjini Srinagar kuna kaburi moja linaloheshimiwa sana kwa vile ni kaburi la Nabii Sahib (Yaani mtume). Neno NABII ambalo linatumika katika lugha mbili tu yaani Kiebrania na Kiarabu liliamsha jazba yake na likamfanya afikie kwenye uamuzi ya kwamba Nabii huyo ametokana na mataifa ya Mashariki ya kati na inaelekea zaidi ya kwamba ni nabii wa

Kiebrania kwa vile hapakutokea Nabii yeote mionganii mwa Waislamu baada ya Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. ambaye kaburi lake liki mjini Madina. Uchunguzi zaidi ukaja kuyathibitisha maoni yake kwani aliambiwa ya kwamba Nabii huyo ambaye pia alijulikana kwa jina la Yus Asaph alikuwa mgeni na alikuja Kashmir kiasi cha miaka 1900 iliyopita. Ushahidi huu pamoja na mwingine mwingi ulimfanya aamini kwamba Nabii aliyezikwa Srinagar hawezi kuwa mtu mwingine isipokuwa Yesu wa Nazareti ambaye alikwenda India kuyatafuta makabila ya Israeli yaliyokuwa yanaishi katika sehemu hizo za majimbo ya kaskazini ya India.

Hapa chini nitaelezea hoja chache ambazo zinayaunga mkono maoni haya:-

1. Upo ushahidi wa kimaaandishi na wa kimdomo kutoka kwa watu mashuhuri wa Srinagar ya kwamba aliye mo ndani ya kaburi linalozungumziwa ni Nabii Yus Asaph ambaye alikuja Kashmir yapata miaka 1900 iliyopita na ambaye pia alii twa Mwana Mfalme. Orodha ndefu ya mashahidi wa jambo hili imo katika Sura ya mwisho ya ALHUDAA ambacho ni kitabu cha kiarabu kilichotungwa na Masihi Aliyeahidiwa na kutangazwa mnamo mwaka 1902 mjini Qadian.

2. Taarifa za kila mwaka za nchi ile pia zinathibitisha kwamba kaburi hili linajulikana kuwa ni la Mtume Yus Asaph. Akigusia kuhusu kaburi hili mwandishi wa TARIKH-I-AZAMI ambayo ni historia ya Kashmir ilioandikwa miaka 200 iliyopita, anasema kwenye ukurasa wa 82 kwamba:-

“Mara baada ya kaburi la Sayyid Nasr-ud-Din kuna kaburi ambalo linajulikana na walio wengi kuwa ni la mtume aliyetumwa kwa wakazi wa Kashmir. Yeye alikuwa mwana mfalme ambaye alikuja Kashmir kutoka nchi ya kigeni. Yeye alikuwa ni mtu aliye halisika sana katika wema, uchamungu na kujitolea. Alifanywa mtume na Mwenyezi Mungu na alijishughulisha na kuwahubiria Wakashmir. Jina lake ilikuwa Yus Asaph.

3. Baada ya kulizuru kaburi hili mnamo mwaka 1903, mishonari mmoja wa Kikristo Mhashamu Weitbrecht ambaye alikuwa mpinzani wa Masihi Aliyahidiwa, aliandika barua moja kwenye gazeti la Kikristo liitwalo EPIPHANY ambamo alisema:-

Katika eneo hili kulikuwa na makaburi mawili ya mawe. Yeye huyo (Mzee mtukufu ambaye alikuwa akiyalinda hayo makaburi) alisema kwamba lile kubwa lililo upande wa Kaskazini ni la Yus Asaph na kwamba lile dogo ni la Sayyid Nasr-ud-Din”<sup>a</sup>

---

- a. Kwa kuwa Mhashamu Weitbrecht amevuruga baadhi ya mambo ya kweli katika barua yake, kulitokea mabishano baina yake na Maulawi
- 

Sher Ali, sahaba mtukufu wa Masihi aliyahidiwa, ambayo yanaweza kurejewa katika REVIEW OF RELIGIONS, Jalada la 2, Na. 11 na 12, 1903; Jalada la 3 Na. 5 May 1904.

4. Katika toleo la Oktober 1909 mhariri wa Review of Religions ameandika kwamba:- “Jambo la pekee kuhusu kaburi hili ni kwamba siyo tu linajulikana kuwa ni kaburi la Nabii Sahib, bali pia linaitwa kaburi la Isa Sahib (Yesu). Mirza Bashir-ud-Din Mahmud Ahmad, mwana wa Masihi Aliyahidiwa alifanya ziara ya kulitembelea kaburi hilo mnamo July 1909; na alipomwuliza bi kizee mmoja (aliyekuwa mrithi wa mwisho mionganoni mwa mnyororo mrefu wa wahudumiaji wa kaburi lile) kaburi lile ni la nani, yeye alijibu, “Ni kaburi la Isa Sahib”. Alipouliza ni kwa sababu gani analiita kaburi la Isa Sahib ilhali Masheikh wanaamini kwamba Isa (Yesu) yuko mbinguni? Yeye alisema, “Waache waamini cho chote kile. Jina hili (Isa) tumekuwa tukilisikia tangu zama za mababu zetu wa zamani sana”.

5. Kwenye ukurasa wa 359 wa kitabu kimoja cha Kiarabu kiiwtacho IKMAL-UD-DIN ambacho kilitungwa yapata miaka elfu moja iliyopita tunasoma maneno yafuatayo:-

kilipomchukua. Ndipo akauacha mwili wake wa udongo na kupaa angani. Na kabla hajakata roho alimwita mwanafunzi wake mmoja aitxae Yabid ambaye alikuwa akimhudumia na kumlinda na ambaye alikuwa mstahiki katika mambo yote na kumuusia kwamba: "Safari yangu ya kuihama dunia hii imekaribia: kwa hiyo ni lazima ufanye kila lililo wajibu wako na wala usibabaike na kuiacha haki na ni lazima utekeleze faradhi zote". Kisha akamwomba yule mwanafunzi amjengee kaburi na baada ya kuinyosha miguu yake, akaelekeza kisogo chake upande wa Magharibi na uso wake upande wa Mashariki na akakata roho"

Zaidi ya hayo tunasoma vile vile ndani ya kitabu hiki ya kwamba Yus Asaph aliuita ujumbe wake BUSHRA (ambalo ndilo jina la Injili kwa Kiarabu na Kiebrania). Kisha akaanza kuufananisha mti na BUSHRA (Injili) ambayo aliwhahubiria watu na elimu na hekima aliyokuwa nayo aliifananisha na chemchem ya maji na aliwafananisha na ndege wale watu ambao waliungana naye na kuikubali dini yake".

6. Sir Francis Younghusband ambaye alikuwa Gavana mkazi wa Kashmir tangu 1909 hadi 1911 ameandika kwamba:-

"Kiasi cha miaka 1900 iliyopita paliishi mtakatifu mmoja katika nchi ya Kashmir aitwaye Yus Asaf ambaye alihubiri kwa njia ya mafumbo mengi sana ambayo yanafanana na yale ya Kristo, kama vile kwa mfano lile fumbo la mpanzi. Kaburi lake liko Srinagar, na nadharia ya Mwanzilishi wa Madhehebu ya Qadian ni kwamba Yus Asaf na Yesu ni yule yule mtu mmoja". Kashmir-described by Sir Francis Younghusband, p. 129-130, London 1911).

7. Moja ya dalili ambazo Dakta Francis Bernier amezitaja katika kitabu chake kiitwacho TRAVELS ili kuthibitisha ya kwamba Mayahudi walipata kuishi katika nchi ya Kashmir ni "hii imani ya

"Yeye huyo (Yus Asaph alitangatanga katika miji na nchi kadhaa mpaka akafika kwenye nchi iitwayo Kashmir. Ndipo akaenda huku na kule ndani ya nchi ile na akakaa na kustakimu humo mpaka kifo

kwamba MUSA alifia mjini Kashmir na ya kwamba kaburi lake liko kiasi cha maili tatu nje ya mji huu,” Ni wazi ya kwamba wakazi wa nchi hii ambao Bernier anasema kwamba ni Waislamu, wasingalisema kwamba MUSA kafia Kashmir na kuzikwa kule, kwa sababu Mtukufu Mtume wa Islam (amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake) alibainisha ya kwamba kaburi la Musa liko nchini Palestina. Inaelekea ya kwamba Bernier hakuelewa sawasawa na akamtaja Musa badala ya Isa. Walakini dalili hii inahakikisha bila ya shaka yo yote ya kwamba mnamo karne ya kumi na saba wakazi wa Kashmir waliamini ya kwamba aliyezikwa katika kaburi lile ni Nabii wa Kiebrania ambaye hadhi yake ni sawa na ile ya Musa (Bernier, Travels in the Moghul Empire, p. 430. Oxford University Press).

8. Baada ya ziara yake ya mwaka 1939 nchini Kashmir, Ahmad Islam aliandika maneno yafuatayo kwenye barua aliyomwandikia mhariri wa gazeti la THE SUNRISE:-

“Punde si punde nikatoka nje ya chumba changu. Nilitaja neno Khanyar kwa mwendesha gari la farasi. Akanijibu kwa shauku kubwa sana: “Je bwana una taka kuiona Rauza ya Nabii Sahib?” Nikamjibu ndiyo, na pale pale tukaanza safari. Baada ya muda mfupi tukaifikia hiyo Rauza. Nikaambiwa ya kwamba wageni wa kila namna kutoka India na nchi za kigeni huja kuliona hili kaburi. Hata Naibu wa Mfalme alikuwa hapa. Nilijawa na shauku nyingi sana kusikia habari hizi.

“Unamaanisha Naibu yupi?” Simjui bwana, ila nina maana ya yule mtu ambaye ana mkono mmoja”. Ni dhahiri alikuwa Lord Halifax Waziri wa nchi za kigeni wa Uingereza ambaye wakati huo alikuwa akiitwa Lord Irwin. Ziara ya Lord Halifax haikupata kutangazwa kwenye magazeti. Au niseme ya kwamba sikumbuki kama nimesoma jambo lolote kuhusiana na habari hii. Hata hivyo inaweza kueleweka ni kwa sababu gani Lord Halifax aliikidhi shauku yake kimya kimya namna hii. Hata hivyo ziara ambayo imefanywa na Naibu wa Mfalme lakini haikutangazwa kabisa, inaifanya ziara hiyo ioneokane kuwa ni yenye sababu nzito. “Unafikiri kaburi hili lina umri gani?” “Ni la zamani sana bwana”.

“Zamani za kiasi gani?” Pale kulikuwa na waendesha tangaa watatu. Wakaanza kutazamana kisha mmoja wao akasema, “Miaka elfu moja mia tisa iliyopita”, akaongeza kwamba huyo alikuwa Nabii ambaye alitoka nchi nyingine. Kaburi hili limekuwa likiheshimwa kwa mamia mengi ya miaka, na hivyo ndivyo tulivyosikia kutoka kwa mababu zetu”. (THE SUNRISE, Jalada la 10 Na. 16, April 22, 1939, Lahore, India (sasa Pakistani).

Marejeo kuhusu kaburi hili yanaonyesha ya kwamba aliyezikwa humo alikuwa na sifa zifuatazo:-

- (i) Mwana mfalme.
- (ii) NABI, yaani Mtume wa Mungu ambaye alitumwa kwa wakazi wa Kashmir.
- (iii) Alizoea kuongea kwa mafumbo.
- (iv) Alikuwa mgeni ambaye alikuja kutoka upande wa Magharibi yapata miaka 1900 iliyopita; na
- (v) Jina lake ni Yus Asaph na aliitwa Isa vile vile.

Baada ya kuwa na yakini na dalili tano zilizotajwa hapo juu, si vigumu kutambua ni nani aliye ndani ya kaburi hilo. Hapakuwa na mwana mfalme ye yote hapo zamani ambaye anaafikiana na sifa hizi isipokuwa mwana mfalme Yesu Mwana wa Daudi.

- (i) Yesu alikuwa mwana mfalme aliyeitwa Mwana wa Daudi (Mathayo 9:27, 20:30) ambaye Mwenyezi Mungu alimtukuza na kumfanya mwana mfalme (Matendo 5:31) na akamfanya kuwa Mwanamfalme wa Wafalme wa dunia (Ufunuo 1:5).
- (ii) Yesu alikuwa NABI, yaani mtume wa Mungu aliyetumwa kwa Kondoo waliopotea wa Nyumba ya Israeli. Yeye alisafiri kutoka Palestina ili kwenda kulihubiri neno la Mungu kwa waisraeli wa Afghanistan na Kashmir.

- (iii) Yesu alizungumza kwa mafumbo. Mahubiri yake aliyaita BUSHRA (Injili) na wanafunzi wake aliwafananisha na ndege. Fumbo la mpanzi limetajwa katika Mathayo 13:3, na “pasipo fumbo yeye hakuwaambia lolote” (Mathayo 13:34).
- (iv) Alisafiri kutoka Palestina hadi Kashmir yapata miaka 1900 iliyopita kwa hiyo zama za watu hawa wawili zinafanana.
- (v) Katika Kurani Tukufu jina la Yesu ni Isa ambalo limefupishwa kutokana na neno la Kiebrania Ishu.

## **YUS ASAF**

Aliitwa Yus Asaf ambalo pia ni jina la Kiebrania. Neno Yus ni matamshi mengine ya neno Yusu au Jesu kwa Kiajemi cha zamani. Kwa Kiajemi cha siku hizi ni Yasu au Jesus na hii pia ni sawa na kiarabu jinsi tuonavyo kwenye tafsiri mpya ya Kiarabu kutokana na Injili ya Kiyunani. Kwa hiyo neno Yus ndilo Yesu na Asaph ni jina la Kibiblia ambalo maana yake ni Mkusanyaji.<sup>a</sup> Tunasoma katika 1 Mambo ya Nyakati ( 16; 4-7) ya kwamba Asaf alikuwa Mlawi aliyejitolea sana katika mambo ya dini na aliteuliwa kuwa mkuu wa wenye kuzihifadhi Zaburi za Daudi.

- 
- a. Angalia kwenye “Nyongeza” ya Facsimile Series of Bagster’s Polyglot Bible ukurasa 33 chini ya kichwa cha maneno ***Proper Names with their meaning.*** Ujumbe wa Yesu ulikuwa wa kuja kuyakusanya na kuyaweka mataifa yote ya Waisraeli katika zizi moja. Hivi asemavyo yeye mwenyewe ya kwamba: “Na nina kondoo wengine ambao si wa zizi hili, wao pia ni lazima niwalete nao wataisikia sauti yangu na kutakuwa na zizi moja na mchungaji mmoja.” (Yohana 10:16) Hii ndiyo sababu Yesu aliitwa Asaf. Alipokuja kuyahubiri mataifa kumi yaliyopotea katika nchi ya Uajemi,

Afghanistan na Kashmir ilikuwa sawa kabisa kumwita Yus Asaf, yaani Yesu Asaf.

Bila ya kufahamu ugunduzi aliofanya Masihi Aliyeahidiwa na kwa kuyaegemeza maoni yao katika hadithi ya Barlaami na Josaphat au Joasaph na hususan kwa kuwategemea wamishonari wa Kikristo ili kumwepushia Yesu kitendo cha kuzikwa kama manabii wengine, waandishi wa Kizungu wamesema kwamba kaburi hili linalozungumziwa ni la Buddha. Kwa mfano Mhashamu Weitbrecht katika barua yake iliyotajwa hapo juu amedai ya kwamba kwa vile matukio yanayomuhusu Yus Asaf katika hekaya za Barlaam na "Ugunduzi ya kwamba Joasaph au Josaphat aliyetajwa kwenye hadithi yetu si mtu mwingine isipokuwa Buddha ulifanywa wakati mmoja na wanazuoni wa Kifaransa, Kijerumani na Kiingereza bila ya kutegemeana. Mwandishi mwenyewe anakiri ya kwamba hadithi hii ilitoka India. Mtu ye yote anaweza kutambua ya kwamba haimhusu mtu mwingine ye yote isipokuwa BUDDHA". (MacDonald: THE STORY OF BARLAAM AND JOASAPH, Introduction, p. 52, Calcutta 1895).

Zaidi ya hayo inasemwa kwamba, "Kwa hakika Barlaam mwenyewe ni Buddha aliyegeuka na hivyo ni ndugu pacha wa Josaphat". (Joseph Jacobs: BARLAM AND JOSAPHAT, Introduction, p. XIIX, London, 1895).

Ni lazima ikumbukwe ya kwamba, "Kwa habari alizozitangaza Masihi Aliyeahidiwa kuhusu kaburi hilo hazikutokana na kisa cha Barlaam na Josaphat. Walakini kama waandishi wa Kizungu wanayo haki ya kumfananisha Josaphat na Buddha, basi na sisi vile vile tunayo haki ya kumfananisha na Yesu. Pia asisahauliwe ya kwamba huyo Yus Asaph ya wa Synagogue kuwa nahiwa ya Bodhi na jiwali siye Asaf limethibitika kuwa linahitaji maelezo na ni lazima liwe mojawapo ya majina ya Bodistava. Na kadhaalika Dakta MacDonald ameandika kwamba:-

mtakatifu wa kawaida tu au sahaba wa nabii mwingine. Naam, kila nabii ni mtakatifu lakini si kila mtakatifu ni Nabii. Kwa hiyo suala letu lipo katikati ya mambo mawili. Imma huyu Yus Asaph wa Srinagar alikuwa Buddha au Yesu Kristo.

Haiwezekani yeeye kuwa Buddha. Kwanza, kwa sababu Buddha hakufia Srinagar, na mwili wake haukuzikwa bali ulichomwa moto. Utafiti wa siku hizi umebainisha mahali alipofia Buddha. “Alikufa na kuchomwa moto mahali paitwapo Kusinagara katika nchi ya Oude akiwa na umri wa miaka 80 mnamo mwaka 543 kabla ya kuzaliwa Kristo. Majivu ya mwili wake yaligawanywa mionganoni mwa watu kadhaa waliokuwa wakiyadai na minara ya ukumbusho wake ikajengwa na majivu haya yakahifadhiwa humo”. (Chamber’s Encyclopaedia, Revised Edition, “Buddhism”, London, 1880).

Dakta T. W. David ameandika kwamba: “Maarufu mionganoni mwa haya ni huu ugunduzi uliofanywa na bwana William Pippe katika shamba la Birdpur linalopakana na mipaka ya jimbo la Kiingereza na lile la Nepal. Aligundua mnara uliojengwa kwa umaridadi na watu wa ukoo wa Sakia ili kuifunika hisa yao ya majivu waliyoipata kutokana na lundo la majivu ya Buddha aliyeunguzwa”. (Encyclopaedia Britannica chini ya Budhism).

Dakta Herman Oldenberg ameandika kwamba:

“Buddha alifia Kusinara Jua lilipokaribia kuchomoza watukufu wa Kushinara waliuchoma mwili wa Buddha mbele ya milango ya Jiji la Kusinara kwa heshima zote zinazotolewa kwa kila mabaki ya wafalme wa Kimataifa”. (Oldenberg: Buddha ukurasa 203).

Kwa hiyo ni, dhahiri ya kwamba Buddha ambaye alifia Kusinagara au Kusinara na kuchomwa moto hawezi kuwa amezikwa ndani ya kaburi linalozungumziwa. Pili, ingalikuwa aliyezikwa humo ni Buddha au Raja, Mwana mfalme au Mtakatifu ye yote wa Kibaniiani, kaburi hilo lingalikuwa mikononi mwa Mabaniiani na wenyewe kulizuru wagalikuwa Mabaniiani au Wahindu badala ya Waislamu. Tatu: Jina

peke yake Yus Asaph, kama nilivyokwisha sema hapo juu ni jina la Kiebrania na inaonekana ni vichekesho kulinasibisha na majina ya Kibani. Je haingekuwa jambo la akili kulitafutia majina yanayofanana na Yus Asaph kuliko yale yanayofanana na Bodisatva? Kwa vile imeshathibitishwa ya kwamba Yus Asaph wa Kashmir si Gautama Buddha tunayo haki ya kusema kwa uthabiti wa moyo ya kwamba hakuwa mtu mwingine isipokuwa Nabii Mwana mfalme Yesu wa Nazareti (amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake).

Uhakika wa ugunduzi uliofanywa na Masihi Aliyahidiwa ya kwamba Yus Asaph aliyezikwa Srinagar si mtu mwingne ila Yesu umethibitishwa kwa njia zote zinazotumiwa katika kuthibitisha matukio ya zamani za kale na uhakika huo unakubalika akilini na uko wazi sana hivi kwamba hata Sheikh Rashid Ridha (wa Cairo, Misri) ambaye alimpinga Masihi Aliyahidiwa maisha yake yote hakuweza kujizua kudokeza juu ya jambo hili. Baada ya kuzinakili hoja zote zenye kulihusu kaburi hili kutoka katika ALHUDAA ambacho ni kitabu cha Kiarabu cha Masihi Aliyahidiwa na kuziweka katika jalada la sita la kitabu chake kiiwtacho TAFSIRI-UL-MANAR chini ya kichwa cha maneno “Kukimbilia kwa Yesu nchini India na kifo chake nchini Kashmir”, Sheikh huyu akasema:-

“Kwa hiyo kukimbilia kwa Yesu nchini India na kufa kwake mjini Srinagar si jambo geni katika ukweli wa kiakili au wa Kihistoria.”

Jaji Docker ameandika kwamba:-

“Hapa ni lazima nitaje kile kisa cha zamani ambacho nilikwisha kirejea. Tafsiri ya kisasa ya kisa hicho imechapishwa katika gazeti liitwalo THE EAST AND WEST miaka michache iliyopita. Kwa kifupi tafsiri hiyo inadai kwamba Yesu hakufia msalabani bali alipona kwa kutibiwa na dawa ya ajabu ambayo ilipakwa katika vidonda vyake ambavyo vikapona katika kipindi cha siku arobaini na kwamba alikwenda India kuyahubiria makabila kumi yaliyopotea ya wana wa Israeli, na hatimaye akafia

Srinagar ambapo hadi hii leo panaonyeshwa kaburi linalosemwa kuwa ni lake.

Ingawaje sijui ushahidi wo wote unaoelekea kuthibitisha kiini cha ukweli wa habari hii, ninapenda kusema ya kwamba katika habari hii hakuna jambo LISILOINGIA AKILINI wala LISILOWEZA KUTOKEA. Kutokana na mazingira mengine ya habari tunaambiwa ya kwamba hadi hii leo katika nchi ya Afghanistan na Bectria kuna makabila ambayo kwa kila hali ni ya namna ya Kiebrania. Inastaajabisha kuona ya kwamba kuna idadi kadhaa ya vifungu vya maneno katika maandiko ya Agano Jipyambavyo kama haviiungi mkono moja kwa moja hadithi hii, basi kwa akali vinaleta maana ile ile. Sasa je haikubaliki akilini kudhania ya kwamba baada ya kuona kwamba usalama wake uko hatarini akibakia kwa muda mrefu zaidi ya siku arobaini katika Judea na Galilaya ili kuwaambia wanafunzi wake habari za Ufalme wa Mungu (Matendo 1:3) akaonelea ni afadhali azipeleke habari hizo za ufalme wa Mungu kwa yale makabila kumi yaliyopotea ya Nyumba ya Israeli?

Tena (ukurasa 77) anasema:-

“Ni lazima nikariri ya kwamba sisi hatujui. Inawezekana ya kwamba baada ya kuyahubiria yale makabila kumi yaliyopotea ya Nyumba ya Israeli katika sehemu zile za mbali Yesu alifia Srinagar na akazikwa kwenye kaburi ambalo hadi hii leo lina jina lake. (Docker: IF JESUS DID NOT DIE UPON THE CROSS, uk. 71, London, 1920).

Katika makala yake iitwayo “THE HEAVENLY HIGH SNOW PEAKS OF KASHMIR”, iliyotolewa katika gazeti la kila mwezi liitwalo ASIA ambalo lilichapishwa katika nchi ya Amerika mnamo mwezi October 1930, John Noel ameandika kwamba:-

“Ni wenye nguvu sana hawa wakulima wa Kashmir ambao ni vipande vya binadamu wenye mabega mapana lakini ni wanyenyekevu na wapole wa tabia. Wana jambo moja ambalo litakupa mshituko mkubwa sana. Wao wanaonekana kushabihiana sana na kila Myahudi ambaye umewahi kumwona siyo kwa sababu wanavaa

magwanda marefu marefu ambayo yanaikumbusha akili yako juu ya magwanda ya Kibiblia bali kwa sababu nyuso zao zina maumbile ya Kiyahudi.

Bahati nasibu ya ajabu, kama tunaweza kuiita ni bahati nasibu, ni kwamba nchini Kashmir kuna simulizi inayoaminika sana kuhusiana na Mayahudi. Kwa miaka chungu nzima kumekuwako na uvumi katika nchi hii ya kwamba kwa hakika Kristo hakufia msalabani bali aliteremshwa na akatokomea kwenda kuyatafuta yale makabila kumi yaliyopotea na kwamba alifika Kashmir, Ladakh na Little Tibet na akazikwa Srinagar. Nimeambiwa ya kwamba simulizi hii ya kale ya Kashmir inayo marejeo yanayomtaja nabii mmoja ambaye aliishi hapa na alifundisha kwa mafumbo kama Yesu na hadithi fupi fupi zenyet kuyatajaa baadhi ya mafumbo hayo zinakaririwa nchini Kashmir hadi leo”.

Pandit Jawahar Lal Nehru, Waziri Mkuu wa India, ameandika katika kitabu chake kiitwacho GLIMPSES OF WORLD HISTORY kwamba:- “Katika sehemu zote za Asia ya kati kama vile Kashmir, Laddakh, Tibet na hata Kaskazini ya sehemu hii kuna imani iliosaki sana mionganii mwa watu ya kwamba Yesu au Isa alitembea katika sehemu zile”. (uk. 84).

Kwa hiyo nina yakini kwamba wakati ambapo wale ambao wamepewa neema ya akili na hekima watatafakari kwa uaminifu, wakitia maanani ya kwamba Yesu alitoka nje ya kaburi akiwa hai pamoja na mwili wake wa udongo ukiwa na vidonda na kwamba hakupaa mbinguni bali aliishi duniani, watafikia kwenye uamuzi ya kwamba mtu aliyezikwa kwenye mtaa wa Khan Yar (Srinagar, Kashmir) ni Yesu Mwana wa Mariamu (amani juu yake).

Hili ndilo jawabu letu kwa wote wale ambao wanawenza kutuuliza kwamba: “Iwapo Yesu hakufia msalabani alikwenda wapi na alifia wapi?

Katika jawabu hili mnapatikana ufumbuzi wa lile swalí gumu sana kuhusu maisha ya Yesu yasiyojulikana. Kama kuna mtu ambaye anaweza kutoa ufumbuzi mwingine wenye kuaminika na wa kiakili zaidi kuliko huu na ajitokeze kwa ufumbuzi wake huo na ulimwengu utajiamulia wenyewe.

Mwishowe ninapenda kusema ya kwamba kama wachimbuaji wa mabaki ya kale wangalilifumua kaburi hili na kulifanyia utafiti bila shaka wangaliona baadhi ya maandishi kwenye mawe au alama zingine zenyé kuunga mkono uvumbuzi uliotajwa hapo juu na kwa njia hiyo wangaliwakomboa mamilioni ya ndugu zao kutokana na kumwabudu binadamu ambaye alitumwa kuja kuwaita watu kwenye ibada ya Mungu mmoja tu.

### **SURA YA KUMI NA NNE BISHARA KUU**

Mtukufu Mtume Muhammad (amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake) alitabiri kwamba Masihi atatokana na Waislamu wenyewe na atatoka mahali palipo Mashariki ya Damascus, yaani India; na kwamba yehe atavunja msalaba, yaani atabainisha itikadi mbovu ya Kikristo kuhusiana na kifo cha Yesu msalabani, ambayo ndiyo uti wa mgongo wa imani ya Kikristo inayokubalika na walio wengi. Kwa kuwa wasomaji wengi wa Kikristo huenda wasielewe kwa urahisi utukufu wa bishara hii, ninapenda kuifafanua zaidi habari hii kwa ajili yao.

Kabla ya kutumwa kwa Mtukufu Mtume Muhammad (amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake). Mayahudi pamoja na Wakristo waliamini kwamba Yesu alifia msalabani. Wayahudi waliamini hivyo ili kuhakikisha kwamba ni nabii mwongo na amelaaniwa na Mwenyezi Mungu. Wakristo waliamini hivyo ili kuhakikisha kwamba yehe ni mtu aliyetolewa kafara na Mwenyezi Mungu kufidia dhambi za ulimwengu mzima na wakaongeza kuamini kwamba alifufuka kutoka katika wafu mnamo siku ya tatu na kisha baada ya kuishi duniani kwa muda wa siku arobaini akapaa mbinguni.

Kinyume na imani hii Mwenyezi Mungu ametangaza ndani ya Kurani Tukufu kwamba Yesu hakufia msalabani. Na Mtukufu Mtume anasema kinaganaga kwamba, “Yesu alikufa akiwa na umri wa miaka mia moja na ishirini (*Isabah fi-shar-his Sahaba jalada la 5 uk. 54 na Kanzul Umal jalada la 7. Habari hizi zimesimuliwa na Ibn Umar na Tabarani. Amezipokea kutoka kwa Hadhrat Faatima.*)

Isitoshe, alipofariki Mtukufu Mtume, Waislamu wote walithibitisha kwamba mitume wote waliomtangulia wamekufa. Wakati Sahaba mmoja wa Mtukufu Mtume, alipotilia mashaka habari za kifo chake na baadhi ya wengine kudai kwamba, “kama Muhammad angalikuwa mtume wa Mungu asingalikufa”, Hathrat Abu Bakri alitoa hotuba na katika hotuba ile akasoma aya ya Kurani Tukufu isemayo: “Muhammad siye ila ni mtume tu; wamekwisha pita mitume kabla yake; basi yeye akifa ua akiuawa, mtarudi nyuma juu ya visigino vyenu?” (*Bukhari, jalada la 3 uk. 63. Osamaniyya Misriyya Press, 1932*).

Baada ya kusikia aya hii mashaka yao yote kuhusu kifo cha Mtukufu Mtume yalitoweka miyoni mwao nao wakakubali kwa moyo mmoja kwamba yeye amekufa kama walivyokufa mitume wengine wote wa kabla yake.

Tena tunasoma katika historia maarufu ya mitume na wafalme ilioandikwa na Abu Jafar Muhammad ibn Jarir at-Tabari kwamba alipofariki Mtukufu Mtume, Waislamu wa Bahrain waliutilia mashaka ukweli wa Mtukufu Mtume na wakarudia imani zao za zamani wakisema kwamba: “Kama Muhammad angekuwa Mtume, asingalikufa”. Jarud bin Mualla aliyekuwa wa ukoo wa Abdul-Qais ambaye alijipatia elimu ya dini ya kutosha alipokuwa akikaa mjini Madina, aliwaliza ndugu zake swali lifuatalo: “Je mnajua ya kwamba kulikuwako na mitume wa Mungu hapo zamani?” Wakajibu ndiyo Kisha akasema “Mnakisia tu au mnajua?” Wakajibu, Tunajua hasa!” Akaendelea kusema, “Mhaweza kuniambia ni nini kilichotokea kwa wote hao? Wakajibu, “Wamekufa.” Akasema: “Muhammad pia amekufa

kama walivyokufa hao na shuhudieni ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah na Muhammad ni Mtume wake.” Baada ya mfano wake huu mzuri watu wote wakamwiga na kumtukuza sana Kiongozi wao Jarud. (*Tariikhur-Rusuli Wal-Muluuki, cha Abu Jaafar Muhammad, ibn Jarir-at-Tabari, uk. 1058-59, Brill, 1890*).

Hivyo basi walishawishika na wakastakimu katika Islam. Kwa hiyo tunaweza kuona ya kwamba alipofariki Mtukufu Waislamu walielewa ya kwamba hakuna kitu cha ajabu katika kufariki kwake kwa kuwa walikwishafariki kabla yake mitume. Hivyo basi kifo cha Yesu ni ukweli ambao ulikubaliwa bila ya mfarakano na masahaba wote wa Mtukufu Mtume (amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake).

Lakini kadiri wakati ulivyopita maelfu na maelfu ya Wakristo wa nchi mbalimbali waliingga katika Islamu. Kwa bahati mbaya, kwa kuwa watu hawa walikuwa na elimu chache ya Kurani Tukufu na mafundisho ya Kiislamu, waliendelea kushikilia mila zao za zamani na mawazo ya Kikristo kumhusu Yesu ambayo pole pole wakayatapakaza mionganini mwa Waislamu. Waislamu walizikubali taarifa hizi za Wakristo kwa kuamini kwamba wao ni ndugu zao kidini na wakaanza kuzieleza aya za Kurani Tukufu kulingana na hekaya za watu hawa. Matokeo yake ni kwamba kifo cha kawaida cha Yesu ambacho kwacho masahaba wote wa Mtukufu Mtume walikubaliana kikakataliwa na Waislamu na imani ya kwamba Yesu alipaa mbinguni akiwa na mwili wake wa udongo na kwamba baadaye atashuka kutoka mbinguni ikawa imeenea sana katika ulimwengu wa Kiislamu hivi kwamba kuzungumza kinyume cha hivyo kunahesabiwa kuwa ni ukafiri.

Ile aya ambamo kifo cha Yesu juu ya msalaba kinakanushwa inasomeka ifuatavyo: “Na kusema kwao (Mayahudi) hakika sisi tumemwua Masihi Isa bin Mariamu, Mtume wa Mungu, ilhali kwa hakika wao hawakumwua wala hawakumsulubisha, bali alifananishwa kwao (yaani alioneckana kana kwamba aliyejufa) na hawakumwua kwa yakini. Bali Mwenyezi Mungu alimnyanyua kwake

(na kumpa neema ya kukaribiana Naye) na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu mwenye hekima. (Kurani Tukufu 4:158 – 159).

Kutokana na matamshi haya bayana ya kwamba Mayahudi hawakumwua Yesu, hakuna Mwislamu awezae kusema kwamba Yesu alifia msalabani. Kwa hiyo kwa upande mmoja Waislamu walikubaliana na taarifa za waumini wenzao waliotokana na Ukristo ya kwamba yule mtu aliyetungikwa msalabani alikuwa kweli, lakini kwa upande mwingine hawakukubali kwamba mtu huyo alikuwa Yesu Kristo. Wakasema ya kwamba wakati Yesu alipotiwa mbaroni na Mayahudi kwenye chumba, Mwenyezi Mungu alimtuma Malaika wake ambaye alimnyanya Yesu na kumpeleka mbinguni kuitia katika dirisha lililotobolewa kwenye dari na yule mlinzi akafanywa afanane na Yesu na wale wasulubishaji wakamsulubisha huyu mahala pa Yesu. Baadhi ya mufasirina wa Kiislamu wamefikia hadi ya kusema kwamba Yesu alikuwa kifo cha kawaida na kubakia mfu kwa muda wa siku tatu lakini baada ya siku hizo tatu akapaa mbinguni. Wazo hili ya kwamba mtu mwingine alifanywa afanane na Kristo halionekani mahali popote ndani ya Kurani Tukufu na wala haliungwi mkono na hata hadithi moja ya Mtukufu Mtume. Hekaya zote kuhusiana na jambo hili hazikubaliki na haziaminiki.

Isitoshe, hatuoni maana yo yote katika kumfanya mtu mwingine afanane na Yesu na kisha kuwakabidhi Mayahudi. Kama Mungu alikwisha mnyanya Yesu mbinguni kulikuwa na haja gani ya kuwakabidhi Mayahudi mtu wa badili? Je Mwenyezi Mungu alitaka kuwafurahisha Mayahudi ili wajivune ya kwamba wao wamemwua Yesu na kuhakikisha kuwa ni mlaaniwa? Tena, haikusemwa mahali popote ya kwamba huyu mtu aliyewekwa mahala pa Yesu alijaribu kukanusha kwamba yeye si Yesu Kristo. Ilikuwa rahisi kwake kusema tu kwamba mimi si Yesu, basi angeachiwa. Au kwa uchache baada ya kuona kuwa ametoweka, ndugu na marafiki zake wangalianza kumtafuta. Kama hadithi hii ni ya kweli basi hakuna haki yo yote kuwalaumu Mayahudi kwa kuamini kwamba Yesu ni mzushi na nabii mwongo. Hawakumwona Yesu akipaa mbinguni na yule mtu aliyefanywa aonekane kama Yesu hakuweza

hata kukana kwamba ye ye si Masihi, na Mayahudi waliimsulubisha huku wakiamini kwamba wana msulubisha Yesu mwenyewe. Kwa hiyo katika kuhukumu jambo hili Mayahudi watasamehewa mbele ya Mwenyezi Mungu kwa kumkataa Yesu. Lakini msamaha kama huo ni kinyume na undani wa aya tunayojadili kwa vile inasema kwamba Mayahudi wanakabiliwa na laana ya Mwenyezi Mungu kwa sababu wanasema kwamba wamemwua msalabani.

Licha ya aya hii, ziko aya zingine nyingi ndani ya Kurani Tukufu zinazoonyesha waziwazi kwamba Yesu alikufa kifo cha kawaida. Kwa mfano tunasoma ndani ya Kurani Tukufu kwamba wakati Mwenyezi Mungu atakapomwuliza Yesu, “Je wewe uliwaambia watu kwamba nishikeni mimi na mama yangu kuwa miungu wawili badala Yangu?” Yesu atajibu, “Wewe ndiwe Mtakatifu; hainipasi mimi kusema yale ambayo sina haki ya kuyasema; kama ningalisema bila shaka Ungalijua; Unayajua yaliyomo nafsini mwangu, lakini mimi siyajui yaliyomo nafsini Mwako; hakika wewe ndiwe Ujuwaye sana mambo ya ghaibu. Sikuwaambia lolote ila yale uliyoniamuru: ya kwamba mwabuduni Mwenyezi Mungu, Mola wangu na Mola wenu; na nilikuwa shahidi juu ya hayo nilipokuwa kati yao, lakini Uliponifisha Wewe Ukawa Mchungaji juu yao, na Wewe ni Shahidi juu ya kila kitu. (5:117-118).

Kutokana na aya hii ni wazi ya kwamba wakati Yesu atakapoulizwa na Mungu siku ya kiyama, atatangaza kwamba alikufa kifo cha kawaida katika wakati ambapo Wakristo watakuwa wameyaacha mafundisho yake. Imani iliyoshikwa na wengi ya kwamba Yesu yungali hai huko mbinguni na kwamba atakuja tena duniani inapingana moja kwa moja na aya hii. Kwani, kama angalipata nafasi ya kuja tena angalikuta kwamba mamilioni ya Wakristo wanamhesabu kuwa yu Mungu.

Hivyo asingaliweza kupata njia ya kukana ya kwamba hakuwaona Wakristo wakimwamini ye ye kuwa ni Mungu kama aya hii inavyosema. Walakini ukweli ni kwamba INGAWAJE YESU

ALITUNDIKWA MSALABANI ye ye hakufa juu ya msalaba bali alikufa kifo cha kawaida ambacho kilifichika machoni pa Waislamu kwa karne nyingi mpaka alipotokea Masihi Aliyeahidiwa ambaye ameufichua ukweli huu. Katika kitabu chake kiitwacho Jesus in India (sura ya pili) Masihi Aliyeahidiwa ametoa maelezo kuhusu aya inayokanusha kifo cha Yesu juu ya msalaba; Mwenyezi Mungu anasema:

“Mayahudi hawakumwua Yesu wala hawakumsulubisha<sup>a</sup> (yaani hawakumfanya afe msalabani); bali walishuku tu ya kwamba alifia msalabani; hawakuwa na ushahidi wo wote wa kuwashawishi na kuwardhisha kwamba Yesu (amani ya Mungu juu yake) alikufa kweli msalabani.

---

- a. Mufasiriina wa Kiislamu wamelielewa vibaya neno MAA SWALABUUHU lilitotumiwa katika Kurani, wakadhani wa kwamba maana yake hawakumpigilia msalabani, na kwa hiyo wakakanusha kupigiliwa kwake msalabani. Ilhali kwa Kiarabu neno SULB lina maana ile ile ya maneno ya Kiingereza TO CRUCIFY, yaani, kuua kwa kupigilia miguu na mikono juu ya msalaba. (Chamber’s Twentieth Century Dictionary). SENTENSI SWALABAHU maana yake ni, “Alimwua kwa njia fulani inayojulikana”. (Lane’s Arabic-English lexicon).

Katika aya hizi Mwenyezi Mungu anasema kwamba ingawaje ni kweli kwamba Yesu alipigiliwa msalabani na kwamba wao walikuwa na nia ya kumwua, si sawa kwa Mayahudi na Wakristo kudhania kwamba Yesu alikufa kweli msalabani; bali Mwenyezi Mungu alitengeneza njia ambazo zilimwepusha Yesu na kifo cha msalaba.

Kama mtu ni mpenda haki basi anatakiwa kusema ya kwamba kilichosemwa na Kurani Tukufu dhidi ya Mayahudi na Wakristo kimetokea kuwa kweli. Mchunguzi maarufu sana wa siku hizi amehakikisha kwamba Yesu aliokolewa na kifo cha msalaba. Uchunguzi wa taarifa zilizoandikwa unaonyesha ya kwamba Mayahudi hawakuweza kulijibu swali ya kwamba: “Ilikuwaje ya kwamba Yesu alikufa katika kipindi cha masaa mawili au matatu

ilihali mifupa yake haikuvujwa?" Hii iliwafanya Mayahudi wazue udhuru na kusema kwamba walimwua kwa upanga ilhali historia ya zamani ya Mayahudi haisemi ya kwamba Yesu aliuawa kwa upanga. Ilisababishwa na Utukufu na Nguvu za Mwenyezi Mungu ya kwamba kukawa giza, na kwamba kukawa na tetemeko la ardhi, na kwamba mkewe Pilato aliona ruya, na kwamba usiku wa Sabato ulikuwa unakaribia ambapo ilikuwa haramu kwa miili iliyosulubiwa kubakia juu ya misalaba, na kwamba kwa sababu ya ruya ya mkewe yule hakimu alishawishika kumwacha huru Yesu. Yote haya yameletwa na Mwenyezi Mungu ili kumwokoa Yesu. Pia Yesu alifanywa azimie ili wamdhanie kwamba amekufa.

Kulikuwa na hofu kuu sana mioyoni mwao ya kwamba kama mtu huyu alikuwa mwongo na kafiri, mbona ishara za kutisha namna hii zimeonyeshwa wakati wa kuteswa kwake? Ishara ambazo hazikuwahi kutokea hapo kabla? Walikuwa wamevurugikiwa sana hivi kwamba hawakuwa na uwezo tena wa kuziridhisha nafsi zao kama kweli Yesu alikwisha kufa au alikuwa katika hali gani. Walakin kwa hakika kilichotokea ulikuwa msaada wa kimbingu wa kumwokoa Yesu. Msaada huu unaashiriwa kwenye aya isemayo: WALAAKIN SHUBBIHA LAHUM; yaani, Mayahudi hawakumwua Yesu, ila Mwenyezi Mungu aliwafanya wafikirie kuwa wamekwishamwua. Hali hii inawatia moyo wacha-Mungu: Yeye Huweza kuwaokoa watumishi Wake jinsi Apendavyo.

Zile ishara za kutisha, kwa mfano tetemeko la ardhi n.k. ziliwatia hofu Wayahudi na wakadhania kwamba adhabu ya mbinguni ilikuwa ikiwashukia. Isitoshe kulikuwa na uangalifu isije miili iliyosulubiwa ikabakia misalabani katika usiku wa Sabato. Kwa kumwona Yesu amezimia, Mayahudi walifikiri kwamba amekufa. Kulikuwapo na giza na kulikuwa na tetemeko la ardhi na wasiwasi mwingi. Pia walikuwa na wasiwasi kuhusu majumba na watoto wao walikuwaje katika giza kama lile na tetemeko la ardhi?

Katika kitabu hicho hicho Masihi Aliyeahidiwa anasema tena kwamba Walakini mimi siiungi mkono ile njia ya wachunguzi wa Kizungu ambao wanataka kuhakikisha kwa njia hii au ile kwamba misingi ya dini ya Buddha ilifika Palestina katika zama za Yesu. Ni jambo la kusikitisha ya kwamba ingawaje jina la Yesu limetajwa katika vitabu vyatani vya dini ya Buddha, wachunguzi hawa wameamua kuchukua njia ngumu ya kutafuta alama za dini ya Buddha nchini Palestina. Kwa nini hawazitafuti nyayo takatifu za Yesu katika ardhi yenyе miamba mingi ya Nepal, Tibet na Kashmir?

Lakini wachunguzi hawa hawawezi kutegemewa kuuvumbua ukweli ambao umefunkwa chini ya “mablanketi” elfu moja ya giza. Ulikuwa ni msaada wa Mwenyezi Mungu ambaye Aliona kutoka mbinguni ya kwamba kuabudiwa kwa binadamu kumekiuka mipaka yote na kuenea ulimwenguni kote na kwamba ibada ya msalaba na ya yule mtu ambaye anafikiriwa kuwa ametolewa kafara imewatenganisha mamilioni ya watu na Mungu wa kweli Ambaye ghera yake imemleta mtumishi wake kwa jina la Yesu wa Nazareti ili kuivunja imani ya msalaba. Kwa hiyo, sawa na ahadi ya zamani ametokeea akiwa Masihi Aliyeahidiwa. Kisha ukafika ule wakati wa kuvunjwa kwa Msalaba, yaani ule wakati ambapo upotofu wa imani ya msalaba utabainishwa. Ingawaje wazo la Yesu kupaa mbinguni ni la upotofu, hata hivyo lilikuwa na siri ndani yake. Siri yenye ni kwamba ukweli wa Kimasihi ulikuwa umesahauliwa na ukatoweka kama maiti inavyoliwa na udongu wa kaburi. Ukweli huu wa Kimasihi ili aminiwa kwamba unapatikana mbinguni katika sura ya binadamu akiwa na mwili wake. Kwa hiyo ni lazima ya kwamba ukweli huu utashuka ardhini katika akheri zamani. Hivyo basi umeshuka katika zama hizi katika sura ya binadamu na UMEVUNJA msalaba... kwa hiyo msifikirie ya kwamba nimekuja na upanga. La hasha Nimekuja ili kuzilingiza panga zote katika ala zake. Ulimwengu umekuwa ukipigana sana katika giza. Watu wengi sana wamewashambulia wale wenye kuwataenia mema, wakaiumiza mioyo ya rafiki zao wa kweli na wakawajeruhi wapenzi wao kwa sababu ya giza hilo. Lakini

sasa hakuna giza. Usiku umeondoka na mchana umekuja, na amebarikiwa yule ambaye hajiveki nyuma tena.

Hivyo ndivyo ilivyotimilizwa ile bishara aliyoitabiri Mtukufu Mtume Muhammad (amani na rehema za Mwenyezi Mungu juu yake) takriban miaka 1350 iliyopita ya kwamba Masihi Aliyahidiwa atavunja msalaba na kubainisha upotofu wa kuamini kifo cha Yesu juu ya msalaba. Pia imetimiza kile kilichosemwa na Yesu mwenyewe ya kwamba wakati wa kuja kwake mara ya pili: "mataifa yote ya ulimwengu yataomboleza (Mathayo 24:30). Ina maana kwamba Wakristo, Mayahudi na Waislamu amba ni wakazi wa ulimwengu (Yaani Palestina) watajuta sana watakapoju kwamba imani zao zote kumhusu Yesu zilikuwa za upotofu.

Kwa kuwa mnamo karne ya tatu kwa Kalenda ya Kikristo, yaani katika zama za Constantine, msalaba ilitangazwa hadharani kuwa ndio alama ya dini ya Kikristo, kadhaalika Mwenyezi Mungu Ametabiri kwa kuititia katika kinywa cha Masihi Aliyahidiwa kwamba misalaba yote itavunjwa wakati Wakristo watakapoelewa ubovu wa imani yao: "Karne ya tatu haitakuwa imepita kuanzia leo, isipokuwa wote wale amba wanashiriki kushuka kwa Yesu kutoka mbinguni, wawe Wakristo au Waislamu watakata tamaa juu ya ushukaji huu na watazachilia mbali imani zao mbovu ambazo hivi sasa wanaziendeleza kwa mapenzi makubwa sana. Kisha kutakuwa na dini moja na kiongozi mmoja ulimwenguni kote. Nimetumwa kuja kuipanda mbegu na nimesha panda. Mbegu hii itachipua na kutoa maua na matunda katika msimu maalum na hakuna awezaye kuing'oa (Ahmad, Masihi aliyahidiwa, Tadhrikiratus-Shahadatain, uk. 65; Qadian, 1903).

Kabla sijamaliza ningependa kuomba alivyoomba Masihi Aliyahidiwa, Nabii wa zama hizi aliyetumwa na Mwenyezi Mungu ili kuja kutimiliza bishara za manabii wa mataifa mbalimbali: Yeye aliomba hivi:-

“Ewe Mwenyezi Mungu Mpenzi, waokoe Wakristo katika ibada ya kumwabudu binadumu kama Mungu na zitimize ahadi za manabii wako kwa ajili ya zama hizi. Wanyanyue majeruhi kutoka katika miiba. Watakase katika chemchem ya wokovu wako ambayo haipatikani ila katika elimu na mapenzi yako. Hakuna wokovu katika damu ya binadamu. Ewe Mungu Uliye Mwingi wa Rehema, Wakristo wamekuwa wakimwabudu binadamu kwa muda mrefu lakini sasa Wahurumie na yafungue macho yao. Ewe Mungu Uliye Mwenye Nguvu na Mwingi wa Rehema, kila kitu kinawezekana kwako. Kwa hiyo Wanansue katika imani zao mbovu za kusulubishwa na damu ya Yesu. Ewe Mungu Uliye Mwenye Nguvu, Nisikilize mimi kwa faida yao na Uzing’arishe nyoyo zao kwa nuru itokayo mbinguni, ili wapate kukuona. Ni nani awezaye kufikiria kwamba wao wanaweza kukuona Wewe? Ni akili ya nani inayokubali kwamba wao wataacha kumwabudu binadamu na watasikiliza sauti Yako? Lakini Ewe Mungu, kila kitu kinawezekana Kwako. Kwa hiyo usiwahilikishe kama Ulivyofanya katika zama za Nuhu. Wao ni viumbe Wako tu. Wahurumie. Ifungue mioyo yao ili waweze kuupokea ukweli.

**J. D. SHAMS,  
Imamu wa Msikiti wa London,  
London, March 14, 1945.**

